**26 MEI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 26 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali; Ofisi ya Rais. Mheshimiwa Athuman Maige.

Na. 402

### Ujenzi wa Nyumba za Walimu Nchini

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga Nyumba za Walimu kufuatia ujenzi wa Shule nyingi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2024/2025 Serikali imetoa shilingi bilioni 13.79, kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za walimu 263 *(one in one)* katika shule za msingi nchini. Vilevile, shilingi bilioni 14.82 imepokelewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya nyumba za walimu 741. Aidha, mwaka 2025/26 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 54 *(two in one)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kutenga fedha za kujenga na kufanya ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwa kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye uhitaji mkubwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwakopesha baiskeli au pikipiki walimu wanaokaa mbali na shule8 ili waweze kwenda shuleni?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu vijijini kuliko mijini kwa sababu, vijijini hakuna nyumba za kupanga, hasa kwa Jimbo la Uyui?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Athuman Almasi Maige kwa swali hili ambalo linalenga kuendelea kuboresha sekta muhimu ya elimu na hasa elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, tayari Serikali imefanya jitihada za kununua pikipiki za kuwawezesha Maafisa Elimu wote wa Kata nchini, ili waweze kufanya kazi yao kwa umakini na wepesi zaidi. Serikali itaendelea kubuni namna mbalimbali za kuendelea kuwawezesha walimu wetu kwa kuwapa vitendeakazi kwa kadiri pesa inavyopatikana ili waweze kuwa na mazingira mazuri zaidi ya kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge juu ya nyumba za walimu, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, tayari nyumba 860 za walimu zimeshajengwa na Serikali inaendelea na jitihada hizo. Utaona katika kipindi cha miaka minne zaidi ya shilingi trilioni 5.1 zimewekezwa katika upande huu wa sekta ya elimu msingi, kwa ajili ya kuboresha

miundombinu na mazingira ya wafanyakazi kwa upande huu wa elimu msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea na jitihada hizo za kujenga nyumba za walimu. Kama iliyoanza kujenga nyumba awali, itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuendelea kujenga nyumba na kwa kuzingatia maeneo yenye uhitaji mkubwa ambayo mara nyingi ni pembezoni, maeneo ya vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za walimu katika Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha, hasa Kata ya Nayobi na Swetisambo, ambapo mazingira yake ni magumu, mwalimu hawawezi hata kupanga nyumba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Catherine Magige kwa swali lake hili zuri. Serikali ya Awamu ya Sita inadhamiria kuendelea kuimarisha sekta ya elimu msingi, kwa maana ya elimu, kutoka madarasa ya awali, shule ya msingi mpaka sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika kipindi cha miaka minne tayari shilingi trilioni 5.1 imewekezwa katika kuendelea kuboresha miundombinu katika sekta hii muhimu. Vilevile, katika miaka minne hiyo, nyumba za walimu 860 zimeshajengwa na Serikali inaendelea kutenga fedha kila mwaka wa bajeti kuhakikisha kwamba, inaendelea kuboresha ya kufanya kazi kwa walimu wetu kwa kuwajengea nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Catherine Magige, nyumba zitajengwa hata huko Ngorongoro ili kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa walimu wetu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Jonas William Mbunda.

Na. 403

**Hitaji la Watumishi wa Afya Katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Watumishi katika Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga ili kupunguza changamoto iliyopo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa vibali vya ajira kila mwaka, ambapo kuanzia mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025 jumla ya watumishi wa kada ya afya 34,720 wameajiriwa na kupangiwa vituo kote nchi. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2024/2025 Halmashauri ya Mji wa Mbinga imepokea jumla ya watumishi 102 wa kada za afya na watumishi 36 wamepangiwa hospitali za wilaya na 66 katika vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa sekta ya afya kwa awamu na kuwapanga katika maeneo yenye upungufu wa wataalam, ikiwemo Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, Serikali bado inaendelea kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali. Vilevile, katika Mji wa Mbinga kuna mahitaji ya wafanyakazi 802 katika idara hiyo ya afya. Waliopo ni 311 na kuna upungufu wa wafanyakazi 478. Kwa hiyo, upungufu huo ni mkubwa na ni zaidi ya nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kufanya hata utaratibu wa msawazisho wa kuhamisha watumishi kutoka sehemu nyingine na kuwapeleka katika Mji wa Mbinga?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Hivi karibuni Serikali ilitoa mwongozo wa kuruhusu watu kujitolea katika fani hiyo ya afya. Nataka nijue, mpango huo umeanza kutekelezwa au bado?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Jonas Mbunda kwa maswali yake mazuri. Pia, ni dhahiri kabisa katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, zaidi ya shilingi trilioni 1.29 zimewekezwa katika kuboresha miundombinu katika hospitali zetu za halmashauri, vituo vya afya, zahanati na kuboresha sekta nzima ya afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa ongezeko la vituo hivi vya kutolea huduma ya afya vinatengeneza mazingira ya uhitaji wa watoa huduma katika sekta hii muhimu. Tayari Serikali katika Kipindi cha mwaka 20220/2021 mpaka 2024/2025 imeajiri watumishi wa kada ya afya 34,720. Pia, inaendelea na mpaka wakati huu kuna kibali kipya, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025, cha zaidi ya watumishi wa kada ya afya 9,000 ambacho kimetoka na wenyewe wataajiriwa na kusambazwa katika maeneo mbalimbali, hasa yale yenye uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Jonas Mbunda kwamba, hata katika Jimbo lake la Mbinga Mjini,

watumishi hawa watapangwa. Vilevile, nitumie nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kufanya msawazo ili yale maeneo ambayo hayana kabisa watumishi wa kada hii muhimu ya afya, vile vituo ambavyo havina watumishi, angalau viweze kupata hawa watumishi huku tukiwa tunasubiri hawa watumishi wapya wanaoajiriwa waweze kupangwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili, ni kweli, namna moja ya kuendelea kuboresha na kuhakikisha tunapata watoa huduma katika vituo vyetu vya kutolea huduma hii ya afya msingi ni pamoja na kuweka watumishi ambao wanajitolea. Moja, ni kuajiri, nyingine ni kuajiri kwa mikataba na tatu ni njia hii ya kuwatumia hawa watumishi wa kada ya afya ambao wanajitolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali tayari imeanza utaratibu huo. Nitumie nafasi hii kuendelea kusisitiza Wakurugenzi wa Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kutumia utaratibu huu ili kuendelea kupunguza uhitaji wa watumishi hao wa kada hii muhimu kabisa ya afya waweze kupatikana ili kutoa huduma bora ya afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Katika Kata ya Mabogini, Zahanati ya Mabogini, Chekereni, Mtakuja na Mserekia kuna upungufu wa watumishi, miundombinu yake ni chakavu sana na hawana vyoo. Pia, wagonjwa wanapokuja pale wanakwenda kwenye vyoo vya *staff*, jambo ambalo linahatarisha afya ya watumishi wa pale. Je, nini mkakati wa Serikali kurekebisha miundombinu hiyo na kupeleka watumishi katika zahanati hizi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Felista njau kwa swali lake hili zuri. Pia, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri

huko Moshi Vijijini aweze kwenda kufanya tathmini katika zahanati hizi ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge na kuweka katika mpango wa bajeti kwamba, ziweze kufanyiwa ukarabati na hasa katika eneo hili la vyoo ambalo Mheshimiwa Mbunge ametaja, liweze kuwa katika hali nzuri kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na jitihada zake za kuhakikisha kwamba, inaboresha hivi vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi ili viweze kuwa katika hali nzuri na viweze kutoa huduma nzuri kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Moni.

**MHE. MOHAMMED L. MONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Upungufu wa watumishi wa kada ya afya kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ni 67%, hii imechangiwa na ongezeko la vituo vya afya pamoja na zahanati. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuongeza watumishi ili kuweza kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mohammed Moni kwa swali lake zuri. Ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inafanya jitihada kubwa sana ya kuendelea kuimarisha sekta hii muhimu ya afya msingi. Pia, kutokana na uwekezaji mkubwa wa kuendeleza miundombinu, ujenzi wa hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati zimejengwa nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya shilingi trilioni 1.29 imewekezwa katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita. Tunafahamu kwamba, kuna uhitaji wa watoa huduma, kwa maana ya watumishi wa kada ya afya. Pia, tayari Serikali inaajiri na inatoa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka wa bajeti fedha zinatengwa na vibali vinatoka kwa ajili ya kuajiri watumishi wa kada ya

afya ambao wanapangwa katika maeneo tofauti, ikiwemo yale yenye uhitaji mkubwa. Vilevile, kuna ajira za mikataba ambazo Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, kupitia mapato ya ndani, wanaweza kuajiri watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna njia nyingine ambayo ni watumishi wa kujitolea, ambao wanajitolea na kulipwa posho kidogo kutoka kwenye fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na jitihada hizi zote. Nikuhakikishie kuwa, Mheshimimiwa Mohammed Moni, watumishi hawa watapangwa katika Wilaya na Jimbo lako la Chemba ili waweze kutoa huduma bora kabisa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Dkt. Angelina Mabula. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

Na. 404

**Kukamilika kwa Miundombinu Katika Vituo vya Afya Kayenze, Sangabuye na Buswelu**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA K.n.y. MHE. DKT. ANGELINA S. MABULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya Vituo vya Afya katika Kata za Kayenze, Sangabuye na Buswelu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vya afya vya Kata ya Kayenze, Sangabuye na Buswelu vina upungufu wa baadhi ya miundombinu, ikiwemo wodi za kulaza wagonjwa, kliniki ya mama, baba na mtoto *(RCH),* jengo la wazazi, jengo la upasuaji na jengo la mionzi. Kituo cha Afya cha Kayenze kilipokea shilingi milioni 500 katika mwaka 2021/2022, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa

nje *(OPD),* jengo la maabara, jengo la wazazi *(Maternity),* jengo la kufulia na kichomea taka. Majengo haya yamekamilika na yanatumika. Aidha, katika mwaka 2024/2025 Halmashauri, kupitia mapato ya ndani imetoa shilingi milioni 70 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya majitaka na umeme katika Kituo cha Afya Kayenze.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume katika Kituo cha Afya Sangabuye. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya katika Manispaa ya Ilemela, kikiwemo Kituo cha Afya cha Buswelu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tayari Serikali imeshaonesha jitihada za kuhakikisha kituo hiki ambacho ni kikongwe toka miaka ya 74 kinahudumia watu wengi sana, kulingana na eneo lilivyo pembezoni. Sasa Serikali haioni uko umuhimu wa kufanya kituo hiki, angalau kiwe na hadhi sawa na hospitali ya wilaya ili kuwasaidia watu wengi zaidi walioko kwenye eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Upatikanaji wa vituo hivi vya afya umekuwa ni muhimu sana kwa sababu unatoa huduma za jirani. Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kuhakikisha kila kata inapata Kituo cha Afya, ikiwemo Kata ya Nyegezi, Jijini Mwanza, Nyamagana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Stanslaus Mabula, kwa maswali yake mazuri kabisa yanayolenga kuimarisha na kusemea sekta hii ya afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja, kwa kumweleza kwamba, Serikali ya Awamu ya

Sita katika kipindi cha miaka minne imefanya uwekezaji wa zaidi ya shilingi trilioni 1.29 kwenye upande huu kwa kujenga na kukarabati hospitali za halmashauri ambazo ni kongwe. Imejenga vituo vya afya zaidi ya 367, imekamilisha zahanati zaidi ya 980 na inaendelea na kazi hiyo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ataona kabisa hata katika vituo hivi vya afya vya Kayenze, Sangabuye na Buswelu tayari Serikali inatenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inaendelea kuboresha miundombinu hii muhimu ili vituo hivi viweze kutoa huduma ya afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaelewa umuhimu mkubwa sana na huduma kubwa inayotolewa katika kituo hiki cha afya, na Mheshimiwa Mbunge ametaka kwamba kituo hiki cha afya kiwe kina hadhi ya hospitali ya halmashauri. Kwa kuwa kila halmashauri imejengewa na inajengewa na fedha zinatengwa kwa awamu kuhakikisha kwamba kila halmashauri inakuwa na hospitali, Serikali itaendelea kuimarisha huduma katika hospitali ya halmashauri hii ili iweze kuhudumia wananchi wakiwemo hao wananchi ambao Mheshimiwa Mbunge ametaka wahudumiwe na kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ujenzi wa vituo vya afya katika kata zote nchini, Serikali inaendelea na jitihada hizo; na ndiyo maana katika kipindi cha miaka minne tu, tayari kuna vituo vya afya 367 ambavyo vimejengwa. Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote ni mashuhuda kwamba hivi karibuni Bunge hili limepitisha nyongeza ya bajeti ya shilingi bilioni 53.5 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo yote 214. Tayari kuna baadhi ya vituo vya afya vimeshaanza kufikishiwa fedha ya awali shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga majengo ya vituo hivyo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Stansalaus Mabula, hata Nyegezi kwenye jimbo lake la Nyamagana

tutakwenda kuhakikisha kwamba fedha inafika shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuanza kujenga majengo ya awamu ya kwanza katika kituo hiki cha afya. Vilevile tutaendelea kufika katika kata nyingine nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Wananchi wa Kata ya Mbelekese iliyopo Iramba Magharibi, wakati Kamati ya *PAC* tulipotembelea pale kwenye minara, walionesha wana adha ya kituo cha afya, takribani kilometa 42. Walianza zamani wakajenga wakaishia kwenye msingi tu, wana shida sana. Sasa kwa nini Serikali isiwape *priority* kwenda kuwajengea kituo cha afya ukizingatia wako mbali na hospitali ya wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Esther Matiko kwa swali lake hili zuri. Ninaomba niendelee kumtaarifu kwamba Serikali inatambua kuna maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa sana wa vituo hivi muhimu vya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika eneo hili la Mbelekese Jimbo la Iramba Magharibi tayari Serikali inafahamu kwamba kuna uhitaji wa kituo hiki cha afya. Mheshimiwa Mbunge wa jimbo amekuwa akipaza sauti yake kusemea uhitaji huu mkubwa wa ujenzi wa kituo hiki cha afya. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na taratibu za kukifikia hiki kituo cha afya ili kiweze kukamilishwa na kiweze kutoa huduma bora za afya kwa ndugu zetu wa Iramba Magharibi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais. Mheshimiwa Maryam Azan.

Na. 405

**Utatuzi wa Kero za Muungano Zilizobaki**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kutatua kero za Muungano zilizobaki ikizingatiwa kuwa imefanya kazi kubwa hadi kubakiza kero nne tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeweka utaratibu wa kutatua changamoto za Muungano kupitia mfumo rasmi wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la vikao hivi ni kuhakikisha kuwa changamoto zote zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kamati hii imesaidia kwa kiasi kikubwa kumaliza changamoto 22 kati ya 25 zilizoibuliwa tangu mwaka 2026. Aidha, Serikali zote mbili zinaendelea kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ambapo kikao cha Kamati hiyo kilifanyika tarehe 4 Aprili, 2025, Ikulu Dar es Salaam ili kujadili hoja nne za Muungano zilizobakia na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kumeibuka wimbi la wapotoshaji wa ukweli kuhusu Muungano huu, je, nini kauli ya Serikali kuhusu wapotoshaji wa Muungano huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa Muungano huu ni Tanganyika na Zanzibar, je, mpaka sasa ni taasisi ngapi za Muungano zimeshafunguliwa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumeibuka ombwe ama baadhi ya watu wanaopotosha kuhusu historia, maendeleo, chimbuko na ukweli kuhusu Muungano huu. Sisi kama Ofisi ya Rais, Muungano tunaosimamia Muungano na Mazingira, tumeona changamoto kubwa ni kwamba pamoja na kazi kubwa tuliyoifanya, bado kuna baadhi ya wananchi ambao hawajafikiwa na taaluma hii ya Muungano, na ndiyo maana tunaendelea kuwaelimisha kupitia vyombo vya habari, redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatoa majarida pamoja na makongamano mbalimbali, ili wananchi waweze kufahamu ukweli kuhusu Muungano huu. Tumekuwa tukitoa vitabu mbalimbali ambavyo vimeeleza historia ya ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii niwaonye sana wananchi wa Tanzania, baadhi yao waache tabia ya kuubeza Muungano huu kwa sababu hapa tulipo ni kwa sababu ya nguvu na Muungano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii nimwambie tu Mheshimiwa kwamba jumla ya taasisi 33 za Muungano zimeshafunguliwa Zanzibar na zimeshaanza kufanya kazi, na hivi tunavyozungumza zinatoa huduma kwa wananchi. Tunalo Jeshi la Polisi, Uhamiaji, *NIDA, BoT,* na *TRA*. Zipo taasisi nyingi zimeshafunguliwa na zinafanya kazi. Pia kuna Ofisi ya Bunge pale ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano ipo Zanzibar. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Michael Kembaki, kwa niaba Mheshimiwa Zaytun.

Na. 406

**Kupatiwa Umeme Mitaa 18 ya Tarime Mjini**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka umeme katika mitaa 18 ambayo haina umeme Halmashauri ya Mji Tarime?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji Tarime ina jumla ya mitaa 81, ambapo kati ya hiyo mitaa 58 tayari ina umeme na mitaa 23 bado haijafikishiwa umeme. Aidha, mitaa 13 inapelekewa umeme kupitia mradi wa *HEP IIA* na Mkandarasi aitwae *Dyname Construction Engineering*. Mitaa 10 iliyobaki itapatiwa umeme katika miradi inayofuata kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Wilaya ya Arusha Mjini kuwa mji wa kitalii, lakini bado kuna changamoto kubwa ya umeme, hasa kwenye maeneo ya pembezoni, hususan kwenye Kata ya Terrat, Mitaa ya Olepolos, Maskiria na Endavlen. Je, ni lini Serikali itaondoa changamoto hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Serikali inatekeleza miradi mbalimbali katika maeneo ambayo yapo pembezoni ama kwa jina lingine tunaita *peri-urban*. Kupitia wakala wetu wa Nishati Vijijini, tunayo miradi ya pembezoni mwa miji *(peri-urban)* inayotekelezwa kwa ajili ya kuendelea kusambaza umeme katika maeneo ya pembezoni mwa miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Jiji hili la Arusha katika ambayo anaisema ya Terrat tutaenda kuangalia. Kama maeneo haya hayapo katika mpango ambao tunao wa kupeleka umeme kwenye maeneo ya pembezoni mwa mji, basi tutaendelea kuyafikishia umeme kupitia miradi mbalimbali ya *TANESCO* ambayo inatekelezwa katika maeneo ya miji katika kuhakikisha kuwa tunaendelea kuimarisha miradi ya usambazaji kwa ajili ya kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa amesema maeneo haya ni mahususi kwa ajili ya utalii, basi nitaenda kuyapitia tuweze kuona, kama hayapo kwenye mpango wowote, basi kwa mwaka ujao wa fedha tutaweka katika mkakati ili na maeneo haya ya pembezoni yafikishiwe umeme kwa ajili ya kuimarisha hali ya utalii katika Kata hii ya Terrat. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Vitongoji vingi katika Wilaya ya Karatu havina umeme. Hata hivyo, vichache vilivyoingia kwenye mradi wa kupelekewa umeme vimepelekewa nguzo 40 pekee, ambazo bado hazitoshelezi na kuna maeneo mengi hayatapata umeme: -

Je, kwa nini Serikali isiongeze idadi hiyo angalau ku-*cover* vitongoji hivyo kwa kuanzia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninashukuru kwa swali zuri la Mheshimiwa Mbunge. Miradi ya vitongoji ambayo inaendelea ni miradi ambayo ina wigo wake maalum kulingana na kazi ambayo amepewa mkandarasi. Nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge, katika mradi wa vitongoji 9,000 ambao sasa hivi ndiyo tunatafuta mkandarasi, Karatu pia ipo katika mradi na inaenda kupewa vitongoji vya ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge miradi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ni miradi endelevu. Vile 15 ilikuwa kwa ajili ya kila jimbo na ilikuwa ni kwa ajili ya wigo maalum, lakini tunaendeleza miradi hii, kwa ule mradi mkubwa wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 20,000. Awamu ya kwanza nilishasema kuwa tumeshaanza sasa hivi kwa kutafuta wakandarasi kwa vitongoji 9,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wilaya nyingi ziko *covered* katika miradi hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutaendelea kupeleka umeme katika vitongoji hivyo kwa miradi hii ambayo inaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Mustafa Rajab.

Na. 407

**Kuwapa Vijana wa Polisi Jamii Motisha**

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB** aliuliza: -

Je, Jeshi la Polisi lina mpango gani wa kuwapatia Vijana wa Polisi Jamii vifaa na posho kama motisha ya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, vikundi vya ulinzi shirikishi au Polisi Jamii hutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Vikundi hivi husimamiwa na kuratibiwa na viongozi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji ambayo yako chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Miji na Wilaya na kwa kushirikisha wananchi, na ndio wanaochangia vifaa na mahitaji mengine ya msingi katika ulinzi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Jeshi la Polisi ni kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi, kutoa mafunzo ya ukamataji salama, pamoja na kufundisha wajibu wa ulinzi shirikishi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rajab.

**MHE. MUSTAFA MWINYIKONDO RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Nianze kwa kulipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi nzuri ndani ya Taifa letu kwa kudumisha amani na utulivu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ni jukumu la taasisi zilizotajwa, lakini kiuhalisia, halmashauri, shehia, na vijiji huwa havitengi bajeti kwenye suala hili. Je, Serikali kupitia Jeshi letu la Polisi halioni haja suala hili kulibeba wao na kulitengea bajeti ili kuwawezesha askari jamii wetu katika maeneo yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kweli Polisi Jamii wanafanya kazi kwenye jamii hasa na askari wetu katika maeneo hayo huwa hawana vitendea kazi kama vile usafiri. Je, Jeshi la Polisi halioni kuwa kuna haja kwa sasa askari wetu katika maeneo yetu yale ya shehia kuwatafutia walau pikipiki ili kufika kwa haraka kwenye matukio?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimpongeze Mustafa Mwinyikondo Rajab kwa ufuatiliaji wake mzuri sana katika kuhakikisha kwamba jeshi linafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza la bajeti kupitia Jeshi la Polisi, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, vikundi hivi vya ulinzi shirikishi husimamiwa na Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji, na wananchi wa eneo husika ndio huchangia kupata vifaa na mahitaji ya msingi ili kazi hiyo iweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili linalohusiana na vitendea kazi, Jeshi la Polisi limeshasambaza mpaka sasa pikipiki 105 katika kata na shehia kwa upande wa Zanzibar. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza ninalishukuru Jeshi la Polisi kwa kutuletea magari ya Polisi. Swali langu, Serikali iliahidi kujenga nyumba za watumishi katika Wilaya ya Hai. Je, lini sasa itatekeleza ahadi hii kwa kujenga nyumba ya *OCD* na mkuu wa kituo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari pamoja na ofisi za ma-*OCD*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Jimbo la Hai pia tutalichukua tuliweke kwenye mpango wetu na tayari kutengewa bajeti kwa ajili ya kuanza ujenzi mara moja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kimsingi Polisi Jamii na hawa waliotajwa kwenye swali la msingi ni watu wanaofanya kazi kwa karibu zaidi na wananchi, lakini wamekuwa na mazingira magumu, hasa ya kutokuwa na nyumba sehemu wanazofanyia kazi na mwendo mrefu kuelekea sehemu za kazi. Je, ni lini sasa Serikali mtaona wajibu wa kuongeza bajeti kwa watu hawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, vikundi tunavyozungumzia ni vikundi vya ulinzi shirikishi ambapo wananchi wa eneo husika huweza kuwachangia vifaa. Kwa kuwa wanatoka kwenye makazi katika eneo husika kwenye kijiji, kitongoji au mtaa

husika, kwa hiyo, Serikali haina mpango wa kuwajengea wananchi mmoja mmoja katika vijiji vyao, ila kila mmoja ajitahidi kuhakikisha kwamba anakuwa na makazi katika eneo hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Gwajima, kwa niaba yake, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 408

**Barabara Ya Wazo Hill – Tegeta – Kwa Ndevu**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapanua barabara inayotokea Kiwanda cha Simenti Wazo *Hill* – Tegeta hadi Kwa Ndevu ambayo ni nyembamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Wazo *Hill* hadi Tegeta Kibaoni yenye urefu wa kilometa mbili. Kwa sasa *TANROADS* wapo kwenye hatua ya manunuzi ya kumpata Mkandarasi atakayefanya kazi ya upanuzi wa barabara hiyo. Mara baada ya manunuzi kukamilika na mkandarasi kupatikana, kazi ya upanuzi itaanza kufanyika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, pamoja na juhudi hizo ambazo ni kubwa, lakini bado kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo inategemewa sana na wananchi wa Madale, Mpiji Mgohe, Msumi, Makabe, pamoja na

Mbezi Luis. Wananchi hawa wote wanapita kwenye barabara hiyo. Hata hivyo, barabara hiyo imezingirwa sana na magari ya simenti pale kwenye eneo la kiwanda kutokea pale kwenye Hospitali ya Kitengule, hali ambayo inasababisha msongamano mkubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuhakikisha barabara hiyo inapitika vizuri kwa ajili ya wananchi wa eneo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, changamoto inayotukuta huko inaikuta pia Barabara ya Mandela katika eneo la Temeke kwa Sokota. Barabara hiyo imekuwa na msongamano mkubwa sana wa magari makubwa na hasa nyakati za asubuhi na jioni. Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza msongamano huo kwa kuweka hata barabara nyingine ya pembeni kuboresha ile barabara ya ziada ili magari yapite kwa urahisi?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge. Hili la barabara hizi za Tegeta ambalo nimelijibu vizuri kwenye jibu la msingi, barabara zote alizozitaja kwanza ziko kwenye mpango wetu wa bajeti wa kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na barabara hii ambayo imeonekana kwenye swali la msingi, lakini pia, na barabara zake zote hizi ambazo amezitaja. Hata akienda kwenye kitabu chetu, ataziona kwamba tunazifanyia marekebisho na upanuzi ili kupunguza huo msongamano ambao Mheshimiwa Mbunge ameusema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano kwenye Barabara ya Mandela – Buguruni hadi kule Kurasini, kwanza hii barabara iko kwenye Mpango wa *BRT* Awamu ya Tano. Eneo hili la Kwa Sokota ni eneo ambalo pia hii barabara litaihusu, lakini mpango wa haraka wa kufanya barabara nyingine tunaomba tulichukue na tuone kama kutakuwa na uwezekano wa kufanya hivyo, kama ni mpango wa haraka ili kupunguza changamoto ya msongamano katika hilo eneo la Kwa Sokota.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nahato.

**MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza swali la nyongeza. Kutoka Zakhiem kwenda Kibonde Maji A na Kibonde Maji B kuelekea mpaka Kijichi kuna changamoto kubwa sana ya barabara. Barabara hizo hazipitiki na shida inapotokea hasa upande ule wa jeshi, waathirika ni wananchi wanaoishi Kibonde Maji B na A. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hiyo inapitika?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba nilichukue swali la Mheshimiwa Nahato kuhusu hiyo barabara ambayo imekuwa na changamoto kubwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi pamoja na wenzetu wa TAMISEMI tutahakikisha kuwa tunalichukua hilo suala na kuona namna ya kupunguza hiyo changamoto ambayo iko katika hizo barabara alizozitaja, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Masumbwe – Lugunga – Nyasato – Kashero mpaka Nyikonga, ni lini itaanza utakelezaji wake, maana kwenye mpango imo?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lipo kwenye mpango lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko kwenye hatua za manunuzi kwenye hiyo barabara, na hasa ikizingatiwa kwamba katika hiyo barabara ndiyo tunatekeleza ule mpango wa Rais ambao wenzetu wa *World Bank* kupitia mpango wa Rais, tunajenga sehemu ya hiyo barabara likiwepo na Daraja la Nyikonga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Moshi - Arusha kuanzia Sangisi hadi Maji ya Chai imeharibika sana. Je, ni upi mpango wa Serikali kufanya matengenezo ya haraka licha ya kwamba tunajua itajengwa kwa kiwango cha barabara nne?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema hiyo barabara tunajenga na wenzetu wa *JAICA* ambayo itakuwa ni barabara ya njia nne, lakini tuna mpango pia wa matengenezo ya haraka pale ambapo barabara inakuwa imeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaomba fedha kwa Mheshimiwa Rais na ameshatoa fedha za dharura kuhusu kutengeneza maeneo yote yale ambayo barabara zimeharibika sana ili wakati tunasubiri ule mpango wa kutengeneza njia nne, tuweze kutengeneza yale maeneo ambayo yameleta changamoto kubwa, hasa hiyo barabara aliyotaja Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Lyazumbi hadi Kabwe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyotaja inakwenda kwenye bandari ambayo Serikali imeijenga ya Kabwe, na tulichofanya sasa hivi tumeshakamilisha usanifu. Kitu cha kwanza ambacho tumefanya kwa sababu inaenda bandarini, inahitaji magari makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tumeanza kupanua na kuongeza uwezo wa madaraja ili yaweze kupitisha magari makubwa

wakati Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuijenga ile barabara yote kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa barabara kutoka Turiani hadi Mziha kusudi barabara ikamilike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumeshaanza kujenga hiyo barabara, tumeshakamilisha kilometa 50 na katika mwaka huu mwaka tunaoendelea nao tumetenga kilometa 30 na tunaendelea kuzijenga hizo barabara, mpango ikiwa ni kuifikisha hiyo barabara Mziha hadi Handeni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia ulisimama au ulikuwa ndiyo unakaa?

Waheshimiwa, tuendelee na Mheshimiwa Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini.

Na. 409

**Ujenzi wa Barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi Hadi Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya kutoka Mtwara Pachani – Nalasi hadi Tunduru itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru yenye urefu wa kilometa 300 imekamilika. Kwa sasa, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa Serikali inaendelea kutafuta fedha kujenga kwa awamu barabara hii na barabara hii ni nguzo ya Jimbo la Tunduru Kusini pamoja na Wilaya ya Namtumbo, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika mwaka mzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Barabara ya Azimio – Mtina - Makande ni barabara ya mkoa ambayo inatengewa fedha kila mwaka kutengenezwa, lakini inakosa mitaro kwa ajili ya kuimarisha barabara hii. Ni lini Serikali sasa itapeleka fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango ya kujenga mitaro kwenye barabara hii ili iweze kupitika mwaka mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali la kwanza kuhusu barabara hii ya Mtwara Pachani – Nalasi – Tunduru kilometa 300, mkakati wa Serikali pamoja na kwamba tumekamilisha usanifu wote, lakini tumekuwa tukijenga kwa kiwango cha lami maeneo yote yale ambayo ni korofi. Pia, mpango wa sasa ni kuendelea na mpango huu wa hasa maeneo yale korofi ikiwemo pia kujenga vipande vya lami katika miji ambayo barabara hiyo inapita ili kuhakikisha tu kwamba, mwaka mzima barabara hiyo inapitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara hiyo aliyoitaja ya pili ya Azimio, ninadhani wiki iliyopita tulijibu swali la msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ombi lake la kutengenezwa mitaro ili barabara isiharibike, tutalifanya. Nimwagize Meneja wa Mkoa wa Ruvuma kuhakikisha kwamba, katika mipango ya matengenezo ya

mwaka huu unaokuja wa fedha, basi mitaro yote iweze kutengenezwa ili kulinda hiyo barabara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay. Mheshimiwa Issaay, wewe ndio jina lako, halafu unatazama nyuma tena!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi. Serikali tayari imemaliza usanifu wa Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani - Magara - Mbulu kwa kiwango cha lami. Je, sasa ujenzi huu wa kiwango cha lami kwa Barabara ya Mbuyuni - Magara - Mbulu utaanza lini? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumeshakamilisha usanifu pia kujenga lile daraja kubwa ambalo tayari Mheshimiwa Makamu wa Rais ameshazindua. Atakubaliana nami kwamba, hii barabara inapita kwenye miinuko mikali sana, *Mbulu Escapement,* ambacho kikubwa ni kukamilisha kwanza kujenga kile kipande chote cha zege, lakini wakati huo Serikali inatafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave. Jamani, ngojeni. Wewe Mheshimiwa Kilave unakumbuka kwenye mpira jana nilikuona…

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Kila mtu anashangashangaa leo humu. *(Kicheko)*

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulisema Mnzava.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Barabara inayoelekea viwanja vyetu vya michezo vilivyoko ndani ya Jimbo la Temeke, Mkapa pamoja na Uhuru, barabara ile ni chakavu sana, lakini bado tunakumbuka kwamba tutakwenda katika michezo ya *AFCON.* Je, lini mtaanza kuipanua na kuiweka sawa sawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili aliloliongea Mheshimiwa Mbunge wa Temeke, Serikali inalifahamu na Wizara ya Michezo na Utamaduni pamoja na Wizara ya Ujenzi, wameshawasiliana kuona ni barabara zipi hasa zitatumika katika mashindano ya *AFCON* ili ziweze kukarabatiwa na kuwa katika kiwango bora kabisa cha Kimataifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Ninataka kujua kauli ya Serikali juu ya ujenzi wa barabara inayounganisha Tanzania na Rwanda kupitia Kijiji cha Rutumu Kata ya Rutunguru, Kijiji cha Nyakakoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote ambazo zinaunganisha nchi na nchi, ni barabara ambazo ni barabara kuu na ziko kwenye mpango. Kijiji alichokitaja, sina uhakika kama ndiyo hii barabara ya Omugakorongo. Kama haiko hivyo, basi itakuwa siyo barabara *actually trunk road,* lakini nitahakikisha kwamba ninaongea na Meneja wa Mkoa ili vijiji hivi alivyovitaja tuweze kujua kama ni barabara inahudumiwa na *TANROADS* ama na wenzetu wa *TARURA,* halafu nitampa jibu sahihi nini mpango wa Serikali kuhusu hiyo barabara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Barabaa ya Nyamiaga – Rusumo, Jimbo la Ngara ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu hii barabara ni ya Uchumi, inaenda mpaka nchi jirani ya Rwanda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo barabara ikishakamilishwa usanifu, Serikali itatafuta fedha ili kuweza kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara ambayo inaunganisha nchi na nchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Sichalwe.

Na. 410

**Ujenzi wa Kituo cha Forodha – Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Forodha Momba ili kupunguza msongamano wa magari Tunduma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2025/2026, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na idara mbalimbali za Serikali zinazohusika na shughuli za kiforodha mipakani, inafanya upembuzi yakinifu *(Feasibility Study)* ili kupata taarifa muhimu kwa kuanzishwa kwa Kituo cha Forodha Wilaya ya Momba. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwanza, kabisa ninaomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba mwaka 2024 Zambia walipitia changamoto kubwa sana ya kukosa mahindi. Kwa hiyo, eneo hili kuna barabara, kwa hiyo, mahindi mengi ambayo yalikuwa yanatoka Tanzania mengi yalipitishwa kutokea kwenye barabara hii. Kwa hiyo, ni eneo la muhimu sana kujengewa kituo cha forodha. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, kwa kuwa ni mipango yenu kwenye mwaka wa fedha 2025/2026, *feasibility study* itakamilika kwa muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa eneo hili licha ya kutoroshwa mahindi, mazao mengine na bidhaa nyingine zinazoingia na kutoka kwenye nchi yetu, wenzetu wa upande wa Zambia kwa kujikinga wameshajenga *gate toll.* Je, ni mpango upi wa dharura wa kulinda barabara hiyo, wakati tunaendelea kujiandaa na kujenga kituo cha forodha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu, ninaomba uniruhusu nimpongeze sana Mheshimiwa Sichalwe kwa namna anavyofuatilia masuala haya ya mipakani sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, amesema ni lini? Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mwaka huu wa fedha ripoti hii ya *feasibility study* itakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu la pili, ninaomba nitumie fursa hii kutoa maelekezo kwa Kamishna wa Mapato, Kamishna Mkuu *TRA* ili kuhakikisha kwamba wameimarisha doria katika njia hiyo ambayo ameitaja na kuhakikisha kwamba tumeendelea kuzuia na kuimarisha mipaka yetu katika suala zima la magendo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei, jiandae Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi ya kuwalipa wananchi wa Vunjo waliopisha ujenzi wa kituo cha forodha cha pamoja pale eneo la Ghona na Mabungo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imelifanyia uhakiki suala hilo la ulipaji fidia, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, fedha hizo zitapatikana kwa wananchi wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi. Serikali kupitia *TRA* iliahidi kuanza kutoa huduma za forodha kwenye Mpaka wa Mgoma na iliahidi kwanza kwa kupeleka ofisi za muda kwa maana ya makontena ili kuanza kutoa huduma hiyo mapema iwezekanavyo. Mpaka sasa hatujaona makontena, na kazi haijaanza. Ni lini sasa *TRA* itaanza kutoa huduma za forodha kwenye mpaka wa Mgoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Serikali bado iko pale pale, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ndani ya mwaka huu wa fedha kabla ya kumalizika, kontena hizo zitakuwa zimefika kwa ajili ya kutoa huduma katika kituo hiki cha forodha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Malembeka.

Na. 411

**Mipaka ya Tanzania na Msumbiji Kuwa Eneo Salama la Biashara**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaruhusu Mipaka ya Tanzania na Msumbiji kuwa eneo salama la kibiashara ili kuinua uchumi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kamati ya Ulinzi ya Wilaya ya Nanyumbu, Mkoani Mtwara imeshajiridhisha kuhusu suala la usalama baada ya tathmini ya kiusalama kuonesha kuwa eneo la Mpaka wa Tanzania na Msumbiji ni salama kuendesha biashara na uwekezaji kwa nia ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na kuwepo na umuhimu wa mpaka huo, Serikali imejenga soko la mpakani, Mtambaswala ambalo baada ya kukamilika lilikabidhiwa Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara. Soko hilo lilijengwa kwa lengo la kukuza na kuendeleza biashara katika mpaka huo ili kuinua uchumi kupitia fursa za biashara zinazopatikana mpakani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nina swali moja, lingine litakuwa ni ombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, katika Kijiji cha Mduhe, Mkachima, Mnavira, Utimbe Sindano hadi Mtambaswala kuna wakati wanaambiwa kwenda shambani ni saa mbili asubuhi na kurudi ni saa tisa. Hali hiyo inafanya washuke kiuchumi. Je, ni lini tahadhari hiyo itatolewa ili wakulima wafanye shughuli zao za kiuchumi bila kupotezewa muda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba, kwa kuwa Waziri amesema usalama upo wa kutosha, pia, nawapongeza wanajeshi wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ulinzi, ningeomba hamasa na ushawishi mkubwa ufanyike katika maeneo hayo ili wawekezaji waende wakawekeze viwanda kwa ajili ya kutoa ajira na kupandisha kipato cha wananchi wa eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa nafasi. Kwanza, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka kwa kufuatilia

kuhusiana na maendeleo hasa ya kiuchumi katika Mkoa wa Mtwara mahususi kule Nanyumbu na hasa mpakani na majirani zetu Msumbiji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inafanya kazi kubwa kuhakikisha tunaendelea kuongeza usalama katika mpaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza ambapo kuna changamoto hii ya baadhi ya wananchi kwenye vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna muda fulani wanaambiwa angalau wasiendelee na shughuli, kwanza, niwaambie na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ili tuweze kufanya maendeleo, lazima kuwe na usalama. Kwa hiyo, ulinzi na usalama ni kitu muhimu na cha kwanza kama ambavyo tuko kwenye afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanafanywa ili kuhakikisha usalama wao wanavyofanya shughuli za maendeleo, iwe ni kilimo au biashara ni salama kwa wananchi wanaofanya shughuli hizo katika vijiji alivyotaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita, imeshachukua hatua kubwa kwa kuweka usalama mkubwa. Kwa hiyo, kadiri muda utakavyokuwa unaenda na usalama utakapokuwa unaimarika, maana yake muda wa kufanya kazi utaongezeka siyo tu saa kumi na mbili inaweza kuwa hata saa ishirini na nne, lakini cha muhimu ni usalama wa Watanzania na wananchi hawa ambao wako kule mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kazi kubwa sana kuvutia wawekezaji katika maeneo tofauti tofauti na hasa amesema hili eneo kwa sababu ni mpakani na wenzetu wanatumia fursa vizuri ya kule Msumbiji na Tanzania, tutaendelea kuvutia wawekezaji waende kuwekeza kule kwa sababu usalama unaendelea kuimarika siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba hili tutalifanya na tutaelekeza wawekezaji kwenda katika eneo hili la Nanyumbu na mikoa hii ya kusini.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Katani Ahmad Katani. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Festo.

Na. 412

**Kubadilishwa kwa Ratiba za Mara kwa Mara za Ndege ya *ATCL***

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kulipa fidia Abiria wa ndege za *ATCL* wanaoingia hasara kutokana na kubadilishwa ratiba ya kusafiri mara kwa mara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma bora kwa abiria wa *ATCL* na mashirika mengine ya ndege yanayotoa huduma za safari za ndege nchini na inachukua hatua kuhakikisha kuwa ratiba za safari zinazingatiwa kadri inavyowezekana. Hata hivyo, mabadiliko ya ratiba yanaweza kutokea kwa sababu za kiutendaji pamoja na sababu zilizo nje ya uwezo wa *ATCL* ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shirika linaendeshwa kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa vya huduma kwa abiria, na huchukua hatua stahiki kuhakikisha haki za abiria zinalindwa kwa mujibu wa Sheria, Taratibu na Miongozo ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* na Jumuiya ya Mashariki ya Ndege Duniani *(International Air Transport Association – IATA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ratiba inapobadilika, hatua zinazochukuliwa ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mapema na kuhakikisha kuwa abiria wamepewa chaguo mbadala, ikiwa ni pamoja na usafiri mbadala, au kurejeshewa nauli pale inapohitajika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imewekeza kwenye Shirika letu la Ndege, na tunaona kwamba inakusudia kwenda kuunganisha Bara lote la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maswali mawili. Swali la kwanza, ni kwamba mbali na majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba, huwa mnatoa taarifa, lakini kumekuwa kunajitokeza pia, kwamba watu wameshafika *airport* na *delay* zinatokea kuanzia pale pale *airport* ya saa tatu, nne mpaka tano. Sasa ipi ni kauli ya Serikali kuhakikisha huduma hii ya ndege ndani ya nchi yetu inakuwa ni nzuri na inavutia pia wasafiri wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, watu wa Mkoa wa Njombe wana matamanio kuwa wanaiona *ATCL*. Ni upi mkakati wa Serikali ambao inategemea kufanya ili Uwanja wa Ndege wa Njombe ujengwe, pia watu wa Mkoa wa Njombe tupate kuiona *ATCL*? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Sanga kwa maswali yake ya nyongeza, lakini hasa kwa kutambua na kuthamini kazi kubwa ambayo Serikali inafanya. Tukiangalia tulikotoka kwenye eneo la anga, tulikuwa na changamoto kubwa. Mwaka 2016 tulikuwa na ndege moja, mwaka 2021 tukawa na ndege tisa, na leo tuna ndege kumi na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha huu wa 2025/2026 ambao tumepitisha juzi bajeti yake, tunakwenda kununua ndege nyingine nne. Hii inamanisha nini? Huduma inazidi kuboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama tulikotoka, tulikuwa na ndege moja na tulikuwa na vituo vichache sana nchini. Leo tuna vituo kumi na tano katika nchi yetu, tuna vituo tisa vya kikanda, yaani katika

nchi tofauti tofauti na pia sasa hivi tunaweza kwenda katika vituo vitatu vya Kimataifa. Haya yote ni mabadiliko makubwa na mapinduzi makubwa kwenye sekta yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, sababu za *delays* kwa sehemu kubwa inachangiwa na masuala ya kitendaji pamoja na *technical* ni pamoja na hali ya hewa, ama ndege tumegundua kwamba ina changamoto. Sasa inaweza ikatokea abiria ameishafika *airport,* nasi tukagundua ndege yetu ina changamoto, hatuwezi kuruhu ndege itoke kwa sababu kwenye Sekta ya Anga jambo la kwanza na muhimu linalozingatiwa na kutazamwa ni usalama kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimsii Mheshimiwa Festo atuvumilie inapotokea hatua hiyo tunakuwa hatuna namna, lazima ndege hiyo ishughulikiwe kwanza, tutazame changamoto ni nini, halafu baada ya hapo tujue tunachukua hatua gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Sanga akiungana na Wabunge wenzake wa Mkoa wa Njombe, wamekuwa ni wahanga na wadau wa muhimu sana kufuatilia maendeleo ya uwanja wa ndege pamoja na ndege za *ATCL* katika mkoa wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie, kwa sasa tuko kwenye hatua za kupata eneo katika Mkoa wa Njombe ili tuweze kujenga kiwanja kikubwa zaidi, kwa sababu katika mwaka wa fedha ujao 2025/2026 pamoja na maboresho ya viwanja vya ndege vinavyoendelea tunajenga viwanja vitatu. Mmoja, Kiabajwa pale Bukoba kwa ajili ya kuunganisha ukanda mzima wa maziwa; wa pili, Serengeti kwa ajili ya kuongeza *entrance* yetu katika hifadhi yetu; na wa tatu, ni uwanja wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe tunatazama fursa zilizopo katika eneo hilo na ndiyo maana tunajenga uwanja mkubwa utakaoruhusu ndege kubwa ya mizigo ili kubeba mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na parachichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukikamilisha hatua hiyo, nakuhakikishia ndege yetu itatua pamoja na mashirika mengine tutaweza kuyashawishi waweze kufanya shughuli zake katika uwanja wa ndege wa Njombe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa ndege hasa inayotoka Mwanza na kwenda Dar es Salaam imekuwa na kupoteza muda ama kuwapotezea wasafiri muda mwingi kukaa *airport,* je, Wizara ama shirika linaonaje kutengeneza utaratibu kama kuna *delay* ili wale wasafiri waweze kupata chakula na vinywaji wakati wamepumzika kuisubiri ndege hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukifanya hivyo na kama kuna maeneo hatujafanya hivyo, nawaelekeza *ATCL* kuhakikisha kwamba pale tunapofanya *cancellations* au *delays,* basi wahakikishe kwamba abiria anapewa angalau huduma za msingi ikiwa ni pamoja na chakula kutokana na usumbufu ambao kimsingi wanakuwa wameupata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ina pilikapilika nyingi sana za watalii na wafanyabiashara ambao wangependa kuutembelea Mji wa Dodoma kupitia Uwanja wa KIA. Je, Serikali ina mpango gani kuanzisha *route* ya *KIA* – Dodoma ili kuwasaidia makundi haya kufika kwenye Mji wao Mkuu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Prof. Ndakidemi kwa kufuatilia safari za Dodoma kwenda Kilimanjaro sawa na Wabunge wa Mwanza -

Dodoma, sawa na Wabunge wa Mbeya – Dodoma. Haya ni maeneo matatu ambayo tumebaini kwamba kuna uhitaji mkubwa sana wa kuunganisha na Makao Makuu yetu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge atuvumilie wakati ambapo kwanza tunakwenda kuongeza ndege za *ATCL* na kutazama uwezekano wa kuanza kwenda kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitumie nafasi hii kuyasihi na kuyaomba mashirika binafsi ambayo hapo awali tulikuwa na ndege chache kwenye baadhi ya maeneo, lakini yalitusaidia na yalitukwamua, ndiyo maana wenzetu wa *flight link* tayari wameshatangaza kuanza safari kutoka Kilimanjaro kwenda mpaka Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba pia *flight link* na mashirika mengine yatazame namna ya kuanzisha *route* kutoka Dodoma kwenda Kilimanjaro, kutoka Dodoma kwenda Mwanza, kutoka Dodoma kwenda Mbeya na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kwa sababu gani? Ukisoma takwimu kwa miaka michache iliyopita, unaona *Market Share* ya *Air Tanzania* inazidi kushuka. Ukiangalia mwaka 2021 ilikuwa na 52.9%, ukiangalia mwaka 2022 ilikuwa 50.9%, ukiangalia 2023 ilikuwa 48.1%, na mwaka 2024 ilikuwa 47.9%. Maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba pamoja na kwamba inaongeza idadi ya abiria, lakini *private sector* wanaongeza zaidi ndege. Huu ndiyo uchumi, na hii ndiyo nchi unayotaka kuiona ambayo *private sector* wanashiriki kikamilifu katika kuleta ndege ili Serikali pia iweze kufanya kazi kubwa ya kujenga miundombinu mipya na kuboresha iliyopo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Elimu, Sayansi Mheshimiwa Gallos. *(Makofi)*

Na. 413

**Kutunga Sera Itakayotoa Kipaumbele katika Elimu kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatunga Sera itakayozitaka Taasisi za Elimu kuboresha mazingira ya kufundishia na kuwapa kipaumbele Watu wenye Ulemavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa watu wenye mahitaji maalum. Katika kutekeleza hilo, Serikali imehuisha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na kuwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, ambayo kupitia matamko yake imeweka mkazo wa kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa watu wenye mahitaji maalum kwa kutoa miongozo mbalimbali ikiwemo, Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Miongozo yote hiyo ina lengo la kuweka mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi zote za elimu na mafunzo nchini. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gallos.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Naomba niulize swali moja la nyongeza. Nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Je, Serikali ina mpango gani juu ya kutatua tatizo la uhaba wa walimu

wanaosomesha kwa kutumia njia ya alama na nukta nundu hususan kwa vijana wanaosoma elimu ya juu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mikakati ya aina mbalimbali ya muda mfupi na vilevile tuna mkakati wa muda mrefu. Katika mkakati wa muda mfupi, hivi sasa vyuo vyetu tumeongeza idadi ya vyuo vinavyotoa walimu wanaofundisha vijana wetu au wanafunzi wetu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni tulikuwa na vyuo vichache sana, lakini sasa hivi tumeongeza na vile tulivyoongeza ni kama ifuatavyo: tumeongeza Chuo cha Patandi, Chuo cha Mpwawa, Chuo cha Kabanga, Chuo cha Askofu Mihayo, Chuo cha UDOM, *University* of Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria pamoja na Chuo Kikuu cha Mkwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vyuo hivi sasa vinatoa elimu hii kwa walimu wale ambao wapo vyuoni kwa lengo la kuhakikisha kwamba tunapata walimu wenye taaluma ya kutumia lugha za alama na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wetu wa mrefu ni maboresho ya Sera pamoja na mitaala yetu. Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu, mwaka 2023 tulipitisha Sera Mpya ya Elimu na Uboreshaji vilevile wa Mitaala. Katika hii Sera ya Elimu sasa inatupelekea kwamba somo hili la lugha ya alama linakuwa ni somo la lazima katika vyuo vyote vitakavyokuwa vinafundisha taaluma ya Ualimu nchini. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Raymond. *(Makofi)*

Na. 414

**Mkopo wa Vifaa na Mitaji kwa Masharti Nafuu**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, Wahitimu wangapi wa mafunzo ya ufundi na Wasichana wangapi wamekopeshwa vifaa na mitaji kwa masharti nafuu kuanzia Julai, 2021 hadi sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Wadau na Wabia mbalimbali wa Maendeleo, imeendelea kufanya jitihada za kuwapatia wahitimu vifaa vya kazi na mitaji midogo kwa ajili ya kuwawezesha kujiajiri kwa kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji kulingana na ujuzi walioupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2021 hadi sasa jumla ya wahitimu 587 wakiwemo wanawake 57 wamepatiwa vitendea kazi *(Startup Kit)* kupitia programu za mafunzo zilizoendeshwa kupitia Mradi wa Kukuza Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali kwa Kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inatarajia kuwawezesha wasichana 3,400 waliopata mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwapatia vitendea kazi *(Startup Kit)* vitakavyowawezesha kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inatoa rai kwa vijana kutumia fursa ya mikopo ya 10% inayotolewa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoka kwenye mapato ya Serikali ili kupata mitaji itakayowawezesha kujiajiri. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; kwa kuwa wakati wanafunzi wanaanza shule uwiano uko pamoja, idadi ya wavulana na wasichana, nini kinachosababisha mafunzo haya ambayo sasa yataleta maendeleo, wasichana kupunjwa chini ya 10% kwa miaka mitano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa jambo hili ni jema na linafungua fursa za maendeleo kwa wote, Serikali ina mpango gani wa kuongeza au kupanua mafunzo haya ili wengi zaidi waweze kunufaika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa mafunzo, tukimaliza ule mzunguko wa elimu ya lazima, huku juu tunapokuja ni lazima vijana wetu waweze kufanya maombi *(application)*. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwa kadri tunavyopokea maombi kwa pande zote mbili kwa jinsia zote mbili, mara nyingi sana tunazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani swali lake ni la msingi sana. Ni kwamba idadi hii ya wanafunzi 57 walionufaika ndogo lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi *startup kit* tulitoa kwa mara ya kwanza mwaka 2024 na tulikuwa tunaanza kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, awamu inayokuja sasa ya 2025/2026 idadi imeongezeka kama nilivyozungumza hapa kwamba itafikia 3,400 na tutakuwa tunaongeza idadi hiyo kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Maimuna.

Na. 415

**Sheria ya Huduma Salama ya Utoaji Mimba**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, Serikali haioni sababu ya kufanya Marejeo ya Sheria kuruhusu utoaji mimba kwa wanaopata mimba kutokana na kubakwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 150 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ni kosa la jinai kutoa mimba au kusaidia kutoa mimba. Aidha, kubaka au kufanya shambulio lolote la kingono ni kosa la jinai. Hivyo, mtu yeyote anayefanya hivyo anakuwa ametenda kosa na anapaswa kuadhibiwa kifungo jela kwa muda usipungua miaka 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa mimba kunaweza kusiwe kosa pale tu kitendo hicho kinapofanyika kwa sababu za kitabibu na imethibishwa na watabibu kuwa kwa kufanya hivyo itakuwa wanaokoa uhai wa mama mjamzito. Hivyo, Serikali inatoa rai kwa mtu yeyote anayefanyiwa vitendo vya ukatili wa aina yoyote ya kingono ikiwemo ubakaji, kutoa taarifa kwa vyombo vyetu vya usalama hususan Jeshi la Polisi ili hatua za kisheria zichukuliwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, Hivyo, tunafanyia kazi mapendekezo hayo kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali ikiwemo Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa

kuwa akina mama wanaobakwa na wanapata ujauzito mara nyingi wanawachukia watoto wale, wakiwaangalia inawakumbusha kitendo kile ambacho wamefanyiwa na mara nyingi inawasababishia msongo wa mawazo au matatizo ya afya ya akili, je, ni kwa nini Serikali isichukue jukumu la kuwatunza watoto hao wasiokuwa na hatia ili wazazi hawa waweze kuishi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kuweza kufanya marejeo ya sheria hiyo ili kuhakikisha mchakato huo unakwenda kwa haraka ili waweze kuwanusuru watoto wale ambao hawana hatia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana muuliza swali. Moja ni kile kitendo ambacho wazazi wale waliopata watoto kwa njia ya ubakwaji kuwachukia wale watoto wenyewe. Niwasihi tu kwamba mtoto hana dhambi na wala hana jambo lolote ambalo linaweza likafanya asitunzwe na yule mzazi. Badala ya kumnyang'anya kumpeleka kwenye kituo cha kulelea watoto, niwasihi tu wawe wavumilivu wakati sheria inapochukua mkondo wake. Kwa sababu yule ambaye alimbaka, kwa vyovyote vile sheria itafuatilia mazingira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika marejeo ya sheria, huu ni ushauri na nimeshajibu kwenye jibu la msingi kwamba tunapitia ili sasa sheria ile iweze kuangalia haya makandokando ambayo yanaonyesha unyanyapaa ndani ya tukio lenyewe kama lilivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia, Mheshimiwa Nusrat.

Na. 416

**Ulinzi kwa Watoto Dhidi ya Udhalilishaji Mitandaoni**

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda Watoto dhidi ya udhalilishaji mitandaoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya Serikali kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto kupitia mitandao ni pamoja na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali za Ulinzi wa Mtoto wa Mwaka 2024. Uanzishwaji na uzinduzi wa Kampeni ya Kitaifa ya Usalama wa Watoto Mtandaoni; Kutoa elimu kwa umma kwa kutumia machapisho mahususi yaliyoandaliwa kwa ajili ya watoto, walimu, wazazi na walezi juu ya matumizi sahihi ya mtandao pamoja na kuandaa *video* fupi za maigizo zitakazoanza kuonyeshwa kwenye vyombo vya habari ili kutoa elimu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Wizara imeanzisha Kituo cha Huduma cha Wateja kinachowawezesha wananchi kupiga simu bila malipo kwa ajili ya kutoa taarifa na kupata elimu ya msaada ya ulinzi na usalama wa mtoto, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza tukisema watoto tunamaanisha watoto chini ya miaka 18. Sasa hivi kuna sintofahamu kubwa sana kwenye mitandao ya kijamii hususan mtandao wa *TikTok* ambapo watoto chini ya 18 wamekuwa wanaonekana wanaingia *live* na wanafanya matendo yasiyofaa pamoja na kucheza uchi. Hili watu wanalifahamu kwa sababu watu wengi tuko *TikTok*.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali inachukua hatua gani ili kuwalinda watoto hawa dhidi ya wao kufanya aidha kwa sababu wengine wanalazimishwa kufanya hivi vitendo na watu wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, cheni ni ndefu sana, lakini wengine wanafanya kwa kutokuwa na ufahamu wa kutosha. Sasa Serikali inachukua hatua gani kuzuia vitendo kama hivi ambavyo vingi kwa kweli vinafanywa na watoto chini ya miaka 18? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa ukiondoa na ukatili wa kwenye mitandao, kuna udhalilishaji mwingine ambao unafanyika kwa watoto mpaka shuleni na majumbani.

Je, Serikali sasa inapanga vipi kushirikiana na TAMISEMI ili waandae majukwaa maalum ya watoto mashuleni ili wajengewe uwezo, wawe wanaweza kuripoti udhalilishaji na ukatili ambao wanafanyiwa katika mazingira yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali itachukua sheria kali kwa mtu yeyote yule ambaye atatuma *video* ambazo hazina maadili na kuonyesha katika mitandao yote ya kijamii. Serikali ipo makini na Serikali ya Awamu ya Sita inajali sana watoto na inaendelea kufanya miongozo mbalimbali kuhakikisha vitendo hivyo na kutuma picha hizo za ovyo zinakomeshwa ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama na watoto wetu wanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, Serikali inashirikiana vizuri na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuandaa miongozo ya ulinzi na usalama kwa watoto pamoja na kuendesha majukwaa hayo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuwapa elimu, ili kuhakikisha majukwaa haya yanaenda kwa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali kupitia Mabaraza ya Watoto katika shule mbalimbali zikiwemo za Msingi na Sekondari yanawawezesha watoto kujiamini, kujieleza na kuhakikisha kwamba pale wanapoona vishiria vya vitendo vya ukatili kuweza kukabiliana navyo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha. Wageni waliopo Bungeni Asubuhi hii ni kama ifuatavyo:-

Wageni wa Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson ambao ni Ndugu Abigail Chams ambaye ni Msanii wa kike wa kwanza kuteuliwa kwenye Tuzo ya Kimataifa. Karibu sana. Pia yupo Ndugu Gabriela Chamungwana, Meneja wa Abigail Chams; Ndugu Seven Mosha, Meneja Mkuu wa Kampuni ya Muziki ya *Sony Africa* na *Sony East Africa;* na Ndugu Getrude Chamungwana, Meneja wa Abigail Chams. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 11 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Kamati ya Maendeleo Kata ya Bonyokwa na Kisukuru wakiongozwa na Diwani wa Bonyokwa na Kisukuru. Mheshimiwa Tumike Malile. Karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Ndugu Ally Gugu, Katibu Mkuu; Ndugu Maduhu Kazi, Naibu Katibu Mkuu; Afande *IGP* Camilius Wambura, *Inspector General Police; CGP* Jeremiah Katungu, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza; *CGF* Ndugu John Masunga; *CGI* Dkt. Anna Makala; Ndugu James Kaji, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA);* na Ndugu Omari Issa, Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi. *(Makofi)*

Pia wapo Ndugu Teofile Bakwea, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza; *CP*. Kombo Hamisi Kombo, Kamishna wa Polisi kutoka Zanzibar; Kamishna Hassan Ali Hassan, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar; na Ndugu Hassan Hajji Hassan, Kaimu Mkurugenzi wa *NIDA* Zanzibar. *(Makofi)*

Pia, wapo Mheshimiwa Queen Sendiga, Mkuu wa Mkoa wa Manyara; Ndugu Emmanuela Kaganda, Mkuu wa Wilaya ya Babati; na Ndugu Peter Toima, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo Ndugu Wallec Mashanda, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe; Ndugu Rasul Shandala, Katibu Tawala Wilaya ya Karagwe; Ndugu Wanja Mtawazo, Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Sheikh Ali Ngeruko, Mwakilishi wa Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania; Sheikh Dkt. Alhad Mussa, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani; na *Fr.* Raphaely Maligite, Mwakilishi wa Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania. *(Makofi)*

Pia, wapo Askofu Dkt. Maasa Ole Gabriel, Katibu wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania; Mch. Dkt. Cyprian Hilinti, Mwakilishi wa Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania; *SACP* William Mkonda, Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani; na Mch. Baraza Kioza, Katibu wa Baraza la Makanisa ya Kipentekoste Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Bashugwa ni familia yake Ndugu Jenifer Bashungwa ambaye ni mke wa Mheshimiwa Waziri; na Ndugu Santo Bashungwa, Mtoto wa Mheshimiwa Waziri. Ahsanteni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Ndugu Ukundi John Sillo ambaye ni mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri. Karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga; Ndugu Amos Mtweve, rafiki yake kutoka Malangali, Ludewa Mkoani Iringa. Karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ambaye ni Ndugu Zuberi Nikata, Katibu wa Mbunge kutoka Namtumbo, Mkoani Songea. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ambao ni wapiga kura wake kutoka Morogoro Vijijini. *(Makofi)*

Wapo wageni Wawili wa Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Mkoani Songwe. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Wakurugenzi wa Bodi ya Sekta ya Ulinzi Binafsi, wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Felix Kagisa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Shaban Hamisi Taletale ambao ni wapiga kuwa wake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 60 na walimu 10 wa Shule ya Msingi Anlex kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Wahadhiri na wanafunzi 25 kutoka Taasisi ya Uhasibu Tanzania, kampasi ya Kigoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanafunzi 75 na walimu watano wa Shule ya Msingi Ebonite kutoka Wilaya ya Ubungo, Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 75 na walimu watano wa wa Shule ya Msingi Doris kutoka Kijichi Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Bashungwa ni Makamishna wa Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Nishati itaendesha semina kuhusu gesi ya petroli *(Liquefied Petrol Gas - LGP)*, iliyoingizwa kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kupikia hapa nchini, na gesi asilia inayozalishwa nchini *(Natural Gas)*. Semina hii itafanyika kesho

Siku ya Jumanne tarehe 27, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge Saa Saba Mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote, mnakaribishwa kuhudhuria semina hiyo muhimu ili kuwajengea uelewa zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya nishati.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ahsanteni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2024/2025 na Kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, pamoja na muhtasari huu, ninaomba hotuba yangu yote ipokelewe na kutambuliwa kama Kumbukumbu Rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika Bunge hili kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea

kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 10 Disemba, 2024. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuliongoza vema Taifa letu na kwa maendeleo makubwa tunayoyashuhudia yakitokea nchini, chini ya uongozi wake. Tunamwombea Rais wetu afya njema na Mwenyezi Mungu amlinde na kumtunza mwanamama huyu shupavu, jasiri mwonesha njia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza nchi yetu. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa maendeleo yenye kasi ya kuijenga Zanzibar kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu hawa kwa kumsadia vyema Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake, pamoja na miongozo wanayonipatia ya kuboresha utendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Pia, ninampongeza Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu waa Chama cha Mapinduzi kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka huu 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge, na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza Bunge hili Tukufu kwa viwango. Ameiheshimisha nchi yetu kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Ninawaomba sana Wapigakura wake wa Jimbo la Uyole mwaka huu wamchague na kumrudisha hapa Bungeni ili Taifa liendelee kumtumia Kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mbunge, na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri unayoifanya ya uwakilishi kwa kuwakilisha vyema wapigakura wako wa Jimbo la Ilala na kumsaidia vyema sana Mheshimiwa Spika kuliongoza vyema Bunge. Ninawaomba Wapigakura wako wa Jimbo la Ilala wakurudishe tena Bungeni mwaka huu ili tuendelee kuchapa kazi na wewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza na kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Bunge na kwa ninyi Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote, kwa ushirikiano mliotupatia katika kipindi chote cha miaka mitano ambayo tumekuwa wote humu Bungeni. Ninamwomba Mwenyezi Mungu amfanyie wepesi kila mmoja wenu ili michakato ya wajumbe ya mwaka huu ya uchaguzi iwe yenye heri na mafanikio kwetu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge mmefanya kazi kubwa ya uwakilishi wa wananchi kwa kujituma na bidii kubwa. Tumeshuhudia pamoja na kazi ya kuwasemea wananchi humu Bungeni, mmegonga hodi mara kwa mara kwenye kila Wizara ili kufuatilia miradi ya maendeleo kwa ajili ya wananchi Majimboni kwenu. Tumekuja Majimboni kwenu na tumeshuhudia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi umekuwa ni wa *speed,* miradi imeenda sana, kazi mmeifanya kubwa na nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Ndugu yangu Mheshimiwa Daniel Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri, Mheshimiwa Daniel Sillo ni mchapakazi. Anafanya kazi za Wizara kwa bidii na uadilifu, ni mnyenyekevu na mpambanaji kwa ajili ya maendeleo ya wapigakura wake wa Jimbo la Babati Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitumie fursa hii kuwaomba wananchi wa Babati Vijijini kuhakikisha wanatumia haki yao ya kidemokrasia ya kumrudisha mpambanaji wao Mheshimiwa Daniel

Sillo Bungeni, mwezi Oktoba mwaka huu 2025. Mmepata Kiongozi makini na mwenye uwezo mkubwa kwa maendeleo ya Babati Vijijini. Hongereni sana wananchi wa Babati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, na Mwenyekiti wa Kamati ya NUU; na Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya NUU. Ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya NUU na Sekretarieti ya Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya NUU imekuwa na msaada mkubwa kwa Serikali, ushauri na maoni ya Kamati siku zote yamelenga kuimarisha utekelezaji wa kazi za Wizara. Ahsanteni sana Kamati ya NUU kwa ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninaishukuru familia yangu; mke wangu Jennifer Bashungwa na watoto wangu Santo, Solana, Sankara na Samora kwa kuniombea na kunipa upendo na ushirikiano mkubwa, na hivyo kunipa utulivu katika kusimamia majukumu ya Wizara na kuweza kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuwashukuru sana waajiri wangu, wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kunipa ushirikiano na kufanya kazi kwa bidii huku tukiwa wamoja na wenye nia thabiti ya kujenga ustawi nzuri kwa maendeleo ya Wilaya yetu ya Karagwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata miradi mingi sana na kwa kila sekta. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetekelezwa vyema chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mwaka huu tunayo kazi moja tu, nayo ni kumpa mitano tena ya kishindo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025, ndani ya nchi yetu tumeendelea kushuhudia uwepo wa amani, usalama, utulivu, na mshikamano kutokana na utendaji na ufanisi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Vyombo vya Usalama vilivyo chini yake. Pia, hali ya

usalama inaendelea kuimarika na hatua zinachukuliwa mara moja pale matishio ya kiusalama yanapobainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali. Ninaomba niseme machache kwa sababu ya muda. Taarifa ya kina kuhusu mafanikio haya inapatikana kwenye kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama limeweza kudumisha usalama, amani na utulivu, na hivyo kuifanya nchi yetu kuendelea kuwa kivutio kwa wawekezaji, wageni, na watalii. Jeshi la Polisi limepokea magari 218 kwa ajili ya matumizi ya Makamishna, Naibu Kamishna, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi, Wakuu wa Polisi wa Wilaya na Vitengo ndani ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, Jeshi la Polisi limepata pikipiki 105 kwa ajili ya Polisi Kata na Shehia. Upatikanaji wa magari na pikipiki utaimarisha utolewaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Idara ya Uhamiaji tunajivunia kuwezesha uingiaji wa wageni nchini na kuongezeka kufikia wageni 1,839,342 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, ikilinganishwa na wageni 511,243 walioingia nchini kwa kipindi kama hicho miaka minne iliyopita. Hizi ni juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo Filamu ya *Royal Tour. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeongezeka kutoka shilingi bilioni 939.08 mwaka wa 2021/2022 hadi kufikia shilingi trilioni 2.06 mwaka huu tunaoomba wa 2025/2026, sawa na ongezeko la 120%. Ninamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na hivyo kuendelea kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewezesha Jeshi la Magereza kutumia nishati safi katika magereza yote 129 nchini kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani. Utekelezaji huu ni sawa na 100% ya lengo la kupeleka nishati safi kwa magereza yote nchini. Hivi sasa magereza 66 kati ya magereza 129 yanatumia huduma ya Mahakama Mtandao. Huduma ya Mahakama Mtandao kwa magereza 63 yaliyobaki itakamilika mwaka 2028/2029. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utolewaji wa huduma hiyo umesaidia kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya mahabusu, kupunguza gharama kwa Serikali katika usafirishaji wa wafungwa na mahabusu, kuokoa muda wa kusikilizwa mashauri ya wafungwa na mahabusu, na upatikanaji wa haki kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, tumenunua mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji, vyenye thamani ya dola milioni 100 za Kimarekani. Hadi kufikia Aprili, 2025, Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepokea magari 40 ya kubebea majeruhi wa majanga, magari 30 ya mawasiliano na kuongoza *operation* za kuzima moto na uokoaji pamoja na karakana sita zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuzalisha jumla ya Vitambulisho vya Taifa 1,243,105, na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,308,774, sawa na 99% ya idadi ya namba za vitambulisho 21,514,741 zilizozalishwa. Aidha, katika kipindi tajwa jumla ya vitambulisho 1,092,160 vimesambazwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyosambazwa kufikia 21,191,598.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niokoe muda kwa kufanya rejea ya maeneo matano ya vipaumbele katika bajeti ya mwaka 2025/2026. Vipaumbele vimeelezwa katika aya ya 27 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uhalifu wa Kimtandao *(Cyber Crimes)*; ulaghai mitandaoni na matumizi yasiyo sahihi ya teknolojia na uhalifu wa kimtandao ni changamoto katika jamii yetu hivi sasa.

Ninaomba nitumie nafasi hii kuwaahidi Watanzania kwamba, vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na vyombo vingine tutapambana nalo usiku na mchana ili kukomesha kukithiri kwa uhalifu mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua shida kubwa inayowapata wananchi katika suala hili la ulaghai, wizi, na matumizi yasiyo sahihi ya mitandao. Katika Bajeti tunayoomba ipitishwe na Bunge leo kwa mwaka wa 2025/2026, shilingi bilioni 2.3 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia upatikanaji wa taarifa za upelelezi wa makosa ya jinai, sanjari na kufanya *operation* za uhalifu wa kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Jerry Silaa, Mbunge, na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; na *TCRA* na watumishi wa Wizara kwa ujumla, kwa ushirikiano katika kupambana na uhalifu wa matumizi hasi katika mitandao. Ninatoa wito kwa wananchi kutumia mitandao na mifumo ya teknolojia kuboresha hali ya maisha na maendeleo ya nchi na siyo vinginevyo. Tumejipanga vyema kuimarisha mashirikiano hasa kupitia Jeshi la Polisi na *TCRA*, kupambana na ujambazi huu mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *operation* iliyofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na *TCRA* katika Wilaya za Ifakara, Sumbawanga, Kinondoni, Ilala, Mbeya Mjini, Arusha Mjini, na Singida Mjini, imewezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 66. Ninatoa pongezi kwa Jeshi la Polisi kwa kufanya *operation* hiyo, na ninaagiza *operation* hizi ziwe endelevu na Doria Mtandaoni *(Online Patrol)* ziimarishwe ili kudhibiti matumizi yasiyo sahihi ya mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama barabarani, matukio ya ajali barabarani yanatokana na makosa ya binadamu hususan uzembe wa madereva, uendeshaji hatari, na mwendokasi. Wizara kupitia Jeshi la Polisi imeandaa mikakati ya kudhibiti matukio ya ajali barabarani kama ilivyoelekezwa na Mheshimiwa Rais kupitia hotuba ya kuukaribisha mwaka 2025, tarehe 31 Disemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati na maelezo ya kina kuhusu matumizi ya teknolojia katika kupambana na ajali barabarani pamoja

na uhalifu kwa ujumla ni kama yalivyoelezwa katika aya ya 42 mpaka ya 45 ya kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Polisi Jamii, ushirikishwaji wa wananchi katika kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu; kwa kutambua kuwa usalama wa jamii ni jukumu la pamoja, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, Makundi Maalumu, Wizara ya Afya na Wizara ya Katiba na Sheria, tunatekeleza mipango ya Kitaifa na Kimataifa ya kupambana na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto. Wizara inashirikiana na mashirika yasiyo ya Kiserikali katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii limetoa mafunzo kwa viongozi wa kijamii ili kuwajengea uwezo wa kutambua, kutoa taarifa, na kuzuia vitendo vya ukatili katika maeneo yao. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwa Watendaji ikiwemo kutoa elimu kuhusu namna ya kushughulikia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji kwa wanawake na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi na ukarabati wa vituo 31 vya Polisi unaendelea kwa gharama za shilingi bilioni 5.52 kama ilivyoelezwa katika aya ya 58 hadi 60 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi, Jeshi la Polisi limepokea shilingi bilioni 34.78 kwa ajili ya ununuzi wa magari 275 ya Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Wakuu wa Vikosi vya Kutuliza Ghasia, na Wakuu wa Upelelezi wa Wilaya. Taratibu za ununuzi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa magari hayo mapya na ya kisasa, utarahisisha utendaji kazi wa Jeshi la Polisi na kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi. Magari hayo yanatarajiwa kupokelewa mwisho wa mwezi Juni, 2025. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 194.95 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, magari haya ni nyongeza ya magari 218 yaliyopokelewa mwezi Machi na Aprili mwaka huu wa 2025 kwa ajili ya matumizi ya Makamishna, Naibu Kamishna, Makamanda wa Polisi wa Mikoa na Vikosi, Wakuu wa Polisi wa Wilaya na Vitengo ndani ya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa idadi hii na viwango hivi vya vitendea kazi, wananchi wetu wasiwe na wasiwasi. Serikali inaendelea na jitihada za kuimarisha usalama wa wananchi wetu na mali zao ili wananchi waendelee kuishi kwa amani ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama ndani ya jamii yetu mijini na vijijini. Watanzania tushikamane kulinda nchi yetu dhidi ya maadui wa nje na ndani. Adui dhidi ya nchi yoyote na nchi yetu ikiwemo hasa kwenye karne hii ya 21, siyo mpaka akudhuru kwa kutumia vifaru kuhesabika, ni mvamizi wa nchi. Adui anaweza kuleta madhara na kuvuruga amani kwa kutumia magenge ya wanaharakati kama ambavyo tuliona siku za hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kujua machungu ya amani ikipotea, angalia nchi zilizo kwenye machafuko ya kuvunjika kwa amani sehemu mbalimbali duniani, hata hapa kwenye Bara letu la Afrika, Watanzania wenzangu hatutakubali kamwe. Tutaendelea kuchukua hatua na kwa mujibu wa sheria kulinda amani na utulivu uliopo ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Uzalishaji Mali la Polisi limeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo Mradi wa Miji Salama *(Safer Cities)*. Maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo kwa awamu ya kwanza yamekamilika ikiwemo kubainisha maeneo yatakayofungwa kamera 4,100 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, na Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi utagharimu Dola za Kimarekani milioni 145.2. Hadi kufukia Aprili 2025, Dola za Marekani milioni 80 sawa na takribani bilioni 231.07 zimetolewa kwa Shirika hilo kupitia mkopo

wa gharama nafuu kutoka *Abu Dhabi Export Office (ADEX)*. Fedha hizo zitatumika kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi katika mikoa hiyo mitatu niliyoitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya ulinzi na usalama magerezani, kama ambavyo nimetaja kwenye mafanikio ya Jeshi la Magereza, moja ya mafanikio makubwa tuliyoyapata chini ya Jeshi la Magereza ni kupungua kwa msongamano wa magereza kwa 20%. Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA, Jeshi la Magereza limepokea makasha 10 kutoka Mahakama ya Tanzania na tunaishukuru sana Mahakama ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, makasha hayo yamefungwa vifaa vitakavyowezesha utoaji wa huduma za Mahakama kwenye magereza 10 nchini. Hatua hii ni mwendelezo wa kuimarisha huduma hiyo ambayo ilishaanza kutolewa katika vituo vya magereza 66 kati ya 129. Aidha, huduma ya Mahakama Mtandao kwa magereza 63 yaliyobaki itakamilika mwaka 2028/2029.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada hizi za kurahisisha upatikanaji wa haki ni miongoni mwa utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya utekelezaji ya huduma ya Mahakama Mtandao magerezani yamesaidia kuipunguzia gharama Serikali za kuwasafirisha mahabusu na wafungwa kwenda Mahakamani kwa kutumia magari, kuokoa muda wa kusikilizwa mashauri ya wafungwa na mahabusu, na upatikanaji wa haki kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Magereza limeanza kutumia fursa za Programu ya Urasimishaji wa Ujuzi unaopatikana nje ya Mfumo Rasmi wa Mafunzo. Programu hiyo inatolewa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)*. Kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya wafungwa 201 wamenufaika na

programu hiyo na kutunukiwa vyeti vya ujuzi katika fani mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii ni mafanikio ya maboresho ya huduma za urekebu ambazo zitasaidia utangamano wa wafungwa katika jamii na kupunguza urudiaji wa makosa kwa wafungwa hao. Wizara itashirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuwasaidia wapate mitaji kupitia mikopo ya 10%. Hata maboresho haya ni utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Haki Jinai kwa Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai kwa jamii yetu ya Watanzania kuwa tayari kuwapokea na kuwapa ushirikiano wafungwa wanaomaliza vifungo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Magereza linatekeleza majukumu yake ya msingi ya uzalishaji, ikiwemo shughuli za viwanda vidogo, ujenzi, na uchimbaji madini. Uzalishaji huo umewezesha ukusanyaji wa mapato ghafi ya jumla ya shilingi bilioni 16.22 kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025. Utekelezaji wa shughuli za miradi ni kama ilivyobainishwa katika aya ya 114 hadi 121 ya kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika la Magereza litaendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye maeneo yake, ikijumuisha takribani ekari 42,000 zinazofaa kwa kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini, na ujenzi wa miundombinu ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia nafasi hii kuwakaribisha wawekezaji ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kushirikiana na Shirika la Magereza katika uwekezaji kupitia fursa lukuki walizonazo kwa lengo la kupunguza utegemezi wa ruzuku kwa Jeshi la Magereza, na ili Jeshi la Magereza liweze kuchangia kwenye uchumi wa Taifa letu kwa kiasi kikubwa kuliko ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kukabiliana na changamoto za utoaji wa huduma bora kwa wananchi, Serikali

kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza Mradi wa Ununuzi wa Mitambo na Vifaa vya Kuzima Moto na Uokoaji wenye thamani ya dola milioni 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, kwa maana ya mwezi uliopita mwaka huu, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea magari 40 ya kubebea wagonjwa, magari 30 ya mawasiliano na kuongozoea *operation* za kuzima moto na uokoaji, karakana sita zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo, gari moja la kubebea maji, mitambo miwili ya kuvuta magari mabovu yaliyopata ajali, shehena ya vifaa vya kuzima moto na uokoaji, pamoja na miundombinu ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kufanya mageuzi ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji haijaishia hapo. Mwisho wa mwezi huu kwa maana ya wiki hii, tunatarajia kupokelewa kwa boti moja ya kuzima moto na uokoaji, magari matano ya kubeba maji, gari moja la uokoaji, mitambo miwili ya kuvuta magari mabovu na yaliyopata ajali, shehena za vifaa vya kuzima moto na uokoaji, pamoja na miundombinu ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa na magari mengine zaidi ya hizi *batch* ambazo nimezitaja ambazo tumepokea na tutapokea wiki hii. Vifaa na magari mengine yatapokelewa mwezi Agosti na Disemba mwaka huu ikiwemo magari 149, boti 22 za kuzima moto na uokoaji, magari matano ya kubebea maji, magari matatu ya kukabiliana na matukio ya kemikali hatarishi, shehena ya vifaa vya miundombinu ya mafunzo ya uokoaji na uzimaji moto, na helikopta moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa mitambo, vifaa vya kuzima moto na uokoaji, kutolewa kwa fedha za ukamilishaji wa miradi na ujenzi wa vituo vya Zimamoto na Uokoaji ni miongoni mwa mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni ukweli usiopingika kwamba, jitihada

tunazoendeleanazo zitaliwezesha jeshi kuwa la kisasa na la viwango vya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea na mapambano dhidi ya wahamiaji haramu nchini, kupitia kampeni ya Mjue Jirani Yako, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara, kupitia Idara ya Uhamiaji, itaendeleza ushirikiano na nchi mbalimbali, hususan zenye idadi kubwa ya wahamiaji haramu, kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kuweka mikakati ya kukabiliana na wahamiaji haramu, kukuza mahusiano na kubadilishana taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa Idara ya Uhamiaji pale wanapowatilia mashaka wageni waliofika kwenye maeneo yao ili kuhakikisha wageni wanaoingia nchini, wanafuata sheria, kanuni na taratibu za ukazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, itaendelea kuimarisha udhibiti wa wahamiaji haramu. Aidha, Idara ya Uhamiaji imejipanga kimkakati kwa kushirikiana na makundi mbalimbali ya wananchi, ikiwemo Watendaji wa Kata na Shehia, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa pamoja na Viongozi wa Vitongoji, Dini na Kimila, ili wadau hawa muhimu sana wawe ni sehemu ya kuelimisha jamii kuhusu namna ya kumtambua mhamiaji au mgeni katika maeneo yao, hususan katika mikoa ya pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *NIDA* Wizara imedhamiria kukamilisha usajili wa watu takribani milioni sita ambao bado hawajasajiliwa kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022 katika kipindi cha miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejiwekea miaka mitatu, angalau kila mwaka *target* ya milioni mbili, ili hawa watu milioni sita ambao bado hawajapata usajili wa *NIDA* kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu tunaoomba bajeti wa 2025/2026, mpaka 2027/2028 tuwe tumekamilisha zoezi la Watanzania wote wenye sifa,

kwa mujibu wa sensa, tuwe tumewasajili na wana vitambulisho vya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya malengo hayo ya miaka mitatu katika mwaka huu wa fedha 2025/2026 tunaoomba shilingi bilioni 3.24 zimetengwa, kwa ajili ya kuendelea na usajili na utambuzi wa watu takribani shilingi milioni 2.4 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Watu waliosajiliwa na kutambuliwa tangu kuanza kwa usajili na utambuzi wamefikia 25,854,970 sawa na 82% ya watu 31,582,976 wenye umri wa kuanzia miaka 18, kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto ya wananchi kubadilisha taarifa zao katika Kanzidata ya *NIDA,* mwongozo maalum umeandaliwa kwa ajili ya kurahisisha marekebisho ya taarifa za wananchi zilizopo katika *Register* ya *NIDA*. Naielekeza *NIDA* kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa, ili kuwezesha wananchi kufanya marekebisho ya taarifa binafsi katika mfumo wa *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NIDA* inaendelea kuboresha huduma zake za usajili na utambuzi, ambapo kwa sasa namba ya utambulisho inapatikana ndani ya siku tano baada ya mwombaji kusajiliwa na kitambulisho kitatoka ndani ya siku 21 tangu kusajiliwa. Tunatambua lipo kundi dogo la wanafunzi wa elimu ya juu ambao hawajafikia umri wa miaka 18. Kundi hilo litapata namba za utambulisho, yaani Jamii Namba, baada ya kuanza usajili wa watu wenye umri wa chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu lipo kisheria. Sheria ya sasa inataka mtu mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea ndio apate Kitambulisho cha *NIDA*. Hata hivyo, kwa kuwa kwenye bajeti hii tumeomba fedha kwa ajili ya kuanza kusajili kuanzia mtoto anapozaliwa mpaka umri wa miaka 18, na umaalum na uhitaji wa wanafunzi wa vyuo vya juu, katika bajeti hii tutaanzanao kuwasajili wakiwa *under-age* ili waweze kupata hivi vitambulisho. Tumetenga fedha maalum katika bajeti hii ninayoiwasilisha ili zoezi hili lianze mara moja baada ya kupitishwa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa wanafunzi wote wanaotarajia kujiunga na vyuo vya elimu ya juu na kati, waliofikisha umri wa miaka 18 na kuendelea, kujitokeza kusajiliwa na kupata Namba ya Utambulisho wa Taifa mapema ili kupunguza msongamano wa waombaji kwenye Ofisi za *NIDA* baada ya dirisha la maombi ya mikopo kufunguliwa. Aidha, waombaji wote wahakikishe kuwa, taarifa wanazowasilisha *NIDA* zinafanana na taarifa zao za kitaaluma, hususani majina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa kuwezesha matumizi ya namba moja ya utambulisho katika kutoa huduma kwa wananchi. Mpango huo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Jamii Namba itatolewa kwa watu wote chini ya miaka 18 na kwa wageni wanaoingia nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamii Namba hiyo itamtambulisha mtu wakati wa kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi za Serikali na Binafsi ndani ya nchi kuanzia anapoipata hadi anapofariki. Jamii Namba hii itaongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi kwa kuwaondolea usumbufu wa kurudiarudia kuwasilisha taarifa na nyaraka wakati wa kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji huu ni katika kuzingatia azma ya Mheshimiwa Rais ya kuondoa usumbufu kwa wananchi wakati wa kupatiwa huduma, kuwaondolea mzigo wa kuwa na vitambulisho vingi kwa ajili ya utambuzi na kuwa na utambulisho mmoja mahali pote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya shilingi bilioni 11.34 zimetengwa, kwa ajili ya kuanza zoezi la majaribio ya kutoa Jamii Namba, ili kuwasajili na kuwatambua watu 235,826 wenye umri chini ya miaka 18 kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022. Majaribio hayo yatafanyika katika Wilaya za Kusini Unguja, Wilaya ya Kilolo Iringa na Wilaya ya Rungwe, Mbeya, na Kwimba baada ya hapo tutaendelea maeneo mengine ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi kirefu *NIDA* imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya utoaji huduma duni kwenye wilaya zote nchini. Waheshimiwa Wabunge, najua changamoto ambazo wananchi wetu wanazipata, mmekuwa mkifuatilia haya mambo hapa Bungeni na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lakini mnaona ni namna gani bajeti hii tumejipanga kwa ajili ya kwenda kutatua changamoto zote ambazo zilikuwa zinawapata wananchi kwenye utoaji wa huduma za *NIDA*. Changamoto hizo zilitokana na ukosefu wa vitendea kazi, uhaba wa watumishi na urasimu usiokuwa na sababu za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la urasimu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mtendaji Mkuu wa *NIDA*, Ndugu yetu Kaji, ameingia akiwa amenyooka na *reformer* mzuri. Kwa hiyo, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania, Mheshimiwa Rais, kupitia bajeti hii, anatuwezesha kuongeza vitendea kazi kwa ajili ya *NIDA* na kuongeza ikama ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaye Mtendaji Mkuu wa taasisi, ambaye amekaa pale kimkakati kuhakikisha tunafanya *reform* sahihi ya kuhakikisha *NIDA* inatoa huduma nzuri kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, jumla ya shilingi bilioni 45.2 zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa ajili ya kuboresha mazingira ya ofisi kwa kununua vitendea kazi, ikiwemo ununuzi wa magari 140, haijapata kutokea, kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwenye hili eneo na mengine ambayo tumeomba ninyi tupitishieni tu, halafu muone kazi ikiendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu unaathiri zaidi watoto na wanawake. Jumla ya wahalifu 19 wanaojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Katika kuimarisha mabambano dhidi ya uhalifu huo, Serikali imefanya maboresho ya sheria kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu, Sura ya 432, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kutoa onyo kwa watu wote wanaojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu kuacha mara moja. Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa watu watakaojihusisha na uhalifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 kazi zitakazotekelezwa na Wizara katika kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu zimeelezwa kwa kina kwenye Kitabu cha Hotuba yangu. Jumla ya shilingi bilioni 2.04 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 ili kutekeleza kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Ndugu zangu Ally Gugu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Dkt. Maduhu Kazi, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ushirikiano wanaonipatia mimi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nawashukuru na kuwapongeza wakuu wa vyombo vya usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha wananchi kutekeleza shughuli zao kijamii na kiuchumi wakiwa na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viongozi hawa naomba niwataje; Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus Wambura; Kamishina Jenerali wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Katungu; Kamishina Jenerali wa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, John Masunga; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala; na ninamshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu James Kaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nawashukuru Wenyeviti wote na Wajumbe wa Bodi za Mashirika yaliyopo chini ya Wizara, pamoja na Kamati za Kitaifa zinazoratibiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ushauri na utendaji kazi wa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru watumishi wote wa Wizara na vyombo vilivyopo chini ya Wizara, ahsanteni sana

watumishi, raia, maafisa, Askari wote *rank and file,* kwa kufanya kazi kwa juhudi na weledi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya niliyoyataja na kazi nzuri ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, yamewezekana kwa sababu, mmefanya kazi nzuri kila mmoja wenu katika eneo lake. Ninawashukuru sana, ninawaomba mwendelee kufanya kazi kwa moyo huo huo wa kujituma bila kuchoka na kwa uzalendo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazishukuru Taasisi za Dini na zisizo za kidini kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuhamasisha amani na utulivu nchini. Ninaishukuru Sekta ya Habari kwa ushirikiano wanaotoa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kurejea wito alioutoa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 5 Mei, mwaka huu wa 2025 wakati wa utoaji wa Tuzo za *Samia Kalamu Awards,* Jijini Dar es Salaam, ambapo alisema na ninanukuu, "Zungumza, Sema, Chambua, lakini uzalendo uwepo. Hapa ndipo ulipozaliwa, hapa ndipo ulipotoka na utakapomalizikia, kwa maana ya kuipenda nchi yetu". *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada hizi endelevu za kuvutia wageni kutoka nje ya nchi kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kuvutia uwekezaji. Kwa kutambua nchi yetu siyo kisiwa, kwa wageni wale wachache au kundi watakaopanga kuja nchini kwa nia ovu ya kuhatarisha amani, hatutakuwa na muhali nao. Wageni hawa waovu hawana nafasi hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Idara ya Uhamiaji kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, kwa utimamu wao katika kudhibiti wageni haramu wa aina niliyoitaja na wale wageni wanaoingia nchini kwa kibali fulani na wakishaingia kwenye jamii yetu wanafanya mambo ambayo ni kinyume na kibali walichoidhinishiwa wakati wanaingia. Wageni hawa ni wahalifu kama wahalifu wengine, watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wananchi wote kwa ujumla na niwasihi tena, kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani. Natoa wito kwa Watanzania kuwa wazalendo, tusikubali kwa hali yoyote ile kutumika au kuwa sehemu ya hila ya aina yoyote ya kusaliti nchi yetu. Tuipende nchi yetu, Mama Tanzania. Hakuna Tanzania nyingine zaidi ya hii tuliyonayo. Ni wajibu wa kila Mtanzania kushiriki katika ulinzi wa amani na usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhitimisha, naomba nisome makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kwa maana ya malengo yetu. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 428, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 24.7 kutoka shilingi bilioni 403.3 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, sawa na ongezeko la 6.12%.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mikakati iliyowekwa na Wizara kufikia lengo hilo ni kuimarisha huduma za Uhamiaji Mtandao *(e-migration),* kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki na ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa 2025/2026, ninaomba Bunge lako liidhinishe Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ya jumla ya shilingi 2,067,161,717,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 701,703,184,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 950,318,192,000 ni mishahara; na shilingi 415,140,341,000 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo shilingi 388,610,747,000 ni fedha za ndani na shilingi 26,529,594,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI MHE. INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2025/26.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuwasilisha katika Bunge hili kwa mara ya kwanza Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2025/26 nikiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Naomba nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 10 Desemba 2024. Aidha, nampongeza Mhe. Rais kwa kuendelea kuliongoza vema Taifa letu katika nyanja mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako, Watanzania na Dunia kwa ujumla imeendelea kushuhudia uwepo wa amani, usalama, utulivu na mshikamano katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni kutokana na uongozi na usimamizi madhubuti wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Utendaji na ufanisi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Vyombo vya Usalama vilivyopo chini yake unaendelea kuimarika kutokana na hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru Viongozi wote wa Kitaifa kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake pamoja na miongozo

wanayonipatia ya kuboresha utendaji wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** Viongozi hao ni pamoja na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukushukuru wewe binafsi Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Pia, namshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia Spika kuliongoza vema Bunge. Bunge hili limekuwa ni kielelezo na mfano wa kuigwa katika kuishauri Serikali ili kuleta maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, nawapongeza na kuwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoutoa katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, namshukuru Mhe. Vita Rashid Kawawa Mbunge wa Jimbo la Namtumbo, na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU), Mhe. Vincent Paul Mbogo Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kusini, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya NUU, Wajumbe na Sekretarieti ya Kamati hiyo. Kamati imechambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara na kutoa ushauri uliosaidia kuboresha bajeti kwa mwaka 2025/26 na utendaji wa Wizara kwa ujumla. Katika kipindi kifupi ambacho nimefanya kazi na Kamati hii, nimefaidika na ushauri na maoni ya msingi yanayonisaidia kuimarisha utekelezaji wa kazi za Wizara.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee naishukuru kwa moyo wa dhati familia yangu (Mke wangu Jennifer na watoto wangu Santo, Solana,

Sankara na Samora) kwa kunipa ushirikiano mkubwa na hivyo kunipa utulivu katika kusimamia majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nawashukuru sana waajiri wangu, wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kushirikiana nami kwa maendeleo ya Wilaya yetu ya Karagwe.

**Mapitio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2024/25**

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya jumla ya Shilingi trilioni 1.71. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 870.43 ni za Mishahara, Shilingi bilioni 551.58 za Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 289.69 za Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, Shilingi bilioni 285.63 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 4.06 ni fedha za nje.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya Shilingi trilioni 1.57 zimepokelewa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kutoka Wizara ya Fedha. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 684.68 ni kwa ajili ya Mishahara, Shilingi bilioni 502.92 ni za Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 384.58 za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizopokelewa ni sawa na asilimia 91.85 ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali**

**12.** *Mheshimiwa Spika,* katika mwaka 2024/25 Wizara ina lengo la kukusanya maduhuli ya Serikali ambayo ni jumla ya Shilingi bilioni 403.30. Hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya Shilingi bilioni 318.53 zimekusanywa sawa na asilimia 78.98 ya lengo.

## B. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26

### Mafanikio yaliyopatikana katika Mwaka 2024/25

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

### Mafanikio ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya watu 844,994 walisajiliwa na kutambuliwa. Idadi hii imeongeza watu waliosajiliwa na kutambuliwa tangu kuanza kwa usajili na utambuzi kufikia watu 25,854,970 sawa na asilimia 81.9 ya watu 31,582,976 wenye umri kuanzia miaka 18 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022. Wizara imedhamiria kukamilisha usajili wa watu takribani milioni sita katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2025/26 – 2027/28.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, jumla ya Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) 757,189 zilizalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Hivyo, kufanya jumla ya NIN zilizozalishwa kufikia 21,514,741 sawa na asilimia 83.2 ya idadi ya watu waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili na utambuzi wa watu nchini. Namba za utambulisho (NIN) 17,879 ambazo bado hazijazalishiwa vitambulisho zinatarajiwa kukamilishwa kabla ya Juni 2025.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuzalisha jumla ya Vitambulisho vya Taifa 1,243,105 na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,308,774 sawa na asilimia 99 ya idadi ya Namba za Utambulisho 21,514,741 zilizozalishwa. Aidha, kwa kipindi hicho jumla ya Vitambulisho vya 1,092,160 vimesambazwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyosambazwa kufikia 21,191,598.

**Mafanikio ya Jeshi la Polisi**

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, nchi yetu imeendelea kudumisha amani, utulivu na usalama, hivyo kufanya nchi yetu kuwa kivutio kwa wawekezaji na wageni. Hali hiyo inatokana na Jeshi la Polisi kushirikiana na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama.

**18.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 makosa makubwa ya jinai yalitolewa taarifa katika vituo vya Polisi yalikuwa makosa 40,022 ikilinganishwa na makosa 43,147 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24. Hivyo, makosa 3,125 yamepungua sawa na asilimia 7.2.

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya magari 218 yamepokelewa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya matumizi ya Makamishna, Naibu Kamishna, Makamanda wa Polisi wa Mikoa/Vikosi, Wakuu wa Polisi Wilaya na Vitengo ndani ya Jeshi la Polisi, pamoja na pikipiki 105 za Polisi Kata na Shehia. Upatikanaji wa magari na pikipiki utaimarisha utolewaji wa huduma kwa wananchi.

**Mafanikio ya Jeshi la Magereza**

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imefanikiwa kuondoa changamoto ya msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani. ***Hata hivyo, kupitia juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita msongamano wa wafungwa na mahabusu magerezani umepungua kutoka 33,7640 mwaka 2020/21 hadi kufikia 27,088 mwezi Aprili 2025. Hii inaonesha wafungwa na mahabusu 6,676 wamepungua magerezani, sawa na asilimia 20 ya uwezo wa kisheria wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902.***

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Jeshi la Magereza imefanikiwa kutumia nishati safi katika magereza yote 129 kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 100 ya lengo ya kupeleka nishati safi kwa magereza yote nchini. ***Namshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa***

***maelekezo yake juu ya matumizi ya nishati safi ambayo yamewezesha Jeshi la Magereza kupata mafaniko haya.***

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuanza kutumia huduma ya mahakama mtandao ambayo kwa sasa inatolewa kwenye magereza 66 kati ya 129. Aidha, huduma ya mahakama mtandao kwa magereza 63 yaliyobaki itakamilika mwaka 2028/29. Utolewaji wa huduma hiyo umesaidia kuharakisha usikilizaji wa mashauri ya mahabusu, kupunguza gharama kwa Serikali katika usafirishaji wa wafungwa na mahabusu, kuokoa muda wa kusikilizwa mashauri ya wafungwa na mahabusu na upatikanaji wa haki kwa wakati, kuboresha hifadhi na kumbukumbu za mashauri.

**Mafanikio ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni kutekelezwa kwa mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100. Hadi kufikia Aprili 2025 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepokea magari 40 ya kubebea majeruhi wa majanga, magari 30 ya mawasiliano na kuongoza operesheni za kuzimamoto na uokoaji, karakana sita (6) zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo.

**Mafanikio ya Idara ya Uhamiaji**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia huduma za uhamiaji imewezesha uingiaji wa wageni kuongezeka kufikia 1,839,342 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 ikilinganishwa na wageni 511,243 walioingia nchini kwa kipindi kama hicho mwaka 2020/21. ***Hizi ni juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kupitia mikakati mbalimbali ikiwemo Filamu ya Royal Tour.***

**Ongezeko la Bajeti**

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 939.08 mwaka 2021/22 hadi kufikia Shilingi trilioni 2.06 mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 120. ***Namshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuongeza bajeti ya Wizara ambayo imeendelea kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wananchi.***

**Mafunzo na Upandishaji Vyeo**

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imeweza kutoa mafunzo kwa jumla ya Maafisa, Wakaguzi, Askari na Watumishi raia 15,800 ndani na nje ya nchi; na kupandishwa vyeo Maafisa, Wakaguzi na Askari 20,706 katika ngazi mbalimbali. Mafunzo hayo na upandishwaji vyeo umesaidia kuongeza morali ya utendaji kazi na ufanisi.

**Uzinduzi wa Mikakati ya Mawasiliano ya Wizara**

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kuzindua Mikakati sita (6) ya Mawasiliano ambayo imeanza kutekelezwa kuanzia mwaka 2024/25 – 2025/26. Mikakati hiyo ilizinduliwa tarehe 09 Januari 2025 kwa lengo la kuimarisha utolewaji wa elimu na taarifa kwa umma.

**Maeneo ya Kipaumbele katika Bajeti ya Mwaka 2025/26**

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itatekeleza maeneo matano (5) ya kipaumbele yafuatayo:

i. Kuendelea kudumisha usalama wa raia na mali zao;
ii. Kuendelea na utekelezaji wa maelekezo ya Mhe. Rais kuhusu Tume ya Haki Jinai;
iii. Kuboresha na kujenga miundombinu ya ofisi na makazi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari;
iv. Kuimarisha na kuboresha huduma za Uhamiaji Mtandao; na
v. Kuanza zoezi la usajili na utambuzi wa watu chini ya umri wa miaka 18.

**Upandishaji Vyeo**

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imewapandisha vyeo jumla ya watumishi 20,706 katika ngazi mbalimbali za uongozi. Kati ya hao, watumishi 52 wa Makao Makuu ya Wizara, watumishi 16,896 ni wa Jeshi la Polisi, 518 wa Jeshi la Magereza, 1,120 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 1,745 wa Idara ya Uhamiaji na 375 wa NIDA. Upandishwaji vyeo umeongeza morali na ufanisi katika utendaji kazi kwa watumishi.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara itawapandisha vyeo jumla ya watumishi 12,272. Kati ya hao, watumishi 123 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 8,325 wa Jeshi la Polisi, 3,551 wa Jeshi la Magereza, 48 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 166 wa Idara ya Uhamiaji na 59 wa NIDA.

**Ajira kwa Askari na Watumishi Raia**

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imeajiri jumla ya watumishi 19,411. Kati ya watumishi hao, 49 wa Makao Makuu ya Wizara, 17,605 Jeshi la Polisi, 725 Jeshi la Magereza, 425 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 558 Idara ya Uhamiaji na 49 NIDA.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatarajia kuajiri watumishi 7,666 kwa mwaka 2025/26. Kati ya hao, watumishi 56 wa Makao Makuu ya Wizara, 5,237 Jeshi la Polisi, 766 Jeshi la Magereza, 1,000 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 457 Idara ya Uhamiaji na 150 NIDA.

**Mafunzo kwa Watumishi**

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara imewezesha mafunzo ya kuwajengea uwezo jumla ya maafisa, askari na watumishi raia 15,849 ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 166 ni wa Makao Makuu ya Wizara, 11,268 Jeshi la Polisi, 789 Jeshi la Magereza, 1,446 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 2,104 Idara ya Uhamiaji na 76 NIDA. Mafunzo hayo yameboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Wizara.

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara imetenga jumla ya Shilingi bilioni 34.88 ili kuwezesha mafunzo kwa watumishi 30,879. Kati ya hao, watumishi 138 ni wa Makao Makuu ya Wizara; 22,500 Jeshi la Polisi, 3,241 Jeshi la Magereza, 2,347 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, 2,611 Idara ya Uhamiaji na 42 wa NIDA.

**Maeneo ya Ujenzi wa Ofisi, Vituo na Makazi**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Shilingi bilioni 1.20 zimepokelewa na Wizara kwa ajili ya upatikanaji wa maeneo 177. Kati ya maeneo hayo 117 ya Jeshi la Polisi, 23 ya Jeshi la Magereza, saba (7) ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 30 ya Idara ya Uhamiaji. Maeneo hayo ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, vituo na makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi bilioni 2.04 zimetengwa kwa mwaka 2025/26 ili kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi, vituo na makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari. Kati ya fedha hizo Shilingi milioni 532.45 za Jeshi la Polisi, Shilingi milioni 795.76 za Jeshi la Magereza, Shilingi milioni 600 za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Shilingi milioni 120 za Idara ya Uhamiaji.

**Makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya Shilingi bilioni 18.85 zimepokelewa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 14.71 ni za Jeshi la Polisi ambapo Shilingi bilioni 14.07 ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari na Shilingi milioni 641.59 za ukarabati wa nyumba za makazi na Shilingi milioni 147.88 za Jeshi la Magereza za ujenzi wa nyumba tano (5) za Askari Gereza Kalilankulukulu mkoani Katavi.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Shilingi bilioni 2.50 ni kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo mawili (2) ya ghorofa ya makazi ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Kikombo Jijini Dodoma na Shilingi bilioni 1.50 za ujenzi wa ghorofa moja (1) la makazi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Idara ya Uhamiaji Msalato Jijini Dodoma. Ujenzi huo utaongeza morali katika utendaji kazi kwa watendaji hao.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 22.50 zimetengwa katika mwaka 2025/26 kwa ajili ya ukamilishaji na uanzishaji wa ujenzi mpya wa Makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari wa Jeshi la Polisi. Kati ya fedha hizo Shilingi milioni 139 ni kwa ajili ya ujenzi wa *rest house*, Shilingi milioni 86.67 za ukarabati wa nyumba za kuishi familia za Askari na Shilingi bilioni 22.28 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za kuishi familia za Askari, mabweni ya wanafunzi na watumishi katika vyuo vya mafunzo ya Polisi Tanzania.

**JESHI LA POLISI**

**Hali ya Usalama Nchini**

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama limefanya doria, misako na operesheni za kubaini, kuzuia, kutanzua na kupambana na uhalifu nchini ikiwemo kwenye barabara kuu na mipakani. Ushirikiano huo umewezesha kudumisha amani na utulivu, hivyo kuifanya nchi yetu kuendelea kuwa kivutio kwa wawekezaji na watalii. Aidha, elimu kwa umma juu ya utekelezaji wa dhana ya ulinzi shirikishi katika kupambana na uhalifu imetolewa.

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi husika makosa makubwa ya jinai 40,022 yalitolewa taarifa katika vituo vya Polisi nchini ikilinganishwa na makosa 43,147 yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24. Takwimu hizi zinaonesha kuwa makosa 3,125 yamepungua sawa na asilimia 7.2. Kupungua kwa makosa hayo kunatokana na elimu inayotolewa kwa jamii, doria, misako na operesheni zinazofanywa kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, operesheni nyingine zilizofanyika ni kudhibiti uhalifu wa matumizi ya silaha ambapo silaha 184 na risasi 429 zilikamatwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025. Silaha hizo ni *Shortgun* 23, bastola 10, *rifle* nne (4), *Mark IV* tatu (3) na Magobole 144. Aidha, nyara za Serikali 2,092 zenye uzito wa kilogramu 23,459.75 zilikamatwa na watuhumiwa 769 walifikishwa mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

**Uhalifu wa Kimtandao (Cyber Crimes)**

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, uhalifu wa kimtandao umekuwa tishio duniani na hapa nchini kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi April 2025, jumla ya makosa 748 yaliripotiwa katika Vituo vya Polisi ikilinganishwa na makosa 865 yaliyoripotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Makosa 117 yamepungua sawa na asilimia 13.5. Kupungua kwa makosa hayo kunatokana na operesheni, kuimarishwa kwa doria mtandaoni (On line Patrol) pamoja na elimu inayoendelea kutolewa kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya mitandao.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, operesheni iliyofanywa na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) katika Mikoa ya Morogoro (Ifakara), Rukwa (Sumbawanga), Dar es Salaam (Kinondoni na Ilala), Mbeya (Mbeya Mjini), Arusha (Arusha Mjini) na Singida (Singida Mjini) iliwezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 66. Aidha, mashauri 50 yalifunguliwa kutokana na operesheni hiyo, ambapo mashauri 34 yako mahakamani na mashauri 16 yako chini ya upelelezi. ***Natoa pongezi kwa Jeshi la Polisi kwa kufanya operesheni hiyo na ninaagiza iwe endelevu. Aidha, natoa onyo kwa watu kujiepusha na uhalifu huo.***

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya uhalifu wa kifedha Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na taasisi nyingine ikiwemo TCRA limeendelea kuchukua hatua za kudhibiti vitendo hivyo. Hatua hizo zimewezesha uhalifu wa kifedha kupungua kwa makosa 90 kutoka makosa 802 mwaka 2023/24 hadi 636 mwaka 2024/25 sawa na asilimia 11.2. Hatua nyingine ni Jeshi la Polisi kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa, kuwapatia mafunzo watendaji ili kuendana na teknolojia na kutoa elimu kwa umma kuhusu uhalifu wa kifedha kwa kutumia mitandao ya simu na ya kijamii.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na uhalifu wa kifedha na kuondoa changamoto hiyo kwa wananchi katika mwaka 2025/26 Jeshi la Polisi litaendelea kuwajengea uwezo watendaji waliopo Kitengo cha Upelelezi wa Uhalifu wa Kifedha (FCU), kuimarisha ushirikiano na wadau, matumizi ya vifaa vya kisasa na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa za nywila. Aidha,

Shilingi bilioni 2.3 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia upatikanaji wa taarifa za upelelezi wa makosa ya jinai sanjari na kufanya operesheni za uhalifu wa kifedha.

**Usalama Barabarani**

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, takwimu zinaonesha katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Aprili, 2025, jumla ya matukio 1,322 yameripotiwa katika Vituo vya Polisi ikilinganishwa na matukio 1,463 yaliyoripotiwa kipindi kama hicho cha mwaka 2023/24. Hii inaonesha matukio 141 yamepungua sawa na asilimia 9.6. Aidha, katika kipindi hicho watu waliokufa kutokana na ajali ni 1,275 ikilinganishwa na idadi ya watu 1,408 waliokufa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2023/24. Hivyo, idadi ya watu waliokufa kwa ajali za barabarani imepungua kwa watu 133 sawa na asilimia 9.4.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, watu 2,278 walijeruhiwa kutokana na ajali kwa kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Aprili 2025, ikilinganishwa na watu 2,166 waliojeruhiwa kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2023/24. Hili ni ongezeko la watu 112 sawa na asilimia 5.2. Mikakati ya Jeshi la Polisi katika kudhibiti matukio ya ajali barabarani ni ifuatayo:

**a) Kutoa elimu kwa wananchi:** Kuendelea kutoa elimu kuhusu usalama barabarani kwa madereva, waendesha baiskeli na watembea kwa miguu katika matumizi sahihi ya barabara wakati wote. Elimu hiyo itatolewa katika maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu ikiwemo mikutano ya jamii, vituo vya usafiri vya mabasi, treni, teksi na bodaboda. Elimu hiyo pia itaendelea kutolewa kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii na tovuti.

**b) Mafunzo kwa Madereva**: kuendelea kuimarisha na kusimamia mafunzo kwa madereva wapya na kutoa mafunzo ya ziada kwa madereva waliopo kazini kuhusu sheria na kanuni za barabarani.

**c) Kuendelea kuboresha miundombinu:** kuendelea kutoa ushauri kwa sekta ya umma na sekta binafsi katika kujenga barabara salama na kuboresha alama na taa za barabarani, kujenga madaraja ya waenda kwa miguu na vidhibiti mwendo kama matuta.

**d) Kuimarisha utekelezaji wa sheria:** kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa magari ili kuhakikisha yanafuata viwango vya usalama na kufuata kanuni, sheria na taratibu za usalama barabarani. Pia, kuchukua na kusimamia sheria na adhabu kali kwa madereva wasiozingatia sheria za barabarani kama vile kuendesha kwa kasi, ulevi na matumizi ya simu wakati wa kuendesha vyombo vya moto, sambamba na kuendelea kufanya doria za masafa marefu (High way Patrol).

**e) Kuwekeza katika TEHAMA na Teknolojia:** kutumia teknolojia ya GPS kufuatilia mienendo ya magari yanapokuwa barabarani na kutoa taarifa za papo hapo za hali ya barabara. Vilevile, kuweka kamera za usalama barabarani katika maeneo muhimu ili kufuatilia mienendo ya madereva na kudhibiti ukiukaji wa sheria.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu matumizi ya teknolojia katika kupambana na ajali barabarani pamoja na uhalifu kwa ujumla ni kama ilivyoelezwa kwa kina katika Aya ya 42 – 45 ya Hotuba.

**Ushirikishwaji wa Wananchi katika Kubaini, Kuzuia na Kutanzua Uhalifu**

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, changamoto zinazokabili utekelezaji wa dhana ya Polisi Jamii nchini Tanzania ni pamoja na: uelewa mdogo wa dhana ya Polisi Jamii kwa wananchi na kusababisha ushiriki mdogo kutoka kwa jamii katika kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu; uhaba wa askari, upungufu wa vitendea kazi ikiwemo magari na pikipiki.

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Jeshi la Polisi limetoa elimu kuhusu kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Elimu hiyo imetolewa kwa wananchi 7,261,728 wakiwemo mabalozi wa amani, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Serikali za Mitaa, wawakilishi wa vikundi vya ulinzi shirikishi, wanawake, vijana na kundi la watu wenye mahitaji maalum.

**52.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mafunzo ya awali ya Utangulizi wa Mahojiano ya Kisayansi kwa Wanawake na Watoto yametolewa kwa watendaji 60 wa dawati la jinsia na watoto ili kuwajengea uwezo wa kushughulikia matukio ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto. Mafunzo hayo yamefadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Aidha, Jeshi la Polisi limefanya mapitio ya mitaala ya kufundishia na kujifunzia somo la kuzuia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kudhibiti mmomonyoko wa maadili na ukatili dhidi ya watoto, Jeshi la Polisi limezindua rasmi kampeni ya **"Tuwaambie kabla hawajaharibiwa"** tarehe 18 Agosti 2024. Hadi kufikia Aprili 2025 kampeni hiyo imewafikia jumla ya wanafunzi 196,458 ili kuwajengea uelewa na uwezo wa kubaini viashiria vya ukatili wa kijinsia na makosa mengine wanapokuwa katika mazingira mapya. Kati ya hao wanafunzi 86,935 ni wa kidato cha kwanza, 62,411 wa kidato cha tano na 47,112 wa mwaka wa kwanza wa elimu ya vyuo vikuu na vyuo vya kati.

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi limeratibu ushiriki wa watendaji 19 katika mkutano wa shirikisho la Askari wa kike na wasimamizi wa sheria duniani uliofanyika Oktoba 2024 katika Jiji la Chicago, Marekani. Vilevile, watendaji 20 walipata mafunzo nchini Ujerumani kuhusu masuala ya kuzuia na kupambana na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto. Pia, Jeshi limezindua mradi uitwao "**Jamii Shirikishi katika Uzalendo na Ulinzi**" uliofanyika mkoani Lindi kwa lengo la kuwashirikisha wananchi wazalendo kwenye ulinzi na usalama.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Jeshi la Polisi litaendelea kuwashirikisha wananchi ili kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu katika maeneo yao. Aidha, Shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo kwa watendaji ikiwemo kutoa elimu kuhusu namna ya kushughulikia ukatili wa kijinsia na unyanyasaji kwa wanawake na watoto. Shilingi milioni 18.50 zimetengwa kugharamia vipindi vya kuelimisha umma kupitia redio na runinga na kuendelea kushirikisha wadau katika kufadhili mafunzo, warsha na makongamano.

**Ulinzi wa Amani Nje ya Nchi**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Jeshi la Polisi limeshiriki katika operesheni za ulinzi wa amani nje ya nchi ambapo Askari 41 wapo misheni zifuatazo: UNMISS 19 na UNISFA watatu (3) – Sudani Kusini; MONUSCO 18 – Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC); na MINUSCA mmoja (1) – Afrika ya Kati. Ushiriki endelevu katika kazi za Ulinzi wa Amani nje ya nchi unawawezesha Askari kuongeza ujuzi, uzoefu na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika mwaka 2025/26, Jeshi la Polisi litaendelea kutoa nafasi kwa Askari kushiriki katika operesheni za ulinzi wa amani nje ya nchi.

**Ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mfuko wa Tuzo na Tozo, ujenzi wa ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa unaendelea, ambapo Mkoa wa Manyara umefikia asilimia 67, Geita asilimia 95 na Mtwara asilimia 78. Miradi hiyo imepangwa kukamilika ifikapo Julai 2025. Vilevile, ujenzi wa ofisi za Makamanda wa Mikoa ya Rufiji, Songwe na Simiyu umeanza na unaendelea. Miradi hii yote imepokea jumla ya Shilingi bilioni 1.60 mwezi Aprili 2025.

**58.** *Mheshimiwa Spika,* ukarabati ofisi ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Ziwani Mkoa wa Mjini Magharibi umekamilika kwa gharama ya Shilingi milioni 113.14. Aidha, Shilingi milioni 875.27 zimetumika kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Kikosi cha Kutuliza Ghasia Madengi Hill Jijini Dodoma. Pia, Shilingi milioni 48 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

**Ujenzi, Ukarabati wa Majengo na Vituo vya Polisi**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi na ukarabati wa vituo 31 vya Polisi unaendelea kwa gharama za Shilingi bilioni 5.52 kama ifuatavyo: Vituo vitatu (3) vya Daraja 'A' kwa gharama ya Shilingi milioni 850; Vituo sita (6) vya Daraja 'B' kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.16; na Vituo 22 vya Daraja 'C' kwa gharama ya Shilingi bilioni 2.51. Aidha, ukarabati umefanyika katika Kituo cha Polisi Daraja 'A' Mkoa wa Tabora kwa gharama ya Shilingi milioni 100. Pia, Shilingi milioni 65 zimepokelewa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Polisi Daraja 'B' Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, Jeshi la Polisi limekamilisha ukarabati wa jengo la ghorofa mbili Kambi ya Ziwani Mkoa wa Mjini Magharibi kwa gharama ya Shilingi milioni 182.19, ghorofa mbili Kambi ya Oysterbay – Dar es Salaam kwa gharama ya Shilingi milioni 50, ghorofa tatu Kambi ya barabara ya Kilwa katika Mkoa wa kipolisi Temeke kwa gharama ya Shilingi milioni 101.9, ukumbi wa mikutano Mkoa wa Dodoma kwa gharama ya Shilingi milioni 382.1 na maktaba ya Chuo cha Polisi Zanzibar - Shilingi milioni 100.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa miradi ifuatayo unaendelea: ghorofa moja la kuishi Askari 12 na familia zao katika Shule ya Polisi Moshi kwa gharama ya Shilingi milioni 475; Zahanati ya Polisi Mkoa wa Songwe – Shilingi milioni 330; jengo la Idara ya wagonjwa wanaotibiwa na kuondoka (OPD) katika Hospitali ya Rufaa ya Jeshi la Polisi barabara ya Kilwa Dar es Salaam – Shilingi milioni 528; na jengo la TEHAMA Makao Makuu Dodoma – Shilingi milioni 300. Pia, Shilingi milioni 58 zimetumika kukarabati jengo la ofisi ya kushughulikia makosa ya kimtandao (Cyber Crime) Dar es Salaam na Shilingi milioni 58 zimetumika kukarabati Ofisi za uchunguzi wa vinasaba (DNA).

**Upatikanaji wa Vitendea Kazi**

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa wananchi, Jeshi la Polisi limepokea Shilingi bilioni 34.78 kwa ajili ya ununuzi wa magari 275 ya Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Wakuu wa Vikosi vya Kutuliza Ghasia na Wakuu wa Upelelezi wa Wilaya taratibu za ununuzi zinaendelea. Magari hayo yanatarajiwa kupokelewa mwishoni mwa mwezi Juni 2025. Upatikanaji wa magari hayo mapya na ya kisasa yataendelea kurahisisha utendaji kazi wa Jeshi ikiwemo kufanya doria za masafa marefu ili kuzuia matukio ya usalama barabarani na makosa ya jinai, kuharakisha upelelezi wa kesi na kuwewezesha Maafisa na Askari kuwahi kwenye maeneo ya matukio (Crime scene).

**63.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Jeshi la Polisi ilipokea magari 218 kwa ajili ya matumizi ya Makamishna, Naibu Kamishna, Makamanda wa Polisi wa Mikoa/Vikosi, Wakuu wa Polisi Wilaya na Vitengo ndani ya Jeshi la Polisi pamoja na pikipiki 105 za Polisi Kata na

Shehia. Pikipiki na magari hayo yalipokelewa mwezi Machi na Aprili 2025.

**64. Mheshimiwa Spika,** pia Jeshi la Polisi limetumia Shilingi bilioni 13.74 kwa ajili ya ununuzi wa redio 6,010 za masafa marefu na mafupi (radio calls) na Shilingi bilioni 7 zimetumika kununua vifaa vya mradi wa alama za vidole *Automated Fingerprint Informan System (AFIS)*.

**65. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Jeshi la Polisi limepokea Shilingi bilioni 12.47 kwa ajili ya ununuzi wa sare za Maafisa, Wakaguzi na Askari pamoja na ununuzi wa vifaa vya ushonaji. Upatikanaji wa sare hizo utaendelea kuimarisha na kuongeza ari ya utendaji kazi sanjari na kuongeza unadhifu. Aidha, kamera za *video* za Wakuu wa Uchunguzi wa Kisayansi wa Mikoa katika mikoa 35 zimenunuliwa kwa gharama ya Shilingi milioni 495. Upatikanaji wa vifaa hivyo utaimarisha utolewaji wa huduma kwa wananchi.

**Upimaji wa Viwanja kwa Maeneo ya Polisi**

**66. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Jeshi la Polisi limepima na kulipa fidia katika maeneo saba (7) yenye mita za mraba 372,427.16 kwenye Mikoa ya Shinyanga na Dodoma kwa gharama ya Shilingi milioni 659. Upatikanaji wa maeneo hayo utawezesha kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi na makazi kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari. Aidha, itasaidia kuepusha migogoro ya ardhi kati ya Jeshi la Polisi na wananchi. Katika mwaka 2025/26, Jeshi la Polisi limetenga Shilingi milioni 532.45 kwa ajili ya kupima viwanja, kupata maeneo mapya na kulipa fidia.

**Fidia na Matibabu kwa Askari**

**67. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25 Jeshi la Polisi limetumia Shilingi milioni 520.81 kutoka katika Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa ajili ya kugharamia matibabu yasiyo kwenye bima ya afya kwa Askari 17 na familia zao sanjari na kulipia fidia kwa Askari 66 walioumia na wengine kufariki wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kazi. Kupitia Mfuko huo maisha yameokolewa kwa baadhi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari waliohitaji matibabu ya haraka. Pia, limeendelea kutia hamasa na kuleta ufanisi wa kutekeleza majukumu ya Jeshi la Polisi.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Jeshi la Polisi limetenga Shilingi bilioni 2.70 katika Mpango wa Matumizi wa Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa ajili ya kugharamia matibabu ya Askari na familia zao pamoja na fedha za kulipa fidia kwa Askari watakaoumia au kufariki wakiwa wanatekeleza majukumu ya Jeshi la Polisi.

**Miradi ya kipaumbele ya Jeshi la Polisi katika Mwaka 2025/26**

**69.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Jeshi la Polisi litaendelea na utekelezaji wa miradi ya kipaumbele ifuatayo: ujenzi wa ofisi na nyumba za makazi ya askari – Shilingi bilioni 10.30; ukarabati wa nyumba za askari – Shilingi milioni 86.67; ujenzi wa vituo vya polisi – Shilingi milioni 868.51; umaliziaji wa ujenzi wa Zahanati ya Polisi Mkoa wa Njombe - Shilingi milioni 150; ujenzi wa mabweni na madarasa katika shule na vyuo vya Polisi nchini – Shilingi bilioni 15.92; na ununuzi wa vitendea kazi – Shilingi bilioni 194.95.

**SHIRIKA LA UZALISHAJI MALI LA JESHI LA POLISI**

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi limeendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, huduma na biashara. Lengo ni kuendelea kuboresha miundombinu ya Jeshi la Polisi ili liendelee kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi. Miradi hiyo ni pamoja na: a) Mradi wa Miji Salama (Safer Cities)

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya utekelezaji wa Mradi wa Miji Salama awamu ya kwanza yamekamilika ikiwemo kubainisha maeneo yatakayofungwa kamera 4,100 katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Dodoma. Mradi utagharimu Dola za Marekani milioni 145.2 na hadi kufikia Aprili 2025 Dola za Marekani milioni 80 sawa na takribani Shilingi bilioni 231.07 zimetolewa kwa Shirika hilo kupitia mkopo wa gharama nafuu kutoka Abu Dhabi Exports Office (ADEX). Fedha hizo zitatumika kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi katika mikoa hiyo mitatu (3).

**a) Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Vyombo vya Moto**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa kwa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) baada ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura ya 103 ya

mwaka 2023. Taratibu za kumpata mbia zimekamilika na mkataba wa utekelezaji unatarajiwa kusainiwa katika mwaka 2025/26.

**73.** ***Mheshimiwa spika,*** mradi utahusu ujenzi wa vituo vya kisasa vya ukaguzi wa vyombo vya moto ikiwemo vituo hamishika vitano (5). Mradi utagharimu wastani wa Dola za Marekani milioni 116.94 sawa na takribani Shilingi bilioni 298.80.

**b) Mradi wa Highway Patrol**

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wabia wa sekta binafsi linatarajia kuwekeza katika miundombinu ya kidijitali itakayoweza kubaini makosa ya usalama barabarani katika barabara kuu nchini. Lengo la mradi huu ni kubaini makosa ya usalama barabarani yanayosababishwa na tabia za kibinadamu. Mradi utatekelezwa kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza itahusisha barabara ya Dar es Salaam (Kijazi interchange) hadi Dodoma (Bunge). Katika awamu hii jumla ya Dola za Marekani milioni 19.94 sawa na takribani Shilingi bilioni 50.95 zinatarajiwa kutumika. Mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka 2025/26.

**Mafunzo ya Umahiri wa Matumizi ya Silaha za Moto**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, Shirika limetoa mafunzo ya umahiri kwa wamiliki wa silaha binafsi, taasisi na kampuni za ulinzi kwa mujibu wa Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi, Sura ya 223 na Kanuni zake za mwaka 2016. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya wamiliki 1,700 wamepatiwa mafunzo nchi nzima. Katika mwaka 2025/26 mafunzo hayo yataendelea kutolewa ili kuwapatia wamiliki weledi na namna bora ya matumizi ya silaha ili zisilete madhara kwa jamii.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Shirika limefanya shughuli za kibiashara ikiwemo kutoa huduma ya usafirishaji wa magari kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda kwenye bandari kavu, huduma ya ulinzi, shughuli za ushonaji wa sare na usindikizaji wa fedha na vito vya thamani. Shughuli hizo zimewezesha kupatikana kwa mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 1.75. Katika mwaka 2025/26

Shirika litaendelea na biashara hizo kwa kukuza wigo wa kazi ili kuongeza mapato.

## JESHI LA MAGEREZA

### Hali ya Ulinzi na Usalama Magerezani

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kupokea, kuhifadhi na kuwahudumia wafungwa na mahabusu wanaoletwa magerezani kwa mujibu wa sheria. Kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, magereza yote nchini yalihifadhi jumla ya wafungwa na mahabusu 27,088. Kati ya idadi hiyo, wafungwa walikuwa 19,400 na mahabusu 7,688.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** hayo ni mafanikio makubwa ya kupungua kwa msongamano magerezani kwa asilimia 20 ikilinganishwa na wafungwa na mahabusu 33,764 waliokuwepo magerezani kwa miaka mitano (5) iliyopita (2020/21 – 2024/25). Kupungua kwa msongamano magerezani kumechangiwa na jitihada za Serikali zikiwemo:

### a) Matumizi ya Adhabu Mbadala

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya adhabu mbadala yamesaidia kuleta mabadiliko chanya ya tabia kwa wafungwa na kupunguza msongamano magerezani. Kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, wafungwa 230 wamenufaika kupitia utaratibu wa *parole* na 1,415 kupitia Kifungo cha Nje (Extra Mural Labour – EML).

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma ya *parole* imeimarishwa kwa kutoa elimu kwa wajumbe 33 wa Bodi za *Parole* za Mikoa na jamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Katika mwaka 2025/26, Shilingi milioni 445.2 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli za huduma za *parole* na kufanya maboresho ya Sheria ya Bodi za Msamaha wa Wafungwa, Sura ya 400.

### b) Msamaha kwa Wafungwa

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa msamaha wa wafungwa katika Maadhimisho ya

Sherehe ya Miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika yaliyofanyika tarehe 9 Desemba 2024 na Miaka 61 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar yaliofanyika tarehe 26 Aprili, 2025.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** msamaha huo umenufaisha wafungwa 6,435 waliokuwa magerezani ambapo wafungwa 64 waliachiwa huru na wafungwa 6,371 walipunguziwa sehemu ya adhabu ya vifungo vyao na kuendelea kubaki magerezani kumalizia adhabu zao.

**Kuimarisha Ulinzi na Usalama Magerezani**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi milioni 274.79 zimepokelewa mwezi Aprili 2025 kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa usimamizi wa taarifa za wafungwa magerezani na kazi ya ukusanyaji wa taarifa zitakazotumika kwenye mfumo huo umefanyika. Aidha, Shilingi milioni 89.66 zimepokelewa mwezi Aprili 2025 kwa ajili ya ununuzi na ufungaji wa vifaa vya ufuatiliaji wa mienendo ya wafungwa na mahabusu magerezani. Mkandarasi wa mradi yupo eneo la mradi na shughuli za ufungaji wa vifaa vya mfumo huo unaendelea katika Gereza Lindi na Gereza Bukoba. Hatua hiyo ina lengo la kuleta ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa shughuli za magereza.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya TEHAMA yameimarishwa katika usikilizaji wa mashauri ya mahabusu kupitia huduma ya Mahakama Mtandao. Katika kuimarisha huduma hiyo Jeshi la Magereza limepokea makasha 10 kutoka Mahakama ya Tanzania. Makasha hayo yamefungwa vifaa vinavyowezesha utoaji wa huduma za Mahakama na yanatumika kama vyumba vya kutolea huduma hiyo kwenye magereza 10 yafuatayo: Arusha, Ukonga, Keko, Segerea, Butimba, Karanga, Maweni, Isanga, Ruanda na Uyui.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hii ni muendelezo wa kuimarisha huduma hiyo ambayo ilishaanza kutolewa katika vituo vya magereza 66 kati ya 129. Aidha, huduma ya mahakama mtandao kwa magereza 63 yaliyobaki itakamilika mwaka 2028/29. Pia, ni miongoni mwa utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Matumizi ya utekelezaji wa Huduma ya Mahakama Mtandao magerezani yamesaidia kuipunguzia gharama Serikali za

kuwasafirisha mahabusu na wafungwa kwenda mahakamani kwa kutumia magari.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** faida nyingine ni kuimarisha hali ya ulinzi na usalama magerezani na kuepusha hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa usafirishaji wa wafungwa na mahabusu kwa kutumia magari; kuokoa muda wa kusikilizwa mashauri ya wafungwa na mahabusu na upatikanaji wa haki kwa wakati; kuboresha hifadhi na kumbukumbu za mashauri; kupunguza matumizi ya rasilimaliwatu ambao wangetumika kusindikiza wafungwa na mahabusu kwenda mahakamani kusikiliza mashauri yao.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Shilingi bilioni 1.79 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika Jeshi la Magereza. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 1.30 ni kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wahalifu waliopo Magerezani, ununuzi na ufungaji wa vifaa vya ulinzi na usalama. Aidha, Shilingi milioni 491.80 ni za kugharamia uendeshaji wa huduma za TEHAMA na kuwezesha mafunzo ya wataalam 30.

**Maboresho ya Huduma za Urekebu**

**a) Urekebu kupitia Programu za Elimu, Stadi za Kazi na Ushirikiano na Taasisi za Elimu**

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za urekebu wa wafungwa magerezani zinatekelezwa kupitia programu za michezo, huduma za kiroho, ushauri wa kisaikolojia, elimu, kilimo na ufugaji. Vilevile, huduma hizo hutolewa kupitia stadi za kazi zinazohusisha shughuli za ujenzi na viwanda vidogo zinazotekelezwa magerezani.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza limeanza kutumia fursa za programu ya urasimishaji wa ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo. Programu hiyo inatolewa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA). Kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya wafungwa 201 wamenufaika na programu hiyo na kutunukiwa vyeti vya ujuzi katika fani za useremala (41), umeme tisa (9), ushonaji (68), uchomeleaji wa vyuma (11), ufundi magari sita (6), ujenzi (34), mapishi (30) na ufundi bomba wawili (2).

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hii ni miongoni mwa mafanikio ya maboresho ya Huduma za Urekebu ambazo zitasaidia utangamano wa wafungwa katika jamii. Aidha, maboresho hayo ni utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Haki Jinai kwa Jeshi la Magereza. ***Natoa rai kwa jamii kuwa tayari kuwapokea na kuwapa ushirikiano wafungwa wanaomaliza vifungo vyao***.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, hati ya makubaliano ya ushirikiano kati ya Jeshi la Magereza na Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) imesainiwa mwezi Desemba 2024. Ushirikiano huo ni katika nyanja za taaluma, ushauri, utafiti, kubadilishana uzoefu, programu za mafunzo kwa wafungwa, uimarishaji wa miundombinu pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia makubaliano hayo Chuo cha Taaluma ya Urekebu cha Magereza kwa kushirikiana na IAA kimeanza kutoa mafunzo ya shahada ya uzamili. Mafunzo hayo yanatolewa katika taaluma za ulinzi wa amani, usalama na stratejia, uongozi, sayansi ya kompyuta pamoja na ununuzi na ugavi ambapo jumla ya wanafunzi 106 wanaendelea na mafunzo.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, katika muendelezo wa utekelezaji wa makubaliano hayo, IAA imetoa kompyuta 25 na vitabu vya kielektroniki 706 kwa TCTA ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na usomaji. Aidha, programu maalumu ya mafunzo na elimu kwa wafungwa imeanza kutekelezwa katika Gereza Arusha kwa njia ya kidijitali. Jumla ya wafungwa 40 wanaendelea na mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Jeshi la Magereza kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi limesaini hati ya makubaliano na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ili kuimarisha programu za elimu ya msingi kwa wafungwa nje ya mfumo rasmi. Makubaliano hayo yanahusisha maeneo yafuatayo: mafunzo kwa walimu wawezeshaji wa program; uandaaji wa machapisho na miongozo ya uendeshaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi; na huduma za ushauri elekezi.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni utafiti na huduma za maktaba; utumiaji wa fursa za utaalam na nguvu kazi; na utambuzi wa programu za elimu msingi nje ya mfumo rasmi zinazotolewa na Jeshi la Magereza kwa wafungwa. Katika mwaka 2025/26, Shilingi milioni 87.30 zimetengwa ili kuwezesha uendeshaji wa programu ya urasimishaji wa ujuzi kwa wafungwa nje ya mfumo rasmi wa mafunzo.

**b) Urekebu Kupitia Shughuli za Kilimo na Viwanda**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 2.39 zimepokelewa Aprili 2025 kwa ajili ya uimarishaji wa shughuli za urekebu kupitia kilimo na viwanda. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 2.35 ni kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo zikiwemo matrekta saba (7), mashine za kupandia mpunga na mahindi tano (5), mashine ya kuvunia mahindi na mpunga mbili (2), mashine ya kuchakata alizeti moja (1) na mashine za kupulizia dawa tano (5). Matrekta na mashine hizo zitapokelewa ifikapo Juni 2025.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Shilingi bilioni 3.89 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Gereza Kitete – Rukwa, ununuzi wa zana na mitambo ya kilimo pamoja na kuwezesha mafunzo kwa maafisa kilimo saba (7) nchini Misri. Aidha, Shilingi milioni 197.19 zimetengwa kwa ajili ya kufanya ukarabati wa miundombinu ya jengo la karakana Gereza Wami Vijana.

**c) Maboresho ya Mitaala na Mafunzo ya Huduma za Urekebu kwa Watumishi**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Chuo cha Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima limeandaa mitaala mipya 10 ya mafunzo ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada. Mitaala hiyo imeidhinishwa na NACTVET kuanza kutumika katika vyuo vya magereza kuanzia mwaka wa masomo 2025/26. Aidha, mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi 32 wa vyuo vya magereza kuhusu matumizi ya mitaala hiyo yamefanyika. Katika mwaka 2025/26 Shilingi milioni 48.60 zimetengwa kwa ajili ya mafunzo na ununuzi wa vifaa vya kufundishia.

**Kubadilishana Ujuzi na Taasisi Nyingine za Urekebu Nje ya Nchi**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho ya huduma za magereza yanahusisha kujifunza kutoka mataifa mengine yaliyofanikiwa katika utoaji wa huduma za urekebu. Maafisa na Askari 24 wa Jeshi la Magereza wapo nchini Shelisheli kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu wa uendeshaji wa shughuli za magereza. Vilevile, Maafisa wawili (2) wanatekeleza jukumu la ulinzi wa amani katika nchi ya Sudani Kusini – UNMISS na Somalia – UNMIT.

**Matumizi ya Nishati Safi Magerezani**

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Magereza imefanikiwa kutumia nishati safi badala ya kuni kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa katika magereza yote 129. Mafanikio hayo yametokana na jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu katika kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034. Hatua hiyo imesaidia kuimarisha utunzaji wa mazingira kwa kuokoa mita za ujazo za kuni 30,000 ambazo zingetokana na uvunaji wa misitu.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025 Shilingi bilioni 2.77 zimepokelewa kutoka REA kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa matumizi ya nishati safi. Fedha hizo zitatumika kujenga mifumo 18 ya gesi vunde, ununuzi wa vyungu vya kupikia 107, ujenzi wa mifumo 12 ya LPG, uimarishaji wa mfumo mmoja wa gesi asilia, uboreshaji wa majiko 76, ununuzi wa mkaa mbadala tani 80 na ununuzi wa mashine 61 za kutengeneza mkaa mbadala ambapo ujenzi wa mifumo 12 ya LPG tayari umefanyika. Aidha, Shilingi milioni 647.91 zimetumika kununua na kukarabati majiko na kulipia gharama za uendeshaji wa gesi.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha matumizi endelevu ya nishati safi, wataalam 135 wamepatiwa mafunzo kwa udhamini wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO). Aidha, jumla ya miti 2,000,000 itapandwa kwenye vituo mbalimbali vya magereza. Katika mwaka 2025/26, Shilingi bilioni 5.70 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa matumizi ya nishati safi.

**Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Magereza**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 3.37 zimepokelewa Aprili 2025 kwa ajili ya kazi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya magereza. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 1.78 ni kwa ajili ya ukarabati wa magereza mawili (2) Keko na Ukonga – Dar es Salaam, Shilingi bilioni 1.44 za kukamilisha ujenzi wa magereza mapya ya Karatu – Arusha na Kilosa – Morogoro na Shilingi milioni 147.88 kukamilisha nyumba tano (5) za Askari Gereza Kalilankulukulu – Katavi.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati mdogo wa magereza umefanyika katika magereza ya Kilwa – Lindi, Tukuyu – Mbeya, Manyoni – Singida, Wami Vijana – Morogoro na Gereza la Mahabusu Morogoro. Jumla ya Shilingi milioni 136.09 zimetumika katika ukarabati wa magereza hayo.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Shilingi bilioni 3.98 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa ofisi mbili (2) za Wakuu wa Magereza wa Mikoa ya Songwe na Geita. Fedha hizo pia zitatumika kuendeleza ujenzi wa magereza mapya ya Msalato – Dodoma, Kaliua – Tabora na Kingurungundwa – Lindi na kufanya ukarabati katika magereza ya Isanga – Dodoma, Uyui – Tabora, Ukonga – Dar es Salaam na Lilungu – Mtwara.

**HUDUMA ZA UANGALIZI WA WAFUNGWA WA VIFUNGO VYA NJE**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inaendelea kusimamia huduma za uangalizi wa wafungwa wa vifungo vya nje. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya Taarifa za Uchunguzi wa Kijamii 5,557 ziliwasilishwa Mahakamani. Taarifa hizo zimewezesha Mahakama kutoa uamuzi wa kuwaweka wafungwa kutumikia vifungo chini ya Sheria ya Huduma za Jamii Sura ya 291 na Sheria ya Kifungo cha Nje kwa Wahalifu Sura ya 247.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia taarifa hizo, jumla ya wafungwa 3,873 walihukumiwa kutumikia adhabu zao kwenye jamii, kati ya hao wanaume ni 3,091 na wanawake ni 782. Wafungwa 3,717 walimaliza

kutumikia vifungo vyao na kurudishwa kwenye jamii kuungana na familia zao. Kati ya hao wanaume ni 2,970 na wanawake 747.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na wafungwa hao kutekeleza adhabu nje ya Magereza, Serikali imeweza kuokoa wastani wa Shilingi bilioni 5.80 ambazo zingetumika kuwalisha wafungwa kama wangetumikia kifungo gerezani. Aidha, Serikali imeweza kuokoa jumla ya Shilingi bilioni 3.09 ambazo zingetumika kuwalipa vibarua kwa kufanya kazi kwenye Taasisi za Umma baada ya kazi hizo kufanywa na wafungwa wa vifungo vya nje.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** programu za urekebishaji wa tabia kwa wafungwa waliowekwa chini ya Sheria ya Huduma za Jamii na Sheria ya Kifungo cha Nje kwa Wahalifu zilifanyika kwa kuzingatia mahitaji ya kila mfungwa. Wafungwa 294 walifundishwa stadi za kazi na maisha na 18 walipewa ujuzi wa ujasiriamali wa biashara ndogondogo ikiwemo kilimo na uvuvi mwambao wa Ziwa Tanganyika mkoani Katavi.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia wafungwa 3,645 walipewa ushauri nasaha kuwasaidia kuishi maisha yasiyotegemea uhalifu, 482 walipewa ushauri wa kisaikolojia na kufundishwa maadili ya jamii na 50 walipewa huduma za urekebu kwa kushirikiana na wadau. Huduma hizo ni pamoja na za kidini, kiafya, kisheria na ujasiriamali. Aidha, wafungwa wanne (4) wagonjwa waliunganishwa na vituo vya afya kupata huduma za ARV na Kifua Kikuu.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitoa elimu ya uhamasishaji kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291 na Sheria ya Kifungo cha Nje kwa Wahalifu, Sura ya 247 kwa wadau wa Haki Jinai na jamii. Elimu pia ilitolewa katika shule za msingi na sekondari, vyuo vya elimu ya kati na juu, kwa wafungwa na mahabusu waliopo magerezani. Jumla ya wadau 356,891 walifikiwa kwa kupatiwa elimu juu ya vifungo vya nje. Zoezi hilo la uelimishaji lilitolewa katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kupitia ushiriki wa Wizara katika Maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi itaratibu na kufuatilia wafungwa 5,500 wanaolengwa kuwekwa chini ya Sheria ya Huduma za Jamii, Sura ya 291 na Sheria ya Kifungo cha Nje kwa Wahalifu, Sura ya 247. Ili kufikia azma hii kazi zitakazofanyika ni: kutoa elimu ya utekelezaji wa programu za vifungo vya nje kwa wadau wa Haki Jinai; kufanya uchunguzi wa kijamii; na kukagua taasisi za Serikali zinazotoa kazi kwa wafungwa wa vifungo vya nje ili kubaini kama zimetimiza vigezo vya kupewa wafungwa.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni kutekeleza programu za urekebishaji wa tabia za wafungwa; kusimamia na kufuatilia wafungwa wanaotekeleza adhabu kwenye mikoa na wilaya ili kuhakikisha amri zilizotolewa na Mahakama dhidi yao zinatekelezwa ipasavyo; na ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wafungwa wa Adhabu Mbadala (NOCMIS). Jumla ya Shilingi bilioni 3.38 zimetengwa katika mwaka 2025/26 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

**SHIRIKA LA MAGEREZA (SHIMA)**

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linatekeleza majukumu yake ya msingi ya uzalishaji katika shughuli za kilimo, viwanda vidogo, ujenzi na uchimbaji madini. Uzalishaji huo umewezesha ukusanyaji wa mapato ghafi ya jumla ya Shilingi bilioni 16.22 hadi kufikia Aprili 2025. Utekelezaji wa shughuli za miradi ni kama ifuatavyo:

**Miradi ya Kilimo**

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya ekari 8,262 zimelimwa mazao yafuatayo: mahindi ekari 4,436, mpunga ekari 1,110, maharage ekari 278, ngano ekari 40, alizeti ekari 70, miwa ekari 300 na michikichi ekari 2,028. Makadirio ya mavuno ni wastani wa tani 9,427.8 kwa mchanganuo ufuatao: mahindi tani 3,992, mpunga tani 666, maharage tani 111, ngano tani 16, alizeti tani 16.8, miwa tani 4,500 na mafuta ya mawese tani 126. Mavuno hayo yatasaidia kuongeza mapato ya Shirika.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Shirika linatarajia kulima jumla ya ekari 11,710. Mazao yatakayolimwa ni kama ifuatavyo: mahindi ekari 5,870, mpunga ekari 1,280, maharage ekari

290, ngano ekari 420, alizeti ekari 200, miwa ekari 1,400 na michikichi ekari 2,250. Makadirio ya mavuno ni wastani wa mahindi tani 7,924.5, mpunga tani 1,440, maharage tani 145, ngano tani 420, alizeti tani 84, miwa tani 21,000 na mafuta ya mawese tani 3,651.2.

**Shughuli za Ujenzi**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.47. Aidha, Shirika linaendelea na ujenzi wa majengo ya TAKUKURU katika Mkoa wa Shinyanga wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.42 ambao umefikia asilimia 83 na utakamilika Juni 2025; ujenzi wa majengo ya TAKUKURU Mkoa wa Morogoro wenye thamani ya Shilingi bilioni 1.46 ambao umeanza Aprili 2025 umefikia asilimia 10 na utakamilika Januari 2026. Vilevile, ujenzi wa Ofisi ya eGA Mkoa wa Iringa kwa Shilingi milioni 490.33 umefikia asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika Juni 2025.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine za ujenzi zinazotekelezwa na Shirika ni kama ifuatavyo: ujenzi wa Uzio wa Ukuta na Vigingi vya Mipaka kwenye Vituo Sita (6) vya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) vya Hombolo – Dodoma umefikia asilimia 77, Dakawa na Ifakara – Morogoro umefikia asilimia 75, Maruku – Kagera umefikia asilimia 21.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ujenzi katika vituo vya TARI Kihinga – Kigoma umefikia asilimia 30 na Kifyulilo – Iringa umefikia asilimia 20. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 3.50 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Oktoba 2025. Shirika litaendelea kuimarisha kikosi chake cha ujenzi kwa kuongeza vitendea kazi na watendaji ili kupata fursa zaidi za zabuni za miradi ya ujenzi.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Magereza kupitia kikosi chake cha ujenzi limefanya kazi mbalimbali kwa kiwango bora miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kiwanda kipya cha viatu Kilimanjaro na Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida. ***Hivyo, naomba nitoe rai kwa taasisi za umma na binafsi kutumia Shirika katika kutekeleza kazi za ujenzi zikiwemo majengo ya ofisi, viwanda, shule, vyuo na nyumba za makazi.***

**Mradi wa Uzalishaji Chokaa Wazo Hill**

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika linatekeleza mradi wa madini wa Wazo Hill wa uzalishaji wa mawe ya chokaa na kifusi cha ujenzi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya Shilingi bilioni 1.35 zimekusanywa kutokana na mauzo ya kifusi cha ujenzi na mawe ya chokaa. Matarajio ni kufikia Shilingi bilioni 1.80 ifikapo Juni 2025.

**Kampuni Tanzu ya Ulinzi – SHIMA Guard Company Limited**

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Magereza kupitia kampuni yake tanzu ya ulinzi (SHIMA Guard Company Limited) linaendelea kutoa ajira kwa vijana ambapo hadi kufikia Aprili 2025 limeajiri jumla ya vijana 603. Aidha, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025 kampuni hii imekusanya kiasi cha mapato cha Shilingi bilioni 2.08.

**Mikakati ya Kuimarisha Shirika la Magereza**

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26 Shirika lina mkakati wa kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji katika eneo la ekari 1,500 ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa lengo la kuchangia usalama wa chakula nchini. Kati hizo, ekari 1,200 zitalimwa mpunga na ekari 300 ni za mahindi.

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Magereza litaendelea kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye maeneo yake ikijumuisha kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na ujenzi wa miundombinu ya biashara. Aidha, natumia nafasi hii kuwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kushirikiana na Shirika hilo katika uwekezaji kupitia fursa hizo kwa lengo la kuongeza mapato. Vilevile, Shirika la Magereza kupitia kampuni yake ya SHIMA Guard litaendelea kutafuta fursa za kutoa huduma za ulinzi kwa sekta ya umma na binafsi ili kuongeza mapato na ajira kwa vijana wa kitanzania.

**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**Huduma za Zimamoto na Uokoaji**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutekeleza jukumu la kuzuia uharibifu wa mali na kuokoa majeruhi kutokana na moto na majanga mengine. Hadi kufikia Aprili 2025 uokoaji umefanyika katika matukio 3,030 na majeruhi 2,451

waliokolewa. Baadhi ya matukio makubwa ni: kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo na kuzama kwa wavuvi katika ziwa Rukwa kutokana na upepo mkali. Katika mwaka 2025/26 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea kutekeleza jukumu hilo ili kuzuia uharibifu wa mali na kuokoa majeruhi kutokana na majanga ya moto na mengine.

**Ukaguzi wa Kinga na Tahadhari ya Moto**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuzuia majanga ya moto, ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya majanga hayo ulifanyika katika mikoa yote nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 ukaguzi umefanyika katika maeneo 67,322 ikilinganishwa na maeneo 53,517 yaliyokaguliwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko hilo la maeneo 13,805 ambalo ni sawa na asilimia 25.80 limetokana na kuongezeka kwa rasilimaliwatu na vitendea kazi.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ukaguzi huo Shilingi bilioni 11.26 zilikusanywa sawa na asilimia 117.54 ya lengo la kukusanya Shilingi bilioni 8.62 kwa kipindi husika. Katika mwaka 2025/26 jumla ya maeneo 131,875 yatakaguliwa ili kufikia lengo la kukagua maeneo 350,000 yaliyopangwa katika mpango mkakati wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa miaka mitano (2021/22 – 2025/26) na Shilingi bilioni 13 zinategemewa kukusanywa.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfumo wa Usimamizi na Tahadhari za Moto umekamilika na unatumika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mfumo huo umewarahisishia wananchi kuomba huduma ya ukaguzi wa kinga na tahadhari dhidi ya moto na kuimarisha usalama katika maeneo yao. ***Natumia fursa hii kuwahamasisha wananchi kuendelea kutumia mfumo huo unaopatikana kupitia https://portal.zimamoto.go.tz.***

**Mitambo, Magari na Vifaa vya Kuzima moto na Uokoaji**

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukabiliana na changamoto za utoaji wa huduma bora kwa wananchi, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatekeleza mradi wa ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuzima moto na uokoaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100. Hadi kufikia Aprili 2025 Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji imepokea magari 40 ya kubebea wagonjwa, magari 30 ya mawasiliano na kuongozea operesheni za

kuzimamoto na uokoaji, karakana sita (6) zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo, gari moja (1) la kubebea maji, mitambo miwili (2) ya kuvuta magari mabovu na yaliyopata ajali, shehena ya vifaa vya kuzima moto na uokoaji pamoja na miundombinu ya mawasiliano.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mwezi Mei 2025 Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji inatarajia kupokea boti moja (1) ya kuzima moto na uokoaji, magari matano (5) ya kubeba maji, gari moja (1) la uokoaji, mitambo miwili (2) ya kuvuta magari mabovu na yaliyopata ajali, shehena za vifaa vya kuzima moto na uokoaji pamoja na miundombinu ya mawasiliano.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Agosti 2025, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kupokea magari 87 ya kuzima moto na uokoaji, boti 22 za kuzima moto na uokoaji, magari matano (5) ya kubebea maji, magari matatu (3) ya kukabiliana na matukio ya kemikali hatarishi pamoja na shehena ya vifaa vya miundombinu ya mafunzo ya uokoaji na uzimaji moto. Aidha, magari 62 ya kuzima moto na uokoaji na Helikopta moja (1) vitapokelewa mwezi Desemba 2025. Pia, katika mwaka 2025/26 Jeshi limetenga Shilingi bilioni 1.22 kwa ajili ya kufunga mfumo wa mawasiliano ya dharura ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji katika shughuli za zimamoto na uokoaji.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Novemba 2024 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea Shilingi bilioni 1.38 kwa ajili ya ununuzi wa magari 21 ya utawala na ukaguzi. Fedha hizo zimelipwa kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na magari hayo yanatarajiwa kupokelewa mwishoni wa mwezi Julai 2025. Pia, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea msaada wa magari mawili (2) ambayo ni gari la kuzima moto kutoka Serikali ya Ujerumani na gari la shughuli za utawala kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Katika mwaka 2025/26 Shilingi bilioni 1.15 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari sita (6) ya utawala na ukaguzi.

**Ununuzi na Ukarabati wa *Fire Hydrants***

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** upungufu wa *fire hydrants* unachangia kupungua kwa ufanisi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika

kutekeleza jukumu la kuzima moto. Wizara kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na Wizara ya Maji inatekeleza mkakati wa kufunga *fire hydrants* 4,256 utakaotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano (5). Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya *fire hydrants* 163 zimefungwa katika mikoa mbalimbali. Pia, katika mwaka 2025/26 Shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *fire hydrants* 270.

**Ujenzi wa Vituo vya Zimamoto na Uokoaji**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma za zimamoto na uokoaji umekuwa na changamoto kutokana na uchache wa vituo vya zimamoto na uokoaji. Katika kupata suluhisho la changamoto hiyo, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na uokoaji inaendelea na ukamilishaji wa vituo saba (7). Hadi kufikia Aprili 2025 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limepokea Shilingi bilioni 2.59 kwa ajili ya ukamilishaji wa vituo hivyo. Ujenzi huo umefikia katika hatua zifuatazo: Njombe asilimia 73; Kagera asilimia 69; Songwe asilimia 50; Simiyu asilimia 48; Manyara asilimia 47; Katavi asilimia 38; na Geita asilimia 38. Ujenzi wa vituo hivyo utakamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Septemba 2025.

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, upatikanaji wa mitambo, vifaa vya kuzima moto na uokoaji na kutolewa kwa fedha za ukamilishaji wa ujenzi wa vituo saba (7) na majengo mawili ya ghorofa Kikombo – Dodoma yenye uwezo wa kuishi familia 20 za askari ni miongoni mwa ***mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi***.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 6.85 zimetengwa katika mwaka 2025/26 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya zimamoto na uokoaji katika Mikoa ya Singida na Mara, ujenzi wa vituo nane (8) vya zimamoto na uokoaji kwa ngazi ya Wilaya (Sengerema, Chalinze, Ruangwa, Mafinga, Nzega, Gairo, Muheza na Bunda) na ukarabati wa vituo viwili (2) vya zimamoto na uokoaji katika Mikoa ya Mbeya na Ruvuma.

**Elimu kwa Umma**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu kinga na tahadhari dhidi ya moto na majanga mengine yakiwemo mafuriko, upepo mkali na radi. Hadi kufikia Aprili 2025 elimu imetolewa kupitia vipindi vya runinga 88 na redio 796. Aidha, katika kipindi husika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeanzisha klabu za zimamoto 211 zenye wanachama 16,577, skauti vikundi 15 vyenye wanachama 2,248 katika shule za msingi na sekondari na vikundi sita (6) vya wazimamoto wa kujitolea vyenye wanachama 438. Vikundi hivyo vinasaidia kutoa elimu na kushiriki kwenye uokoaji pindi majanga yanapotokea.

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Shilingi milioni 219.47 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa elimu kwa umma na uhamasishaji wa jamii kujiunga na vikundi vya wazimamoto wa kujitolea. Vilevile, Shilingi milioni 35.76 zimetengwa kwa ajili ya kuzindua kampeni ya "***Usiogope Jiokoe***" ambapo wananchi wataelimishwa namna ya kuwa jasiri kupambana na kujiokoa kwenye matukio ya moto na majanga mengine pamoja na matumizi sahihi ya namba ya dharura 114.

**IDARA YA UHAMIAJI**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kudhibiti uingiaji, ukaaji na utokaji wa wageni na raia nchini. Lengo ni kuimarisha usalama na maendeleo katika sekta mbalimbali kwa jamii na kukuza uchumi.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 jumla ya wageni 1,839,342 waliingia ikilinganishwa na wageni 1,695,350 waliongia katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, jumla ya wageni 1,698,420 walitoka nchini ikilinganishwa na wageni 1,579,925 waliotoka mwaka 2023/24. Pia, jumla ya Watanzania 400,434 walitoka nchini na 376,011 waliingia katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 ikilinganishwa na Watanzania 417,341 waliotoka nchini na 386,681 walioingia nchini katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2023/24.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** ongezeko la wageni walioingia nchini linatokana na juhudi zinazofanywa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu ya kuwavutia wageni kutembelea Tanzania kwa shughuli za utalii, uwekezaji, biashara na shughuli za kijamii ambazo zimesaidia kukuza diplomasia ya uchumi kwa lengo la kuongeza tija na maendeleo ya Taifa.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliziondoa nchi za Azerbaijan, Djibouti, Equatorial Guinea, Ethiopia, Kazakhstan, Senegal na Sri Lanka katika orodha ya nchi zilizopo katika utaratibu wa viza rejea. Hatua hiyo imerahisisha na kuongeza idadi ya wageni wanaoingia nchini kwa uwekezaji na maendeleo ya teknolojia sambamba na kukua kwa mapato yasiyokuwa ya kodi kutokana na huduma za uhamiaji zinazotolewa kwa wageni.

**Utoaji wa Vibali vya Ukaazi kwa Wageni**

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa na kusimamia huduma za vibali vya ukaazi kwa wageni wanaoingia nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya vibali vya ukaazi 18,299 vilitolewa kwa madaraja yafuatayo: Daraja A – 2,566; Daraja B – 12,090; na Daraja C – 3,643 ikilinganishwa na vibali 18,813 Daraja A – 2,825; Daraja B – 12,460; na Daraja C – 3,528 vilivyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** sanjari na utoaji wa vibali vya ukaazi kwa wageni, Idara imetoa jumla ya Hati za Mfuasi 4,225 na Hati za Msamaha 680 ikilinganishwa na Hati za Mfuasi 2,901 na Hati za Msamaha 874 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24. Aidha, Viza 908,960 zilitolewa kwa wageni walioomba kuingia nchini ikilinganishwa na Viza 777,104 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

**Pasipoti na Hati za Dharura**

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za Pasipoti na Hati za Dharura zimetolewa kwa Watanzania waliokidhi vigezo na wenye nia ya kusafiria nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025

jumla ya Pasipoti 114,448 zimetolewa ikilinganishwa na Pasipoti 141,762 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kati ya Pasipoti hizo, 561 zilikuwa za Kibalozi, 216 za Kiutumishi na 113,671 za Kawaida.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na changamoto katika uombaji wa Pasipoti ikiwemo ujazaji wa fomu za maombi na uwasilishaji wa nyaraka zinazohitajika. Ili kuondoa changamoto hizo, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji itaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ujazaji wa fomu za maombi ya Pasipoti na kuwasilisha nyaraka zinazohitajika ikiwemo kupata kibali cha Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) kwa waombaji wa Pasipoti waliopata kazi nje ya nchi. Lengo ni kuhakikisha huduma bora za Pasipoti zinatolewa kwa wakati kwa Watanzania wanaotaka kusafiri nje ya nchi.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hati za Safari za Dharura 204,387 zimetolewa ikilinganishwa na Hati 237,872 zilizotolewa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kwa mwaka 2025/26, huduma hizo zitaendelea kutolewa kwa Raia wa Tanzania ili kuwawezesha kusafiri nje ya nchi kulingana na mahitaji yao.

**Operesheni, Misako na Doria**

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Idara ya Uhamiaji imefanya doria, misako na operesheni maalum za kuwabaini na kuwaondosha wahamiaji haramu na wageni wanaoishi nchini kinyume cha Sheria. Hatua za kisheria zimechukuliwa kwa Watanzania wanaojihusisha na usafirishaji haramu wa wahamiaji. Hadi kufikia Aprili 2025 jumla ya watuhumiwa 23,315 wa makosa ya kiuhamiaji walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ambapo kati yao 13,045 waliondoshwa nchini.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** raia wa kigeni 2,777 walimaliza vifungo vyao katika magereza mbalimbali hapa nchini na kurudishwa katika nchi zao. Katika kuendelea na mapambano dhini ya wahamiaji haramu nchini kupitia kampeni ya ***"Mjue Jirani Yako"*** inayolenga kuwajengea uwelewa wananchi ili waweze kushiriki katika kulinda usalama wa nchi.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kampeni hiyo, jumla ya vipindi 301 vya redio (28), mikutano ya hadhara (217), vikundi vya uhamiaji shuleni (56), na maonesho ya kitaifa katika mikoa na maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu vimefanyika kuanzia mwezi Julai 2024 hadi Aprili 2025. Lengo ni kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za uhamiaji.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Wizara kwa kushirikikiana na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama itaendelea kuimarisha udhibiti wa wahamiaji haramu. Aidha, itaendelea kushirikisha makundi mbalimbali ya wananchi ikiwemo watendaji wa kata na shehia, wenyeviti wa vijiji na mitaa pamoja na viongozi wa vitongoji, dini na kimila ili kuwa sehemu ya kuelimisha jamii namna ya kumtambua mhamiaji au mgeni katika maeneo yao hususan katika mikoa ya pembezoni. Mikoa hiyo ni pamoja na Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mtwara, Rukwa, Ruvuma, Tanga na Kisiwa cha Pemba.

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, vikao vya ujirani mwema vimefanyika na nchi jirani zinazopakana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan zenye idadi kubwa ya wahamiaji haramu kwa lengo la kubadilishana uzoefu, mikakati ya kukabiliana na wahamiaji haramu, kukuza mahusiano na kubadilishana taarifa. ***Naomba kutoa rai kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa kwa Idara ya Uhamiaji pale wanapowatilia mashaka wageni waliofika kwenye maeneo yao ili kuhakikisha wageni wanaoingia nchini wanafuata sheria, kanuni na taratibu za ukaazi wao***.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa jumla ya Shilingi bilioni 3.29 za ununuzi wa magari 13 kwa ajili ya Idara ya Uhamiaji. Hadi mwezi Aprili, Idara ya Uhamiaji imepokea magari saba (7) na magari sita (6) yanategemewa kupokelewa mwezi Julai 2025. Aidha, kwa mwaka 2025/26 zimetengwa jumla ya Shilingi bilioni 3.19 kwa ajili ununuzi wa magari 11 na pikipiki 20.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, mifumo ya udhibiti na usimamizi wa mipaka itaimarishwa ili kuhakikisha wageni wanaoingia nchini

wanapitia vituo vinavyotambulika kwa mujibu wa sheria, pamoja na kuhakikisha mifumo ya uhamiaji inasomana na taasisi nyingine ili kuimarisha usalama na uchumi wa nchi. Katika kudhibiti mianya na njia zisizo rasmi Idara ya Uhamiaji itaendelea kufanya misako, doria, kaguzi za mara kwa mara ili kuwabaini wageni wasiofuata sheria za nchi.

**Mapitio ya Sheria na Makubaliano (MoU) na Nchi nyingine**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Septemba 2024 Bunge lako lilifanya marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura 54 kupitia Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na. 2 ya mwaka 2024. Pamoja na mambo mengine, marekebisho hayo yaliboresha maeneo yafuatayo: kuanzishwa kwa Bodi ya Uendeshaji ya Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Tanzania (TRITA) pamoja na kutambua matumizi ya njia za mifumo ya kielektroniki katika utoaji wa huduma za Uhamiaji Mtandao.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Serikali inatekeleza itifaki mbalimbali, Serikali imeingia makubaliano (MoU) na nchi za Afrika Kusini, Algeria, Angola, Brazil, China, Cuba, India, Indonesia, Kenya, Korea Kusini, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Norway, Uganda, Uturuki, Vietnam na Zambia. Lengo ni kukuza mahusiano pamoja na kurahisisha uingiaji na utokaji wa raia na wageni kwa kufutiana malipo ya Viza kwa watu wanaotumia Pasipoti za Kibalozi na za Kiutumishi; kushirikiana katika kudhibiti uhamiaji haramu *(illegal immigration)* na uhamiaji magendo (human smuggling); kubadilishana taarifa za kiintelijensia zinazosaidia kudhibiti mitandao ya fedha haramu ambayo hufadhili uhamiaji magendo.

**Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwezi Februari 2025, Idara ya Uhamiaji ilipokea jumla ya Shilingi bilioni 2.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa mchanganuo ufuatao:

Shilingi milioni 103.23 kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mtwara ambao kwa sasa umefikia asilimia 93 na Shilingi bilioni 1.5 kwa ujenzi wa Nyumba za makazi ya Maafisa, Wakaguzi na Askari Msalato Dodoma ambao utekelezaji umefikia asilimia 17. Aidha, jumla ya

Shilingi milioni 600 zimeelekezwa kukamilisha miradi ya ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji katika Wilaya za Buhigwe – Kigoma, pamoja na Vituo vya Uhamiaji vya mipakani vya Chikongo Wilaya ya Tandahimba na Mkenda – Nakawale mkoani Ruvuma.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Shilingi milioni 143.78 zimepokelewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Bagamoyo; Shilingi milioni 252.33 kukarabati majengo ya Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda (TRITA) kilichopo mjini Moshi; na ukamilishaji wa miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Uhamiaji Wilaya ya Mlele, Butiama na Mufindi kwa Shilingi milioni 70 kila moja. Aidha, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Uhamiaji Makao Makuu Jijini Dodoma umefikia asilimia 69 na unatarajia kukamilika Agosti 2025.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi bilioni 5.30 zimetengwa katika mwaka 2025/26 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji, ambapo Mkoa wa Songwe imetengewa Shilingi milioni 862.27, Simiyu Shilingi bilioni 1.50 na kumalizia ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Buhigwe – Shilingi milioni 150.80. Aidha, Shilingi bilioni 1.45 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi ya Maafisa na Askari watakaohudumia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Jijini Dodoma. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni ujenzi wa nyumba za Makazi ya Wakufunzi katika Chuo cha Raphael Kubaga Mkoani Tanga, ambapo jumla ya Shilingi milioni 600 zimetengwa.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango wa uboreshaji wa miundombinu ya mifumo ya TEHAMA kwa mwaka 2024/25 Idara ya Uhamiaji imeingia Mkataba wa jumla ya Shilingi bilioni 3 wa ununuzi wa vifaa vya TEHAMA. Hadi kufikia Aprili 2025 Shilingi bilioni 1.58 zimepokelewa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo. Pia, jumla ya Shilingi bilioni 69.08 zimetengwa katika mwaka 2025/26 ili kuboresha miundombinu ya mifumo ya Uhamiaji Mtandao kwa kufunga mifumo katika maeneo ambayo hayakufungwa mifumo hiyo.

## MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA (NIDA)

### Hali ya Usajili na Utambuzi wa Watu Nchini

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imesajili na kutambua watu 844,994 nchini. Aidha, watu waliosajiliwa na kutambuliwa tangu kuanza kwa usajili na utambuzi umefikia 25,854,970 sawa na asilimia 81.9 ya watu 31,582,976 wenye umri kuanzia miaka 18 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imedhamiria kukamilisha usajili wa watu takribani milioni sita katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2025/26 – 2027/28. Katika mwaka 2025/26 Shilingi bilioni 5.81 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usajili na utambuzi wa watu 2,389,290 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, jumla ya Namba za Utambulisho wa Taifa (NIN) 757,189 zilizalishwa na kugawiwa kwa wananchi. Hivyo, kufanya jumla ya NIN zilizozalishwa kufikia 21,514,741 sawa na asilimia 83.2 ya idadi ya watu waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi la usajili na utambuzi wa watu nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/26, Mamlaka imetenga Shilingi milioni 461.4 kwa ajili ya kuchakata na kutatua maombi ya wananchi 4,342,926 waliosajiliwa lakini maombi yao hayajafikia hatua ya kuzalisha NINs.

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA pia imesajili na kutambua Watanzania 1,300 wanaoishi nje ya nchi (Diaspora) kupitia Balozi za Tanzania zilizopo katika nchi hizo. Zoezi hilo limefanyika katika Nchi za Comoro, Marekani, Ubelgiji, Uingereza, Uholanzi, na Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE). Kati ya Watanzania hao, 852 walifanyiwa usajili wa maombi ya Kitambulisho cha Taifa na 707 walipatiwa Namba za Utambulisho na Vitambulisho vya Taifa. Aidha, uhakiki wa taarifa pamoja na uraia kwa Watanzania 145 waliosalia unaendelea, na namba na Vitambulisho vya Taifa vitazalishwa kwa maombi yatakayokidhi vigezo. ***Natoa wito kwa Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuwa wazalendo na wasikubali kamwe kutumika katika hila ya aina yoyote ya kusaliti nchi yao, ndugu, marafiki na jamii yao kwa ujumla***.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA imeandaa Mwongozo Maalum kwa ajili ya kurahisisha marekebisho ya taarifa za wananchi zilizopo katika Rejista ya NIDA. Elimu kwa umma imetolewa kuhusu taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kuwezesha wananchi kufanya marekebisho ya taarifa binafsi katika mfumo wa NIDA. Katika kipindi cha Julai hadi Aprili 2025, jumla ya wananchi 12,121 wamepatiwa huduma za kurekebisha taarifa zao.

**Uzalishaji na Usambazaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa Wananchi**

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 vitambulisho 1,243,105 vimezalishwa na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,308,774 sawa na asilimia 99 ya idadi ya Namba za Utambulisho 21,514,741 zilizozalishwa. Aidha, vitambulisho vya Taifa 1,092,160 vimesambazwa kwa wananchi na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyosambazwa kufikia 21,191,598.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, Namba za Utambulisho (NIN) 17,879 ambazo bado hazijazalishiwa vitambulisho zinatarajiwa kukamilishwa kabla ya Juni 2025. Vilevile, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26 Shilingi bilioni 3.45 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa kadi zitakazowezesha uzalishaji vitambulisho vya Taifa vya watu wote wenye NINs katika kipindi hicho.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** NIDA imetekeleza mpango wa urejeshaji wa Vitambulisho vya Taifa kutoka kwenye kata, vijiji na shehia ambavyo havijachukuliwa baada ya ugawaji wa jumla kukamilika. Ugawaji huu ulitekelezwa katika wilaya zote 150 za Tanzania Bara na Zanzibar. Vitambulisho vilirejeshwa katika ofisi za usajili za wilaya na kuingizwa katika programu maalum iliyowezesha kutuma ujumbe mfupi wa simu (SMS) kwa waombaji kuwaelekeza vilipo vitambulisho vyao na kuwasisitiza kufika kuvichukua. Mpango huo ulizinduliwa rasmi tarehe 06 Januari 2025 katika ofisi za NIDA za wilaya zote nchini ikiwa ni mkakati mahsusi wa kutatua changamoto za upatikanaji wa vitambulisho kwa wananchi.

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia utaratibu huo jumla ya wananchi 1,268,694 wametumiwa ujumbe mfupi na wanaendelea kufika katika ofisi za NIDA kuchukua vitambulisho. Kupitia utaratibu huo jumla ya

wananchi 565,876 wamejitokeza kuchukua vitambulisho vyao. ***Naomba nitoe rai kwa wananchi wote ambao hawajachukua vitambulisho vyao vya Taifa kufika katika ofisi za NIDA za wilaya mara wapatapo ujumbe mfupi wa simu.***

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha vitambulisho vinavyozalishwa vinawafikia wananchi kwa wakati, NIDA itaendelea na utaratibu wa kutuma ujumbe mfupi wa simu (sms) kwa wananchi ambao vitambulisho vyao vimezalishwa ili kuwapa taarifa ya kuvichukua kutoka ofisi za usajili za wilaya waliposajiliwa.

**Utambulisho wa Watu kwa Kutumia Jamii Namba**

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa kutoa na kuwezesha matumizi ya Namba moja ya Utambulisho katika kutoa huduma kwa wananchi. Mpango huo ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa tarehe 11 Agosti 2023 wakati wa uzinduzi wa Mkongo wa Baharini wa Mawasiliano wa Airtel2 Africa Jijini Dar es Salaam. Mhe. Rais alielekeza namba hiyo ijulikane kwa jina la Jamii Namba, ambayo ni namba ya Kitambulisho cha Taifa inayotolewa na NIDA.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Jamii Namba itatolewa kwa watu wote chini ya miaka 18 na kwa wageni wanaoingia nchini. Aidha, utekelezaji huo utaongeza wigo wa makundi yanayotambuliwa na NIDA, kutoka makundi manne ambayo ni raia wa Tanzania, Wakimbizi, Walowezi na Wageni Wakazi wanaoishi nchini na kufikia makundi matano.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** namba hiyo itamtambulisha mtu wakati wa kupata huduma mbalimbali zinazotolewa na taasisi za Serikali na binafsi ndani ya nchi kuanzia anapoipata hadi anapofariki. ***Utekelezaji huu ni katika kuzingatia azma ya Mhe. Rais ya kuondoa usumbufu kwa wananchi wakati wa kupatiwa huduma, kuwaondolea mzigo wa kuwa na vitambulisho vingi kwa ajili ya utambuzi na kuwa na utambulisho mmoja mahali pote***.

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 na Aprili 2025 NIDA imekamilisha ujenzi wa mfumo wa usajili wa watoto na wageni

wanaoingia na kukaa nchini chini ya miezi miwili. Aidha, NIDA imekamilisha ujenzi wa mfumo wa maunganisho (Jamii Namba Gateway) ya mifumo ya NIDA, Idara ya Uhamiaji, RITA na ZCSRA unaowezesha ubadilishanaji wa taarifa na kurahisisha utoaji wa Jamii Namba.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo huo pia, unawezesha mgeni anayeingia nchini kupata Jamii Namba akiwa bado yuko kiwanja cha ndege au ofisi za uhamiaji mipakani. Vilevile, mfumo unawezesha mtoto anapozaliwa kupata Jamii Namba kabla ya kutoka hospitalini pale wazazi watakapokuwa wameweza kumpa mtoto jina. Ujenzi wa mifumo hiyo niliyoitaja umewezeshwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** utolewaji wa jamii namba utasaidia katika mambo yafuatayo: kupunguza gharama kubwa kwa Serikali zinazotokana na kujirudia kwa uwekezaji na utekelezaji wa majukumu kwenye taasisi za Serikali; kuongeza ufanisi katika kuwahudumia wananchi kwa kuwaondolea usumbufu wa kurudia kuwasilisha taarifa na nyaraka wakati wa kupata huduma; na kudhibiti udanganyifu ambao unaisababishia Serikali hasara kubwa.

**178.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 jumla ya Shilingi bilioni 11.34 zimetengwa kwa ajili ya kuanza zoezi la majaribio ya kutoa Jamii Namba ili kuwasajili na kuwatambua watu 235,826 wenye umri chini ya miaka 18. Majaribio hayo yatafanyika katika Wilaya za Kusini – Kusini Unguja, Kilolo – Iringa na Rungwe – Mbeya. Lengo ni kupata uzoefu pamoja na kubaini changamoto kabla ya kuanza utekelezaji wa mpango huo kwa nchi nzima katika mwaka wa fedha 2026/27.

**Uunganishaji wa Mfumo wa Usajili na Utambuzi na Mifumo ya Taasisi Nyingine**

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 NIDA imeunganisha taasisi 16 kwenye mfumo wa ushirikishaji taarifa, hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kufikia 124. Kati ya hizo, taasisi 59 ni za Serikali na 65 ni za binafsi. Aidha, hadi kufikia mwisho wa mwaka 2025/26 jumla ya taasisi 20 zinatarajiwa

kuunganishwa katika mfumo wa ushirikishaji taarifa na hivyo kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa watu na kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia matumizi ya mifumo ya kidigitali.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** uunganishaji wa mifumo hiyo unaepusha wananchi kurudia kuwasilisha taarifa zao ambazo tayari zipo NIDA pale wanapohitajika kupatiwa huduma kwenye taasisi za umma au binafsi. Uunganishaji huo wa mifumo pia unawaongezea watoa huduma ufanisi kwenye kutoa huduma kwa kuwawezesha kupata taarifa za utambulisho wa mtu ndani ya muda mfupi.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, NIDA kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unaosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeunda mfumo mpya wa kushirikisha taarifa unaoitwa *Jamii Exchange*. Madhumuni ya kuunda mfumo huo ni kuwezesha taarifa binafsi za mtu kushirikishwa baada ya mhusika kuridhia ushirikishwaji huo kama inavyoelekezwa na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022 (Personal Data Protection Act, 2022). Aidha, *Jamii exchange* imeundwa ili kuendana na teknolojia mpya za ushirikishaji taarifa. Mfumo huo umeleta mabadiliko makubwa ya utunzanji wa taarifa, uhuru wa kusimamia taarifa binafsi na usalama wa taarifa za watu.

**Ujenzi wa Ofisi za Usajili na Utambuzi Watu**

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya ujenzi wa ofisi za usajili 33 yameanza. Aidha, Mshauri Elekezi, Kampuni ya *Daeyeong Ubitec Limited* kutoka Korea Kusini anaendelea na kazi ya usanifu wa majengo, mifumo na miundombinu ya TEHAMA pamoja na maandalizi ya nyaraka za zabuni ya kumpata mkandarasi.

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 29.13 zimetengwa kwa mwaka 2025/26 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za usajili katika Wilaya 31, ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya NIDA – Dodoma na ujenzi wa Kituo cha TEHAMA – Kibaha. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 5.51 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 23.62 ni fedha za nje ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini.

**Ununuzi wa Vitendea Kazi**

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 NIDA imepokea Shilingi bilioni 3.37 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo magari 21, samani za ofisi, vifaa vya usajili na vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 NIDA itaendelea kuboresha mazingira ya ofisi kwa kununua vitendea kazi ikiwemo ununuzi wa magari 140 na samani za ofisi kwa ajili ya shughuli za usajili na utambuzi Tanzania Bara na Zanzibar. Jumla ya Shilingi bilioni 45.20 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari, vifaa vya usajili na vifaa vya TEHAMA na maboresho ya mifumo.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**186.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2025, Tanzania ilikuwa na jumla ya waomba hifadhi na wakimbizi 239,660. Kati ya hao, 152,848 ni wenye asili ya Burundi, 86,144 ni wenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na 668 ni kutoka mataifa mengine. Katika kipindi hicho, Wizara imewapokea na kuwasajili waomba hifadhi wapya 2,975 kutoka Afghanistan, Burundi, Cameroon, Eritrea, DRC, Misri, Palestina, Rwanda, Sudani, Sudani Kusini, Syria, Ujerumani, Ukraine, Uturuki na Yemen.

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwatafutia wakimbizi suluhisho la kudumu, hadi kufikia Aprili 2025, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), imefanikiwa kutoa suluhisho la kudumu kwa wakimbizi 10,168. Kati yao wakimbizi 6,292 walirejea kwa hiari Burundi na wakimbizi 3,876 walihamishiwa nchi za Marekani (2,953), Canada (300), Australia (11), Sweden (599) na Ufaransa (13).

**Matumizi ya Nishati Safi katika Kambi za Wakimbizi**

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia jitihada za urejeshaji mazingira, jumla ya miti 461,436 ilipandwa katika kambi za wakimbizi. Majiko banifu 5,316 yalitengenezwa na kilogramu 200,000 za mkaa mbadala zilitengenezwa na kugawanywa kwa wakimbizi ili

kuendelea kupunguza matumizi ya kuni kama nishati ya kupikia. Aidha, katika maeneo yote ya mikusanyiko ya watu zaidi ya 100 katika kambi za wakimbizi ikiwemo vituo vya afya na maeneo ya urejeaji, gesi inatumika kama nishati ya kupikia.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi bilioni 3.01 zimetengwa katika mwaka 2025/26 kwa ajili ya kazi zifuatazo: kuandaa vikao vya kitaifa vya kujadili maombi ya hifadhi ya wakimbizi nchini; kusimamia na kuimarisha ulinzi na usalama katika kambi; kusimamia utoaji wa huduma zote muhimu zinazotolewa na mashirika mbalimbali ndani ya kambi; kuwatafutia wakimbizi suluhisho la kudumu kwa njia ya urejeaji katika nchi za asili; na kuhakikisha shughuli za urejeshaji mazingira zinatekelezwa katika kambi na maeneo yanayozunguka kambi.

**USAJILI NA USIMAMIZI WA JUMUIYA ZA KIRAIA**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imesajili jumla ya Jumuiya za Kiraia 184 ambapo kati ya hizo, jumuiya 97 ni za kidini na 87 zisizo za kidini. Wizara imefuatilia utendaji wa jumuiya hizo kwa kufanya uhakiki na ukaguzi kwa madhumuni ya kujiridhisha iwapo zinajiendesha kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake. Aidha, elimu imetolewa kwa wananchi kuhusu aina ya taasisi, jumuiya na vikundi vinavyopaswa kusajiliwa ili kuwezesha wananchi kuendesha shughuli zao katika mazingira yanayozingatia sheria za nchi.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Jumuiya imefanya ukaguzi kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika Mikoa ya Dodoma, Kagera, Kigoma, Katavi, Simiyu, Shinyanga na Tabora. Katika ukaguzi huo, jumla ya Jumuiya 307 zilikaguliwa na kubaini uwepo wa taasisi za dini ambazo hazina usajili na hazizingatii masharti ya usajili. Pamoja na ukaguzi huo, viongozi wa taasisi za dini walisisitizwa kuzingatia masharti ya usajili ili kuendelea kudumisha amani na utulivu nchini. Aidha, jumuiya 1,200 zimetangazwa katika Gazeti la Serikali kwa ajili ya kufutwa kwa kutokidhi matakwa ya kisheria.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, Wizara imetumia Shilingi milioni 162.59 kwa ajili ya kuboresha Mfumo wa Ki-elektroniki wa Usajili na Usimamizi wa Jumuiya (Registration of Societies Management Information System – RSMIS). Mfumo huo umewezesha kuhakiki taarifa za Jumuiya za Kiraia 9,433 kati ya Jumuiya 11,708 zilizosajiliwa hadi kufikia tarehe 01 Mei 2025 na kuziingiza katika kanzidata.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, mfumo umesaidia wananchi kupata *control number* kwenye mfumo, kulipa ada na tozo za Jumuiya, na kuwasilisha nyaraka ambazo awali zilitakiwa kuwasilishwa zikiwa katika nakala ngumu (Hard copies) katika Ofisi ya Msajili wa Jumuiya. ***Natumia fursa hii kuwahamasisha wananchi kuendelea kutumia mfumo wa RSMIS unaopatikana kupitia http://rsmis.moha.go.tz ili kupata huduma za usajili, kufanya malipo na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za Jumuiya za Kiraia zilizosajiliwa kwa urahisi.***

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Shilingi bilioni 1.07 zimetengwa kwa ajili ya kazi zifuatazo: kusajili na kuhakiki jumuiya za kidini na zisizo za kidini; kufanya ukaguzi wa jumuiya; kufanya marekebisho ya Sheria ya Jumuiya, Sura 337; kutoa elimu juu ya umuhimu wa kusajili vikundi na vyama vya kiraia; kuboresha vitendea kazi na maslahi ya watumishi wa Ofisi ya Msajili wa Jumuiya na kuwajengea uwezo wa kufanya uchambuzi na tathmini ya vihatarishi vya kiusalama; kufanya kampeni za uhamasishaji wa kusajili taasisi, vyama na vikundi; kushiriki katika maonesho ya kitaifa; na kuanzisha ofisi za kanda na wilaya.

## UHALIFU WA USAFIRISHAJI HARAMU WA BINADAMU

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, jumla ya waathirika 156 wa uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu waliokolewa na kusaidiwa. Uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu unaathiri zaidi watoto na wanawake, ambapo kati ya waathirika hao, 102 walikuwa watoto na 54 walikuwa watu wazima. Aidha, waathirika 119 waliokolewa hapa nchini na 37 waliokolewa nje ya nchi hususan katika nchi za Malaysia (14), Thailand (12), China (6), Oman (4) na Dubai (1).

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi hiyo imepungua ikilinganishwa na waathirika 184 waliookolewa kipindi kama hicho mwaka 2023/24 kutokana na jitihada za Serikali za kuelimisha umma na kuongeza operesheni za kudhibiti mitandao inayojihusisha na uhalifu huo. Aidha, jumla ya wahalifu 19 wanaojihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025 Wizara imetoa mafunzo kwa wadau 939 wa Haki Jinai kuhusu kudhibiti usafirishaji haramu wa binadamu ikilinganishwa na wadau 157 waliopewa mafunzo kama hayo mwaka 2023/24. Idadi hiyo imeongezeka kutokana na jitihada za Serikali kuongeza fedha za kutoa mafunzo na uungwaji mkono kutoka kwa wadau.

**198.** ***Mheshimiwa Spika****,* Wizara imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu uhalifu wa usafirishaji haramu wa binadamu na madhara yake. Aidha, elimu hiyo imetolewa kwa wadau 1,720 kupitia makongamano yaliyofanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza, Simiyu na Kusini Unguja. Wadau hao ni pamoja na Watendaji wa Kata na Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji, Masheha, Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Kisiasa, Walimu na Wajumbe wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto.

**199.** ***Mheshimiwa Spika****,* elimu pia imetolewa kwa wanafunzi 2,320 wa shule za msingi, sekondari na vyuo pamoja na wananchi 960 walioshiriki maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu yaliyofanyika Jijini Dodoma tarehe 30 Julai 2024. Ili kuwafikia wananchi wengi, hususan walioko vijijini, Wizara kupitia mitandao ya simu za mikononi ilituma ujumbe mfupi wa simu za mkononi kwa wananchi ili kuwatahadharisha na uhalifu huo.

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu huo, Serikali imefanya marekebisho madogo ya Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura ya 432 ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wake. Marekebisho hayo yanaipa nguvu ya kisheria Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu

wa Binadamu kuingia mahali popote kwa lengo la kuzuia na kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu; kuomba taarifa au kumuita na kumuhoji mtu yeyote anayejihusisha na usafirishaji haramu wa binadamu; na kuongezeka kwa idadi ya kesi zinazochunguzwa kufikia 77 katika kipindi cha Oktoba 2024 hadi Aprili 2025, ikilinganishwa na kesi 22 zilizochunguzwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

**201.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2025/26 Wizara imepanga kufanya kazi zifuatazo: kuanzisha Kituo cha kupokea Taarifa za Uhalifu wa Usafirishaji Haramu wa Binadamu (*Counter Trafficking in Persons Call Centre*) ambapo wananchi watapiga simu bure kuripoti vitendo hivyo kupitia namba ya dharura 195; kuanzisha Mfumo wa Kupokea, Kusimamia na Kuhifadhi Taarifa za Usafirishaji Haramu wa Binadamu (TIPMIS); kukamilisha ujenzi wa kituo salama kwa ajili ya kutoa hifadhi ya muda na ulinzi kwa waathirika na mashahidi wa usafirishaji haramu wa binadamu Jijini Dodoma na kuanza ujenzi wa kituo kama hicho Jijini Dar es Salaam; na kuandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu kwa mwaka 2025/26 – 2027/28.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa kufanyika ni: kuanzisha ofisi ndogo ya Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu Dar es Salaam; kufanya uchunguzi na operesheni za kudhibiti mitandao inayojihusisha na uhalifu huo; kuokoa, kusaidia na kuwaunganisha waathirika na familia zao; kutoa mafunzo kwa wadau na elimu kwa umma; kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kikanda; na kununua vitendea kazi muhimu ikiwemo kompyuta na samani za ofisi. Jumla ya Shilingi bilioni 2.04 zimetengwa katika mwaka 2025/26 ili kutekeleza kazi hizo.

## C. SHUKRANI

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Mhe. Daniel B. Sillo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Ndugu Ally S. Gugu Katibu Mkuu na Dkt. Maduhu I. Kazi Naibu Katibu Mkuu kwa kunipa ushirikiano katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya Wizara.

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, nawapongeza Wakuu wa Vyombo vya Usalama vilivyopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu nchini na kuwezesha wananchi kutekeleza shughuli za kijamii na kiuchumi. Viongozi hao ni: Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi, Camillus M. Wambura; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Jeremiah Y. Katungu; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John W. Masunga; na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna P. Makakala. Aidha, namshukuru Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu James W. Kaji.

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nawashukuru Mhe. Balozi Khamis Kagasheki ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole na Meja Jenerali Mstaafu Hamisi R. Semfuko, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Magereza, Ndugu Omari Issa, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi, IGP Mstaafu Balozi Ernest J. Mangu, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Mhe. Jaji Stephen Magoiga, Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Huduma kwa Jamii kwa usimamizi mzuri wa bodi hizo. Pia, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati na Bodi hizo kwa ushauri na utendaji kazi wa ufanisi.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi wakiwemo Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Makamishna, Makamishna Wasaidizi, Wakuu wa Vitengo, Maafisa, Wakaguzi na askari kwa kufanya kazi kwa juhudi na weledi.

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa shukrani kwa nchi za India, Marekani, Saudi Arabia, Singapore, Ujerumani, Urusi, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Jamhuri ya Watu wa China, na Umoja wa Ulaya (EU). Aidha, nitoe shukrani kwa Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni: IOM, UNDP, UNHCR, UNICEF, UN–Women na WFP. Taasisi za Elimu na Makampuni yafuatayo: CAMARTEC, Chuo cha Uhasibu – Arusha, Chuo cha Ustawi wa Jamii – Dar es Salaam, NACTVET, PUMA Energy, REA, STAMICO, Taifa Gas, TPA, VETA, Benki za CRDB na NMB.

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru Taasisi za Kidini na zisizo za Kidini kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika kuhamasisha amani na utulivu nchini. Pia, nawashukuru wananchi wote kwa ujumla na niwasihi kujiepusha na vitendo vya uvunjifu wa amani.

**209.** ***Mheshimiwa Spika***, naishukuru sekta ya habari kwa kufanya kazi kwa uzalendo na ushirikiano wanaotoa kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Serikali kwa ujumla. ***Naomba kurejea wito alioutoa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 05 Mei 2025 wakati wa utoaji wa Tuzo za Samia Kalamu Awards Jijini Dar es Salaam, ambapo alisema na ninanukuu "zungumza, sema, chambua lakini uzalendo uwepo, hapa ndipo ulipozaliwa, hapa ndipo ulipotoka na utakapomalizikia"***.

**D. HITIMISHO**

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/26**

**210.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/26 Wizara imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 428,000,000,000 ikiwa ni ongezeko la Shilingi 24,700,000,000 kutoka Shilingi 403,300,000,000 mwaka 2024/25 sawa na asilimia 6.12. Miongoni mwa mikakati iliyowekwa na Wizara kufikia lengo hilo ni kuimarisha huduma za Uhamiaji Mtandao (e-immigration); kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki; na ununuzi wa vitendea kazi vya kisasa.

**Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2025/26**

**211.** ***Mheshimiwa Spika,*** bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeongezeka kutoka Shilingi trilioni 1.71 mwaka 2024/25 hadi kufikia Shilingi trilioni 2.06 mwaka 2025/26, sawa na ongezeko la asilimia 21. ***Kwa niaba ya Viongozi na Watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi namshukuru kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuingozea bajeti Wizara ambayo itaboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.***

**212.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba Bunge lako liidhinishe Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2025/26 ya jumla ya **Shilingi 2,067,161,717,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 701,703,184,000**

ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 950,318,192,000** ni Mishahara na **Shilingi 415,140,341,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, **Shilingi 388,610,747,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 26,529,594,000** ni fedha za nje.

**209. *Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

Innocent Lugha Bashungwa (Mb.)
**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
21 Mei, 2025

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, kwa kusoma *very professionally*. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa NUU. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote naomba Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mambo ya Ndani ya nchi kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iingie yote kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa naomba nianze kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake maridhawa na kwa kusimamia ipasavyo uboreshaji wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na kuboresha na kuimarisha mfumo wa haki jinai nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Maelezo ya Jumla. Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge; kuwa kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika mwezi Machi, 2025 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni ya 117 (1) hadi Kanuni 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MHE. VITA R. KAWAWA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inajumuisha mafungu matano ambayo ni:-

(i) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
(ii) Fungu 28 – Jeshi la Polisi;
(iii) Fungu 29 – Jeshi la Magereza;
(iv) Fungu 51 – Wizara, ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho *(NIDA);* na
(v) Fungu 98 – Idara la Uhamiaji

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu nne ambazo ni: -

(i) Sehemu ya kwanza inayoeleza maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi, mawanda na muundo wa taarifa;

(ii) Sehemu ya pili inayobainisha uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Sehemu ya tatu inayoelezea uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iv) Sehemu ya Nne inayobainisha maoni na ushauri pamoja na kuhitimisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni namba 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi miwili ambayo ni miradi ya ujenzi wa Kituo cha Zimamoto na Ukoaji Mkoani Manyara pamoja na mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara. Taarifa ya kina kuhusu hali ya miradi iliyokaguliwa ni kama ilivyoelezwa katika Kiambatanisho namba moja cha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa miradi inakabiliwa na changamoto za kibajeti kubwa mbili. Moja, ni baadhi ya miradi kutokupata kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge; na changamoto ya pili ni kutokupata fedha kwa wakati kwa miradi iliyopokea fedha. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa: -

(i) Si jambo jema kwa miradi inayotekelezwa na vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha na Bunge ni jambo

linalokwamisha lengo la kuwa na miradi inayotekelezwa na Wizara hii; na *(Makofi)*

(iii) Utekelezaji wa miradi inayokwama kutokana na changamoto za kifedha unatatiza azma ya Serikali ya kuimarisha vyombo vinavyohusika na usalama wa raia na mali zao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa taarifa ya uzingatiaji wa maoni na ushauri. Wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali ya mpango na bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri kuhusu uzingatiaji wa ushauri huo. Taarifa ya kina kuhusu uzingatiaji wa maoni ya ushauri wa Kamati umeelezwa katika kiambatisho namba mbili cha taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 403.3 kwa mafungu yote matano. Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara hadi kufukia mwezi Februari, 2025 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa ni shilingi bilioni 263.37 sawa na 65% ya lengo la mwaka lililopangwa. Taarifa ya kina kuhusu ukusanyaji wa maduhuli ni kama inavyoelezwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, Bajeti iliyoidhinishwa Bunge, hutoa matokeo yaliyotarajiwa iwapo fedha zinapatikana kama ilivyokusudiwa. Ili kujiridhisha na matokeo ya Bunge kuidhinisha bajeti, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha. Uchambuzi huo ulibaini yafuatayo:-

(i) Kiasi cha jumla ya fedha zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Februari, 2025 ni 67% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara. Kiasi hicho kilipatikana katika kipindi cha robo ya tatu ya muda wa utekelezaji ambacho ni sawa na 75%;

(ii) Wakati Bunge lilipoidhinisha bajeti ya Wizara hii, kiasi cha matumizi ya uendeshaji *(OC)* kilikuwa ni 32% ya jumla ya bajeti ya mafungu yote. Upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya aina hiyo umekuwa ni 32% ya jumla ya fedha kiasi kilichopatikana kwa mafungu yote;

(iii) Kiasi cha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo kilikuwa ni 17% ya bajeti yote ya Wizara wakati Bunge lililopitisha Bajeti hiyo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo ni 21% ya jumla ya fedha iliyopokelewa na Wizara;

(iv) Kiasi cha fedha kilichopatikana kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 85% ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo;

(v) Jeshi la Polisi limepokea zaidi ya 98% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fungu hilo;

(vi) Jeshi la Magereza (Fungu 29), Wizara yenyewe (Fungu 51) na Jeshi la Uhamiaji (Fungu 93) walipokea fedha za maendeleo chini ya 50%;

(vii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni 64% ya kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo; na

(viii) Jumla ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matano ni 83% ya jumla ya bajeti ya Wizara nzima iliyoidhinishwa na Bunge. Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya matumizi hayo ni 64% ya jumla ya kiasi cha fedha zote kilichopokelewa kwa mafungu yote matano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ni wa kuridhisha. Uchambuzi umeonesha kuwa, kwa mafungu yote Wizara imepokea

zaidi ya 50% ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, uchambuzi unaonesha kuwa kuna mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, Fungu 29 - Jeshi la Magereza, Fungu 51- Wizara; na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji, yamepata fedha za maendeleo chini ya 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, ni dhahiri kwamba: -

(i) Kwa ujumla uendeshaji wa shughuli za kuhakikisha usalama wa raia na mali zao haukukabiliwa na changamoto kubwa. Hili limethibitishwa na taarifa za usalama wa raia zinazoonesha hali ya usalama kwa ujumla ni shwari na madhubuti;

(ii) Mipango ya kuboresha huduma za urekebu pamoja na miundombinu ya magereza kwa lengo la kuongeza tija ya kuwa na magereza nchini, inafaa kuwekewa mkazo zaidi kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Mipango ya thabiti ya huduma za uhamiaji, wakimbizi, uangalizi, vitambulisho vya Taifa, usajili wa jumuiya za kidini na zisizo za kidini, biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu ni miongoni mwa mambo yanayohitaji kuwekewa mkazo katika kipindi kilichobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Kamati ilichambua mpango wa utekelezaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kulinganisha na majukumu ya msingi ya Wizara na vyombo vyake vyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi umeonesha namna mipango iliyobainishwa na Wizara inavyowezesha kuimarisha usalama wa raia na mali zao, utulivu na amani nchini, udhibiti wa uingiaji na utokaji nchini, usajili wa

jumuiya, huduma za vitambulisho vya Taifa pamoja na mambo mengine kuhusu majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio na Mapato ya Mwaka 2025/2026 umeonesha mambo yafuatayo: -

(i) Kiasi cha mapato kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kimeongezeka kwa asilimia sita ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Hata hivyo, uzoefu wa ukusanyaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya 65% hadi kipindi cha robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji;

(ii) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28 – Jeshi la Polisi, Fungu 29 – Jeshi la Magereza na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji yanategemewa kufanikisha ongezeko la makadirio ya mapato. Uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulionesha kuwa Jeshi la Polisi halikuwa limefika 75% wakati wa robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji;

(iii) Makadirio ya makusanyo kwa Fungu 51 – Wizara yenyewe yanalingana na makadirio kwa Mwaka wa Fedha unaokwisha yaani 2024/2025; na

(iv) Makadirio ya makusanyo kwa Fungu 29 – Jeshi la Magereza yameongezeka kwa 25%. Uzoefu wa makusanyo unaonesha kuwa makadirio ya fungu hili yanaweza kuongezwa na kukusanywa zaidi kuliko lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kidigitali, uhaba wa vitendea kazi na upungufu wa rasilimali watu vinaendelea kuwa changamoto. Uzoefu wa hali katika kipindi cha miaka mitano unaonesha kuwa mambo hayo yamekuwa yakiathiri makusanyo ya mapato. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 changamoto hizo zisipofanyiwa kazi, lengo la makusanyo linalowekwa linaweza lisifikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti kwa

mwaka 2024/2025. Aidha, ulinganisho ulifanyika ili kubaini uwiano wa miradi inayopangwa kutekelezwa na shughuli za kawaida za uendeshaji. Kutokana na uchambuzi huo ilibainika kama ifuatavyo: -

(i) Matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa 18% ya jumla ya bajeti, kama inavyoonekana katika kielelezo namba sita cha taarifa yetu hii;

(ii) Makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo yameongezeka kwa 26% ikilinganishwa na makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Uwiano wa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa bajeti nzima ya mafungu yote ya Wizara umeongezeka kwa wastani wa 1.4% kama inavyoonekana katika kielelezo namba saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ujumla. Uchambuzi wa jumla wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unaonesha yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Wizara hii imeongezeka kwa 17% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/2025;

(ii) Makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi, usalama, amani na utulivu nchini; na

(iii) Makadirio ya matumizi yaliyowasilishwa yasipoidhinishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, majukumu ya Wizara hii yatakuwa mashakani na shughuli za umma nchini zitaingia matatani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maoni, ushauri na hitimisho; uchambuzi ulioelezewa katika taarifa hii umeiwezesha Kamati kuwa na mtazamo na maoni yafuatayo:-

(i) Umefika wakati sasa Wizara itekeleze ipasavyo maelekezo ya kuanza kutoa jamii namba kwa watu;

(ii) Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ina majukumu makubwa katika usajili wa taasisi za kidini na zisizo za kidini. Hata hivyo, ofisi hii haitekelezi ipasavyo majukumu yake kwa kuwa ni ofisi tu ndani ya Wizara, na hivyo inashindwa kutoa huduma kwa ufanisi hadi ngazi ya kata na mtaa. Hali hii inasababisha uwepo wa taasisi za dini ambazo hazijasajiliwa, lakini zinatoa huduma. Hivyo, imefika wakati sasa Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iwe taasisi kamili;

(iii) Uboreshaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika nyanja ya vifaa na zana za kisasa, uende sambamba na kutoa mafunzo kwa Askari juu ya matumizi na utunzaji wa vifaa na zana hizo;

(iv) Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa na kujivunia. Hata hivyo, ni muhimu juhudi hizo ziende sambamba kuimarisha matumizi ya vifaa na zana za kisasa za kiteknolojia;

(v) Uwepo wa wakimbizi nje ya makambi na hifadhi ya wakimbizi kinyume na sheria na taratibu ni suala linalopaswa kupewa kipaumbele na kushughulikiwa ipasavyo na Wizara. Suala hili lisiposhughulikiwa kikamilifu, athari zake ni kubwa kwa nchi. Hivyo, Serikali iwabaini na kuwachukulia hatua stahiki wakimbizi wote walio nje na kambi na hifadhi ya wakimbizi kinyume na sheria na taratibu za wakimbizi;

(vi) Biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu inakua kwa kasi nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 ipo haja ya Wizara kutoa mkazo katika mapambano ya kuzuia na kukabiliana na biashara hii haramu ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu athari zake; na

(vii) Ni wakati mwafaka sasa kwa Wizara kuweka mkakati wa kupata ardhi kwa ajili ya matumizi ya vyombo vilivyo chini ya Wizara hii kwa matumizi ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa jumla:-

(i) Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kutaongeza ufanisi wa majeshi hayo katika utendaji kazi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli;

(ii) Kukua kwa teknolojia kunachangia kuibuka kwa uhalifu mpya na njia mpya za uhalifu. Ili kukabiliana na hali hii, Serikali iimarishe matumizi ya zana na vifaa vya kidigitali katika utendaji kazi wa majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Suala hili liende sambamba na kuimarisha mafunzo kwa askari na watumishi; *(Makofi)*

(iii) Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa umma juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, kuhusu athari zake na namna ya kukabiliana na biashara hiyo inayokua kwa kasi nchini; na

(iv) Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ikamilishe mchakato wa kuanza kutumia jamii namba. Kufanya hivyo kutasaidia mwananchi kuwa na namba moja ya utambulisho katika kila nyanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri mahsusi, Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji:-

(i) Serikali ihakikishe ujenzi unaoendelea wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mikoa mbalimbali unazingatia matumizi ya vifaa na zana za kisasa za kitekonolojia kwa matumizi ya sasa na baadaye. Kufanya hivyo kutasaidia majengo hayo kutumika kwa tija iliyokusudiwa;

(ii) Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutoa mafunzo ya kisasa ya matumizi ya vifaa vya kisasa vya uokozi na kuzima moto kwa askari wake juu ya matumizi na utunzaji wa vifaa vinavyotarajiwa kupokelewa kuanzia mwaka huu 2025; na

(iii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lifanye tathmini ya mkakati wake wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya moto na majanga

mbalimbali. Tathmini hiyo itumike kuzigeuza changamoto zilizopo kama fursa ya kuimarisha utekelezaji wa elimu kwa umma kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 28 -Jeshi la Polisi:-

(i) Jeshi la Polisi liendelee kusimamia inavyostahili katika kuhakikisha Askari wa Jeshi la Polisi wanazingatia sheria, kanuni, taratibu, miiko, weledi, tamaduni na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao; na

(ii) Jeshi la Polisi liendelee kuimarisha ushiriki wa jamii katika dhana nzima ya usalama wa raia na mali zao. Kufanya hivyo kutasaidia jeshi hilo kuongeza huduma zake kwa wananchi na hivyo kuimarisha mapambo ya uhalifu katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 29 - Jeshi la Magereza:-

(i) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa magereza mapya mawili pamoja na ukarabati wa magereza makuu manne kwa mwaka wa fedha 2025/2026; mantiki ya kutenga fedha hizo itapatikana ikiwa Jeshi la Magereza litakamilisha hatua za awali kwa wakati na kuomba fedha kwa kuzingatia mpango uliowekwa;

(ii) Ili kufikia tija na malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa mafunzo ya urekebu, Serikali iboreshe miundombinu chakavu ya magereza nchini; na *(Makofi)*

(iii) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu na kuimarisha Mfumo wa Mahakama Mtandao katika magereza nchini ikiwa ni sehemu ya uimarishaiji wa mfumo wa Haki Jinai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 51- Wizara: -

(i) Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kwa kuhakikisha kuwa inatekeleza mpango wa utambuzi

wa watu kwa kutoa jamii namba kwa raia halali wa Tanzania ikiwemo watoto kuanzia chini ya mwezi mmoja; na

(ii) Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iwe Mamlaka/Taasisi kamili inayojitegemea. Kufanya hivyo kutasaidia taasisi hiyo kutekeleza majukumu yake kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mtaa na wilaya, tofauti na sasa ambapo inatekeleza majukumu yake kama idara ndani ya Wizara.

(iii) Serikali iweke Mkakati unaotekelezeka wa kuhakikisha inawabaini na kuchukulia hatua stahiki wakimbizi wote walio nje ya kambi na makazi ya wakimbizi kinyume na sheria na taratibu za wakimbizi;

(iv) Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Kimataifa na Kitaifa iharakishe mpango wake wa kuwarejesha wakimbizi katika nchi zao. Kwani wakimbizi wengi walioko nchini hali ya amani, utulivu na usalama imeimarika katika nchi zao; na

(v) Wizara iweke mkakati kuhakikisha vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii vinapata maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya wakati ujao kutokana na ukweli kuwa matumizi ya ardhi yanaongezeka kwa kasi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Fungu 93 – Uhamiaji: Serikali ifunge mfumo wa uhamiaji Mtandao katika Ofisi zote za Uhamiaji zisizo na mifumo hiyo sambamba na mfumo wa udhibiti wa mipaka kwenye vituo 26 vya kuingia na kutoka nchini. Kufanya hivyo kutaimarisha udhibiti wa uingiaji na utokaji wa raia na wageni nchini kupitia mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee na mkakati wa makusudi wa kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1,000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani ikiwemo kutumia Mifumo ya Udhibiti Mipaka *(E-border System)*. Kufanya hivyo kutasaidia kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu pamoja na bidhaa za magendo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ninapenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao kwangu umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Mbunge na Naibu Waziri; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge, pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Ally Senga Gugu; Naibu Katibu Mkuu; na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka. Aidha, ninapenda kuishukuru Sekretariati ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii, lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**26 MEI, 2025**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, kwa wasilisho hili, naliomba Bunge lako tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali kisha liidhinishe Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja pamoja na maoni na ushauri wa Kamati.

### 1.2 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kanuni hizo kwa pamoja, zimeweka masharti yanayohusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kabla ya kujadiliwa Bungeni. Kwa masharti hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilifanya uchambuzi na kupata maudhui ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na uchambuzi huo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge yaliyohusu kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaokwisha. Kazi hiyo,

ilifanyika kati ya tarehe 12 na 18 Machi, 2025. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulitumia matokeo ya ziara ya ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi.

### 1.3 Mawanda ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, mawanda ya Taarifa ya Uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanategemea muundo na majukumu ya Wizara inayohusika. Muundo na Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi umejengwa kwenye msingi wa Hati Idhini kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 383 na 385 la tarehe 7 Mei, 2021 pamoja na marekebisho yaliyofanyika kwa Tangazo la Serikali Na. 534 la tarehe 2 Julai, 2021.[1]

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ilianzishwa na kupewa majukumu ya kushughulikia uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa sera zinazohusu usalama wa raia na mali zao, uhamiaji, wakimbizi na uraia nchini. Aidha, Wizara hii inahusika na utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Jeshi la Uhamiaji. Vilevile, Wizara imepewa wajibu wa kusimamia na kuratibu masuala ya Huduma za Wakimbizi, Vitambulisho vya Taifa, Usajili wa Jumuiya za Kidini na zisizo za kidini, kupambana na Biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu na Huduma za Uangalizi (Probation).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa wigo huo wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, uchambuzi uliofanywa na Kamati umejumuisha Mafungu matano (5) ya kibajeti ambayo ni:-

(i) Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;

(ii) Fungu 28 - Jeshi la Polisi;

(iii) Fungu 29 - Jeshi la Magereza;

[1] Taz. https://www.moha.go.tz

(iv) Fungu 51 - Wizara (Makao Makuu) ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA); na

(v) Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilitengwa kwenye Mafungu hayo. Aidha, Bajeti inayoombwa na Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2025/2026 nayo imetengwa kwenye Mafungu hayo. Kwa msingi huo, Uchambuzi unaozingatia mafungu hayo, umegusa wigo mpana wa dhima ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**1.4 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia urahisi wa kuelezea matokeo ya uchambuzi kwa namna inayoweza kueleweka kwa pamoja na masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu Muundo wa Taarifa ya Kamati ya Bunge inayoingia Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza inayoeleza maelezo ya utangulizi na kubainisha msingi, mawanda na muundo wa Taarifa;
(b) Sehemu ya Pili inayobainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025;
(c) Sehemu ya Tatu inayoelezea uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa fedha 2025/2026; na
(d) Sehemu ya Nne inayobainisha Maoni na Ushauri pamoja na kuhitimisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muundo huo, Kamati inaamini kuwa maudhui na mtiririko huu utakuwa na manufaa kwa Bunge na kwa Wabunge watakaopata fursa ya kuchangia katika hoja hii. Aidha, maoni na ushauri wa Kamati utapata msingi na kuwa rahisi kuzingatiwa na Bunge na Mtoa Hoja.

**26 MEI, 2025**

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2024/2025 NA MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Masharti ya Kanuni ya 117(1) na (2) ya Kanuni za Bunge yamebainisha idadi ya siku kwa ajili ya kutembelea miradi na kufanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti. Jumla ya siku zisizozidi saba zilipaswa kutumika kwenye ziara hizo na siku zisizozidi tisa zilipaswa kutumika kwa ajili ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti. Nafurahi kulijulisha Bunge kuwa masharti hayo yalizingatiwa. Kwa kufanya hivyo, Kamati inaweza kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Miradi iliyoidhinishiwa Fedha kwa mwaka 2024/2025;

(b) Kubainisha mwenendo wa upatikanaji wa fedha ulivyo ikilinganishwa na makusudio ya Bunge lilipopitisha Bajeti ya Wizara hiyo;

(c) Kulinganisha uzoefu unaojitokeza katika utekelezaji wa bajeti inayokwisha na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka unaofuata; na

(d) Kutoa ushauri utakaoliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo wajibu wa kuishauri Serikali wakati wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

### 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya Taarifa inahusu uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa lengo la kufafanua hatua iliyofikiwa hadi kufikia Mwezi Februari 2025. Ufafanuzi huo unagusa mambo matano yafuatayo:-

(i) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2024/2025;

(ii) Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri;

(iii) Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato
(iv) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina
(v) Hatua iliyofikiwa katika Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, mambo hayo matano yanatoa taswira muhimu kwa Bunge kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Bunge litakapotaarifiwa kuhusu mambo hayo, litakuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kujadili hotuba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliyoiweka mezani mapema leo hii.

**2.2.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara hii ilipaswa kutekeleza jumla ya miradi 25 katika Mikoa mbalimbali nchini. Hata hivyo, kwa madhumuni ya masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea miradi miwili inayotekelezwa katika Mkoa wa Manyara. Ufafanuzi wa hali ya Utekelezaji wa Miradi hiyo unaonekana katika **Kiambatisho Na. 01** cha Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya Utekelezaji wa Miradi inakabiliwa na changamoto za kibajeti kubwa mbili: Moja ni baadhi ya miradi kutokupata kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na changamoto ya pili ni kutokupata fedha kwa wakati kwa miradi iliyopokea fedha. Kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa:

(i) Si jambo jema kwa Miradi inayotekelezwa na vyombo vya Ulinzi na Usalama vilivyo chini ya Wizara hii kutopewa fedha za maendeleo kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi iliyoidhinishiwa fedha na Bunge ni jambo linalokwamisha lengo la kuwa na miradi inayotekelezwa na Wizara hii;

(iii) Utekelezaji wa miradi unaokwama kutokana na changamoto za kifedha unatatiza azma ya Serikali ya kuimarisha vyombo vinavyohusika na usalama wa raia na mali zao kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mtazamo huo, upo umuhimu kwa Serikali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2024/2025. Aidha, uzoefu wa mkwamo wa utekelezaji wa miradi kwa mwaka wa fedha unaokwisha unastahili kutumika ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaokuja.

### 2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa Kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri kwenye Maeneo mbalimbali ya Mpango na Bajeti ya Wizara hii. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia ushauri unaotolewa, Kamati ilipokea maelezo ya Waziri kuhusu uzingatiaji wa ushauri huo. Maelezo kamili kuhusu maelezo hayo yanafafanuliwa katika **Kiambatisho Na. 02**.

### 2.2.3 Uchambuzi wa Hali ya Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa hali ya ukusanyaji wa mapato yaliyokadiriwa umezingatia ulinganisho wa namna zifuatazo:-

(i) Ulinganisho wa hali ya ukusanyaji kati ya Februari 2024 na Februari 2025.
(ii) Ulinganisho wa kiasi kilichokusanywa na Makadirio kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 01**

**Kielelezo Na. 1 Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Makusanyo kwa kila Fungu**

| FUNGU | Makadirio ya Mapato kwa mwaka 2024/2025 | Makusanyo hadi Februari, 2025 | Asilimia |
|---|---|---|---|
| **14 – Zimamoto** | 11,500,000,000 | 9,088,440,377.5 | 79 |
| **28 – Polisi** | 110,500,000,000 | 63,581,373,564 | 58 |
| **29 – Magereza** | 800,000,000 | 774,995,464 | 97 |
| **51 - Wizara** | 500,000,000 | 262,720,809 | 52 |


| | | | |
|---|---|---|---|
| **93 - Uhamiaji** | 280,000,000,000 | 189,666,862,083.89 | 68 |
| **JUMLA** | **403,300,000,000** | **263,374,392,298.39** | 65 |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***


(iii) Ulinganisho wa Mchango wa kiasi kinachokusanywa kwenye kila Fungu na mchango wa kiasi kilichokadiriwa kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 02.**

**Kielelezo Na. 2 Ulinganisho wa Makadirio ya Mchango wa Kila Fungu katika Mapato na Mchango halisi kwenye Makusanyo**

**MCHANGO WA KILA FUNGU WAKATI MAKADIRIO**




**MCHANGO WA KILA FUNGU KATIKA MAKUSANYO**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, vigezo vitatu vilivyotajwa, vimezingatiwa katika Uchambuzi kwa kuwa vinabainisha uthabiti wa makadirio na ufanisi wa juhudi za ukusanyaji wa mapato. Aidha, uchambuzi wa namna hiyo unaonesha sehemu zinazohitaji kuwekewa mkazo na sehemu zinazostahili kutumainiwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa vigezo hivyo, Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi kilichokusanywa hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 ni sawa na **asilimia 65** ya lengo la mwaka lililopangwa;

(ii) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yakilinganishwa na makadirio yalifikia **asilimia 79,** Uhamiaji **asimia 68** na Jeshi la Polisi **asilimia 58;**

(iii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza yaliyofikia **asilimia 97** ya lengo la Fungu hilo kwa mwaka na Wizara Makao Makuu yaliyofikia **asilimia 52** ya lengo;

(iv) Makusanyo ya jumla kwa wizara nzima yamefikia **asilimia 65** pungufu kidogo ya kiwango kilichostahili. Hali hiyo imetokana na Fungu 28 na 51 kushindwa kufikia lengo la makusanyo lilowekwa kufikia Mwezi Machi, 2025;

(v) Makusanyo ya Jeshi la Zimamoto yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 3** Taarifa zinaonesha yamechangia kwa **asilimia 4** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2025;

(vi) Makusanyo ya Jeshi la Polisi, yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 27** na yamechangia **asilimia 28** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2025;

(vii) Makusanyo ya Jeshi la Magereza**,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.2** lakini yamechangia kwa **asilimia 0.3** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2025;

(viii) Makusanyo ya Wizara yenyewe**,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 0.12** lakini yamechangia kwa **asilimia 0.10** kwenye kiasi kilichokusanywa hadi Mwezi Februari, 2025; na

(ix) Makusanyo ya Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji**,** yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa **asilimia 69**, taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu hilo limechangia **asilimia 72** ya kiasi kilichokusanywa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaweza kuongeza lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, Jeshi la Polisi na Wizara zinahitaji kuongeza juhudi kidogo ili kuboresha makusanyo yanayotakiwa. Aidha, kuna umuhimu wa kufanya tathmini ya lengo la makusanyo kwa upande wa Jeshi la Magereza kwani Kamati inaamini inaweza kukusanya zaidi ya lengo lililowekwa.

### 2.2.4 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** bajeti inayoidhinishwa na Bunge hutoa matokeo yaliyotarajiwa iwapo fedha zinapatikana kama ilivyokusudiwa. Ili kujiridhisha na matokeo ya Bunge kuidhinisha Bajeti, Kamati ilichambua mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia mambo yafuatayo:- (i) Kiwango cha Jumla ya fedha iliyopatikana ikilinganishwa na jumla ya bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa Wizara hii kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 03**.

**Kielelezo Na. 3 Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na Kiasi cha Fedha iliyopatikana kwa kila Fungu**


| FUNGU | Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2024/2025 | Asilimia | Fedha iliyopatikana hadi Februari 2025 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **14-Zimamoto** | 66,237,270,000 | 4 | 42,539,341,463.27 | 3.6 |
| **28-Polisi** | 1,136,734,791,000 | 66.4 | 824,247,966,918.76 | 70.5 |
| **29-Magereza** | 306,419,189,000 | 18 | 174,385,965,631 | 14.9 |
| **51-Wizara** | 71,442,192,000 | 4 | 42,483,467,008.05 | 3.6 |
| **93-Uhamiaji** | 130,877,545,000 | 7.6 | 84,478,979,624.45 | 7 |
| **JUMLA** | **1,711,710,987,000** | **100** | **1,168,135,720,645.5** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***


(ii) Uwiano wa aina ya matumizi wakati wa kupitisha bajeti ukilinganishwa na uwiano wa aina hizo kwa fedha zilizopatikana kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 04**.

**Kielelezo Na. 4 Makadirio ya Uwiano wa Aina za Matumizi ukilinganishwa na Uwiano wa Upatikanaji wa fedha kwa Aina za Matumizi**

**Uwiano wakati wa Makadirio**





**Uwiano katika upatikanaji wa fedha**





***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

(iii) Uwiano wa bajeti za Mafungu matano kama ilivyopitishwa na Bunge ukilinganishwa na uwiano wa fedha zilizopatikana kwa mafungu yote matano kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 05**;

**Kielelezo Na. 5 Uwiano wa Bajeti kwa kila Fungu ukilinganishwa na Uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa Miongoni mwa Mafungu hayo Uwiano wakati wa makadirio Uwiano katika upatikanaji wa fedha**




***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

(iv) Kiwango cha fedha zilizopatikana hadi kufikia Mwezi Februari 2025 kikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2024.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo hivyo ni viashiria muhimu vya mwenendo wa kisera katika usalama wa raia na mali zao kwenye shughuli za umma kwa ujumla. Ulinganishaji unabainisha maeneo yanayohitaji msisitizo na ambayo yanaimarisha shughuli za umma, ustawi, amani na utulivu nchini. Mambo hayo kwa ujumla ni sehemu ya mambo muhimu yanayostahili jicho la chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia hayo, Uchambuzi umebainisha yafuatayo:-

(i) Kiasi cha Jumla ya fedha zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Februari, 2025, ni **asilimia 67** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara. Kiasi hicho kilipatikana katika kipindi cha robo ya tatu ya muda wa utekelezaji ambacho ni sawa na **asilima 75**;

(ii) Wakati Bunge lilipoidhinisha Bajeti ya Wizara hii, Kiasi cha Matumizi ya Uendeshaji (OC) kilikuwa ni **asilimia 32** ya Jumla ya Bajeti ya Mafungu yote. upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya aina hiyo umekuwa ni **asilima 32** ya jumla ya fedha kiasi kilichopatikana kwa Mafungu yote.

(iii) Kiasi cha fedha kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kilikuwa ni **asilimia 17** ya bajeti yote ya Wizara wakati Bunge lililopitisha Bajeti. Lakini hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 fedha zilizopatikana kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 21** ya Jumla ya fedha iliyopokelewa na Wizara.

(iv) Kiasi cha Fedha kilichopatikana kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 85** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo.

(v) Jeshi la Polisi limepokea zaidi ya **asilimia 98** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu hilo; wakati Jeshi la Magereza (Fungu 29) lilikuwa limepokea **asilimia 15** tu ya fedha za miradi ya maendeleo;

(vi) Jeshi la Magereza (Fungu 29), Wizara yenyewe (Fungu 51) na Jeshi la Uhamiaji (Fungu 93) walipokea fedha za maendeleo **chini ya asilimia 50.**

(vii) Kiasi cha Fedha kilichopokelewa na Wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni **asilimia 64** ya kiasi cha bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo.

(viii) Jumla ya Kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yote matano ni **asilimia 83** ya jumla ya bajeti ya Wizara nzima iliyoidhinishwa na Bunge. Lakini kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya matumizi hayo ni **asilimia 64** ya jumla ya kiasi cha cha fedha zote kilichopokelewa kwa mafungu yote matano.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa mtiririko wa fedha kwa ajili ya Mishahara na Matumizi

Mengineyo kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ni wa kuridhisha. Uchambuzi umeonesha kuwa Kwa Mafungu yote, Wizara imepokea zaidi ya **asilimia 50** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Mishahara na matumizi Mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, uchambuzi umeonesha kuwa kuna mtiririko wa fedha usioridhisha. Kwa mfano, Fungu 29 Jeshi la Magereza, Fungu 51-Wizara na Fungu 93 Jeshi la Uhamiaji yamepata fedha za maendeleo chini ya **asilimia 50.**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hali hiyo ni dhahiri kwamba:

(i) Kwa ujumla uendeshaji wa shughuli za kuhakikisha usalama wa raia na mali zao haukukabiliwa na changamoto kubwa. Hili limethibitishwa na taarifa za usalama wa raia zinazoonesha hali ya usalama kwa ujumla ni shwari na madhubuti;

(ii) Mipango ya kuboresha huduma za urekebu pamoja na miundombinu ya Magereza kwa lengo la kuongeza tija ya kuwa na magereza nchini inafaa kuwekewa mkazo zaidi kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Mipango thabiti ya huduma za uhamiaji, wakimbizi, uangalizi, vitambulisho vya taifa, usajili wa Jumuiya za kidini na zisizo za kidini, Biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu ni miongoni mwa mambo yanayohitaji kuwekewa mkazo katika kipindi kilichobaki kabla ya kumaliza Mwaka wa fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge yalitaka uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ili uzoefu wake utumike kwa mwaka wa fedha unaofuata. Aidha, uchambuzi wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2025/2026 unafanyika kwa madhumuni ya kuendana na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za umma chini ya Wizara hii. Kwa madhumuni hayo uchambuzi uliofanyika uligusa maeneo yafuatayo:

(i) Mpango unaolengwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
(ii) Malengo ya ukusanyaji wa mapato;
(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida; na
(iv) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

### 3.2 Uchambuzi wa Mpango wa Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ulilenga kubaini iwapo, fedha zinazoombwa kuidhinishwa na Bunge zinawezesha tija ya majukumu ya Wizara hii. Kufikia azma hiyo, Kamati ilichambua Mpango wa utekelezaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kulinganisha na majukumu ya msingi ya wizara na vyombo vyake vyote.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi umeonesha namna mipango iliyobainishwa na Wizara inavyowezesha kuimarisha usalama wa raia na mali zao, utulivu na amani nchini, udhibiti wa uingiaji na utokaji nchini, usajili wa Jumuiya, huduma za vitambulisho vya Taifa pamoja na mambo mengine kuhusu majukumu ya Wizara hii.

**3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii umefanyika kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Ulinganisho wa lengo la mapato kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na ukusanyaji ili kuona uhalisia wa lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(ii) Uwiano wa mchango wa makadirio kwa kila Fungu ikilinganishwa na uzoefu wa mchango wa makusanyo ya kila Fungu kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Uwiano wa bajeti ya matumizi kwa lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ukilinganishwa na hali ilivyokuwa kwa ukusanyaji na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Lengo ni kujiridhisha zaidi na maeneo yanayohitaji msisitizo katika ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi yanaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha mapato kinachokadiriwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kimeongezeka kwa **asilimia 6** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025. Hata hivyo, uzoefu wa ukusanyaji kwa mwaka wa fedha unaoisha ulionesha kumudu kukusanya **asilimia 65** hadi kipindi cha robo ya tatu ya kipindi cha utekelezaji.

(ii) Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Fungu 28-Jeshi la Polisi, Fungu 29- Jeshi la Magereza na Fungu 93 - Jeshi la Uhamiaji yanategemewa kufanikisha ongezeko la makadirio ya mapato. Lakini uzoefu wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulionesha kuwa Jeshi la Polisi halikuwa limefika **asilimia 75** wakati wa robo ya tatu ya Kipindi cha Utekelezaji.

(iii) Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 51- Wizara yenyewe yanalingana na makadirio kwa mwaka wa fedha unaokwisha yaani 2024/2025.

(iv) Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 29 – Jeshi la Magereza yameongezeka kwa **asilimia 25.** Uzoefu wa makusanyo unaonesha kuwa Makadirio ya Fungu hili yanaweza kuongezwa na kukusanywa zaidi kuliko lengo lililowekwa.


**Mheshimiwa Spika**, kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kidigitali, uhaba wa vitendea kazi na upungufu wa rasilimaliwatu vinaendelea kuwa changamoto. Uzoefu wa hali katika kipindi cha miaka mitano unaonesha kuwa, mambo hayo yamekuwa yakiathiri makusanyo ya mapato. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, changamoto hizo zisipofanyiwa kazi lengo la makusanyo linalowekwa linaweza lisifikiwe.

**3.3.1 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Makadirio ya bajeti ya Maendeleo ulifanyika kwa kulinganisha na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ulinganisho ulifanyika ili kubaini uwiano wa miradi inayopangwa kutekelezwa na shughuli za kawaida za uendeshaji. Kutokana na uchambuzi huo ilibainika kama ifuatavyo:-

(i) Matumizi kwa ajili ya Miradi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa **asilimia 18** ya jumla ya Bajeti kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 06.**

**Kielelezo Na. 6 Mchanganuo wa Aina za Matumizi kwa Asilimia ya Jumla ya Bajeti inayokadiriwa**





***Chanzo: Randama ya Wizara***

(ii) Makadirio ya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo yameongezeka kwa **asilimia 26** ikilinganishwa na Makadirio ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;


(iii) Uwiano wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Mafungu yote ya Wizara Umeongezeka kwa wastani wa **asilimia 1.4** kama inavyoonekana katika **Kielelezo Na. 07**.

**Kielelezo Na. 7 Ulinganisho wa Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ukilinganishwa na uwiano wa makadirio ya Bajeti hiyo kwa Mwaka 2025/2026**

**Makadirio kwa mwaka 2024/2025**




**Makadirio kwa mwaka 2025/2026**




***Chanzo: Randama ya Wizara***

**3.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ujumla**

**Mheshimiwa Spika,** Mbali na uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa jumla wa makadirio kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii imeongezeka kwa **asilimia 17** ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo halitakuwa na mantiki iwapo Wizara haitahakikisha kuwa, Mafungu yote yanakamilisha taratibu za awali za kuomba fedha kwa wakati na kwamba HAZINA itatoa fedha zinazohusika kama inavyostahili.

(iii) Makadirio ya Matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi, usalama, amani na utulivu nchini; na

(iv) Makadirio ya Matumizi yaliyowasilishwa yasipoidhinishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, majukumu ya Wizara hii yatakuwa mashakani na shughuli za umma nchini zitaingia matatani.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

### 4.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi ulioelezewa katika Taarifa hii, umejenga msingi wa jumla wa mtazamo na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja. Aidha, Mtazamo huo unazingatia matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji na ufuatiliaji wa kawaida wa shughuli za Wizara hii. Kwa msingi huo, Kamati ina mtazamo na maoni yafuatayo:-

(i) Umefika wakati sasa Wizara itekeleze ipasavyo maelekezo ya kuanza kutoa jamii namba kwa watu wote nchini;

(ii) Ofisi ya Msajili wa Jumuiya ina majukumu makubwa katika usajili wa Taasisi za kidini na zisizo za kidini; hata hivyo Ofisi hii haitekelezi ipasavyo majukumu yake kwa kuwa ni ofisi ndani ya Wizara na hivyo inashindwa kutoa huduma kwa ufanisi hadi ngazi ya kata na mtaa. Hali inayosababisha uwepo wa Taasisi za dini ambazo hazijasajiliwa lakini zinatoa huduma. Hivyo, imefika wakati sasa Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iwe Taasisi Kamili.

(iii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaanza kupokea zana na vifaa vya kisasa kwa ajili ya uokozi na kuzimamoto katika mwaka huu 2025. Hivyo, kuna umuhimu wa kuboresha ofisi zilizopo na kujenga ofisi mpya katika maeneo ambayo hayana ofisi ili

kuimarisha huduma kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kutunza zana na vifaa hivyo.

(iv) Uboreshaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika nyanja ya vifaa na zana za kisasa uende sambamba na kutoa mafunzo kwa Askari juu ya matumizi na utunzaji wa vifaa na zana hizo;

(v) Makadirio ya matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo yatakuwa na mantiki ikiwa Wizara kupitia Taasisi zake zitaweka utaratibu mzuri wa kuanza na kukamilisha taratibu za awali mapema ili kuweza kuomba fedha hizo HAZINA kwa wakati. Kushindwa kukamilisha taratibu hizo mapema si jambo lenye afya kwa miradi ya Maendeleo;

(vi) Juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika kuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama vilivyo chini ya Wizara hii ni jambo la kupongezwa na kujivunia. Hata hivyo ni muhimu juhudi hizo ziende sambamba kuimarisha matumizi ya vifaa na zana za kisasa za kiteknolojia;

(vii) Pamoja na juhudi za Serikali katika kutatua changamoto ya Uhaba wa vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii, bado changamoto hii inaendelea kuathiri utendaji wa vyombo hivyo; isipoendelea kupatiwa utatuzi, utendaji utaendelea kuathirika;

(viii) Matumizi ya vifaa vya kisasa na vya kidijitali kwa vyombo vya Ulinzi chini ya Wizara hii ni suala lisiloepukika kwa sasa. Hivyo, kuimarisha matumizi ya vifaa hivyo ni kuboresha utendaji wa vyombo pamoja na kuimarisha hali ya usalama wa raia na mali zao kama ilivyobainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, ukurasa wa 155-160; na

(ix) Uwepo wa wakimbizi nje ya makambi na makazi ya wakimbizi ni suala linalopaswa kupewa kipaumbele na kushughulikiwa ipasavyo na Wizara. Suala hili lisiposhughulikiwa kikamilifu athari zake ni kubwa kwa nchi. Hivyo, Serikali iwabaini na kuwachukulia hatua stahili wakimbizi wote walio nje na makazi

na hifadhi ya wakimbizi kinyume na Sheria na taratibu za wakimbizi.

(x) Biashara haramu ya usafirishaji wa Binadamu inakuwa kwa kasi nchini. Katika mwaka wa fedha 2025/26 ipo haja ya Wizara kutoa mkazo katika mapambano ya kuzuia na kukabiliana na biashara hii haramu ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu athari zake.

(xi) Wizara iweke mkakati wa kupata ardhi kwa ajili ya matumizi ya vyombo vilivyo chini ya Wizara hii kwa matumizi ya baadae. Kufanya hivyo kutasaidia Kwenda sambamba na kutanuka kwa makazi na shughuli za kiuchumi pamoja na mahitaji ya baadaye.

### 4.2 Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa Maoni na mtazamo niliyotoa, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iweke utaratibu mzuri na unaotekelezeka wa kuanza mapema maandalizi ya awali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuweza kuomba fedha za Maendeleo HAZINA kwa Mafungu yote Matano kwa kuzingatia mipango iliyowekwa na kwa wakati.

(ii) Serikali iendelee kuboresha hali ya vyombo vya usafiri na usafirishaji kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara hii. Kufanya hivyo, kutaboresha utendaji kazi wa Majeshi haya katika kukabiliana na uhalifu pamoja na majanga mbalimbali na hivyo kuboresha hali ya usalama wa raia na mali zao.

(iii) Serikali iendelee na mkakati wake wa kuboresha hali ya vifaa na vitendea kazi kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Kufanya hivyo kutaongeza ufanisi wa Majeshi hayo katika utendaji kazi ikiwemo ukusanyaji wa maduhuli.

(iv) Pamoja na juhudi za Serikali kuongeza ajira kwa Majeshi yaliyo chini ya Wizara katika kipindi cha miaka minne iliyopita; Serikali

iendelee kuviwezesha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuajiri Askari wengi zaidi ili kuimarisha utendaji kazi wa vyombo hivyo katika kuhudumia wananchi na hivyo kwenda sambamba na mahitaji halisi pamoja na ukuaji wa makazi na shughuli za kiuchumi.

(v) Kukua kwa teknolojia kunachangia kuibuka kwa uhalifu mpya na njia mpya za uhalifu. Ili kukabiliana na hali hii, Serikali iimarishe matumizi ya zana na vifaa vya kidigitali katika utendaji kazi wa Majeshi yaliyo chini ya Wizara ya Mambo ya ndani. Suala hili liende sambamba na kuimarisha mafunzo kwa Askari na Watumishi.

(vi) Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa umma juu ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu kuhusu athari zake na namna ya kukabiliana na biashara hiyo inayokuwa kwa kasi nchini.

(vii) Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ikamilishe mchakato wa kuanza kutumia Jamii Namba. Kufanya hivyo kutasaidia mwananchi kuwa na namba moja ya utambulisho katika kila nyanja.

### 4.3 Ushauri Mahsusi

**Mheshimiwa Spika**, Zaidi ya Ushauri wa jumla, Kamati inao ushauri kwa kila Fungu kulingana na yaliyobainika. Ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

### 4.3.1 Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

**Mheshimiwa Spika**, Ili kufanikisha ustawi wa watu nchini kutokana na shughuli mbalimbali za jamii na za umma, Huduma za Zimamoto na uokoaji zinahitaji kuendelea kuboreshwa. Kamati inashauri kuwa:

(i) Serikali ihakikishe Ujenzi unaoendelea wa Ofisi za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika Mikoa mbalimbali unazingatia matumizi ya vifaa na zana za kisasa za kitekonolojia kwa matumizi ya sasa na baadae. Kufanya hivyo kutasaidia majengo hayo kutumika kwa tija iliyokusudiwa; na

(ii) Jeshi la Zimamoto na Ukoaji lijipange kutoa mafunzo ya kisasa ya matumizi ya vifaa vya kisasa vya uokozi na kuzimamoto kwa Askari wake juu ya matumizi na utunzaji wa vifaa vinavyotarajiwa kupokelewa kuanzia mwaka huu 2025.

(iii) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lifanye tathmini ya mkakati wake wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya moto na majanga mbalimbali. Tathmini hiyo itumike kuzigeuza changamoto zilizopo kama fursa ya kuimarisha utekelezaji wa elimu kwa umma kwa kuzingatia matumizi ya teknolojia.

### 4.3.2 Fungu 28- Jeshi la Polisi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua nafasi ya Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kufanikisha amani, utulivu na ustawi katika Jamii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendelee kusimamia inavyostahili katika kuhakikisha Askari wa Jeshi la Polisi wanazingatia Sheria, Kanuni, taratibu, miiko, weledi, tamaduni na maadili ya Jeshi la Polisi katika utendaji kazi wao;

(ii) Jeshi la Polisi lijikite kwenye matumizi ya vifaa vya kiteknolojia katika kukabiliana na uhalifu pamoja na kuimarisha usalama barabarani. Kufanya hivyo kutasaidia kuboresha utendaji wa Jeshi hilo ikiwemo mbinu za kukabliana na uhalifu unaotokana na matumizi ya teknolojia pamoja na kudhibiti usalama barabarani; na

(iii) Jeshi la Polisi liendelee kuimarisha ushiriki wa Jamii katika dhana nzima ya Usalama wa Raia na mali zao. Kufanya hivyo kutasaidia Jeshi hilo kusogeza huduma zake kwa wananchi na hivyo kuimarisha mapambo ya uhalifu katika Jamii.

### 4.3.3 Fungu 29 - Jeshi la Magereza

**Mheshimiwa Spika**, ili kudhibiti amani katika jamii kwa kuimarisha huduma za magereza na kuongeza tija ya shughuli za urekebu magerezani, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha Ujenzi wa Magereza mapya mawili pamoja na kukarabati Magereza Makuu manne kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mantiki ya kutenga fedha hizo itapatikana ikiwa Jeshi litakamilisha hatua za awali na kuomba fedha kwa kuzingatia mpango uliowekwa.

(ii) Ili kufikia tija na malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa mafunzo ya urekebu; Serikali iboreshe miundombinu chakavu ya magereza nchini.

(iii) Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu na kuimarisha Mfumo wa Mahakama Mtandao katika Magereza nchini Ikiwa ni sehemu ya uimarishaiji wa mfumo wa Haki Jinai.

**4.3.4 Fungu 51- Wizara**

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa taarifa na makadirio kwa Fungu 51 umeipa kamati nafasi ya kushauri ifuatavyo:-

(i) Wizara iisimamie kwa karibu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhakikisha kuwa inatekeleza mpango wa utambuzi wa watu kwa kutoa Jamii Namba kwa Raia halali wa Tanzania ikiwemo watoto kuanzia chini ya mwezi mmoja.

(ii) Ofisi ya Msajili wa Jumuiya iwe Mamlaka/Taasisi kamili inayojitegemea. Kufanya hivyo kutasaidia taasisi hiyo kutekeleza majukumu yake kuanzia ngazi ya kitongoji, Kijiji, Mtaa na Wilaya, tofauti na sasa ambapo inatekeleza majukumu yake kama idara ndani ya Wizara.

(iii) Serikali iweke Mkakati unaotekelezeka wa kuhakikisha inawabaini na kuchukulia hatua stahiki wakimbizi wote walio nje ya makambi na makazi ya wakimbizi kinyume na sheria na taratibu za wakimbizi.

(iv) Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa kimataifa na Kitaifa iharakishe mpango wake wa kuwarejesha wakimbizi katika

nchi zao. Kwani wakimbizi wengi walioko nchini hali ya amani, utulivu na usalama imeimarika katika nchi zao.

(v) Wizara iweke mkakati kuhakikisha vyombo vya ulinzi vilivyo chini ya Wizara hii vinapata maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya wakati ujao kutokana na ukweli kuwa matumizi ya ardhi yanaongezeka kwa kasi nchini.

**4.3.5 Fungu 93 - Uhamiaji**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jeshi la Uhamiaji, Kamati inashauri kuwa:

(i) Serikali iendelee kusimamia inavyostahili katika kuhakikisha Askari wa Idara ya Uhamiaji wanazingatia Sheria, Kanuni, taratibu, miiko, weledi, tamaduni na maadili ya Idara hiyo katika utendaji kazi wao.

(ii) Serikali iendelee kuiwezesha Idara ya Uhamiaji kupata vyombo vya usafiri na usafirishaji ili kuboresha utendaji kazi na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(iii) Serikali ifunge mfumo wa uhamiaji Mtandao katika Ofisi zote za Uhamiaji zisizo na mifumo hiyo sambamba na mfumo wa udhibiti wa mipaka kwenye Vituo 26 vya kuingia na kutoka nchini. Kufanya hivyo kutaimarisha udhibiti wa uingiaji na utokaji wa raia na wageni nchini kupitia mipaka yetu.

(iv) Serikali iendelee na mkakati wa makusudi wa kudhibiti mianya ya njia zisizo rasmi zaidi ya 1000 katika mikoa mbalimbali ya mipakani ikiwemo kutumia mifumo ya udhibiti mipaka (e-border). Kufanya hivyo kutasaidia kudhibiti uingiaji wa wahamiaji haramu pamoja na bidhaa za magendo nchini; na

(v) Serikali isimamie na kuhakikisha ujenzi wa majengo ya Idara ya Uhamiaji unaondelea katika maeneo mbalimbali nchini unazingatia matumizi ya vifaa vya kiteknolojia kwa kuzingatia wakati wa sasa na ujao.

### 4.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

1. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dr. Alfred James Kimea, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Minza Simon Mjika, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb), pamoja na Katibu Mkuu Ndg. Ally Senga Gugu na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka I. Leonard. Aidha, napenda

kuishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashidi Kawawa, Mb.
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

26 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ninamshukuru sana Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mwenyekitii wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Taarifa hiyo ya Kamati.

Sasa tunaanza na wachangiaji wetu, tutaanza na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa kwanza katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Nianze kwa kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyoendelea kuweka amani na utulivu kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge Msukuma pamoja na wananchi wangu tunaungana na Mheshimiwa Rais kwenye kauli aliyoitoa kuhusiana na usalama wa nchi yetu, tunampongeza sana na sisi wananchi wake tunasema aendelee kusonga mbele katika kuhakikisha analinda usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ni huru na hatuingiliani kwenye *East Africa* kuhusu masuala ya kisiasa. Kila nchi ina mambo yake. Tumeona suala lililotokea juzi la wanaharakati na yaliyowapata. Tumeona jinsi vyombo vyetu vinavyotukanwa. Pia, tumeona Mheshimiwa Rais wetu anavyotukanwa na majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wabunge wa Bunge hili tutakuwa wa mwisho kukubali kuona Rais wetu anatukanwa halafu tukakaa kimya. Nawaomba wanasiasa wenzangu wa Tanzania, tumepata matatizo mengi sana ya majaribio ya kupoteza amani yetu. Tulipatwa na tatizo la Rufiji, vyombo vyetu vilifanya kazi kubwa sana na sisi kama Wabunge (mimi nilikuwa Mbunge) tulifika mpaka mahali tukaahirisha Shughuli za Bunge kujadili usalama wa watu wa Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata tatizo la kusini, Msumbiji, majaribio yale tulilalamika sana, tukapata tatizo la *panya road* ninadhani kwenye Bunge hili, tukalalamika sana. Vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vilifanya kazi kwa utulivu na amani ikarudi na taarifa ikawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba ndugu zangu wanasiasa (Wabunge) sisi tumekuja humu kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi na sisi ndiyo tumepewa dhamana ya kuwasemea wananchi wetu, hakuna Mbunge hata mmoja anayetaka kuona jimboni kwake kunanuka. Hakuna Mbunge hata mmoja anayeona vyombo vyetu vya ulinzi na usalama havifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wanasiasa wenzangu tusiingie *disco* la Kimasai ambalo hatujui kulicheza. Hawa wenzetu wamekuja kutoka Kenya, tuwaombe, nao wanaangalia Bunge hili. Sisi Tanzania hatuna cha kujifunza Kenya, hatuna hata kimoja cha kujifunza. Tunawazidi siasa, tunawazidi akili, tunawazidi kila kitu na wala suala la Kiingereza sisi siyo kipaumbele, tuna maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana vyombo vya ulinzi na usalama, msikubali kuwaruhusu watu hawa waje watuharibie nchi yetu. Naomba sana Mwangi na Martha Karua sijui,

ndio vinara wa *Gen Z* kule, wameharibu nchi yao, wamewekwa na ndani, wametoka kule wamekuja tena Tanzania. Tunawaomba Wakenya; hatuna ugomvi na Wakenya wa kawaida, tuna ugomvi na wanaharakati, na sisi tupo tayari kupambana nao majukwaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana Wakenya, tunafanya nao biashara, tunafanya mambo mengi ya kiuchumi, Marais wetu wanaheshimiana, waje Tanzania kuja kujifunza, waje Tanzania kuja kutalii, lakini wasije kutujaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kama Mbunge ninaomba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, ninajua wanapitia wakati mgumu, wakati mwingine na sisi tunawasema, lakini wazibe masikio. Nnadhani jeshini huwa hamfundishwi siasa, wafanye kazi yao. Kama mtu anatuchokoza, sisi tunahitaji kuendelea kuniga tai, hatutaki kinuke. Hatuhitaji suala la kunuka kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na viongozi wetu, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama sisi tunaviamini kwa asilimia mia moja, haya ni majaribu na yatapita, endeleeni kufanya kazi. Nimemsikia mwanasiasa mwenzetu mmoja, rafiki yangu amepigapiga, akaingilia mpaka na maamuzi ya Rais. Jamani, tulikuwa na Awamu ya Tano humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mbunge, mwamba Marehemu hakuna mtu alinyanyua mdomo, hakuna mikutano na hata hiyo *press* ungepiga jioni, angekuwa nayo jamaa. Sasa tusimwone mama mpole tukatumia hii nafasi kumwingilia mpaka na maamuzi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote tumeapa kulinda Katiba. Rais wetu ameapa kulinda Katiba na kulinda usalama wa nchi yetu. Aachiwe nafasi afanye kazi. Haya majaribu mnayofanya, Samia tunaye na tunatamba naye mpaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu wanasiasa, suala la usalama tusilifanye la majaribio. Tuliguswa tu

*panya road,* ninyi watu wa Dar es Salaam humu ndani mlipiga kelele eeh, sasa kimeanza kidogo kidogo. Hiki tukikiacha,…*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kenya wakati wa utawala wa Uhuru, watu walikuwa wakipotea hivi, kabla ya kufanya uchunguzi vinasingiziwa vyombo vya ulinzi na usalama. Wakabagaza vyombo vyao, wakadhalilika. Matokeo yake, vyombo vimefanya uchunguzi vikaenda kukumbana na Shakahola watu 200 wamefungiwa na mtu mmoja, lakini mmeshavikana vyombo vyenu, mnawakatisha watu tamaa, kwa sababu leo tupo wote humu na mimi hii ndiyo nafasi yangu kwa ajili ya kuwawakilisha wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba vyombo vya usalama, hata mimi nikikosea wanitie ndani ili wengine wasalimike. Lazima wafanye kazi yao tusiwaingilie. Hata wanasiasa ninaona kama labda joto limeanza. Mimi nilikuwa ninaangalia hata *clip* nikawa ninamwangalia mdogo wangu Askofu Gwajima hapa, labda kuna joto jimboni, maana ile *press* mimi sikuielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba wanasiasa, tunaporudi kwenda kuchanguliwa, tukisimama majukwaani, tuahidi vitu tunavyoviweza. Mkiahidi vitu vikubwa ambavyo haviwezekani matokeo yake mwishoni mnaanza kutafuta huruma ya wananchi. Mimi ninakaa Mikocheni, tunasubiri kwenda Japan kwa Gwajima. Alituahidi kwenda Japan, tunamsubiri atupeleke. Alisema atatupeleka Japan na Ujerumani tukabadilishane uzoefu, na mimi niliandika jina, ni mwananchi wake wa Mikocheni, tunakusubiri atupeleke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusilete *pressure* za majimbo tukaanza kuingilia mamlaka. Mheshimiwa Rais ana nafasi ya kumtengua yeyote na kumweka mtu yeyote. Tusitumie upole wa Mama Samia kuanza kuingia mpaka *state* kwenda kupanga na kupangua, hapana. Wananchi wetu kule wanatushangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimepokea zaidi ya simu 200, wanasema kesho Mambo ya Ndani hatutaki kusikiliza chochote, hata kituo cha Polisi usiombe, hata gari usiombe, tuwatie moyo Polisi,

tuwatie moyo vyombo vya ulinzi na usalama, tunataka kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi niwaulize, tukianza kuwadogosha Askari wetu, tumefanya kazi kubwa, tumejenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, tumejenga Daraja la Busisi, tumejenga mwendokasi, kama hamna amani, haya si yataharibika? Kuna haja gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tunaitengeneza kuna watu wanakesha hawalali kwa ajili yetu. Sisi tunapiga tai, tunabadilisha simu, kuna watu wanashinda na mabunduki huko kufikiria sisi tunaamkaje? Wakati sisi tunasinzia na wake zetu, watu wengine wanakesha kuona humu ndani watu walale, waamke kesho waende kazini. Nawaomba sana Wabunge wenzangu wa Bunge hili, tuvitie moyo vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua mnapitia vitu vingi, hata mimi mwenyewe Mbunge Musukuma sipendi mtu apotee, lakini siwezi kutoa hukumu nani amewapoteza? Vyombo vyetu kwa weledi mlionao fanyeni kazi halafu toeni taarifa. Haiwezekani kila kitu kinalalamikiwa leo, kesho unapewa majibu, hao watu wanaofanya hayo matukio nao wamejipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa vyombo vyetu tunaviamini, kama walifanya vizuri Rufiji, wakafanya vizuri Msumbiji, hili nalo litapita. Tunawaomba waongeze weledi, lakini sisi kama Wabunge wa Bunge hili tunaungana mkono sana na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu *IGP* Camillius Wambura wala asirudi nyuma. Pengine watu wanampima kwa kaumbo kake, lakini sisi na Mheshimiwa Rais tunaamini tupo mikono salama. Vyombo vyote, kamanda wa *Immigration,* tena mimi nilishangaa mliwarudisha wa nini? Mngewaingiza ndani, tuwapeleke na kulima, inawezekana kule Kenya hakuna mashamba. Lindeni mipaka yetu, watu waingie humu kwa vibali. Kama amekuja kufanya biashara alipie kibali cha biashara. Huwezi kuja kutembea halafu ukaanza kwenda kuning'inia Mahakamani na kutoa *press*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Taifa huru, wasituingilie na Taifa letu. Hata sisi tunayo midomo, nao wanafanya kampeni, wanafanya mikutano na sisi tunao Wabunge wa Kenya wengi tu marafiki zetu, tunashirikiana kwa mawazo kwenye simu, lakini hatujawahi kwenda kupanda majukwaani kudogosha Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, jeshi letu ni la weledi kwa kweli. Hata ukiangalia wao wanasema wameendelea; hivi unaendelea wakati kila siku Rais anapewa majina, sasa hivi "Elchapo" sijui mara "Kasongo". Kila siku mara anapondwa viatu kwenye msafara. Tunataka tuwe na jeshi la *design* hiyo? Hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka jeshi letu liendelee na mwendo mdundo ule ule. Mtu yeyote anayeingia Tanzania ajue akileta mchezo Wambura yupo kazini na wenzie, atanyea kwenye debe au atakula rungu. Hii ni haki yetu, lazima tuilinde nchi yetu kwa wivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilienda China siku moja, nikakodisha teksi. Sasa nikawa ninabishana na mkalimani wangu, mimi Kiingereza sikijui. Wakati tunabishana, nikawa nasema mbona sioni Wachina wakizungumza kuhusu Rais wao? Yule dereva teksi alishika breki karibu tuumane meno mle ndani. Akasema ninyi mmekuja kwa ajili ya biashara au mmekuja kwa ajili ya kumsema Rais wetu? Akatuambia mimi hata nilivyowabeba msinilipe, akatuacha kituoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nawaomba, hii ndiyo *system* tunayotaka kwenda nayo kwenye hii nchi. Tumwache Rais afanye kazi. Rais anakaa kila siku anachorwa, na kadhalika, nawaomba vyombo vya ulinzi na usalama, tumepitisha sheria humu, hata kumchora Rais wetu, kumtukana Rais wetu, ni kukamata kwa sababu tulikubaliana humu ndani Bungeni. Tumetunga sheria halafu tunaiogopa wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama wa Taifa tumetunga humu, Sheria ya Polisi, Sheria ya Mitandao tumetunga humu, ikianza kutekelezwa, tena tunarudi nyuma kukaa majukwaani, hapana!

Anayeumia na hizi sheria alete hoja humu Bungeni, atuambie kama yeye anataka kinuke ama watu wafanye kazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma kwa mchango huo ambao ninaamini kabisa una mantiki pana kwa maslahi ya amani ya Taifa letu.

Tunaendelea na Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara yetu hii pendwa ya Mambo ya Ndani ambayo ndiyo mhimili kwa kweli wa mambo yetu yote kwa sababu bila amani, na usalama hakuna jambo lolote linaloweza likafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mbunge mwenzangu ambaye amemaliza, ametengeneza *road map* nzuri sana. Jambo la kwanza anasema, tuvitie moyo vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, nami niseme tunaanza kumtia moyo Amiri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu ya Tanzania mwanajenshi ni Askari yeyote aliyeajiriwa kwa muda maalumu au wa kudumu katika vyombo vyetu vya Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Polisi, na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo, hivi vyote ni vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Kwa hiyo, Amiri Jeshi Mkuu ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kuanza kumtia moyo na yeye. Kabla sijaenda mbali sana, niwashukuru sana Askari wetu. Polisi wetu wanafanya kazi kubwa tunafahamu na siku moja hapa niliwaambia Watanzania, ukimwona askari bwana yupo anasikia kiu, nini wewe mpe tu hela ya maji, kazi iendelee kwa sababu kwa kweli wanajitoa kwa kiasi kikubwa kwa ajili yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa ninaangalia *clip* moja ya jirani zetu ambao Mheshimiwa amesema hapa, gari yao ya Polisi ilikuwa imepinduka, wakawa wamekusanyika pale wenyewe wanaosema wao ni wajanja wana akili kubwa, wanasema hawa tusiwatoe kwa sababu wao huwa wanatufuatilia fuatilia usiku. Hao wenzetu nchi nyingine jirani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu huwezi kuchagua Jirani, basi tunamshukuru Mungu kwa kutupa majirani hao, tutaendana, nao na tutajipanga kupambana na tutajipanga kushirikiana nao. Pale watakapotaka ushirikiano wa amani, tupo tayari kushirikiana nao, lakini pia hatutawaruhusu majirani zetu kuvuruga amani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi askari wetu tunaishi nao vizuri, tunajua zipo changamoto ndogo ndogo. Ndugu zangu Watanzania, nichukue fursa hii kuwaambia, changamoto tulizonazo bado hazijafikia hatua ya sisi kutoheshimiana, wala kufika mahali kuhatarisha amani na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi bado nchi yetu ni kisiwa cha amani. Hapa tumezungukwa, hata hao wanaotutukana wakipata matatizo wanategemea wakimbilie Tanzania. Kila upande wa Taifa letu umezungukwa na Taifa ambalo wanatuona sisi ni kisiwa cha amani na tumekuwa tukitoa msaada. Vijana wetu hawa Askari wamekwenda katika kila nchi kulinda amani na utulivu wa Mataifa haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawasaidia majirani zetu kwa amani, tunawasaidia kwa jasho la damu, Tunawasaidia kwa damu za watoto wetu. Askari wetu wanakufa kwenye Mataifa mengine kwa sababu ya kulinda amani. Hii ni kwa sababu tulijengewa misingi hii tangu Mwalimu Nyerere. Alitutuma kupambana kuokoa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tulifanya kazi hiyo na hii ndiyo Tanzania. Ndugu zangu hatuwezi kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mmoja anashangaa anasema, *Gen Z* wa Kenya wamejitolea, lakini anachora kwamba *Gen Z* wa Tanzania wamelala. Tunataka tuwaambie vijana wetu

wamejengwa katika misingi ya baba zao, "*like father, like son*." Tumewafundisha vijana wetu uzalendo, ujasiri, uhodari na tumewafundisha pia kutafuta fedha, siyo kwa kutukana watu, kuuza maneno kwenye mitandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wetu hawataungana na mambo ya kipumbavu kwa sababu lazima tukubaliane kwamba, Biblia inasema katika Isaya 32:17, amani ni zao la haki. Haki tuliyoijenga kwenye Taifa hili ndiyo inayozalisha amani, na amani hiyo inaleta matunda ya utulivu na matumaini. Watoto wetu wana utulivu, wana matumaini kwa sababu wamejengwa katika misingi ya amani na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasitake kutuaminisha kwamba sisi kwetu hakuna haki. Sisi kwetu haki ipo. Hizi changamoto nyingine ni ndogo ndogo ambazo zipo katika Taifa na hata kwenye familia zipo. Baba na mama mnaweza mkagongana, ni changamoto, zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema kama kuna changamoto, sema ili tusaidiane, na amekuwa ni Rais msikivu. Tuliposema, amechukua hatua, amefanyika kazi. Sasa tunawaomba sana ndugu zetu, ninyi Kenya ni majirani zetu, tunawaheshimu, tunafanya na nyie kazi. Tunaomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaza sana usiku, nikasema, kwani hawa wana shida gani? Mmoja ameuliza akasema, hivi ninyi Watanzania, sisi tunapiga kelele tunasema, tunawatukana mpo kimya, mna mpango gani? Mnataka kuturoga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikagundua lipo tatizo kubwa sana la afya ya akili katika Taifa lile. Niwashauri bure, siyo dhambi. Sisi wenzenu *CAG* wetu, yule *Auditor General*. Nao wana *Auditor General* wao wa Kenya, amefanya uchambuzi wa suala la afya ya akili nchini na tunatengeneza *mechanism* ya kusaidiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati mwingine unapomkuta mama mtu mzima, msomi aliyesoma sheria anaondoka kwake, anapanda na nauli, bahati mbaya ukimwangalia uso wake hauna matumaini; ukimwangalia uso ule sijui ni mkorogo umedunda, sijui alisahau kupaka poda, anakuja kutuchonganisha, ile siyo hali ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichokifanya Askari wetu ni kumdhibiti kwa sababu ukishaona mtu akili yake haifanyi kazi vizuri, unamsaidia kumdhibiti. Kazi ya Jeshi letu la Polisi ni kubaini na kudhibiti, ndiyo kazi yao nyingine. Wakati mwingine Jeshi la Polisi, nashukuru Mheshimiwa Waziri amesoma katika ukurasa wa 23. Moja ya mambo wanayofanya ni pamoja na *operation,* na vitu vingine. Wametanzua uhalifu, hiyo ndiyo namna ya kutanzua uhalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania tuna moyo na wao, mtu asiwabagaze. Tungeshangaa sana watu wanakuja hapa wanaanzisha mambo yao ya maandamano, wametoka nchi nyingine wanavuruga vijana wetu; wanakuja kuzuia utulivu wa utendaji wa Mahakama, chombo kinachotoa haki katika Taifa letu, halafu wao wapo. Tungeshangaa sana. Hatujashangaa, tunawatia moyo, tuko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema hivi, uzio, wigo wa ulinzi wa Taifa letu haujajengwa kama ule ukuta wa China *(China Great War)*. Haujajengwa kama ukuta wa Babeli, uzio wa ulinzi wa Taifa letu umejengwa kwa mioyo ya uzalendo wa vijana wetu. Umejengwa kwa maji ya damu ya vijana wetu. Hawatakuwa tayari, na tunaomba tuwaambie, jamani eeh, hiyo ni *trailer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mwingine anasema sema, jamani nasikia hao Askari Polisi wanapiga. Hiyo ni *trailer*. Tena nyie mmekutana na Polisi ambao sisi tunashinda nao kila siku. Yaani ambao wamezoea zoea kidogo mambo ya uraia. Tuna wengine wanafanana na miti na udongo. Tukiwatoa hao, shughuli yake mtaiona. Hatuyataki hayo. Hatutaki tufike huko. Hatutaki tufike huko, na tunaomba tuheshimiane ndugu zetu Kenya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu, *Your Excellence Honorable Ruto,* tunakuheshimu sana. *Do something*. Demokrasia, *that is not democracy in Kenya.* Hiyo ni vurugu. Nasi kama jirani zenu tunasikitika, kwa nini Taifa linayumba kiasi hicho na ninyi mpo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi Askari wao na wao wamewazoea. Tuliwaona kwenye maandamano, mwandamanaji analeta vurugu, anakunywa maji, anampatia na askari naye anakunywa. Tanzania hicho kitu hakipo, na hili Jeshi la Polisi hatujaliunda sisi. Liliundwa tangu mwaka 1919 na mkoloni. Ilijulikana tu kuna watu watafanya vituko, lazima waswekwe ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilikuwa nafanya ziara Iringa, waliniuliza, Mheshimiwa Mbunge, yaani kile Kituo cha Ipogolo, tukikamatwa lalalalah, hali yake ni mbaya! Tunapigwa sijui, tunafanya nini? Nikawaambia, Polisi siyo lazima uende; na bahati mbaya sana, wale Polisi sisi tumewapa virungu, tumewapa bunduki, tumewapa maji washawasha. Sasa ukienda pale unategemea utapata nini? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kupetiwapetiwa mwanangu, nenda hospitali, wale ndio wamesomea jinsi ya kupetipeti. Kwa hiyo, ndugu zangu tunaomba tuwaambie, sisi Tanzania tunasikitika sana, lakini nimtie moyo Mheshimiwa Rais wangu Mama Samia, huo ndiyo upande wa pili wa shilingi wa kuwa Amiri Jeshi Mkuu na kuwa Rais. Sisi wenyewe tumetulia, lakini wanatoka watu wengine wanakubagaza, wanajua yupo. Kwa sababu kama hawajui, milio ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huku Tanzania huwa tunasema, ukiona manyoya, kashaliwa. Ukiona mlio, kapigwa. Sasa tunawaomba sana, sisi tutaendelea kulinda amani na utulivu wa Taifa letu na hatutakuwa tayari; ndugu zangu Watanzania, vijana wangu, tunashukuru tuna vijana wa kiume wanaoandamana, wanatafuta kiki siyo kwenye maandamano. Wanatafuta kiki kufanya kazi, wanatafuta kiki kwenye kilimo, wanatafuta kiki wako na bodaboda na bajaji wanatafuta maisha; wanatafuta kiki wako na malori usiku na mchana, wanatafuta kiki wako kazini. Hawawezi kutafuta kiki kwa vijana wao wanaokaa

kwenye mitandao wanatukana watu, na lazima mliangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru Viongozi wa Kenya, tunawashukuru baadhi wa wananchi wa Kenya, wameongea wao wenyewe, wametoa majibu wao wenyewe, lakini lazima wafanye kitu. Hatuwezi kuwa na majirani wa *style* hii, ambao wanaanza tu kumtukana Rais wa watu bila sababu za msingi. Kawakosea nini mama yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuja kufanya nini? Wewe unaenda nyumbani kwa watu, unaambiwa bwana, utaratibu huku ndiyo chooni. Ingia huku, huku hutakiwi kuingia. Unang'ang'ania kwa nini hawaniruhusu niingie choo chao? Wewe vipi? Sisi hatutaki. Halafu huwezi kuja kusaidia kitu, hatujashindana. Sisi wanasiasa wetu ni wanasiasa wetu, tutasaidiana wenyewe, tutapanga wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, yale mambo madogo madogo ambayo tunarekebisha, tuendelee kurekebishana na mengine tutaambizana, lakini kwenye suala la usalama wa Taifa letu, hatutaacha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ahsante sana Mheshimiwa Jesca Jonathani Msambatavangu. Nilimtaja Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, halafu Mheshimiwa Felista Deogratius Njau, ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nami kabla ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima na kutuwezesha leo kukutana humu kujadili mambo ya msingi kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni Watanzania, hatuna sehemu nyingine ya kwenda. Hapa ndiyo kwetu na Wizara tunayoijadili ndiyo inatufanya tulale, tuamke tukiwa salama. Wale wanaokwenda *club*

usiku waende wakacheze warudi nyumbani walale wakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabla sijaenda mbali, nampongeza na kumtia moyo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye pia kwa mujibu wa Katiba yetu na Sheria za Nchi yetu, ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi wa Ulinzi na Usalama wa Nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana kwa namna ambavyo amefanya kazi yake katika kitengo hicho na vitengo vingine na kuifanya nchi yetu mpaka leo hapa, mimi nimetoka nyumbani salama, nimefika hapa salama na naamini nitarudi salama kwa amani na utulivu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais hongera sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa pongezi. Ni mzembe kidogo kupongeza watu, lakini Mheshimiwa Waziri naomba nikupongeze. Umeonyesha uwezo mkubwa kwenye kila Wizara unayopelekwa, lakini Wizara hii wamekupatia kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka Wizara ya Ulinzi Mheshimiwa Waziri alifanya kazi nzuri na sasa yuko hapa. Kwa hiyo, kama kuna watu wanafikiri yuko kwa bahati mbaya, naomba niwape pole. Mheshimiwa Waziri hongera, kazi unafanya vizuri na sisi kazi yetu ni kukushauri na kurekebisha pale kwenye shida kidogo, lakini jiamini, hii kazi unaiweza na unaifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, Kaka yangu Mheshimiwa Sillo, ana uzoefu na kazi hizi za Kibunge. Amekuwa Mwenyekiti wa Kamati nyeti humu na sasa ni Naibu Waziri, endeleeni kuchapa kazi. Wamezungukwa na watendaji wazuri kwenye Wizara yao na vyombo vinavyowazunguka viko imara, kazi tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa sababu tuna kazi kubwa kama nchi, na Wizara hii ni muhimu kwa nchi yetu. Nchi yetu, siyo nchi nyingine, Wizara ya Mambo ya Ndani. Kwa hiyo, nadhani sasa nataka iendelee kuwa bora zaidi, nami kama Mbunge, kazi yangu leo ni

kuboresha ambapo panapohitaji kuboreshwa na kutia moyo panapohitaji kutiwa moyo ili tuendelee kuwa na hii amani tuliyonayo, na ikiwezekana iwe bora zaidi na zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii kuna Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji. Mheshimiwa Waziri, hawa watu wanafanya kazi yao vizuri. Kinachotakiwa, sisi ni kuwaongezea tu nguvu, lakini ametaja hapa kuna Zimamoto na kuna watu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wawili nafikiri tunatakiwa tuwaongezee kiki zaidi. Bado mambo yao siyo mazuri kama ya Jeshi la Polisi, ya Uhamiaji, na Magereza. Nadhani bado Jeshi letu la Zimamoto tunatakiwa kuliimarisha zaidi na zaidi kwa sababu tunaendelea, uchumi umekua, maendeleo yako bayana. Kwa hiyo, ni lazima tuwaongezee nguvu na vifaa na weledi, wafanye kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watu wa Vitambulisho vya Taifa hawa wanatakiwa kuamshwa zaidi. Nadhani bado na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati amesema bado wanakuangusha hawa watu. Umesema kuna Mkurugenzi amekuja mpya, na Waziri ameingia mpya pale, hebu sasa waende kwa kasi ambayo Waziri anafikiri kichwani na imani aliyoionyesha kwa Mkurugenzi, waende wakapabadilishe. Hawa wa vitambulisho bado wanatuacha katika safari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa ujumla wake Wizara ya Mambo ya Ndani inayasimamia haya majeshi yetu; Polisi, Magereza na Uhamiaji. Leo naomba nizungumze kidogo kuhusu jeshi ambalo kila tukiamka tunakutana nalo, Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu wanafanya kazi nzuri sana, na sisi kabla hatujazungumza sana, na hatujalaumu sana, mimi namwona Askari yule anayetoka *CCP*. Akitoka pale anakuwa *very pure,* yaani ni Askari halisi, mzalendo aliyefundishwa, anayekwenda kutumikia Taifa lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tunalo jukumu la kumfanya aendelee kuifanya kazi yake kwa weledi. Askari wetu ni binadamu kama sisi, wanazo familia kama sisi, wanauguliwa watoto kama sisi, wana mahitaji kama sisi. Sasa kwa sababu ya namna ambavyo tumewafundisha na nchi yetu kwa kweli askari wamefundishwa wakaiva, wana utii wa sheria, wanafuata miiko na *professionalism*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine wanapokuwa wana upungufu, wanakosa sehemu za kusemea. Nadhani Bunge hili ni sehemu sahihi ya kuzungumzia maslahi, maisha bora na utendaji mzuri wenye raha kwa Askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja duniani hapa huwa anakula kwa urefu wa kamba yake. Ukikuta dereva wa lori, yeye ataambiwa na kampuni yake kwamba huko njiani usipakie watu, lakini atatafuta *gap,* atapakia, kwa sababu yeye ana lori; lakini askari wetu umempa bunduki, umempa *PGO*, umempa Kituo cha Polisi, umemweka mwingine barabarani, ukampa kila kitu, lakini unasahau huyu mtu anahitaji nyumba ya kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, askari wetu hawana nyumba ya kuishi, wanadaiwa pango, kodi haitoshi, maslahi yao siyo mazuri. Huyu askari mwisho wa siku anafanyaje? Atatumia kile ulichompa angalau kuweka mambo yake sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa mwisho wa siku tunaangalia tu upande wa pili; Askari wanakula rushwa, Askari barabarani wanaonea watu, lakini sisi tunatakiwa tujiangalie. Kama Bunge, kama Serikali Askari hawa wanapotaka uhamisho tunawapa fedha zao za uhamisho kwa muda? Askari hawa wanapopata matatizo kazini, tunawafidia kwa muda? Wanapoenda likizo, tunawalipa likizo kwa muda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani huu ni wakati mwafaka, Mheshimiwa Waziri ameingia, aende akaliboreshe zaidi Jeshi la Polisi. Polisi wetu hawatakiwi kuwa wanyonge. Polisi wanafanya kazi nzuri, hawatakiwi kuwa wanafika wakati eti *uniform* zinapoisha aanze

kutafuta, akajipendekeze wapi apate *uniform*. Jeshi la Polisi linatakiwa liwe na *uniform* muda wote, nyingi zilizozidi idadi ya askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari wetu kazi zao wanazozifanya ndizo zinatufanya sisi hapa tuwe na ujeuri huu. Kazi nzuri walizozifanya ndiyo zimewafanya watu waliokuja ku-*test* mitambo kukuta iko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajivuna hapa mitambo yetu imetestiwa, kuna watu wamekutana nayo iko imara kwa sababu ya hawa Askari wetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aangalie sana hawa watu wetu. Tunayo sababu ya kuwaangalia kwa jicho la pili, wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyumba. Askari kweli anakuja kupanga Uswahilini, anapanga na watu ambao baadaye watafanya uhalifu akawakamate. Sasa akitakiwa akamkamate mama mwenye nyumba, atamkamataje na wakati huo anadaiwa kodi ya miezi miwili? Mwisho wa siku tunamshusha morali ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, ameleta bajeti kubwa hapa, lakini kwanza Wizara ya Fedha, pesa zinazoenda kwenye Jeshi la Polisi, zitoke kwa muda tusisikie 60%, tusisikie asilimia ngapi. *OC* za Polisi ziende kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi ukipiga simu kuna uhalifu hawana mafuta kwenye gari, wanafanyaje? Gari haina matairi, yaani unakuta Jeshi la Polisi gari yao imeisha matairi, wanaenda kudoea halmashauri yale matairi yaliyotolewa kwenye zile gari zilizokuwa pale, ndiyo wanaweka kwenye magari. Jeshi letu haliwezi kuwa hivyo. Yaani tuwahudumieni kama wanavyotuhudumia. Bado tunafanya kazi vizuri, lakini tunatakiwa kufanya vizuri zaidi, askari wetu wawe *comfortable* kazini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nisizungumze sana, nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti yake hii itapita, nami nitaiunga mkono na ninaomba achukue mawazo yote niliyompa

ayafanyie kazi kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Nilimtaja Mheshimiwa Felista Deogratius Njau. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos na Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani. Ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunipa afya na uhai niweze kusema machache saa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu niweze kuwapongeza watu wetu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa na kizalendo wanayoifanya kwenye Taifa letu. Wakati tuko hapa Bungeni tumetulia tunawaza ya kwetu, wenyewe hawalali, hawasinzii kuhakikisha amani ya Taifa letu inalindwa. Ninawapongeza sana. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri Innocent Bashungwa na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya pamoja na Watendaji wake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninampongeza Mama yetu shujaa, Mama Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa weledi mkubwa na ushujaa wake imara katika kuliongoza Taifa katika siku ya leo. Amani, utulivu tulionao ni matunda ya haki, lakini na wajibu ambao watu wanatakiwa kuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimempongeza Mheshimiwa Rais kipekee, kwa sababu yako mengi ya msingi ambayo ameyafanya kwa utashi wake wa kisiasa bila kusukumwa na ushawishi wa pande yoyote. Mwaka wa fedha 2021/2022 nilisimama kwenye Bunge lako Tukufu nikiwa ninalia juu ya mrundikano Magereza wa Mahabusu na Wafungwa walikuwa wamejaa magerezani na kusababisha adha kubwa, magonjwa ya mlipuko pamoja na fedha nyingi za Serikali ambazo zilikuwa zinalisha hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usikivu wa Mama huyu shujaa mwaka wa fedha 2023/2024, 2024/2025 aliunda Tume ya Haki Jinai.

Haya ni matunda ya usikivu na namna alivyo na uzalendo namba moja katika Taifa letu. Alivyounda Tume hii pamoja na mambo mengine, Tume hii iliangalia hili suala la mrundikano magerezani. Rais Samia Suluhu Hassan, alilisimamia kidete na hatimaye mwaka wa fedha 2024/2025 sasa tumeenda kupumua na hakuna mrundikano magerezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme mwaka wa fedha 2022/2023 kulikuwa kuna wafungwa, magerezani pamoja na mahabusu 32,300. Leo ninavyoongea wako 27,500. Ni kwanini ninasema hili, Magereza yetu uwezo wa kubeba wafungwa pamoja na Mahabusu ni 29,900, unaweza kuona kuna upungufu mkubwa magerezani na watu wapo *comfortable*. Kwa maana magerezani ni mtakuja, nisipoenda mimi atakuwepo mwingine. Kwa hiyo, Rais ameandaa mazingira mazuri kwa wafungwa pamoja na mahabusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika haya, Mheshimiwa Rais amesimamia pesa za walipakodi. Kwa upungufu huu, kuna upungufu wa wafungwa na mahabusu 4,900 uki-*convert* kwa pesa ya kitanzania ambapo Mfungwa au Mahabusu anakula 5,000 kwa siku, maana yake Mheshimiwa Rais ameokoa bilioni nane na *something*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalendo haupimwi kwa maneno unapimwa kwa vitendo na katika hili madarasa 36 yanaweza kujengwa kwa hizi fedha. Huu ndiyo uzalendo tunaoongea, huu ndiyo upendo wa mwanamke huyu tunauongea siyo upendo wa maneno. Katika hili ametoa msamaha kwa wafungwa, ameweza kuendesha ya kuunda hichi chombo kupitia watu wetu, ameunda hichi chombo cha Mahakama Mtandao. Kuna changamoto katika Mahakama Mtandao. Maana yake ni nini, Wizara ichukue hatua ya kuelimisha Watanzania faida za Mahakama Mtandao ni nini, kwa maana wengi hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea Gereza la Isanga, tukakuta wafungwa wanasikiliza kesi zao kwenye Mahakama ya Mtandao *comfortable*, maana yake ni nini? Mrundikano umepungua lakini watu wako imara wanasilikiza kesi zao. Kuna changamoto ya *internet*, ninaomba Mheshimiwa Waziri alishughulikie hili, wakati kesi

zinaendelea kuna kukatikakatika kwa mtandao kwa hiyo kuleta adha kwa wasikilizaji na Waendesha Mashtaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kuna uhaba wa wataalam wa TEHAMA ambao wanaendesha mitambo ile. Ninaomba kupitia Magereza waajiriwe watu wenye weledi wa kuweza kusimamia hili. Vilevile kuna changamoto za nyumba zenye huo Mfumo wa Mahakama Mtandao, Waziri aliangalie ili dhima iweze kuchukuliwa inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo ninalipongeza Jeshi la Magereza wanafanya kazi ya kizalendo na ya utu, lakini ninaishauri Serikali, hawa watu wawekewe miundombinu thabiti, wana ekari zaidi ya 42,000 nchi nzima, lakini hawana vifaa vya kisasa vya kilimo. Ninaomba watu hawa wapewe vifaa vya kisasa, kwenye Taifa letu mvua ikinyesha badala ya kupiga magoti na kumshukuru Mwenyezi Mungu, watu wanaingia kusali kuomba na kulia kwa kuwa watavunjiwa nyumba na barabara zitaharibika kwa sababu hatujatengeneza miundombinu ya kupita maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Jeshi letu la Magereza liwezeshwe kutengeneza miundombinu ya kuvuna maji ya mvua, haya maji yasiwe kilio yawe kicheko ili yasaidie kunyeshea kwenye mazao watakayo yalima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee kwenye Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi linafanya kazi yake nzuri sana, kwa weledi mkubwa sana utulivu wa Tanzania ni matokeo haya. Ninaomba niwapongeze kwa namna ya tofauti, lakini kuna vituo ambavyo haviko sawa, Kituo cha Kata ya Mabogini Jimbo la Moshi Vijijini, Askari wanaogopa kukaa ndani, kituo kimebomoka hakifai kufanyia kazi. Ninaomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa aniambie ni lini kituo hiki kitajengwa ili kulinda wananchi zaidi ya 50,000 kwenye Kata ya Mabogini ambao wanategemea usalama wa hili Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa kuliko yote nikemee tabia mbaya ambayo watu wanaichukua *AI* wanaenda kuleta michezo ya ajabu, wanachora picha siyo nzuri kwa ajili ya kufanya

*bulling* kwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan. Kama Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ninakataa na ninakemea kitendo hiki, kwa sababu hakikubaliki. Kama Viongozi kwenye Taifa hili, kwenye Biblia wapo, kwenye Masaafu wapo; na kwenye *Quraan* wapo, waheshimiwe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aheshimiwe, siyo kumfanyia *bulling* kwa sababu ni mwanamke, eti kwa sababu kawaje. *No!* Ninakataa kitendo hiki, kwa sababu siyo afya kwa Taifa letu, Rais wetu yupo eti kwenye mitandao mara kachorwa katuni hii, mara katuni ile, ninakemea washindwe na walegee. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ni wanawake hatuwezi kuruhusu, haturuhusu tukio hili liendelee kutokea, tena wasijenge mazoea wakome, wasijenge mazoea. Kwa sababu wakijenga mazoea, watazoea kidogo kidogo, baadaye tutaona wameingia chumbani, watoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hayo, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante sana Mheshimiwa Felista Deogratius Njau kwa mchango wako mzuri sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na *IGP* kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa ajili ya Taifa hili. Ninawapongeza kwa mambo makubwa wanayoifanyia Tanzania. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri, amekuwa Waziri kati ya Mawaziri lakini kwa namna ya kipekee amekuwa Waziri wa kiraka pale ambapo Mama anaona sasa hapa ninamhitaji. Siyo hilo tu, tutume salamu Jimboni waturudishie kwa maana yeye ni rasirimali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru na kuwapongeza pia Makamishna wote, kwa namna ya kipekee nimpongeze Kamishna wetu Kombo kutoka Zanzibar, kwa kazi kubwa anayoifanya hususani

pale alipotugusa sisi wanawake viongozi wa Zanzibar, kutatua, kuondosha, kuhangaika na suala la unyanyasaji kwa wanawake na watoto. Kamishna, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninampongeza na kumshukuru Rais wangu Mama yetu Samia Rais, ambaye amekuwa Rais wa mfano ndani ya Nchi za Afrika. Tunapata taabu, Watanzania tuna uvumilivu, lakini namna wanavyotuona uvumilivu tulionao jambo kubwa la kupongeza ni Rais wetu kwa namna ya kipekee anavyotufundisha uvumilivu Watanzania. Pia uvumilivu wetu unaimarishwa na Jeshi la Polisi, namna wanavyoilinda Tanzania na namna wanavyofanya kazi ndani ya Tanzania wanatufunza Watanzania kuwa watu wavumilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu sasa umepita Watanzania tunavumilia na tunavumilia tena, lakini inafika wakati Jeshi la Polisi, leo Wabunge tumeamua kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya, hatuna sehemu ya kusema, kwa sababu ukija kila sehemu Mama amefanya vizuri na ameliimarisha Jeshi la Polisi vizuri. Tunachokitaka kwao, waende wakakomeshe vitendo vinavyoendelea kufanywa ndani ya mitandao vya kumdhalilisha Rais wetu. Waende wakaifanye kazi ya kuingia ndani ya mitandao kama walivyofanya kazi ya kupambana na majambazi wanaotumia vyombo vya moto, hawakuwashinda na walikuwa wanakuja na vyombo vya moto. Sasa tunataka waingie kwenye mitandao, kazi iliyopo kule vitoto vidogo hata kunyonya havijamaliza kwa wazee wao, kila mtu ana maneno na lugha anayoizungumza ambayo haistahili kuambiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu amekuwa akijitoa kwa ajili ya Taifa hili kwa namna ya kipekee, hakika Mungu alimwita kuwa Rais, tumwangalie kwa namna ya kipekee. Toka siku yake ya kwanza wakati mimba yake inatungwa Mwenyezi Mungu alijua kwamba anamtengeneza Rais Samia kuwa Rais wa Tanzania. Alijua fika kwamba, huyu ninamtengeneza kuwa Rais ndiyo maana akawa na roho ya uvumilivu, ambayo hata sisi viongozi tuliopo humu tusingeweza kuvumilia. Alimtengeneza kuwa mwanamke jasiri, kati ya

vitu ambavyo tunajivunia pamoja na ujasiri wa mama yetu kuweza kuvumilia hali inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wote Rais wetu anatuasa, halahala jirani, tumevumilia majirani, lakini imefika wakati mama watoto wake tumeshindwa kuvumilia, tumeshindwa hatuwezi, hakuna mtoto anayeweza kuthubutu kuvumilia kumwona mzazi wake anatukanwa, hakuna mtoto anayeweza kukaa kimya kumwona mzazi wake anatukanwa. Mama ametufunza tukae kimya, kwenye hotuba zake amesema mzigo huu anaweza kuubeba ila sisi watoto wako hatuwezi kuubeba, tumechoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaambie Vyombo vya Ulinzi na Usalama kuna kenge wa ndani halafu kuna kenge wa nje, washughulike na kenge wa ndani halafu wamalize na hao wa nje. Kumekuwa kuna vitoto hata vidogo mtu akipata, uhuru tunao Tanzania, tunafanya tunachokitaka lakini siyo kumgusa Rais wetu kwa vile unavyotaka mwenyewe. Kama tunataka twende kwenye *debate* za matusi, tutawafungulia Dotto Magari mmoja tu atamalizana nao. Bila kuweka mtu mwingine, Dotto Magari mmoja tu Kenya nzima watamtambua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na uvumulivu wa kutosha, lakini imefika wakati, Mheshimiwa Waziri, kazi ya ulinzi wa nchi hii ipo vizuri, kazi ya Jeshi la Polisi kulinda wananchi na mali zao upo vizuri, tunashindwa sasa kudhibiti mitandao, hatuwezi kuona nchi yetu inatawaliwa na mitandao. Jeshi la Polisi waangalie kwa umakini katika kitu kitakacholeta dhoruba ni pamoja na mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mtandao umekuwa unatumika vibaya ndani ya Tanzania, tunavumilia lakini tumechoka. Tunaomba mchukue hatua, hatuwezi Jeshi la Polisi kila siku Mama yetu Rais wetu anahangaika niboreshe wapi, niboreshe mishahara, niboreshe posho zao, niboreshe hiki, niwapatie magari, anahangaika kwa namna ya kipekee, tumlipe kitu kidogo tu, kumlinda yeye ni jukumu letu sisi, jukumu lao wao kama Jeshi la Polisi, jukumu letu sisi Wabunge, lakini jukumu la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni muda wa kumlinda Rais wetu, ni muda wa kulilinda Taifa letu kupitia Rais wetu, amevumilia lakini na yeye ni binadamu anachoka, lakini tabia ya Mama hawezi kusema kwa watoto wake kama anachoka, siku zote Mama hawezi kuona watoto wake wanalala njaa, yuko tayari kubeba jembe kulima ila watoto wale na kushiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala la mitandao kuna mambo mengi, hili suala la mitandao Mheshimiwa Waziri ninategemea, nilishawahi kuzungumza na wewe siyo mara moja, siyo mara mbili na ninashukuru kuna baadhi ya vitu naviona unavichukulia hatua. Suala la mitandao limekuwa tishio ndani ya Tanzania, kuna wengine huwa wanaiga, wamo ndani ya Tanzania, lakini wanataka kuiga vitu ambavyo siyo vya utamaduni wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kitu kimoja Mama yetu Samia anachokilinda kwa nguvu zake zote, pamoja na kulinda utamaduni wa Mtanzania na amani ya Mtanzania. Nguvu pekee ya kumpa ni kusimama sisi kama Bunge, kusimama sisi kama Watanzania kuhakikisha kwamba, tunamwambia Mama songa mbele tuko na wewe. Tutahakikisha hakuna siku mama yetu atakayotetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la wananchi wa Tanzania wanapopata fursa ya kwenda nchi za nje kufanya kazi, ile ni fursa ya kipekee na ninaiomba Serikali yangu Mheshimiwa Waziri, wasizuiliwe lakini kuwe na ufuatiliaji wa kina, hususani kwa watoto wanawake wanaokwenda mbali na nchi ya Tanzania kwenda kupambana na maisha yao, kuwe na fursa. Ninaomba Idara ya Uhamiaji washughulike na hawa mapaparazi wanaowachukua wadogo zetu na ndugu zetu wa kike kuwapeleka huko na baadaye taarifa zao zinakuwa siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahakikishe mtoto yeyote wa Kitanzania anapoondoka hapa, wajue ni nani kamchukua na wapi anakwenda na ule mfumo wa kufika kule kunyang'anywa *passport* zao, kunyang'anywa simu zao, kukosa uhuru na haki ya kibinadamu siyo sawa. Ninaomba kama viongozi tulishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mambo ambayo sisi Watanzania kwa sasa yanatusumbua katika nchi hii, ukiacha suala la mitandao ambalo linatusumbua basi na suala la ndugu zetu wa kike wanapoenda kujitafutia riziki nchi mbalimbali wanapoenda kule wanafika wananyanyasika. Mheshimiwa Waziri amekuwa akifanya kazi kubwa ndani ya Serikali, amekuwa akifanya mambo mengi ndani ya Serikali, lakini kuna watoto sasa hivi ndani ya Tanzania pia wanaiga, siyo utamaduni wetu, siyo utamaduni wetu shughulika na hili jambo wanaamua kuji-*record* kuweka dhihaka, kusema maneno mabovu juu ya Serikali, kusema maneno mabaya juu ya Rais wetu, hatuwezi kushughulishwa na kenge wa ndani ya bwawa tuliolitengeneza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri leo ninadhani umeona, Wabunge wote wamekuja letu kubwa ni kuipongeza Wizara ila tunataka mapambano dhidi ya mitandao iongezeke. Kama walivyoongeza nguvu kwenye masuala ya ujambazi, ubakaji na huku kwenye suala la matusi hususani pale, bora mtu akae atutukane sisi Wabunge, lakini siyo kumgusa Rais, siyo kumgusa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amebeba mzigo mkubwa, ameibeba Tanzania kwa mzigo mkubwa na kwa wakati ambao hakuutarajia. Mama kwa ujasiri wake ametuvusha, Mama kwa ujasiri wake ameipeleka Tanzania hapa ilipo. Tunajua hakuna mwanaume rahisi rahisi anakubali kuona kwamba kashindwa na mwanamke. Namna Mama yetu anavyofanya kazi kuna Mataifa, kuna wanaume wanamuone choyo, kuna wanaume wanamuonea wivu, lakini tunawaambia watulie, hiyo ndiyo namna mwanamke anavyofanya kazi na huo ndiyo ujasiri wa mwanamke anavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ninaunga mkono bajeti hii ipite, ninaiunga mkono mia kwa mia. Ahsante kwa hayo machache. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos kwa mchango wako mzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla sijampa fursa mchangiaji anayefuata ninaomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Ndugu Joachim Leonsi, *MNEC* kutoka Mkoa wa Manyara na Ndugu Shaban Mrisho, Katibu wa CCM Mkoa wa Manyara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kuna wageni wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Maafisa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Taasisi zake na Wadau wa Taasisi za Fedha, *Azania Bank*, Benki ya Watu wa Zanzibar, *NBC, CRDB* na *NMB;* wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Kagera na Kamati ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya CCM Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Paschal Rwamgata. Karibuni sana wajumbe hao kutoka Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Tuna vile vile Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi na Madiwani wa Wilaya ya Karagwe wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri Mheshimiwa Wallec Mashanda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Naibu Makamishna kutoka Vyombo vya Usalama vilivyopo Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi: Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji; ninaona bado hawajaingia. *(Makofi)*

Tuna pia Wanahabari na Wafanyakazi wa Ofisi ya Mbunge wakiongozwa na Ndugu Ivo Ndisanye. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Wajumbe wa Baraza la Usalama Barabarani Taifa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Manyara, Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Babati Vijijini na Wajumbe wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi, Mkoa wa Manyara. Karibuni sana wageni kutoka Manyara. *(Makofi)*

Tuna pia wageni 53 wa Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wa Kata kutoka Jimbo la Bagamoyo, Mkoa wa Pwani. Karibuni sana wageni wetu kutoka huko Bagamoyo. *(Makofi)*

Wapo vile vile wageni ambao wametembelea Bunge leo hii kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 50 na walimu nane wa Shule ya Awali na Msingi Micaih ya Jijini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Tunao Wanakwaya 29 kutoka Kwaya ya Upendo KKKT *Azania Front* ya Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanakwaya wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hii Wizara muhimu sana katika nchi yetu. Jambo la kwanza nimshukuru na nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ndugu yetu Mheshimiwa Bashungwa ambaye anaitwa ni kiraka wa Mama. Anapewa kila eneo lenye matatizo, anapelekwa anamaliza. Ni mtu mahiri sana, lakini ni mmojawapo wa Mawaziri wastaarabu sana katika nchi yetu. Ninampongeza kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi pia kwa Mheshimiwa Naibu wake Mheshimiwa Sillo, mchapakazi ametoka kwenye Bajeti ameshika vizuri Wizara na kusaidia, Katibu Mkuu wa Wizara, na *IGP* Wambura anayetoka kwenye Mkoa wa Mara; ametuheshimisha sana watu wa Mkoa wa Mara. Anafanya kazi nzuri maana yake ni kwamba akistaafu Mama tena ataona Mkoa wa Mara unastahili tena kupata mtu wa aina hiyo. Ametuheshimisha sana na ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mama yetu vilevile anafanya kazi nzuri sana yule wa uhamiaji. Sasa sijui yule ataendelea kuwepo maana yake ile wameongeza hata mikataba, kama mikataba yake imeisha nyie ongezeni tu anafanya kazi vizuri. Ni msikivu sana yule mama na anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wote wa Wizara, Polisi wote wa Wizara wanaofanya kazi na Makamishna wote wanafanya kazi nzuri sana. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tukubaliane kuna nchi duniani hazina vyombo vya ndani, hazina polisi, lakini kwa nchi za Kiafrika kama sisi Tanzania, polisi wakikosekana hata dakika moja wote mtakuwa mko ndani. Mtajifungia na mali zenu zote zitaenda. Kwa hiyo polisi ni watu muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri tuangalie maslahi ya polisi. Tuangalie wapi tunakwama katika kuwalipa vizuri polisi kwani wanafanya kazi usiku na mchana. Vyombo vya usalama vyote tuangalie. Polisi wanasema tuangalie namna gani tunawasaidia kupata uwezo wa kuendesha shughuli zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwapa magari 218 na pikipiki 105. Amefanya kazi nzuri sana ya kuwapa. Ili tuweze kujenga usalama wa kutosha kwenye nchi yetu, lazima polisi na vyombo vingine vya usalama vipate usafiri na vipate maslahi ya kuwatosha ili wapunguze gadhabu zao katika maisha yao ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi huru na siyo huru tu; katika Mataifa mengi ya Afrika sijui kama kuna mengine sisi ndiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Taifa letu ndiyo linaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni nchi huru, inahitaji amani, inahitaji usalama, inahitaji ulinzi wake wa kutosha, inahitaji kujilinda yenyewe, ina utamaduni tofauti, ina siasa tofauti, ina watu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndiyo kipekee huko nyuma mpaka leo ninadhani ulikuwa ukienda Dar es Salaam mpaka uende kwa balozi ndiyo uende wakujue kwamba umetokea wapi. Balozi ya nyumba 10 kwa nchi yetu analinda mtu, hakuna nchi nyingine ya

kufanya hivyo. Kwa hiyo sisi ni nchi pekee ambayo inaweza kufanya kazi zake kwa kujilinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaongea hapa na wenzangu tumeona chombo muhimu sana duniani *CNN* kutoka Marekani kinasema Mheshimiwa Rais Samia hapingi wanaharakati bali anapinga kuingiliwa na wanaharakati. Hapingi wanaharakati amesema anapinga upotoshaji na kuingiliwa kwa wanaharakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima kila nchi iwe na uwezo wake; kwa sababu gani? Sisi tuna wanaharakati wa ndani wafanye uwanaharakati wao lakini siyo tupokee wanaharakati kutoka maeneo mengine waje kuingia kwenye nchi yetu; hapana. Mheshimiwa Bashugwa na *IGP* Wambura kazi hiyo waifanye iende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaangalia hapa ripoti mbalimbali. Nimeangalia ripoti ya *Global Peace Index* ya 2024; ile ripoti ya amani inasema, dunia ya leo imepata misukosuko ya migogoro na ghasia na watu wengi wanakufa kwa ajili ya migogoro na hizo ghasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti inasema dunia ijipange kujilinda usalama wake katika nchi yake (ijilinde kiusalama). Kwa hiyo ripoti imesema wazi 2024. Sasa ni nini kinafanyika? Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lazima alinde usalama wa nchi yetu na pengine huwa ninasikia maneno tu wanasema Mheshimiwa Rais mpole, Mheshimiwa Rais mpole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Rais aliwahi kutokea kuwa mpole, haipo na ndiyo maana anaitwa Amiri Jeshi Mkuu. Amiri Jeshi Mkuu maana yake ni kwamba Jeshi halifuati sheria linafuata amri. Sasa huwezi kuwa Amiri Jeshi Mkuu halafu ukawa mpole, haiwezekani. Kwa hiyo kwa vyovyote vile Rais ni *system* na Mama Samia ni jina la mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaposema Mama Samia ni Rais wa nchi maana yake anafuata, ni Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi. Pale

ambapo nchi yake inaingiliwa anakuwa tofauti na niwaambie Waheshimiwa Wabunge sijui kama mnamtazama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote ukimwona Mama inaonekana usalama wa nchi unayumba utamwona machoni, anabadilika kabisa. Anakwambia, ukisikia mama anasema hii hapana ujue amefika mwisho. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais analinda usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ripoti hii ya *Global Peace Index* imeonyesha kwamba kuna nchi 10 zaidi Afrika zenye amani zaidi. Nchi ya kwanza ameitaja Mauritius, imekuja Madagascar, imekuja Botswana, imekuja Ghana, imekuja Zambia, imekuja Namibia, imekuja Tanzania, imekuja Siera Leone, imekuja Liberia, na imekuja Angola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya Mheshimiwa Rais wetu anaposema nchi yetu ni nchi pekee ya kimbilio la Afrika Mashariki, unakataa nini? Wewe unakataa nini? Ripoti imesema, katika nchi zilizotajwa hapa Nchi za Afrika Mashariki ni Tanzania peke yake na ni ya saba. Kwa hiyo sisi tulikuwa wa kwanza na tunaenda hivi, lakini mwishoni tutakwenda kuanguka kama hatutalinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwaombe kwamba katika nchi yetu lazima tulinde amani yetu. Tumekuwa uhuru wetu tuliupata tofauti, ni moja ya nchi zilipata uhuru wake na uhuru tulioupata ulikuwa ni uhuru wa amani, hatukutoa damu tulipata uhuru wa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetazama *clip* nyingi sana, niwashukuru sana wale viongozi wa Kenya na wananchi wa Kenya waliopinga hatua za wale watu wanaharakati kuja kutuingilia hapa. Wamepinga sana, nimeona wananchi wanapinga, nimeona viongozi wanapinga; tunawashukuru sana lakini tunawalaani wale wanaomwandika Mheshimiwa Rais vibaya na wale wanatukana Mheshimiwa Rais wetu tunawalaani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kenya ni nchi yetu sisi tuko pamoja, tunapendana, tunafanya biashara, tuishi pamoja. Niwaombe Waheshimiwa Marais wasiingilie hivyo vitu vya watu wahuni wahuni hawa wanaokuja kutuvuruga na wenyewe tukaingia kwenye uhuni hapa bali wakubaliane kwamba wale wote ambao wanatenda nje ya sheria wakamatwe katika nchi zao kwa sababu siasa za Kenya siyo siasa za Tanzania. Kwa hiyo niombe na niwashukuru sana wale watu wa Kenya wanaokataa mambo hayo, wanaopinga uharamu walioufanya wanaharakati waliokuwepo ili tuendelee na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hayo kwa sababu nchi yetu inahitaji amani. Tunahitaji amani sana sana sana na hakuna mtu anaweza kupinga na hakuna mtu anaweza kusema kwamba tunaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Shirika la Fedha Duniani limeonyesha mpaka sasa nchi yetu pato la Taifa ni kama bilioni 85.6 hivi na linasema kwamba, kama Tanzania itaenda na amani yake hivyo hapo ilivyo ikifika 2028, nchi yetu itakuwa na pato la Taifa ambalo litakuwepo shilingi bilioni 136.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hatuwezi kulinda mikakati yetu ya kimaendeleo na miradi ya kimkakati ambayo tunayo, hatuwezi kufikia hilo pato. Kwa hiyo tunaomba amani yetu iendelee kulindwa. Viongozi wetu wa polisi, viongozi wetu wa kijeshi na watu wote wa Tanzania tuendelee kulinda amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niiombe Serikali ya CCM huko tunakokwenda tuanze kufanya *vetting* ya watu wanaoingia madarakani na hata sisi Waheshimiwa Wabunge tufanyiwe *vetting.* Hii habari ya kuandaa watu na kuwapa madaraka halafu katikati hapa anaanza kutukana Serikali; hapana! Tufanye *vetting* ili wazalendo wa nchi hii waendelee kupewa vyeo na wale wahuni wahuni wakae pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Nilimtaja Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa, Waziri wetu wa Mambo ya Ndani na Mheshimiwa Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana kwani ni watu makini, watu wanyenyekevu sana. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuona kwamba wanaweza wakamsaidia katika kuhakikisha kwamba mnasimamia Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hongera sana kwa kaka zangu, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria kwa upande wa Afrika, Afrika ya Mashariki na Dunia, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *it is a sovereign state* (hii ni nchi huru). Ninakwenda mbali kusema kwamba Taifa letu ndilo Taifa lenye historia Afrika. Ninarudia; Taifa hili ndilo Taifa lenye historia Afrika ya kuwafanya Mataifa ya Afrika wawe wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili liliwafanya Msumbiji wakawa wamoja, Taifa hili liliwafanya Zambia wakawa wamoja kama mnasoma historia, Taifa hili liliwafanya Namibia wakawa wamoja, Taifa hili liliwafanya South Africa wakawa wamoja, Taifa hili liliwafanya Comoro, Seychelles na nchi zingine kuwa wamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili lilirudisha *stability* na umoja Uganda, Taifa hili hata hao Kenya baadhi ya wanaharakati wanaojaribu kufikiri kwamba hili Taifa ni la hovyo, walipoanza kuchinjana miaka michache iliyopita, ni Taifa hili lilikwenda Kenya likarudisha umoja, amani na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimnukuu Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Baba wa Taifa letu, Kiongozi aliyekuwa amepewa karama na Mungu ya kuliunganisha Afrika na kuiunganisha Tanzania alisema: *"Ninajua nitakufa sitapona ugonjwa huu, ninawaacha Watanzania wangu ninaondoka nikiwa*

*nimewaachia Taifa moja lenye umoja na amani. Wosia wangu kwao, waipende nchi yao kama wanavyowapenda mama zao wajue hakuna nchi nyingine zaidi ya Tanzania." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno aliyatamka Baba wa Taifa akiwa kitandani hospitalini London. Baba wa Taifa alijua kwa sababu alikuwa Rais wa nchi hii, aliona viashiria vyote ambavyo vilikuwa vinanyemelea kuligawa Taifa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu wa wakati huo Mwalimu Nyerere akiwa amestaafu, kitandani karibu mauti inataka kumfika, roho wa Mungu alimshukia akiwa kitandani akasema nitoe maneno gani ya kuhakikisha *stability*, umoja, mshikamano wa Taifa langu utakuwa salama kwa miaka 100 ijayo? Akasema, "Ninawaasa Watanzania walipende Taifa lao kama wanavyompenda mama yao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie tumebahatika kupata Rais Mama katika Taifa letu, tumebahatika kupata Rais Mwanamama katika Taifa letu. Sisi Watanzania hatujafundishwa kebehi, sisi watoto wa Mwalimu Nyerere hatujafundishwa kuwachukia majirani na ndiyo maana waliponyanyaswa, walipobaguliwa tulikwenda kuwapigania tukatoa damu za Watanzania, tukamwaga damu za watu wetu, majeshi yetu na vyombo vya ulinzi na usalama vikaenda kujitoa muhanga kuleta *stability* ya Mataifa ya Afrika, mfano ambao hauwezi kuigwa na Taifa lolote lililopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ndiyo Taifa liliamua ku-*sacrifice* maendeleo ya watu wake, watoto wetu wakakosa elimu bora, vizazi vyetu vikakosa usafiri bora tuka-*sacrifice* kuliunganisha Bara la Afrika. Tunaomba tuwakumbushe majirani zetu wa Kenya na Mataifa mengine na hili tunazungumza kutoka kwenye Bunge, Chombo kilicho huru cha Kikatiba, tunawaonya sana wanaharakati wanaofikiri ya kwamba Taifa hili ni choo kila mtu anaweza kwenda kujisaidia na kutoka. Ninataka niwaambie kwa Viongozi waliopo madarakani na sisi vijana ambao tutakuja kukabidhiwa Taifa hili, hakuna kiumbe chochote kitaweza kuligawa Taifa hili. Hili ni onyo kutoka kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambie, sisi Watanzania tunampenda Mheshimiwa Rais Ruto wa Kenya, sisi Watanzania tunampenda Mheshimiwa Rais Yoweri Museveni wa Uganda, sisi Watanzania tunampenda Mheshimiwa Paul Kagame wa Rwanda, sisi Watanzania tunampenda Mheshimiwa Rais wa Burundi, tunampenda Mheshimiwa Rais wa Kongo na Mataifa yote ya Sudan na Somalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania hatuna chokochoko ila ninawaonya majirani zetu, *they should never ever dare again,* wasije tena; ninatoa onyo. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninatoa onyo kwa vibaraka wanaokubali kutumika kwenye Mataifa yao, Tanzania siyo mahali salama kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili linaye Kiongozi Mheshimiwa Rais Mwanamama jasiri, shupavu na mzalendo ambaye amefanya mambo makubwa kwa Taifa hili. Sisi kama chombo kinachowakilisha wananchi kwenye Bunge hili tutalinda Taifa letu, tutalinda nchi yetu kwa wivu mkubwa, kwa gharama kubwa na Mungu atusaidie tutakwenda kushinda kila majaribio yanayotaka kuligawa Taifa hili kwa misingi ya ukabila, kwa misingi ya dini, kwa maslahi ya watu wachache wanaowatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninataka nitoe pongezi kwa Jeshi letu la Polisi Tanzania na vyombo vyote vya ulinzi na usalama. Ninataka niwaambieni yalipokuja majaribio ya kuligawa Taifa letu vipande, Rufiji na mikoa mingine Jeshi hili hili ambalo wanalisonta vidole lilisimama na kurudisha amani na utulivu wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie yalipokuja majaribio ya kigaidi kwenye mikoa ya Kusini na sehemu zingine, sisi tunalala, lakini majemedari hawa usiku na mchana wanagharimu hata familia zao wanalinda amani ya Taifa hili. Wapo tayari kupoteza maisha kulinda umoja na mshikamano wa Taifa letu. *IGP* Wambura popote ulipo wewe na makamanda wake na askari wake, ninataka nimwambie asitishwe, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lipo na yeye, lipo na askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wangu popote pale alipo, akipata ujumbe kusikia ujumbe wangu ninamwomba mwakani uchumi ukikaa vizuri apandishe mishahara ya watu wetu hawa, majemedari hawa, vinara hawa, wanaolilinda Taifa letu kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, ninataka niwaase Watanzania wote wanaolipenda Taifa lao, nyakati hizi Mheshimiwa Waziri amesema vita vya kimaslahi ya Kitaifa, vita vya Kikanda, *geo-political politics* za duniani siyo lazima Taifa likuvamie na vifaru. Chokochoko zinazopenyezwa kwenye Taifa letu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama wasimame imara. Baba wa Taifa kaburini alipo anawaangalia wao, anawaangalia Watanzania, anawaangalia kila mmoja kuhakikisha tunatimiza jukumu letu la Kikatiba la kuilinda Tanzania kwa gharama yoyote ile. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu kwa kutukumbusha wosia muhimu sana wa Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa letu. Ninaamini Watanzania wanakumbuka.

Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia asubuhi hii na michango yenu yote ambayo ninaamini kabisa ina tija kwa Taifa letu. Mimi pia ninawaunga mkono kwamba vyombo vyetu vya ulinzi vinafanya kazi kubwa na vina stahiki kupewa moyo na kuweza kuwezeshwa zaidi. Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Sillo ninaamini kabisa bajeti yenu ikipita leo ya shilingi trilioni 2.67, mambo yote yaliyozungumzwa yataenda kufanyiwa kazi na nchi yetu itakuwa na amani zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nina tangazo la wageni ambao wapo muda huu. Tuna wageni 70 wa Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan ambao ni Wanakwaya wa Kwaya ya Bikira Maria Mama wa Mungu (BMM) wa Parokia ya Mtakatifu Yohana wa

Mungu kutoka Yombo Vituka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wanakwaya wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla sijasitisha Shughuli za Bunge ninaomba niwataje wachangiaji watakaoanza kuchangia jioni hii ya leo ambao ni Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na Mheshimiwa Juma Othman Hija.

Baada ya kuwataja hawa wachangiaji wa jioni, ninasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.02 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mheshimiwa Juma Usonge na Mheshimiwa Juma Othman Hija wajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kuniruhusu nichangie hotuba hii ya Wizara ya

Mambo ya Ndani. Wizara muhimu kabisa iliyobeba dhima ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kuchangia kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutumia nguvu kubwa na busara nyingi kuliwezesha Jeshi la Polisi na kulibadilisha liwe na weledi. Jambo hili halikuwa rahisi, miaka iliyopita Polisi walikuwa na kazi ngumu sana ya kufanya, pesa nyingi ambazo Mheshimiwa Waziri amezitaja katika hotuba yake, ili kulijenga upya Jeshi la Polisi na vyombo vyake vingine, Uhamiaji na Magereza, zimefanya Jeshi hili na Wizara nzima ibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, Mheshimiwa Waziri kwa kutekeleza vyema maono ya Mheshimiwa Rais na bila kuwasahau Ndugu *IGP* Wambura, *CGP* Katungu, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Wamefanya kazi nzuri sana kwa kipindi ambacho wamekuwa madarakani, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mapema tumesikia jinsi Wabunge walivyopata uchungu na kusema waziwazi kwamba, tulikosewa. Kumkosea Rais wetu lilikuwa jambo baya sana, lakini sisi wananchi wote wa Tanzania tumeumia kwa kitendo cha jirani waliokuja hapa, kuvaa njuga na kuanza kusema mambo ambayo, kwanza hawatuhusu sisi na wala sisi hatuwahusu. Wamejitokea tu wanakuja kusema mambo ya hovyo hapa kwetu, ninasema, vyombo vya ulinzi na usalama vimefanya jambo kubwa sana, ila mimi naona kwamba, wangeenda mbele kidogo, ili hao watu wasiseme kabisa tena huko tunakokwenda. Tumewafanyia, wamekiona kilichomtoa kanga manyoya, lakini ninafikiri tungeenda mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akumulikaye mchana na moto usiku atakuchoma na moto. Kwa hiyo, tusikubali tena watu wa namna hii kuja kwetu wakiwa na mdomo wazi, kuja kutusema au kututukania kiongozi wetu, tusikubali tena. Waziri na vyombo vyake vya usalama wawafuatilieni hao watu maana ni vigumu kwamba, walikuja peke yao. Tumekuwa na *quote,* tunanukuu busara ya Baba yetu wa Taifa Mwalimu Nyerere aliposema, shoka halikati mti mpaka liwe na mpini,

inawezekana kuna mpini wa mtu umebaki hapa. Wafuatilie ili na huo mpini wautupilie mbali libakie shoka ambalo haliwezi kukata kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tumeona hivi karibuni watu wameanza kuacha uadilifu na utii kwa taasisi, hasa Taasisi ya Rais. Haijulikani kimetokea nini, lakini kuna dalili zote kwamba, kuna watu fulani wameanza kuwa juu na kuota mapembe juu ya Taasisi ya Rais. Hatumsemi Rais, hawasemi Rais, wanasema taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia *clip* moja hapa, mtu mmoja mwenzetu, ndiyo ninasema mpini, shoka halikati bila mpini, lazima kuna mpini, anasema huenda anavyoamini yeye, aliona teuzi zote zilizofanywa na taasisi hazikuwa sahihi na anaomba atoe maoni yake yeye. Sasa maoni ya mtu binafsi na taasisi, kipi kikubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapungufu haya yakiachwa kuendelea yanaweza yakatuletea matatizo huko baadaye. Mheshimiwa Waziri na vyombo vya ulinzi na usalama vifanye kazi yake na ninashauri sana ikiwezekana mambo haya yafanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nirejee kidogo kulisemea Jeshi la Polisi. Hawa Polisi tunaowaona hapa wakisaidiwa na sekta ya ulinzi binafsi na sisi tukawa na imani kwa sababu, wao wanafanya kazi ya ulinzi wa raia na mali zetu; wako Polisi wamebadilisha amani tuliyonayo na maisha yao, wamebadilisha imani tuliyonayo sisi hapa kula na kushiba na kulala na maisha yao. Wamefariki, wamefia kazini watu hawa, tutawalipa nini familia zao walizoziacha na baba zao waliowaacha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa wanawategemea, wametangulia mbele za haki. Haiwezekani mtu atoke nje aje adharau *system* yote hii na watu wanaifia bila sisi kuisemea na hasa waliofariki kazini. Sisi tuna haki ya kuwasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana wale Askari Polisi ambao wamefariki kazini, hata wale wa sekta ya ulinzi binafsi, Serikali

iwaangalie, iwakumbuke, iwatie kwenye kumbukumbu rasmi kwamba, hawa wamekufa kwa sababu ya uzalendo. Hili litasaidia vijana wengine kuingia Jeshi la Polisi na kwenye sekta ya ulinzi kwa nguvu zaidi wakiwa na nia ya kumtetea na kumlinda Rais wao, ambaye ndiye Kamanda Mkuu wa Ulinzi na Usalama wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi nilikuwa ninatetemeka. Ninaogopa sana kwamba, kuna mmoja wetu humu ndani naye kaanza ku-*querry,* anauliza imekuwakuwaje hawa watu? Imekuwaje, mimi nimeshangaa sana! Iko haja ya kufuatilia kanuni za watu kama sisi, *status* kama yetu, tunapotoka nje unasema ninalivua gwanda, kama Koti la Ubunge, nalivua gwanda la unanii na u-*NEC* kauvua na kiapo kakivua!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu sana. Lipo suala la sekta binafsi ya ulinzi, naomba pia, ufikirie kuwa na Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi. Itasaidia sana kuwasogeza karibu sekta ya ulinzi binafsi wafanye kazi moja na Jeshi la Polisi, kazi ile ya ulinzi wa raia na mali zao, lakini waanzishiwe Mamlaka yao chini ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige. Anafuatia Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mheshimiwa Juma Othman Hija, na Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, wajiandae.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia jioni hii kwenye Hotuba ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa yao hapa leo asubuhi, lakini pia, ninawapongeza sana vyombo vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri, ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Tanzania kuridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa, lakini jukumu la kulinda amani pamoja na ushirikiano wetu ni letu sisi, kama nchi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hatua nzuri; juzi, Mei 19, alipokuwa akizungumza na viongozi mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuhusiana na kuzindua ile Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001, Mheshimiwa Rais ametamka maneno kuashiria kwamba, hajafurahishwa na vitu vinavyoendelea sasa hivi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo baadhi ya Wabunge hapa asubuhi tulipokuwa tukiwasikiliza, inadhihirisha wazi kabisa sisi, kama Taifa na kama viongozi hatujafurahishwa na kauli za wenzetu, majirani zetu, ambao tunawapenda, lakini wapo baadhi ya vijana wanaharakati, wanadhihaki mamlaka vibaya kama vile wametumwa na nchi yao. Sisi, kama viongozi, hatujafurahishwa hata kidogo, tunamuunga mkono sana Mheshimiwa Rais kwa kauli ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimepewa jukumu kubwa la kulinda na pia, kuhakikisha amani ya nchi inakuwa salama zaidi. Kwa hiyo, tuwaombe sana wenzetu, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, lazima tuwe makini sana, hususan kipindi hiki ambacho tunaelekea kwenye uchaguzi. Hawa watu ambao wanajiita wanaharakati nyakati zote hizo walikuwa hawaonekani, sasa tunaelekea kwenye harakati hizi za uchaguzi ndiyo wanajileta katika nchi yetu. Tusipokuwa makini wanaweza wakaja kutupoteza na sisi Tanzania tukawa kama nchi za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalipongeza sana Jeshi letu la Polisi. Ni Jeshi imara, liko vizuri kabisa kwa hiyo, waendelee kupiga kazi, lakini pia, kuitunza tunu yetu, ambayo imeachwa na viongozi wetu waliotangulia. Pia ninamtia moyo sana Mheshimiwa Rais aendelee siku zote kukumbusha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pale vinapojisahau. Mheshimiwa Rais ameapa kuhakikisha kwamba, kwenye kipindi chake cha uongozi amani yetu haiwezi kupotea. Kwa hiyo, ninampongeza sana kwa kauli yake hiyo ya kutamka kabisa na kuvipa tahadhari vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo pia, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, Wizara yake hususan, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi vizuri, lakini miongoni mwa majeshi ambayo *perception* ya nje huko inaonekana kuna vitu fulanifulani bado havijakaa vizuri. Tuangalie kwenye bajeti hii na bajeti nyingine zinazokuja tuhakikishe wenzetu wa Jeshi la Polisi wanaongezewa mishahara, hili ni mhimu sana. Wenzetu wanafanya kazi saa 24, leo hii kama wasingekuwepo hawa ndugu zetu wala tusingekuwepo tunajadili mambo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara, Mheshimiwa Rais ni msikivu mzuri, ninaamini wakimpelea *proposal* ya kuwaongezea mishahara wenzetu hawa kwa hilo hana shida, anaweza kuwaongezea mishahara. Ukipita hata barabarani utakuta askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, utawakuta askari wetu hata zile *uniform* zimepauka kwa jua kali. Kwa hiyo, naomba sana Wizara, hawa wenzetu wanafanya kazi ya kizalendo, hawafanyi kwa maslahi ya mtu au jambo fulani, wanafanya kazi kwa niaba yetu sisi, kama raia na wananchi. Kwa hiyo, lazima tulipe hadhi Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi jirani hapa, ndogo tu, kwa mfano kama Rwanda; hata ukipita barabarani unawakuta askari wamekaa *smart* kabisa, wako vizuri na mimi hamu yangu ni kuona Jeshi letu la Polisi tukipita barabarani tunakuta wako *smart,* wanavaa vizuri kabisa, hawacheki na mtu wako kwenye kazi zao. Kwa hiyo, ninadhani tukielekea huko tutakuwa tuko vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie. Mheshimiwa Waziri kila mwaka hapa kwenye bajeti hii nimekuwa nikizungumzia vituo vyangu vya polisi. Nina Kituo changu cha Polisi cha Hani, Lungalunga, ni miaka, siku zote nikisimama hapa nakizungumzia. Mheshimiwa Waziri kabla ya ku-*wind up* anaweza akafanya mawasiliano kule Kaskazini Unguja akakiulizia hicho Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana walitenga zaidi ya shilingi milioni 80, kituo hicho mnataka kukijenga kwa daraja la B, lakini mpaka leo hii hakuna shughuli yoyote inayoendelea. Mheshimiwa

Waziri atakapokuja ku-*wind up* ninaomba nipate majibu ya kituo changu hiki cha Polisi kilichopo Lungalunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina Kituo kingine cha Polisi kiko Pwani Mchangani, nacho ndiyo hivyohivyo. Kituo hicho wananchi wamejitolea kutoa eneo lao, lakini kuna mwekezaji pale, mzungu, *Ocean Paradise* na *Neptune* wametutengenezea kituo cha polisi kizuri, lakini toka mwaka juzi mpaka leo hii kituo kile bado hakijakamilika. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara, pale palipobakia, wale wenzetu wameshakitengeneza bado kama 30%, ninaiomba Wizara yake basi kipindi hiki kilichobakia, hebu twendeni kule tukakimalizie kile Kituo cha Polisi, ili wananchi wa Pwani Mchangani na maeneo yale yote jirani wapate Kituo kile cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninakushukuru sana na pia ninaunga mkono hoja ya Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Usonge Hamad. Nilimtaja Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri wajiandae.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaungana na Wabunge wenzangu ambao wamechukua nafasi kubwa katika kumpongeza Mheshimiwa Rais tangu asubuhi mpaka sasa. Mheshimiwa Rais ni tunu kwetu. Mheshimiwa Rais ni mtu ambaye tumeletewa sisi na Mwenyezi Mungu kwa hiyo, mimi ninatoa ushauri mmoja tu kwa wenzangu, ambapo mambo mawili haya yaende sambamba; tunapomsifu na kumpongeza Mheshimiwa Rais basi, ni vema tukamwombea pia. Tunampongeza kwa juhudi zake, lakini tuchukue nafasi ya kumwombea, yeye ni binadamu, ana maadui nje na ndani. Kwa hiyo, tunapokaa tunampongeza basi, ninaomba tuendelee kumwombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi naye, kwa juhudi kubwa ambazo anazifanya katika Kisiwa chetu cha Zanzibar. *Speed* yake ni kubwa, kwa muda mfupi tumeona maendeleo makubwa ambayo yamepatikana kule kwetu Zanzibar. Hivi sasa Zanzibar maisha ya shamba na mjini hayapishani sana, *almost* yanakaribiana, unachokikuta mjini basi na shamba kipo. Kwa hiyo, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt.Hussein. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii vile vile kumpongeza sana Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyotayarisha ripoti hii na kuiwasilisha katika Bunge letu Tukufu kwa umakini sana. Hawa lazima tuwapongeze, waendelee kufanya juhudi zao kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo katika mchango wangu, kutokana na muda, nitachangia jambo moja tu, lakini nitachambua kwa urefu kidogo. Katika hotuba ya Wizara hii ya mwaka jana 2024 aliweka vipaumbele sita; moja kati ya vipaumbele hivyo ilikuwa ni kukamilisha na kuendeleza ujenzi wa vituo vya polisi na makazi ya askari wetu. Kipaumbele hiki ndicho tuliongelea sana Wabunge wakati ule, mwaka jana 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu, ninaishukuru sana Serikali kwa kutujengea Kituo katika Kisiwa kile cha Tumbatu, lakini mpaka sasa kituo kile bado hakijamalizwa. Kwa hiyo, ombi letu kwa Wizara hii ni tunaomba kituo kile kimalizwe kwa sababu, mahitaji ya ni makubwa na kila siku yanaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa katika bajeti yao ya mwaka huu wa fedha 2025/2026, katika Aya ya 68 wameweka, wanakarabati vituo 31. Wametenga shilingi bilioni 5.2, kwa ajili ya kukarabati na kujenga vituo vingine, lakini Waziri hakusema kwamba, vituo 31 hivi kimoja kiko Lindi, kimoja kiko Makunduchi, kimoja kiko Tumbatu! Kwa hiyo, hatujui katika maeneo yetu ni kituo gani kitafaidika katika Bajeti hii ya Mwaka huu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie, katika vituo hivi, katika *concern* hii

na wewe Kituo chako cha Tumbatu kimo au hakimo na kwa nini hakimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la makazi kwa kweli bado ni tatizo sana katika vituo vyetu vya polisi. Kituo changu cha Mkokotoni, tuna kituo cha kisasa pale lakini makazi yake ya pale Mkokotoni kwa kweli hayaridhishi hata kidogo. Kwa hiyo ninaomba sana Wizara iziangalie zile nyumba katika Kituo kile cha Mkokotoni ili izikarabati. Kuna nyumba pale zimejengwa kabla ya Mapinduzi, kwa kweli hazistahili kabisa kukaa askari. Kwa hiyo ni vema na pale napo tukapata makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua sisi wengi katika kuishi kwetu tunaamini kwamba vitendea kazi katika Wizara hii ni bunduki, risasi, mabomu na mengine; lakini makazi pia ni kitendea kazi. Unapomkosesha askari makazi hawezi kutenda kazi yake kwa ufanisi. Kwa hiyo makazi ni miongoni mwa vitendea kazi, siyo bunduki tu. Kwa hiyo tunaomba Wizara ichukue hatua ya kutosha ya kuridhisha juu ya askari wetu hawa ambao wamo kwenye vituo hivi, hasa vile *scattered* ambavyo vipo mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Juma Othuman Hija. Nilimtaja Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri na Mheshimiwa Haji Amour Haji, wajiandae.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote kwanza ninaomba niombe radhi na unisamehe kwa sababu leo tuko na Wizara moja ambayo ni muhimu sana. Kwa hiyo ninaomba ukubali nikukwaze kidogo kwa muda wako; kwa sababu ninadhani yako mambo kama Taifa lazima tujifunze. Kwa hiyo nitakuomba univumilie, hata yule mwenye *alarm* aweke kidogo pembeni ili itusaidie, ninakuomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Pili, ninaomba kumpongeza

Mheshimiwa Rais. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu kwanza tuko kwenye kipindi kigumu, pili kama Amiri Jeshi Mkuu na tatu kama mama. Yote haya anayo yeye mtu mmoja, jambo ambalo ku-*balance* kati ya ujemedari mkuu, urais, na umama ni mambo magumu sana, lakini bado ameendelea kuwa Rais, ameendelea kuwa Jemedari Mkuu, vilevile ameendelea kuwa Mama. Ningependa kumwomba kwa niaba yangu na kwa niaba yenu mama aendelee kutulea. Kwa sababu bila hivyo sisi vijana wake hasira ziko kwenye utosi; sasa ili tufike lazima atushike mikono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake, kazi yake ni kubwa. Tunapozungumza Wizara hii ndiyo Wizara ambayo inatulinda kwenye kila hali. Wanatulinda nyumbani, wanalinda mali zetu, wanalinda mipaka yetu; kwa sababu Wizara hii kuna Polisi, kuna Uhamiaji na kuna Magereza. Kwa hiyo hawa ni watu ambao wanafanya kazi zetu nyingi. Kuna *NIDA* humo; zote hizi ni kazi za ulinzi na wenzetu wanazifanya vizuri; na kwa kweli tunashukuru sana na waendelee kufanya kazi hii. Ni ngumu, lakini waendelee kufanya kwa sababu ndiyo wajibu tuliowapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa pia kuipongeza Serikali kwa sababu Wizara hii ni Wizara kubwa, Wizara hii ina majukumu mengi; lakini pamoja na majukumu mengi Serikali imekubali kuwapa bajeti nzuri. Ukiangalia kwenye hesabu za harakaharaka mpaka hivi tulivyo wamefika karibuni 60% ya uwezesho kwa Serikali, ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hiyo ningependa kuiomba Serikali, kwamba sasa hivi tuko kwenye kipindi kigumu, kipindi cha majaribio. Kipindi ambacho tunaelekea kwenye uchaguzi na uchaguzi ambao ukiuangalia unaona kama vile kuna chembe za shari. Sasa chembe hizi za shari maana yake ni cheche inayokwenda huko mbele. Kama hatukuishikilia vizuri maana yake inaweza ikaliharibu Taifa. Ninasikitika sana kwamba mambo yanayotokea wazee wetu wapo wengi, lakini huwasikii hii wakiona kwamba Taifa limetetereka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme hivi; pamoja na kwamba inawezekana Katiba yetu ina mapungufu, sheria zina mapungufu na kwamba tunahitaji kubadilisha, lakini hatubadilishi kama inavyokuja radi, kubadilisha Katiba na sheria ni mchakato. Sasa imefika mahali wako watu wanaamini kwamba wao ndiyo wana haki kamili za kuwa Watanzania. Wako watu wanaamini Katiba hii ni ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwakumbushe hawa marafiki zangu. Huko zamani yalikuweko mataifa mawili, sikuwepo na wala wengi wetu humu hawakuwepo. Kulikuwa na Taifa linaitwa Tanganyika, kulikuwa na Taifa linaitwa Zanzibar, haya yalikuwa ni mataifa mawili tofauti. Sasa, ili iwe Tanzania maana yake kila mmoja aliacha mamlaka na uhuru wake tukatengeneza kitu kimoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inasikitisha kuwaona wanasiasa wetu wanatoka barabarani wanafanya ubaguzi, wanavunja sheria halafu wako wazee, watu wazima hawasemi kitu; lakini mama amekubali kuvumilia. Sasa ninaomba niseme hivi; kwanza mtu anayeitwa Mama Samia Suluhu Hassan hakuanza yeye na mchakato wa Katiba. Mchakato huu ulimkuta akiwa miongoni mwa Mawaziri, lakini hajakataa kuendeleza. Ila suala hili si la kufunga na kufungua macho. Sasa tabia zinazoendelea za kumshambulia mtu kwa uanawake wake, kwa anakotoka hii haiko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo huwezi ukasema unasimama hadharani unasema huyu mwanamke anatoka kwao, mwanamke gani wakati huyu ni Rais wa Jamhuri? Hii ni kuvunjiana heshima, hii ni dharau na sisi kwenye Katiba na sheria tumeambiwa kwamba binadamu sote ni sawa, hakuna aliye bora mbele ya mwenzake. Mbona wazee wetu wengine hawasemi ambao wanaonekana wana busara? Hivi hizi busara ni za kutukana tu viongozi? Mbona hawa wanapokosea hawaambiwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana hawa wazee ambao tunawaamini kwamba wana busara ni busara hizo hizo wazitumie kuwakanya vijana wao. Kwa sababu sisi pia damu inatuuma kwamba anatukanwa Rais wetu, anatukanwa Jemedari halafu wale wazee

wamenyamaza kimya. Linapotokea jambo lingine huku wanakuwa *frontline* kumshambulia Rais, hili hatulikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa sana kuwaomba, kwamba wakubali na waelewe kwamba Tanzania siyo Tanganyika, Tanzania ni Tanzania, kwa maana ni Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Sasa watu hapa wasije vifua mbele wakaanza huyu ni Mzanzibar, huyu ni Mzanzibara hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unisamehe sana, ninazungumza hili nikiwa ninasikitika; kwa sababu sisi wengine hatujawahi kuiona Tanganyika wala Zanzibar, sisi tumeiona Tanzania. Kwa hiyo wanapokuja vijana wenzetu; na kwa bahati mbaya sana ni vijana wenzetu ambao tunawaona wengine tumewazidi umri, wengine mwaka 2000 walikuwa vyuo vikuu humu tunakumbana nao pale *UDSM,* leo ndiyo wamekuwa mstari wa mbele wanatukana Jamhuri. Hawa wameshiriki kwenye chaguzi zaidi ya tatu wameshinda; lakini kwa sababu wameona mazingira hayako sawa na wanajua kwamba wakiingia huko watapigwa. Leo Katiba hii na sheria haifai ambayo imewa-*favor* mara tatu, hili haliko sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana, kwanza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, kuna mahali au iko namna tunaweza tukachekeana ila kwenye hili Jamhuri imetingishwa na walioitingisha tunawafahamu, kwenye hili tusioneane haya. Kwa sababu huwezi ukatingisha kitu ambacho ndiyo *foundation* yetu. Sisi sote humu tumekuja kwa sababu ya kitu kinaitwa Jamhuri. Mimi sikuja hapa kwa sababu ni Mzanzibar wala huyu hakuja kwa sababu ni Mmakonde, amekuja kwa sababu ni Mtanzania. Kwa hiyo tabia ya kuanza kubaguana tukadhani kwamba ubaguzi utatusaidia, hautusaidii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka sitini imepita Jamhuri hii imelindwa sasa leo wako wajanja wanafikiri kwa sababu ya ulafi wa madaraka, kwa kudhani kwamba uchaguzi lazima wao washinde, hili hatulikubali. Haiwezekani njaa ya madaraka na ulafi wa mamlaka wakataka kutuchafulia Taifa, sisi hatukubali. Ninaomba wazee wetu, wale ambao tunaamini wana busara waendelee kuangalia pande zote mbili, wasiipige tu Serikali eti kwa sababu lazima fulani ashinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie, Chama Cha Mapinduzi kama sikosei kina wanachama halali hai wasiopungua milioni 13. Sisi tangu mwaka 1995 hatujawahi kufika milioni tisa. Kwa hiyo tukiamua kuingia uwanjani sasa hivi sisi tunawapiga asubuhi, kwa namba tu. Kwa hiyo ningeomba kwa heshima na taadhima, ningetamani tutoe darasa kubwa sana, lakini ombi langu kwa vijana wenzetu ambao hawaelewi *foundation* na Bahati mbaya wengi wao wamesoma sheria, lakini sheria kwao zinafanya kazi wakiwa zinawa-*favor* wao tu, wakiona hazina *favor* kwao, inakuwa ndiyo hazifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubali kwamba inawezekana upo upungufu, lakini suala la kurekebisha sheria si leo na kesho, linahitaji mchakato, mchakato ambao unakwenda kwa *seasons*. Tunakubaliana, kwamba baada ya zoezi hili tunaweza tukaendelea lakini si leo. Kwa hiyo ningeomba sana; na hawa vijana wenzetu waelewe kwamba tumenyamaza si kwa sababu hatuna akili na tumenyamaza si kwa sababu eti wao wamesoma sana kuliko wengine, au wao ni Watanzania sana kuliko wengine, hapana. Tanzania ni ya kwetu tutailinda sote na tutafaidika sote, si wao tu. Kwa hiyo wasijitoe wakadhani kwamba wana uhalali, wao ni halali kuongoza Tanzania, kwamba ni lazima waongoze wao tu, hili halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu la kwanza; kwanza waheshimu sheria, kwa sababu sheria ndiyo imefanya wao wawepo hapa, bila ya sheria hizi wao wasingekuwepo. La pili; kwa sababu watu hawajakatazwa kutekeleza sheria, kufuata sheria waendelee kufuata sheria, lakini kubwa kuliko yote tuheshimiane kwa sababu Taifa ni la kwetu.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zahor muda wako umekwisha.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho; Wizara hii ni kubwa sana na Wizara hii ndiyo inatufanya tuishi

kwa salama na amani. Ombi langu maalum, ninaiomba sana Wizara na Serikali ihakikishe kwamba tunawaongezea bajeti kwa sababu tunaelekea mahali pabaya. Wenzetu hawaoni kwamba wamepasua ukuta wa Jamhuri ya Muungano na sisi tutaulinda tutaziba ufa huo kwa nguvu zetu zote. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zuena Athuman Bushiri wajiandae Mheshimiwa Haji Amour Haji pamoja na Profesa Patrick.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninaungana na wenzangu wote walioanza kuchangia bajeti hii asubuhi ya leo kuwapongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi nzuri sana ambazo wamezifanya. Pia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa busara zake na hekima za kuiongoza nchi hii katika hali ya ustaarabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema ustaarabu kwa sababu gani; yaliyotokea, ya wanaharakati, kama Rais angekuwa ni mtu wa pupa tungeleta ugomvi kati ya nchi hizi mbili; lakini kwa hekima zake na ustaarabu alisema maneno machache, tu tunaomba mtuache na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana Jeshi la Polisi kwa kuwa ninatambua kwamba Jeshi hili linafanya kazi usiku na mchana. Sisi Watanzania tunalala ndani, hatuna wasiwasi, tukijua kwamba vijana wetu Jeshi letu liko nje linafanya kazi. Kwa hili ambalo limetokea hivi majuzi, la wanaharakati hawa tumeliona kwamba Jeshi hili linafanya kazi usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi nitarudi kuwapongeza Waziri wa Wizara hii, mdogo wangu Bashungwa kwa kazi nzuri ambazo anafanya. Ninaomba jimbo lake wamwone kwa jicho la ziada, wamrudishe tena katika uchaguzi huu ili aendelee kulitumikia Taifa; pia bila kumsahau Naibu Waziri, Mheshimiwa Sillo. Wakiungana kwa pamoja wote kwa pamoja wanamsaidia Mheshimiwa Rais kufanya kazi yake naye kuendelea kufanya kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizi nitaelekea katika Mkoa wangu wa Kilimanjaro, kuhusu nyumba na makazi ya watumishi. Nimesimama katika Bunge lako hili mara nyingi sana nikiongelea kuhusu nyumba za makazi ya baadhi ya nyumba za polisi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Nitaongelea nyumba za makazi ya polisi katika Jimbo la Same Mashariki Kituo cha Polisi cha Gonja Maole ambacho kimejengwa mnamo mwaka 1958.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba vituo vyote vilivyojengwa kipindi cha mkoloni vimechoka. Vimechoka miundombinu yake, vimechoka hata mtazamo tu ukivitazama. Ninaongea kwa masikitiko makubwa sana kwa sababu kituo hiki nimekiongelea sana hapa Bungeni. Kituo hiki kinavuja, kituo hiki nyumba za makazi zote zinavuja, kituo hiki miundombinu yake ya vyoo si rafiki; imefika mahali ambapo askari wetu wanachimba vyoo jirani ya vyoo vya zamani. Hili ni jambo ambalo ukiangalia hata uchimbaji wao wa vyoo ni sehemu ndogo tu wanachimba. Kwa hiyo kiafya si jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali yangu sikivu, katika orodha ambazo Mheshimiwa Bashungwa amezisema na katika bajeti aliyotenga ya kukarabati, ninaomba akuja atueleze sisi wakazi wa Same Mashariki, je, ni lini atakarabati kituo hiki, kituo ambacho ni cha zamani sana, ni cha kipindi cha mkoloni? Tunaomba tupate majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiko Kituo kingine cha Polisi cha Mkuu Rombo. Kituo hiki kinavuja sana; kinavuja kiasi kwamba hata wao wanashindwa kufanya kazi wakati mvua zikiwa zinaendelea kunyesha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuena muda wako umekwisha.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilimtaja Mheshimiwa Haji Amour Haji, jiandae Profesa Patrick.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kuniona ili niweze kuchangia Wizara yetu hii muhimu sana ya Mambo ya Ndani. Kwa kweli hii Wizara ndiyo yenye mambo mengi sana na yenye uhai wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote nimpongeze Jemedari wetu, Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaiongoza nchi yetu hii ya Tanzania na namna alivyokuwa na *philosophy* zake za *4Rs* na vilevile namna anavyoweza kutuongoza. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Bashungwa kwa namna alivyowasilisha bajei yake hii leo, ambapo asubuhi yake ulisema kwamba ni *excellent* bajeti. Kwa hiyo kama ni *excellent* pia na mimi ninampongeza kwa namna ambavyo ulivyomsifu. Pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Sillo, hongera sana kwa namna wanavyofanya kazi zao za Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote niwapongeze wakuu wa vyombo vyote vya Wizara ya Mambo ya Ndani, akiwemo *IGP* pamoja na wakuu wote wa Uhamiaji na Magereza kwa namna ambavyo wanafanya kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli niseme ule ukweli, leo tangu asubuhi yale maneno ambayo yameanza kutoka kwa Mheshimiwa Musukuma mpaka kuja sasa hivi maana yake nitasema kama vile nilishiba kidogo. Tuseme ule ukweli, kwamba Wizara yetu hii ya Mambo ya Ndani ni Wizara mama na ukweli hasa wakati mwingine mtu anavyoweza kuja kuichokoza kama ni nchi maana yake anafanya uchokozi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yalizungumzwa mengi sana hapa ambayo ni ya uchokozi kwa upande wa nchi yetu. Kwa watu wa kiintelijensia *(intelligence),* maana yake kuna mambo ambayo ukiyagusa, kama ni ya nchi, maana yake mtu wewe kwa zamani unapotea; lakini kwa sasa hivi kwa vile kwamba tumesonga mbele

maana yake yatawakuta hawa yaliyowakuta; kwa mfano kama wale waliokuja, wakaja kuchokoza nchi yetu maana yake yamewakuta yaliyowakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote, wakati mwingine inawezekana pengine kuna watu wamo ndani ya nchi yetu hii wanagusa mihimili ambayo ni muhimu sana katika nchi ambayo kwa upande wa kiulinzi maana yake tunasema *confidential,* ukigusa kitu ambacho ni *confidential* maana yake ni hatari sana, inawezekana pengine ukauawa au ukaenda na maji, kwa mujibu wa namna ambavyo ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika hotuba ya bajeti nigusie upande wa ajira, hasa nitagusia kwa kutoa ushauri ambapo ajira zetu hasa kwa upande wa tasnia zetu hasa Zanzibar tunaguswa na Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Idara ya Vitambulisho. Sasa labda kwenye suala la ajira ningetoa pengine mapendekezo kwa upande wa Zanzibar kutokana na ile namna ya sifa ya Zanzibar na namna ya utamaduni ambao tuliouzoea kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine inapokuja nafasi za ajira zinazohusiana na Jeshi la Polisi au Uhamiaji, au upande wa vitambulisho ambavyo vinaihusu Jamhuri na ikaja kwa upande wa Zanzibar pia, moja kwa moja Zanzibar kunakuwa na utamaduni wake. Sasa ninashauri ule utamaduni ambao wameuzoea Zanzibar maana yake pengine wau-*copy* pia vilevile kwa namna ya kipaumbele cha upande wa Zanzibar maana yake tuufanye huo huo. Kwa mfano, tunapotangaza zile ajira tunazitangaza kwa ujumla wa Kimuungano lakini Zanzibar kuna utamaduni wake. Zanzibar ili mtu uweze kupata ajira kwanza awe na *ID* ya Mzanzibari, la pili lazima awe na barua ya sheha na kingine kitafuatia sifa zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninazungumza hivyo? Ninazungumza hivyo kwa sababu zile ajira zinavyokuja zinakuja kijumla jumla. Sasa tunakuwa tunashindwa kutathmini Wazanzibari wangapi ambao wamepata zile nafasi za ajira, lakini ikiwa nafasi zile zinakuja kwa mtiririko wa kwamba kuna *ID* ya Mzanzibari pamoja na hicho Kitambulisho cha Mtanzania na barua ya sheha, bila shaka maana

yake tutawapata wale watahiniwa waliokuwa *purely* kutoka Zanzibar pamoja na kwamba wanakuja kutumikia Jeshi la Polisi au Uhamiaji. Pamoja na yote hayo katika ushauri ambao nimeutoa pia nije kwa upande wa kampuni za ulinzi binafsi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Patrick, jiandae Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii muhimu na nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze sana Waziri na wasaidizi wake wote kwa kazi kubwa wanayofanya kwenye kulinda usalama wa ndani wa nchi yetu. Pia, nimpongeze sana *RPC* wangu kule Kilimanjaro Ndugu Simon Maigwa na *OCD* wangu Aziz Kalokola; hawa watu wananisaidia sana jimboni kwangu. Amani ni nzuri na mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu kuipongeza Serikali, hasa *IGP* kwa kazi nzuri anayoifanya. Nimwombe *IGP,* polisi wote na *system* yote ya Wizara ya Mambo ya Ndani tumsaidie Rais wetu kulinda Katiba ya nchi yetu. Tusiruhusu watu walete chokochoko hapa. Wanaleta chokochoko. Tulishawahi kung'atwa na nyoka, kwenye mwaka wa 1977 *senior politicians* kutoka kwenye Taifa fulani walianza chokochoko hivi hivi tukaua ule Umoja wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Afrika Mashari ikafa. Akaja Idi Amin akaanza chokochoko hivi hivi mpaka tukapigana vita. Sasa haya mambo tusije tukayadharau, yanaanza kidogo kidogo hivi, lakini mwishoni yanakuja kutupeleka mahali pabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba *IGP* wetu na Jeshi lake, wasimame imara tumsaidie Rais kulinda Katiba, tusiruhusu maadui

hapa nchini. Niwape mfano, ukiwa una makando kando *America* anakuweka kwenye *blacklist* anakwambia usije kwenye nchi yangu. Ninaomba, hawa watu ambao tumeshajua siyo watu wazuri kwetu piga kwenye *blacklist* asiwaruhusu waingie hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimpe Mheshimiwa Waziri ombi kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini, yeye ni Waziri msikivu sana, mimi ndiye Mbunge wa Jimbo, mimi sidandii, yaani mimi ndiyo nimewekwa pale ninahudumia wananchi wangu. Nilishakwenda kumwomba vitu anisaidie kama Mbunge wake. Mabogini ni kata ambayo kila mtu anataka adandie ili aonekane amesema kwa sababu kuna wapigakura wengi. Mheshimiwa Waziri nilishamwomba tujenge vituo vya polisi kule Mabogini akaniahidi kwamba atanisaidia. Kwa hiyo, hilo lililosemwa hapa leo nilishamwomba na alikubali kwamba atanisaidia. Kuna kitu ambacho Mheshimiwa Mchengerwa aliombwa akuletee wakati amekuja kule Moshi, aliombwa kwamba pale *CCP* kuna eneo la shabaha ambalo wananchi wa Mabogini wanamwomba kaeneo kadogo ili wajenge shule, zahanati na kituo cha polisi cha kusaidia watu. Nilishamwona na ninaomba aendelee kulifikiria hili jambo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mchango wangu utahusu changamoto za ajali barabarani hapa Tanzania na nini Jeshi la Polisi lifanye ili kukabiliana na changamoto hizi. Tumeona kwamba takwimu ambazo ametoa Mheshimiwa Waziri kwamba kutokea Julai 2024 mpaka Aprili mwaka huu zimetokea ajali 1,322, wamekufa watu 1,275 na pia watu wameumia. Kuna watu wameumizwa kwenye ajali, kadri ya watu 2,000 hivi. Sasa nimwombe, hii idadi ni kubwa sana inabidi tufanye kitu cha ziada, tujiongeze kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tuwekeze kwenye tochi za kisasa kule barabarani ambazo zitakuwa zinakaa *permanently* zikimulika maeneo maarufu, kwa mfano pale kwenye *traffic lights* tukiweka taa pale ya kisasa. Kwenye maeneo ambayo yana makatazo ya kukimbia zaidi ya *speed* fulani tuweke taa pale zikae pale ziwe zinapiga picha bila polisi kuwa pale zitakuwa zinachukua picha hizi picha zinakwenda kwenye kanzidata fulani kwenye

mamlaka ambayo inadhibiti mambo ya ajali. Kwa sababu James Kaji amefanya kazi nzuri tunaunganisha taarifa za vitambulisho za hawa wenye magari *sign* inatumwa moja kwa moja kule mtu anapigwa faini analipa na asipolipa anapelekwa jela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kusema ukweli lazima tubadilike kidogo kwa sababu Jeshi la Polisi lina maaskari wachache hawatoshi. Kwa hiyo, tunahitaji tujiongeze kidogo ili tuwekeze kwenye teknolojia itakayosaidia nchi kupambana na hili tatizo sugu la raia wetu kufa bila sababu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa mwenye jimbo, muda wako umekwisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, wajiandae Mheshimiwa Abbas Tarimba na Mheshimiwa Sylvia.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nami fursa ya kuchangia. Leo nitachangia kwa ustaarabu sana ninaumwa kichwa lakini nitajitahidi. Kwanza kabisa nianze kwa kweli kwa kumpongeza Mama Samia kwa jinsi ambavyo ameonesha, hasa kwenye Wizara hii muhimu sana. Huko nyuma ilikuwa haitengewi fedha kihivyo, lakini tunaona *trend* ya kuweza kuboresha Wizara hii muhimu sana ya Mambo ya Ndani na nimekuwa ni msemaji mzuri sana. Kwa hiyo ninafuatilia kila *item* ambayo inaongezwa au kuboreshwa zaidi. Pia, niwapongeze Mawaziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa sababu ya muda tunatambua umuhimu wao sana katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwanza kwa kuomba. Tunapokuwa tunapitisha hapa basi Serikali ihakikishe kwamba inapeleka fedha kwa wakati na hata Kamati imeainisha hapa kwamba kuna majeshi mengine ambayo yanacheleweshewa, hasa

Zimamoto na Magereza. Tunaomba sana waweze kuhakikisha kwamba fedha zinaenda kwa wakati kutekeleza yale ambayo yamepangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Zimamoto kwa ujumla na baadaye nitaenda kule Tarime. Kwa kweli tunajua kazi yao kubwa sana. Tunajua nchi yetu imeendelea sasa hivi; uwekezaji mkubwa wa majengo makubwa ambapo wanahitaji kuwa na ofisi na magari, wametaja hapa wameleta magari lakini bado ninaona kama hayatakidhi kokote. Kwa hiyo, tuendelee kuwekeza kuhakikisha kwamba tuna magari ya kisasa ambapo tunapopata majanga watu hawa waweze kwenda kuokoa *on time,* tofauti na unakuta wanapata majanga ya moto mpaka jengo linateketea lote bila kupata msaada wowote ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijielekeza kule kwetu Tarime, Jeshi la Zimamoto Wilaya ya Tarime; Jeshi la Zimamoto ambalo liko *based* Tarime linahudumia Rorya na Tarime, lakini hawana ofisi kabisa. Pale walipo wamepewa tu ofisi ya muda na halmashauri ya wilaya na wameshapewa *demand notes* ya kuweza kuondoka mwezi wa saba. Kwa hiyo, hawana ofisi. Wameshaleta maombi mara kadhaa pamoja na mchoro. Wana eneo tayari kabisa na hati wanayo, eneo la *square metre 798.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba hawa watu katika fedha ambazo wamezitenga; nimeona kwa Mkoa wa Mara tunapata Ofisi mbili, ninaomba Tarime iwe mojawapo ukizingatia inahudumia Rorya, Tarime kwenyewe, Sirari pamoja na kule Nyamwaga. Sasa hivi tumewekeza kule, hata Serikali imewekeza na sekta binafsi imewekeza. Tuna jengo la kisasa la soko ambalo ni zaidi ya shilingi bilioni tisa wamejenga kule Tarime. Kuna hoteli nyingi za kisasa na kuna jengo la kanda maalum Tarime zuri kabisa wammetujengea kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunahitaji gari la zimamoto la kisasa, lililopo ni gari la lita 1,000 tu tena ambalo limefanyiwa *modification.* Halina *capacity* kabisa kwa sababu halina *form* ya kuweza kuzima moto wa mafuta na halina *fire hydrant.* Tunaomba *the modern one*. Wametangaza hapa na niombe katika yale magari 150

liende moja Tarime lingine liende Rorya, maana yake ni wilaya mbili ambazo zinazohudumiwa na hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda sasa kwenye Uhamiaji na nianze kwa Taifa, Idara ya Uhamiaji ni idara nyeti sana na hata mjadala wa leo hapa kwa kiwango kingine umetekwa na mambo haya ambayo Idara ya Uhamiaji inahusika zaidi, lakini hawana Ofisi. Wana ofisi wamepanga tu hapa ya Kitaifa. Hebu na wenyewe tuwajengee ofisi ambayo ni nzuri kabisa ambayo wakikaa kule watafanya vitu vyao na wataweka *machinery* zote zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kule Tarime tumeshaongea mara kadhaa hapa, Idara ya Uhamiaji hawana jengo na wanajua tuko mpakani. Jengo lililopo miundombinu ni mibovu sana haikidhi kabisa mahitaji ya Idara ya Uhamiaji, lakini na wenyewe vilevile wana eneo waweze kuwapatia fedha wajenge ofisi nzuri kabisa kama ambavyo wamefanya kwenye jengo la Jeshi la Polisi na wenyewe wawe na jengo zuri kabisa pale wako mpakani, waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenyewe pia wanahitaji gari. Wana gari moja na ni bovu hali-*operate* kabisa. Kwa hiyo, sasa hivi ni kama wako *crippled* kabisa kule Tarime na wanajua tuko mpakani. Tunaomba sana waweze kutusaidia tuweze kupata gari.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye Jeshi la Magereza. Ninashukuru sana hata hapa wamesema Kamati miundombinu ya Magereza nyingi ni chakavu sana, ni ya zamani, lakini hata hawa watu nyumba zao wanazoishi hazina hadhi kabisa. Hawa watu wanafanya kazi kubwa sana. Kule wanapeleka wafungwa pamoja na mahabusu wenye *calibre* tofauti, lakini wanakaa na hawa watu *24/7*. Basi hata wakitoka kazini wakirudi nyumbani waweze kukaa kwenye sehemu ambazo wanakaa kwa starehe kabisa na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kama ambavyo wamefanya kwenye Jeshi la Polisi na kwingine waweze kuwajengea nyumba ambazo ni stahiki zao, unakaa nyumba kwanza ni chumba

kimoja bado kivuje, nyumba nyingine ni za tope. Hatuwatendei haki hawa binadamu na wenyewe wajihisi kwamba wapo kwenye jeshi hili. Wizara ya mambo ya ndani waweze kutendewa kama vile wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo magereza ambayo yanabeba wafungwa tu, ikiwemo ya Matongo ambayo niliitaja, Nanjirinji kule Lindi, Ngara na kwingine. Magereza haya yapo kwa ajili ya uzalishaji lakini unakuta yana wafungwa wachache na askari magereza wengi. Sasa nilikuwa ninashauri wafanye tafiti ya kina waweze kufunga baadhi ya magereza yabaki machache tu ambayo yatatoa tija kwenye uzalishaji, kwa mfano, Gereza la kule Matongo Simiyu ni gereza ambalo lina ekari zaidi ya 1,200, lakini wanatumia ekari 10 tu kulima. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, muda wako umekwisha.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado ni dakika tano tu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko hata jana Simba walitaka muda uongezwe wakafunge goli tano wakashindwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba basi dakika mbili tu. Ninaomba.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde tatu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika mbili tu.

**NAIBU SPIKA:** Sekunde tatu.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana. Basi nimalizie kwa hii ambayo ni *topic (current issue)* ya mambo ya *cyber bullying* kwa mama yetu, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambapo kwa kweli kama Taifa hatuwezi tukaruhusu. Mama alikuja na *4R's*. Tunajua kabisa mimi ni mpinzani,

huko nyuma tulikuwa hatuwezi kufanya hata vikao vya kamati kuu ya chama ndani ya jengo. Tulikuwa hatuwezi kufanya hata mikutano ya hadhara, lakini Mama *through 4R's* zake watu wanafanya mikutano ya hadhara Tanzania, mtu unakuwa na *freedom of expression*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi siyo mara ya kwanza, nilishawahi kukaa gerezani. Siyo mara ya kwanza kiongozi wa upinzani kupelekwa gerezani. Mheshimiwa Mbowe alishakaa mienzi minne nikiwa naye, tukatoka. Baadaye akaja akapewa tena akaenda gerezani kwa miezi nane kwa *treason*. Hatukuona haya mambo yakitokea. *So, at the time* ni lazima tujiulize kama nchi, kuna kitu *behind the carpet,* yaani kwa nini sasa hivi? Kwa hiyo, tusitumie hiyo *opportunity* ambayo Mama ametoa na *4R's* zake kuharibu Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, demokrasia ni gharama, lakini amani, usalama, ulinzi na utulivu wa nchi yetu ni gharama sana. Lazima tuangalie, leo tuna hii amani tunaweza tukaona kwamba tuko vizuri tukafanya kila tunachofanya. Tukafanya *any kind of bullying* kwenye mitandao na mbaya zaidi tunasema Wakenya wanafanya, lakini Watanzania tunachukua tunasambaza kwenye mitandao na mamlaka husika za nchi wako wapi kuona kwamba *okay cyber bullying* inafanywa na hao watu wa nje, lakini zinasambazwa kwenye mitandao ya Kitanzania, *where are we?* Kwa nini tunaruhusu hii? Ni udhalilishaji na unaweza ukaona kama ni udhalilishaji kwa sababu Rais wetu ni mwanamke. Nikafikiri mama angekuwa ni mwanaume hizi *cyber bullying* ambazo zinaendelea zingeweza kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukatae tukiendelea kujua kwamba sisi sote ni watoto wa mama Afrika Mashariki, Mamlaka za Nchi ya Tanzania na mamlaka za nchi jirani ambapo sijaona nchi jirani mamlaka zake ziki-*condemn* hili. Washirikiane; Mambo ya Ndani ya hapa, Idara ya Mawasiliano na kule Kenya, tuwakamate hawa *Gen-Z* wakome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *clips* nyingine ukisimkiliza *tone* ni ya Kiswahili, ni Mtanzania. *They are just hiding* kwa wale ambao wanatokea Kenya *they are pretending* wanamdhalilisha mama.

Wasitweze utu wa mtu. Siyo tu kwa Rais, mimi ni *activist* wa haki za binadamu, siwezi kuruhusu kumtweza hata mtoto wa darasa la kwanza. *Leave alone the president* ambaye ndiye amebeba nembo ya Taifa letu. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Matiko na mamlaka hii imewekwa na Mwenyezi Mungu. Nenda kwenye Warumi 13(1-2). Mheshimiwa Bashungwa, nilikuwa kwenye Kamati hii *almost* miaka 15 na miaka yote malalamiko yalikuwa ni nyumba na makazi ya vyombo. *National House* wana *project* sasa hivi ya kuingia mkataba na mwekezaji kujenga nyumba *almost* laki moja. Sasa vyombo vya ulinzi nendeni mkawahi *slot* yenu. Usingoje wakuletee; mfuate mkurugenzi, "Ninasikia una mpango huu na sisi tuna shida hii," sawa ndugu yangu? Haya.

Mheshimiwa Tarimba, jiandae Mheshimiwa Sigula na Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kwa mara ya kwanza ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Esther Matiko. Mheshimiwa Esther Matiko yeye ni Mwana-CHADEMA, lakini kwa kila hali ukimwangalia anafaa sana kuvaa jezi ya njano na kijani. Huyu ni mwanahalisi kabisa, ni Mtanzania halisi mzalendo anajua na kuheshimu mamlaka za nchi hii. Hivyo, acha nimpongeze na ninamkaribisha sana kwenye chama chetu, Chama Cha Mapinduzi, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Mtandao wa *Tiktok* kwenye *page* moja inaitwa *Ujiji Online TV* yupo dada mmoja Mkenya anajiita Batuli na ninafikiri hii *clip* nimeiona hata kwenye kundi la Wabunge wa CCM ikisambaa, niliiona mapema. Huyu dada anasema hivi, yeye ni mwanaharakati na anapenda sana uwanaharakati na anaposikia kuna mambo ya uwanaharakati hupenda kujipeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa alivyokuwa kwao Mombasa akaona kundi la Wakenya wenzake wanajikusanya kwenda kwenye Ubalozi wa Tanzania kwenda kupiga kelele, kuikashifu Serikali na kumkashifu Rais wetu. Yeye akaenda, lakini alipofika kule

mazungumzo yale yaliyokuwa yakizungumzwa pale akagundua kwamba wote hawa wanaojifanya ni wanaharakati kumbe wanalipwa na wazungu. Wanalipwa na wazungu kuja kutuchafua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikajiuliza, hivi kweli huyu mtu anaitwa Martha Karua na wenzake wote hela ilivyo ngumu kiasi hiki apate hela ya kupanda ndege, aje kwetu Dar es Salaam, Tanzania, akae hoteli na apate kula chakula, kwa mapenzi gani na Watanzania, kuanzia lini anatupenda huyu mtu? Hizi ni fedha wanazopewa na kwa kuwa sisi tumeshawatambua; niipongeze sana Serikali, watu kama vile wakija, tena badala ya kuwarudisha, tia ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye dunia kuna seti mbili tu za sheria: *International Law* na *Domestic Law*. *Domestic Laws* zinabakia katika uwanda wa Kitanzania. Hatutaki mtu mwingine atuonee huruma au atupende kwa sheria zetu za ndani. Watuache wenyewe na sheria zetu za ndani. Hata hizo sheria za kimataifa ni mahusiano tu. Sasa huyo Martha Karua ndugu yangu ana tui lake jikoni huko hajalimaliza, anakuja kutafuta ugali wetu, wa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo tusipoyaangalia vizuri ndiyo yanayoleta chokochoko ndani ya Taifa letu. Kuna mtu mmoja hapa ndani mwenzetu Mbunge tena ana nafasi ya kuzungumza humu ndani, ana nafasi ya kuzungumza kwenye *NEC* na ana nafasi ya kukutana na wakubwa anaanza kutuchonokoa, ameanza kutuchokonoa. Ninakiuliza Chama changu Chama Cha Mapinduzi huyu bwana ana kadi ya chama huyu hivi basi tukae tuwe na mtu kama huyu ambaye anatusumbua, anatoa mifano ya kutisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiswahili bwana ni sisi watu wa pwani tunakijua, tumejifunza shule pia, kitu kinachoitwa *literature (fasihi)*. Wewe unaanza kutoa mifano, anatoa mifano anasema bandari ikiuzwa. Sisi tunajua unalenga wapi ndugu yangu huko uliko, tunakujua unalenga wapi halafu unatoa mifano mibaya kwa Rais wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ambaye tunampenda, mtu ambaye amejitoa kwa ajili ya Tanzania hii, unakwenda kugusa familia yake, unagusaje familia yake, mtoto wake unajua jinsi ya kupata mtoto wewe? Unajua jinsi ya kulea? Unamtaja mtoto wake kipenzi kwamba akitobolewa macho Mungu akulaani kabisa huko uliko na hayo yasitimie kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anatoa mfano kwamba, mtoto akitolewa macho sijui na nini, unataja majina ya watu halafu unasema ni mfano, sisi Kiswahili ndio lugha yetu tumefundishwa, shule tumesoma, tunajua fasihi, tunajua kutafsiri. Huna mema kwa Tanzania, hana mema kwa Tanzania huyu bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana awepo, haya maneno tukiyasema angekuwepo pale, lakini bahati mbaya hayumo humu ndani, huko aliko ayasikie, halafu yeye atujibu, potelea mbali lolote na liwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumze maneno hayo kwa sababu yameniumiza unamtaja Rais ambaye anajipambanua kuitumikia nchi hii. Tanzania imepata maendeleo ya haraka ndani ya miaka minne kuliko kipindi kingine. Kwangu Kinondoni kuna mambo mzigo tumeletewa trilioni 1.3 Jimbo gani ambalo limepelekewa fedha nyingi kiasi hicho kwa mara moja? Halafu wewe unakwenda kumchokoza mtu ambaye anatuokoa sisi wana Kinondoni, sisi hatukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilizungumza na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Kinondoni, nikamuuliza nyie mko wapi? Watu wanafanya makosa madogo tu wanaitwa kwenye Kamati za Maadili, wanaitwa kwenye Kamati za Siasa, jambo zito kama lile halafu wanakaa kimya, nililisema hili na huko anakonisikia Mwenyekiti wangu anaitwa Shaweji Mkumbura. Mheshimiwa Shaweji namwambia kwamba, sisi haturidhiki Rais wetu kufanyiwa dhihaka tena wanafanyiwa dhihaka na watu wa Kinondoni hatukubali. Asipochukua hatua nami Mwenyekiti nitamtilia wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nilisimama nilitaka niseme mambo haya kwa sababu sisi wana Kinondoni yametukwaza sana. Ninaomba nimtie moyo Rais wangu Mwenyezi Mungu amjalie awe na moyo wa udhibiti kuweza kuyahimili haya mambo yatapita tu haya na nchi hii tutafanya uchaguzi wetu tutakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nikupe pole Naibu Spika ndiyo kukua huko…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha kaa chini.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigula, jiandae Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa nami niweke mchango wangu katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa fursa ya kusimama katika Bunge hili Tukufu. Lakini kwa namna ya pekee sana, niipongeze sana Wizara pamoja na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kazi kubwa sana wanayoifanya katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwanza, kwa kuona umuhimu wa Wizara hii kwa miaka hii minne ya Daktari Samia Suluhu Hassan bajeti imetoka kutoka shilingi 9,000,000,000 mpaka 2,000,000,000,000 tunaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara kwa sababu kwa miaka minne hii kuna vitu ambavyo tumekuwa tukishauri kama Wabunge. Kutoka kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, tumeona

mambo mengi sana yamefanyiwa kazi ikiwemo kuongeza magari na vitendea kazi kwa askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuondoa msongamano wa mahabusu na magereza, huko kwa wafungwa pia matumizi ya nishati safi, leo magereza zetu wanatumia nishati safi. Pia wameanzisha miradi ili Serikali iweze kuokoa fedha. Kwa hiyo, wizara imejitahidi sana kupokea maoni, ushauri na maelekezo ya Wabunge tunawapongeza sana kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna moja ambalo limeachwa. Mheshimiwa Waziri nakufahamu wewe ni msikivu sana kama mmeweza kufanyia kazi haya mambo mengine. Lipo suala la *PGO* ambalo tumekuwa tukilizungumza sana kwa muda mrefu. *PGO* imepitwa na wakati, ni muda sasa tuifanyie marekebisho ili tuendelee kuboresha maslahi ya askari wetu na watumishi wa sekta hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni kijana na katika umri wangu ambao niko hapa duniani sijawahi kusikia sauti ya risasi, sijawahi kusikia sauti ya mabomu, sijawahi kusikia heka heka ya vita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata nafasi ya kuishi mikoa ambayo ipo pembezoni. Tumepata bahati ya kuwatunza wenzetu ambao nchi zao zimekumbwa na changamoto ya usalama. Sasa kwa mazingira ambayo tumeyaona kwa wenzetu namna ambavyo wanaishi suala la usalama wa nchi yetu siyo suala la mzaha mzaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaona tuko humu ndani tunapata amani ya kujadili ni kwa sababu vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya kazi yao. Leo tusingepata fursa ya kukaa hapa kama tusingekuwa na amani. Sasa, sisi vijana tunapoona kwamba, kuna kundi la watu linataka kuhatarisha amani ya Taifa letu hatuwezi kuvumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitumie nafasi hii kumpongeza sana *IGP* baba yangu Wambura, hongera sana kwa kazi kubwa

anayoifanya. Leo tunaona kwenye Taifa letu watu ambao Taifa lao limewashinda na wanajiita wanaharakati. Nadiriki kusema ni wanaharakati njaa, wanaharakati uchwara. Wameharibu ndani ya Taifa lao, wanakuja kwetu kuanza kuondoa amani tuliyonayo. Nimwombe sana *IGP* asikubaliane na suala hili hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania siyo utamaduni wetu kutukana viongozi nami naongea hapa kama kijana ambaye nimelelewa na Chama Cha Mapinduzi, siyo utamaduni wetu kutukana viongozi. Leo tunapoona Rais wetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda umekwisha malizia.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoona Rais wetu anatukanwa na watu ambao wanajiona kwamba wao wana nafasi ya kumtukana, niombe sana *IGP* ashughulike nao ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia asubuhi sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi, tumesema *IGP* hapo hapo shikilia kuhakikisha watu hawa wanashika adabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani kuona leo kiongozi wa Taifa hili akiwa mama, akiwa mwanamke kwa kazi anazozifanya leo alipwe kutukanwa kwenye mitandao, haiwezekani na sisi vijana hatuko tayari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninaomba niungane na Mwenyekiti wetu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Kawaida, amesema kama Serikali haitaingilia kati suala la Rais kutukanwa sisi vijana wa Chama Cha Mapinduzi tutaingilia kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na muda ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sigula kuna watu wanalilia ndizi, lakini mkungu si wao. Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, jiandae Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi. Kwanza, nianze kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu yao yote ya uongozi lakini kuu ya Taifa kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusaidia kumshauri Mheshimiwa Rais inapobidi pia kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa upande wangu kwanza nikumbushe katika bajeti iliyopita niliomba boti kwa ajili ya uokoaji katika Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa lina mawimbi sana na kila wakati kunatokea dharura, hata hivi juzi wamefariki watu wawili pale Lipingu. Kwa hiyo, ninaomba tupate boti la uokoaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru pia kwa gari ambalo ameliongeza katika Wilaya yetu ya Nyasa. Niombe pia kupata chombo cha moto ikiwa ni pikipiki au gari kwa ajili ya Tarafa ya Mpepo, ambayo nayo imekuwa kama imejitenga lakini kuna maeneo hatarishi yale ya Hifadhi za Lipalamba pia ni mpakani. Kwa hiyo, ninaomba atuangalie katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hiyo nizidi kuwapongeza wanawake viongozi katika Wizara hii ambao wanatimiza wajibu wao vizuri. Mengi wameongea wenzangu na kwa kweli itabidi labda awe kichaa asiweze kuunga mkono na yeyote atakayesimama lazima atapenda aizungumzie hoja hii iliyoleta utata na mkanganyiko kati ya nchi na nchi na hao wanaharakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa niko mwishoni sasa tumesikiliza mambo mengi makubwa na mazito walioshauri Waheshimiwa Wabunge. Ninaomba kusema jambo hili; Mheshimiwa Rais wetu kama ambavyo tulimsikia kwa sauti ya Amiri Jeshi Mkuu, Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini akiwa ni sauti ya mama, sauti ya mwanamke alizungumza kwa sauti ya kukemea kuonyesha kwamba, ni jambo zito. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi dira yetu ya Tanzania ambayo inaisha muda wake imeweka amani na utulivu kama kipaumbele na hata tunayoenda kuwa nayo bado itazingatia amani na utulivu ndiyo tunu yetu ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatukuchagua pesa, hatukuchagua kitu kingine tumechagua amani na utulivu kwa sababu ndiyo kioo, msingi wa maisha na msingi wa maendeleo na nchi yetu kuwa na furaha kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja, mama yetu sisi siyo mbaya ni mtu mwema sana. Akazitambua 4R akizungumzia maridhiano, masuala ya uvumilivu, masuala ya kufanya marekebisho na kujenga upya. Kwa hali hii sisi na wenzetu hawa jirani zetu, wa Kenya sisi ni ndugu, ni marafiki, tunategemeana. Pamoja na hayo tuliyoongea sisi tunawaambia wajitathmini waangalie warudi upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ndugu yetu dada Martha ametuangusha wanawake tunaolilia kupata nafasi nyingi za uongozi, yeye anadanganywa na wanaume anaenda kufanya vitu visivyostahili, hajatuheshimisha kama wanawake. Kwani alishindwa nini hata angepiga simu kuomba *appointment* kwa Mheshimiwa Rais wetu, dada ninaomba tuongee jambo hili likoje? Amesahau kama huyu Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan ndiyo alienda kumtembelea Mheshimiwa Lissu akiwa Kenya hospitali?...

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesahu ndiye alienda kumchukua kule…

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa msemaji ana dakika tano sasa unapotoa taarifa unachukua muda wake, haya Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, umesahu…

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja, Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa nategemea ridhaa yako tu ukiona muda hautoshi basi nitakaa.

**NAIBU SPIKA:** Nimeshakuambia ndiyo nimekuita hivyo.

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Nimekwambia toa taarifa yako.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anachangia vizuri...

**NAIBU SPIKA:** Majimboni kuna nini mbona kila mtu akiingia humu ndani kachanganyikiwa tu?

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu ya yaliyotokea jana ndiyo yametuchanganya, ya kule Zanzibar ndiyo yametuchanganya.

**NAIBU SPIKA:** Haya taarifa.

**MHE. KILUMBE S. NGE'NDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ni kwamba ninataka kumpa taarifa mzungumzaji ambaye anazungumza vizuri kwamba wala Martha hakudanganywa na wanaume. Unajua kwamba, mashetani wako wanaume na wanawake, yeye ana ushetani wake mwenyewe peke yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kama umeona hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba hata Mheshimiwa Lissu alipokimbia nchi yake na kwenda nchi nyingine kule Ubelgiji Mheshimiwa Rais wetu alimfuata akamwambia mdogo wangu njoo twende nyumbani, huu ni upendo wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi sisi tunaheshimu mahakama hata Bunge hili kesi ikiwa mahakamani hatuingilii, tunasubiri mahakama ifanye kazi yake kwa uhuru, wao kitu gani kiliwatuma? Mheshimiwa Martha Kalua kimsingi alichezea masharubu ya simba akifikiria amekufa, Simba Tanzania hajafa bado yupo macho. Ukigusa kipande cha ardhi tunakushughulikia, ukichezea mamlaka tunakushughulikia. Nirudie kusema tena wakome! Wakome! Wakome! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nimpe neno la faraja, namzungumzia huyu mama tu ndugu yetu Dada Martha, kukosea si tatizo, tatizo ni kurudia kosa. Bado ana nafasi ya kujiweka vizuri ili kesho aje awe kiongozi mzuri wa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya muda wako umekwisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zetu za Afrika Mashariki, lakini ampigie mama aongee naye kama dada yake. Tunamshauri…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya muda wako umekwisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, wajiandae Mheshimiwa Maryam Omar na Mheshimiwa Profesa Shukrani. Mheshimiwa Anatropia hayupo, Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuongea neno katika hoja hii iliyopo mezani. Kutokana na uchache wa muda nitakwenda moja kwa moja katika pointi zangu. Kwanza, ninaipongeza sana Wizara kwa namna wanavyojitoa na kufanya kazi nzuri. Nina changamoto mbili, tatu hizi na nitaanzia katika Ofisi za Uhamiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa kuna sehemu tunatakiwa kuwekeza sana basi ni Ofisi za Uhamiaji. Ofisi za Uhamiaji ni changamoto kubwa sana hata ukiangalia ofisi yetu ya Uhamiaji Dodoma haifanani kuwa ni ofisi iliyopo makao makuu ya nchi kusema ukweli ni jambo la aibu sana. Kwa hiyo, tujitahidi tuweze kuwekeza katika Ofisi za Uhamiaji ili mradi twende sawa na nchi yetu Tanzania inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitajielekeza moja kwa moja hapo hapo Uhamiaji katika vitambulisho vya *NIDA*. Ofisi za vitambulisho vya *NIDA* hasa kwa Mkoa wangu Kaskazini Pemba ni changamoto kubwa. Mkoa wa Kaskazini Pemba Wilaya ya Wete Ofisi za *NIDA* ya Mkoa na Wilaya ipo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Mheshimiwa Salama pale ndiyo kuna ofisi ya *NIDA,* ukienda ni chumba tu hivi, hapo ndiyo kuna Ofisi ya *NIDA* ya wilaya hapo hapo ndio kuna Ofisi ya *NIDA* ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake hapa aniambie ni kiasi gani katika bajeti hii tutapata kule Kaskazini na sisi angalau tuweze kujenga ofisi inayoendana na maendeleo yetu kwa sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, niende moja kwa moja kwenye Jeshi letu la Zimamoto. Mheshimiwa Waziri kiukweli Jeshi letu la Zimamoto linataka liwezeshwe na liwezeshwe liwe sawasawa na Jeshi la Wananchi la Tanzania kwa sababu hili ni jeshi muhimu sana. Tunashukuru kule Kaskazini ipo ofisi moja wameongeza pale Kijichame,

lakini bado vitendea kazi ni hafifu sana kiasi ambacho hata ikitokea changamoto hawawezi kufika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo sasa niende moja kwa moja kwa wanaharakati. Wanaharakati wa ndani ya nchi na wanaharakati wa nje ya nchi. Mheshimiwa Waziri mwiba uchomapo ndipo utokapo. Hili jambo kama halikuanzia hapa nyumbani wa nje asingeweza kufanya haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mama, huyu mama ni mama mvumilivu mno kwa yanayotendeka hata ingekuwa ni mimi nadhani hapa tungekuwa tunazungumza lugha nyingine, si kitu rahisi!

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kitu rahisi Mama anadhalilishwa mno, Mama anadhihakiwa hebu tujiulize ni kwa uanawake wake? Ni kwa Uzanzibar au tuseme ni kwa udini? Mambo yamekuwa mengi. Walitokea wanaharakati, umeshasema *no reform* tulia, baki na *no reform* yako. Vyama 19, hivi vyama 18 vilivyobaki tutakwenda kwenye uchaguzi, kama ameshindwa asikimbie na mpira kwapani, aachie mpira tunaoweza tuendelee nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaumia sana. Mimi ni mwanamke, ni mama, najisikia huzuni sana ninavyoingia kwenye mitandao ya kijamii na kuona yanayoendelea eti Mheshimiwa Samia anafananishwa ni kama kikatuni fulani tu hivi, mara anatokea mtu anakifinyafinya, kweli? Na sisi tupo tu? Siyo kwamba hatuwezi kusema tunawaangalia wao wanaatupeleka wapi? Kama akipewa ruhusa kila mtu aseme hapa, wasemaji wanaotoka nje na wa ndani ya nchi watatafuta pakwenda, hii kazi tunaiweza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tumechoka, kuna msemo wa Kiswahili unasema ukicheka na nyani utavuna mabua, hatutaki sisi tuje tuvune mabua. Huu siyo muda tena wa kucheka na nyani. Ninayasema haya na uzuri mama yangu Mheshimiwa Taska yuko pale anasikia, hizi Wizara mbili nyinyi sasa hivi macho yetu sisi tunawaangalia ninyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Waziri, niungane na wenzangu waliopita katika kuchangia, tulikosea kweli yule Mheshimiwa Martha Karua kumrejesha kule na hili kosa lisitokee tena hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mtu anatoka huko analeta ujinga wake hapa, halafu eti anarejeshwa mzima salama salimini kweli? Yule anayesema anadai kapigwa eti anashuka kwenye gari anajichechemeza kweli? Yule alikuwa apigwe arudi na mitungi ya gesi kule kwao, anapumulia gesi, wangejua Tanzania, wangeona makali ya Jeshi la Tanzania, lakini eti leo mtu anadai kapigwa anazungumza tu kule anaendelea kuzungumza. Tumemwacha Martha Karua anaendelea kuzungumza akiwa Kenya kule, ninamwomba Mheshimiwa Waziri hili lisitokee tena. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, anayekuja kwetu tunamalizana naye hapa hapa, anayeingia ndani ya kumi na nane zetu tumalizane naye hapa hapa, wanavyotaka tunataka. Sisi hatujashindwa na sisi hatuwaogopi, wasifikirie kama walivyoweza kufanya kule kwao, watakuja kuchochea Tanzania iwe hivyo, Tanzania ni nchi tunayoheshimiana, Tanzania ni nchi ambayo tunaishi kwa urafiki na udugu, sisi tunaheshimu sheria zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao tuliwaona kule, walienda kunajisi mpaka Bunge lao, nchi gani ile? Eti halafu mtu anakwambia tukasoma kwao, tukasome nini? kipi tukasome?

**NAIBU SPIKA:** Haya Mheshimiwa.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hatuna cha kusoma kwa Wakenya isipokuwa Wakenya watoke kule waje wajifunze kwetu, waje watalii kwenye nchi yetu waone.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam ahsante.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafundishwe namna ya siasa inavyofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, naona Mheshimiwa Naibu Spika ananiangalia, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, wajiandae Mheshimiwa Ritta Kabati na Naibu Waziri.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi na kwa ajili ya muda niende katika hoja mbili ambazo na ninatamani kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitangulie kusema kwamba utulivu na amani iliyopo nchini kwetu Tanzania ni matokeo ya kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali yetu kupitia Wizara yetu ya Mambo ya Ndani na Vyombo Vyetu vya Ulinzi na Usalama wa Raia, lakini pia na Taasisi za Dini ambazo sisi ni waumini katika madhehebu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya amani iliyopo tuna sababu zote za kumpongeza Mheshimiwa Rais, ambaye ni Amiri Jeshi Mkuu kwa jinsi ambavyo anaendesha nchi kwa ustahilimivu mkubwa. Pia tuna sababu ya kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na Majeshi yetu yote ya Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji na Mamlaka ya *NIDA* ambazo ni Taasisi chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu niongelee mambo mawili makubwa, jambo la kwanza likiwa ni uboreshaji wa miundombinu na mazingira bora ya kazi ya Majeshi yetu. Ili Majeshi yetu yaweze kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi wanahitaji sana vitendea kazi, miundombinu bora pia na mazingira bora ya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitapenda kutaja ofisi ambazo niliziona binafsi kwa sababu ya kutokwenda huko lakini mifano michache, siyo afya kwa Jeshi letu kwamba ukarabati wa ofisi pamoja na ununuaji samani *(furniture)* ufanywe na wadau, wadau hao wakati mwingine waweza kuwa ni miongoni mwa wahalifu kiasi kwamba wanalifanya Jeshi letu kukosa kuwawajibisha pale wanapokuwa wanatakiwa

kuwajibishwa, kwa sababu wamekuwa sehemu ya kufanya ukarabati wa ofisi au ununuzi wa samani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo afya pia kwa Jeshi letu kwa mfano, unataka kuandikiwa *RB* halafu unaambiwa rimu ya karatasi iliisha jana, hapana, hiyo siyo afya! Au mhalifu amepatikana, lakini unaambiwa gari la Polisi halina mafuta na kwa hiyo afanyaje sasa mteja? Kwa hiyo, tunatamani kwamba mambo haya Serikali iweze kupeleka fedha kwa kadri zinavyopitishwa hapa ili vitendea kazi vyao visipotee wakati wowote ule, waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kuhusu vitendea kazi ni maslahi ya wanajeshi yaaangaliwe vizuri ili kwao iweze kuwa motisha ya kufanya kazi na hasa wakati wanapokuwa wanastaafu. Wakati mwingine wanapokuwa wamestaafu unakuta kwamba malipo yao yanakuwa kidogo na wanashindwa kuendana na kazi nzuri ambayo wameifanya ya kulinda usalama wetu raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni sehemu ya 188 na 189 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Katika sehemu hii amesema hivi ninaomba ninukuu: *‘‘kwamba kati ya Julai, 2024 na Aprili, 2025 Jumuiya za Kidini 97 na 87 zisizo za kidini zilisajiliwa, sehemu ya 189 katika ukaguzi uliofanyika katika Mikoa saba tu Tanzania, taasisi 307 zilikaguliwa na kubaini uwepo wa taasisi za dini ambazo hazina usajili na hazizingatii masharti ya usajili’’. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu kumekuwepo na utitiri wa Taasisi za Dini ambazo hazina usajili na wakati mwingine zimetumika kama njia ya utapeli na wakati mwingine taasisi hizi hujiingizia kipato kuliko misingi wanayosimamia. Mfano, kuna taasisi ambayo unakuta watumishi anakwambia ili umwone mtumishi *consultancy fee* ni laki tano. Hivi huo si utapeli? Yaani mtumishi kwanza misingi ya neno lenyewe linasema kwamba mmepewa bure toeni bure, wewe unaniwekea *consultancy fee* ya laki tano ili kukuona mtumishi, nadhani kwamba taasisi za jinsi hii ni vichaka ambavyo vinataka kuwaibia Watanzania na hazipaswi kuruhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa nini baadhi ya taasisi hizi wanauza vitu kwa bei ambayo siyo bei ya soko? Yaani maji ambayo yanauzwa 2,000 lakini watumishi wanauza 5,000 mimi nadhani siyo sawa. Pia tumeshuhudia watumishi wengine wanafanya udanganyifu mkubwa kwamba, nimeenda hadi mbinguni nimeonana na Mungu na wako. Katika nchi hii wanaendesha taasisi zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tu ya muda tusikubali kuwa na taasisi ambazo hazijasajiliwa na wakati mwingine hata zilizosajiliwa zinakwenda kinyume na misingi ya usajili wao, kwa sababu kinakuwa ni kichaka cha kuwaibia Watanzania, lakini pia na upotoshaji mkubwa, kwa hiyo, Serikali yetu iwe macho. Hata hizi chokochoko ambazo tumeziongea sana hapa zitakuja wakati mwingine kwa kupitishiwa katika taasisi ambazo zinakaa hapa nchini kwa lengo la kuleta mambo ya injili na imani wakati hazina usajili na wakati zinaendesha biashara. Kama ni hivyo *consultancy fee* ya laki tano, tukatoze kodi pale kama wanakubali kuuza maji ya 2,000 yakauzwa 5,000 tutoze kodi pale ili Taifa liweze kupata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaona umewasha *microphone,* wanaomba bajeti ya trilioni 2.6, ninaunga mkono hoja na tuwapitishie wafanye kazi. Ahsante sana kwa mchango wangu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, jiandae Naibu Waziri.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwisho. Kwanza ninawapongeza wachangiaji wote wa leo kwa kuona kwamba Mheshimiwa Rais wetu hatendewi haki, nami nitaanza na nukuu ya neno la Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisoma Warumi 13 mstari wa kwanza unasema: "*Kila mtu na aitii mamlaka iliyokuu kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu, na ile iliyopo imeamriwa na Mungu.*" Ukisoma mstari wa pili unasema hivi: "*Amuasie mwenye mamlaka hushindana na agizo la Mungu, nao washindanao watajipatia hukumu.*" Hii ya mwisho inasema: "*Kwa maana watawalao hawatishi*

*watu kwa sababu ya matendo mema bali kwa sababu ya matendo mabaya". (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa nukuu hii niombe sasa Mheshimiwa wetu aheshimiwe, ametuheshimisha nchi yetu, Mheshimiwa Rais wetu amepata Tuzo nyingi sana za kimataifa kuhakikisha kwamba nchi yetu sasa hivi kimataifa inatambulika kwa kazi nzuri sana ambayo ameifanya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo tuombe wote hiki kikundi ambacho cha nchi jirani kinachomtukana Rais wetu sasa iwe basi, sisi wenyewe Watanzania tumeamua kumlinda Rais wetu na tunamwomba *IGP* sasa achukue kazi yake aendelee, maana sasa Rais wetu anachezewa. Tunaomba nchi yetu iendelee kuwa na amani, nchi yetu ni kisiwa cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee sasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya, lakini nimpongeze pia Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kumsaidia Waziri katika kazi hii, *IGP* nipongeze Wakuu wote ambao wako katika Mamlaka hii ya Mambo ya Ndani. Ninawapongeza sana lakini nisimsahau *RPC* wetu wa Iringa ambaye amekuwa akifanya kazi nzuri sana kuhakikisha mkoa wetu unakuwa na amani na Askari wote wa Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema kwamba moyo usiyokuwa na shukrani hukausha mema yote, ninaishukuru sana Serikali kwa kuhakikisha kwamba sasa Ofisi ya Wilaya ya Kilolo cha Polisi kinajengwa na kwa kweli tumeona sasa hivi wanamalizia. Hata hivyo, niombe kwamba sasa nyumba ya *OCD* tunaomba ijengwe pale Iringa kwenye kituo, lakini pia tuombe nyumba za makazi ya Polisi Kilolo hawajawahi kujengewa, tunaomba sasa hivi wajenge ili wasiendelee kuishi nje ya kituo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tushukuru sana pia, tunashukuru kwa magari ambayo tumeletewa katika Mkoa wetu wa Iringa yatatusaidia, lakini tunaomba sasa bajeti ya mafuta itengwe na ya matengenezo ili yale magari yaweze kufanya kazi inayotakiwa. Ninaomba Serikali iwe inatambua wanaochangia Jeshi la Polisi kwa mfano, kwenye Mkoa wetu wa Iringa kwa kweli tunaye Mheshimiwa

*M-NEC* wetu *ASAS ABRI* amekuwa akichangia mambo mengi sana katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza amechangia dawati, ujenzi wa dawati, amechangia ujenzi wa makazi ya familia sita pale katika makazi ya Polisi, lakini amejenga Kituo cha Polisi cha Mbigili pale Kilolo. Pia anaendelea kujenga Kituo cha Nyang'olo, lakini pia alisema atanunua kamera kwa ajili ya kuongoza magari kwenye Mlima Kitonga. Sasa watu kama hawa ninaomba kwanza Serikali iwe inawatambua na kuwapatia Tuzo maalum ili waendelee kuchangia katika Jeshi hili. Hata mimi mwenyewe ninaomba tu wanipongeze nilijenga Kituo cha Polisi pale Semtema, pia nitambulike kwa mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Iringa una changamoto nyingi sana, kwanza makazi ya Polisi wote wa Mkoa wa Iringa ni chakavu sana, kwa hiyo niombe bajeti iletwe ili makazi ya Polisi yaweze kukarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba sasa tumesikia leo kwamba magari ya Zimamoto yapo. Sisi pale Iringa katika Wilaya ya Mufindi na Wilaya ya Kilolo imekuwa ikijitokeza moto mara kwa mara katika ile misitu, wananchi wanapata hasara pia hata Serikali inapata hasara kwa ile misitu ambayo tumekuwa tukiitunza kwa muda mrefu, sasa tunaomba tupatiwe gari la Zimamoto pale Mufundi na gari lingine la Zimamoto kule Kilolo ili moto ukijitokeza tuweze kupunguza hasara ambazo zimekuwa zikijitokeza kwa wingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na mkwamo mwingi sana wa magari katika barabara ya Kitonga, tunaomba *crane* moja ambayo ameisema hapo basi tuletewe ili kusiwepo na mkwamo wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwamba tulikuwa tuna mwingiliano mkubwa sana kati ya Hospitali ya Mkoa na Magereza yetu ya Mkoa, sasa tumesikia leo kwamba kuna pesa itatoka ili ujenzi Mlolo gereza liweze kuhama na hii nafikiri wananchi wa Iringa leo watashukuru wataipongeza Serikali, kwa sababu kumekuwa kuna

mwingiliano ambao umekuwa ikisababisha hata Madaktari wetu kukosa nyumba za kuishi pale katika Hospitali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niombe ule mkakati wa kuhakikisha kwamba tunatoa Gereza lile la Kihesa Mgagao pale Kilolo liondolewe, kwa sababu lile gereza tunataka sasa liwe ni utalii kwa sababu kuna wenzetu waliishi pale na hata kule South Africa gereza sasa hivi siyo gereza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati ahsante kwa kujenga Kituo cha Polisi na muda wako umekwisha.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake nyingi katika Taifa letu hususan ustawi wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kidIplomasia na mshikamano na kutuepusha na majanga mbalimbali wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi anavyoliongoza Taifa letu na kutekeleza kwa kiwango kikubwa sana Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wetu wa Mambo ya Ndani; Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na vyombo vyote vya ulinzi vilivyoko chini ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge letu kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kupitia taarifa yao waliyoiwasilisha mbele ya Bunge letu hili, hongera sana Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninaomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo ya bajeti ya Wizara hii muhimu sana kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kama ilivyowasilishwa mbele ya Bunge letu. Kwanza, tunaiomba sana Serikali yetu ijitahidi kupeleka fedha zinazoombwa kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu kama inavyombwa mbele ya Bunge letu ili kufanikisha mpango wao wa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Serikali yetu itafute ufumbuzi wa ukamilishaji wa miradi ya maendeleo inayopangwa kwenye bajeti, ukarabati na ujenzi wa ofisi za wilaya, mikoa, majengo ya magereza, makazi ya askari, kote nchini kwa kuwa majengo mengi hayapo na mengine ni chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta magari ya Jeshi la Zimamoto kwa ngazi ya wilaya na mikoa nchini ili kukabiliana na majanga mengi sana yanayoathiri uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali yetu iangalie uwezekano wa kulipa madeni ya watoa huduma kwa wakati katika Wizara hii ya ulinzi na usalama ili kuleta tija zaidi na mafanikio makubwa sana kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Serikali isimamie suala la utoaji na upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kutafuta fedha na vitendea kazi na kutoa elimu kwa wananchi ili kufikia lengo la kila Mtanzania awe na Kitambulisho cha Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza wewe na Maafisa wetu kwa kulipongeza vizuri sana Bunge letu hongera na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Waziri aliangalie suala la malipo ya posho na usafiri kwa Askari wa Iringa pale tangu mwaka 2019. Je, wamelipwa stahiki zao zote?

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mungu kwa uzima na afya, ninamshukuru Mungu kwa ajili ya Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu kwa afya, zaidi sana nimtie moyo Rais wetu kwa uvumilivu na ujasiri wake kwani ni mengi anayapitia eeh Mungu umsaidie kwani uongozi wake ni wa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani na nianze kwa kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri kwani mambo mengi yamefanyika kwa makini na tunayaona, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kusimamia na kuhakikisha askari wanapata matumizi yao ya vifaa vya utendaji na na kadhalika ili kufanikisha amani, utulivu na ustawi katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuhakikisha Askari wa Jeshi la Polisi wanazingatia sheria, kanuni na taratibu, miiko na weledi, tamaduni na maadili ya Jeshi la Polisi na ili haya wayafuate ni kuhakikisha askari wetu wanapata nyumba za kuishi za uhakika katika kambi zao ili wanapokuwa kazini wajue wanapomaliza kazi wanakwenda kwenye nyumba zao zenye amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa magereza yako matunda mazuri kwa kupunguza mrundikano magerezani, hili Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan amelitendea haki jambo hili. Niombe sana Wizara iliangalie Gereza la Keko kwani liko katikati ya wananchi na pia haliridhishi, miundombinu ya gereza lenyewe na hata nyumba za askari. Niombe sana muwaangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Naibu wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Katibu Mkuu Ndugu Ally Senga Gugu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Maduhu I. Kazi, watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye majukumu ya ulinzi wa usalama wa raia hapa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwapongeze Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro Ndugu Simon Maigwa na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Moshi *(OCD),* Ndugu Azizi Musa Kalokola, kwa mafanikio yao makubwa ya kudhibiti matukio ya usalama katika jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ni miundombinu muhimu sana iliyotengenezwa kusaidia binadamu kurahisisha mawasiliano toka sehemu moja hadi nyingine kwa kutumia usafiri kama vile magari, trekta, pikipiki na baiskeli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo utahusu changamoto za ajali barabarani na umuhimu wa kuwekeza kwenye teknolojia za kisasa kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa ajali hizi zinachangiwa na mwendokasi wa madereva pamoja na kutokufuata sheria na alama za usalama barabarani. Takwimu zinaonesha kwamba kati ya Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ajali 1,322 za barabarani zilitokea Tanzania na kusababisha vifo 1,275; pia katika kipindi hicho, watu 2,278 walijeruhiwa. Idadi ya vifo na majeruhi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi hapa nchini kupitia Maafisa wa Kitengo cha Usalama Barabarani wamekuwa nguzo kubwa kwenye kudhibiti ajali za barabarani. Pamoja na jitihada za Jeshi la Polisi, bado tatizo hili ni kubwa na utatuzi wake umekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na unyeti wa changamoto za ajali barabarani, kuna umuhimu wa Taifa letu kufanya mageuzi makubwa ya mikakati ya kudhibiti ajali hizi ikiwa ni pamoja na kuanza kutumia teknolojia za kisasa ili kukabiliana na hawa wahalifu kwa sababu *traffic police* hawezi kuwepo maeneo yote ya barabara na hata kwenye zile sehemu nyeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia inayotumika sasa hivi ni ile ya polisi kusimama barabarani na kukagua waendeshaji. Pia kwa uchache, polisi husimama barabarani na kutumia kifaa cha kupimia mwendo barabarani, tulivyozoea kuviita *torch* kwa lugha yetu ya barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hizi *torch* mfumo huu unamwezesha askari anapofika eneo lenye ukomo wa mwendo, mfano *50 kilometer per hour,* huirekebisha kamera ipige picha iwapo *speed* ya chombo itavuka *50 kilometer per hour.* Askari akishafanya hivi, kinachoendelea ni kuitumia hiyo picha kama ushahidi wa mhusika kuvunja sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kudumu kwa changamoto hii ni kuwekeza katika teknolojia za usalama barabarani ambazo zinakuwepo muda wote. Kwa mfano, kama tukiwa na kamera za kudumu katika maeneo yote yenye taa za kuruhusu magari *(traffic lights)* kupita au yenye makatazo ya ku-*overtake* au kukimbia kwa mwendo wa *30 kilometer per hour, 50 kilometer per hour, 80 kilometer per hour* au *120 kilometer per hour,* picha za kamera zinazochukuliwa zitawasiliana moja kwa moja na kanzidata za mamlaka zingine na mmiliki wa chombo atakuwa amejulikana na atapelekewa faini moja kwa moja kwenye anuani yake ya makazi bila ya mazungumzo yoyote kwa sababu ushahidi wa picha utakuwepo. Makosa kama haya huwa hayana mjadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamera za uchunguzi ni nini? Hizi ni kamera za *video* zinazotumiwa kwa madhumuni ya kutazama eneo. Kamera hizi mara nyingi huunganishwa kwenye kifaa cha kurekodi na zinaweza kutazamwa na mwendeshaji au afisa wa kutekeleza sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia hii huhitaji nishati ya umeme. Kwa kuwa manispaa, miji na majiji mengi ya Tanzania yamefanikiwa kufunga taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua, hili litarahisisha uwekaji wa kamera zitazotumia nishati ya jua pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za kamera hizi ni:-

(i) Kunasa ushahidi utakaotumika kuwawajibisha madereva wazembe waendeshao mwendo mkali, wasababishao ajali na kukimbia eneo la tukio, wavunjao sheria makusudi kama kupita njia za mwendokasi, kutosimama inapooneshwa taa nyekundu au kwenye alama za vivuko.

(ii) Kuwatia hofu madereva kutovunja ya Sheria za Usalama Barabarani kwa kuamini wanaonwa na kamera.

(iii) Kuwapunguzia Maafisa Usalama Barabarani ugumu wa kazi na kupunguza mianya ya rushwa.

(iv) Kuwapatia polisi taarifa sahihi za vyanzo vya ajali ili kulinda madereva wasio na hatia na kuwezesha maboresho ya mikakati ya kudhibiti ajali.

(v) Kuwawezesha polisi kudhibiti suala zima la foleni barabarani na kufuatilia maeneo hatarishi kama madaraja yaliyofurika ili kuyafunga na kuzuia maafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwekeza kwenye teknolojia ya kamera za barabarani zitasaidia kupunguza kiwango cha uhalifu katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kamera za uchunguzi zitawarahisishia polisi uchunguzi wa uhalifu na kuwapatia taarifa za kijasusi kuhusu upangaji na utekelezaji matukio wa vikundi vya wahalifu, kuwatambua wahalifu na kuwawezesha kuwasili kwa wakati maeneo ya matukio ili kuzuia uhalifu kabla haujafanyika.

(ii) Kamera za uchunguzi pia zitatumika katika ushahidi mahakamani ili kuharakisha uchunguzi na kuwalinda wasio na hatia. Endapo unashutumiwa kimakosa, kamera za uchunguzi zinaweza kutoa ushahidi wa *video* kuwa hukuwepo eneo la tukio au hukufanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha matumizi ya teknolojia hizi, ni vyema mamlaka zitunge sheria zitakazoruhusu na kutoa miongozo ya matumizi ya teknolojia hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nihitimishe kwa kusema kwamba kamera za uchunguzi zinaweza kutupatia faida lukuki za kiusalama katika barabara zetu. Zama zimebadilika na ni wakati muafaka sasa kwa mamlaka za Jeshi la Polisi, kubadilika na kuendana na teknolojia mpya kama kamera za uchunguzi ili kutatua changamoto za usalama barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu ambayo ni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyenipa afya njema na kukutana jioni hii kwa ajili ya mjadala huu muhimu sana kwa ajili ya mustakabali mzima wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu walionitangulia kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Pia niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri kwa

Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Nimhakikishie Mheshimiwa Rais na Watanzania wote nafasi hii nitaitumia kwa manufaa makubwa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Makamu Rais kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu pamoja na viongozi wote ambao wanatupa mwongozo na maelekezo ambayo kwa kweli yamekuwa chachu katika utendaji kazi wa Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi ambavyo wanaendesha Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa sana. Pia ninamshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Bashungwa. Mheshimiwa Bashungwa amekuwa ni Waziri, Mwalimu, amekuwa ni kaka mchapakazi, lakini amekuwa ni kiongozi mahiri kabisa ambaye anahakikisha kwamba kama Wizara tunafanya kazi kama timu. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, nimhakikishie kwamba mimi kama msaidizi wake namba moja nitafanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa katika kukusaidia kazi ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi kuishukuru sana Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalma ikiongozwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Vincent Mbogo, Makamu Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa wanayofanya, maono yao, mapendekezo yao imekuwa chachu kubwa pia katika utendaji kazi ndani ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru Watendaji wa Wizara hii Katibu Mkuu, Ndugu yetu Ally Gugu, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Maduhu Kazi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii, Wakuu wa Idara pamoja na vitengo kwa ushirikiano mkubwa wanaotupa katika utendaji kazi wa ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza sana Wakuu wetu wa Vyombo vya Ulinzi ambavyo viko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Ninawapongeza sana Kamishna Jenerali Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini *IGP* Camillus Wambura; Mkuu wa Jeshi la Magereza Kamishna Jenerali Jeremiah Katundu; Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Kamishna Jenerali John Masunga; pamoja na Mkuu wa Idara yetu ya Uhamiaji Dkt. Anna Makakala kwa kazi kubwa wanayofanya katika nchi yetu. Pia na Mtendaji Mkuu wa *NIDA*, Ndugu yetu James Kaji ambaye pia ameanza kazi kwa kasi kubwa sana, tunawapongeza sana kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi na salamu za pongezi basi naomba niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara yetu, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge wote wameonesha uzalendo mkubwa sana kwa Taifa letu hongera sana, niwahakikishie michango yao yote waliyotoa tumeichukua kama Wizara na tunaendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe ufafanuzi wa hoja chache kutokana na muda. Hoja ya kwanza inaenda Fungu la 14 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na hoja iliruhusu Jeshi la Zimamoto na Uokoaji liongezewe nguvu na vifaa. Ninachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameleta mapinduzi makubwa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kwa upande wa ajira, tayari ajira 671 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kati ya hao askari 246 tayari wako kazini, Askari 425 wapo kwenye mafunzo hivi ninavyozungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha unaokuja tunaouzungumzia hapa 2025/2026 tunatarajia kuajiri askari 1,000 wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Hii yote ni kuboresha utendaji kazi wa Jeshi letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza pia tunajenga vituo saba (miradi ambayo imeshapokea fedha zote) katika mikoa ifuatayo; Kituo cha Kuzimia Moto Mkoa wa Manyara, Njombe, Simiyu,

Geita, Katavi, Kagera na Songwe. Jumla ya fedha shilingi bilioni 2.59 zimeshapokelewa na kazi inatarajiwa kumalizika ifikapo mwezi Septemba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeshanunua zaidi ya magari 12 makubwa yaliyosambazwa kwenye Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. Bado Jeshi linaendelea kutengeneza mradi mkubwa ambao unagharimu Dola za Marekani milioni 100 ambapo mradi huu unaenda kununua vifaa vingi vya uokoaji na zimamoto ambapo ukisoma ukurasa wa 67 wa Mheshimiwa Waziri ametaja miradi. Pia, tunapata vitendeakazi kama magari ya zimamoto yapatayo 150 ambayo yatasambazwa kwenye wilaya zote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameongea Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati na wengine wengi kwamba, hawana magari ya zimamoto. Niwahakikishie Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeshanunua magari 150 kwa ajili ya zimamoto katika wilaya zote hapa nchini na baadhi ya mikoa ambayo bado haina magari hayo ya zimamoto na uokoaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ununuzi wa magari, tumenunua boti 23 (ameongea Mheshimiwa Stella Manyanya), boti 23 za uokoaji zinaenda kwenye Maziwa Makuu (Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.) Kwa hiyo, Mheshimiwa Stella Manyanya nimhakikishie boti zinakuja kwa ajili ya uokoaji katika Maziwa Makuu hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na boti hizo, tuna magari 40 ya kubebea wagonjwa, magari 30 ya mawasiliano na *helicopter* moja. Haya yote ni katika kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 tunaoujadili hapa, Jeshi limetengewa shilingi 18,013,513,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hoja hii ya Zimamoto na Uokoaji, ninaomba niende kwenye Fungu 29 Jeshi la Magereza. Kulikuwa na hoja ya Serikali kupunguza msongamano magerezani kupitia maelekezo ya Tume ya Haki Jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kupitia mipango mbalimbali, Serikali kwa kuzingatia mapendekezo ya Haki Jinai imeanza kutumia adhabu mbadala kwa makosa ambayo si hatarishi kwa jamii, kama vile; wafungwa kwenda kumaliza vifungo nje ya magereza na kufanya huduma za kijamii, kifungo cha nje pamoja na kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu kwamba mtu asikamatwe bila upelelezi kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili tumelinganisha kwa mwezi Machi, 2022 tulikuwa na wafungwa na mahabusu 32,371 lakini mwezi Machi mwaka huu 2025 tuna wafungwa 27,227. Kwa hiyo, punguzo ni kubwa na tunaendelea kuboresha kuhakikisha kwamba, magereza yetu haya yanakuwa hayana msongamano mkubwa tena kwa wafungwa na mahabusu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine Serikali iboreshe miundombinu ya Mahakama Mtandao. Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Mahakama imeendelea kufanya kazi hii ya kuboresha huduma ya Mahakama Mtandao ambapo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, tayari Jeshi la Magereza limepokea makasha 10 kwa ajili ya Mahakma Mtandao ambayo yamesaidia sana kurahisisha usikilizwaji wa kesi na kupunguza gharama kwa Serikali kuwapeleka mahabusu kwenye Mahakama na kuwarudisha rumande au magerezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Magereza inajenga vyumba saba vya Mahakama Mtandao hivi sasa katika Magereza ya Sumbawanga (Rukwa), Lindi, Musoma (Mara), Mkuza (Pwani), Geita, Bariadi (Simiyu) na Babati (Manyara). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu Jeshi la Magereza kutengeneza miundombinu ya kuwezesha uvunaji wa maji ya mvua. Jambo hili linafanyika na Jeshi la Magereza limeshaanza

kufanya jambo hili kwa kuchimba visima na mabwawa makubwa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua. Haya yanasaidia katika kilimo cha umwagiliaji pamoja na ufugaji wa samaki. Hanang inafanyika katika maeneo ya Ubena na kilimo kule Urambo, Sumbawanga sambamba na mabwawa ya ufugaji wa samaki katika Magereza ya Pawaga yapo Mkoani Iringa na Kwamgumi kule Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu Serikali iwapatie makazi safi Askari na Maafisa wa Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza limeendelea kutenga fedha kwenye mapato ya ndani na limeendelea kujenga nyumba za askari wake. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali iliunga mkono juhudi za Jeshi la Magereza kwa kutenga shilingi 147,881,000 kwa ajili ya kumalizia nyumba tano za Gereza la Kalilankulukulu zilizojengwa kwa uratibu huo na kukamilisha nyumba tano za Kikosi Maalum cha Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu Serikali kupitia Jeshi la Magereza iajiri wataalam wa TEHAMA. Tayari Serikali kupitia Jeshi la Magereza imeshaajiri wataalam wa TEHAMA watano na tayari wameshaanza kazi. Tayari katika huu mwaka wa fedha, hawa wameshapangiwa kazi lakini Jeshi limepewa kibali cha kuajiri tena askari wataalam wa TEHAMA wapatao 55 kuhakikisha kwamba wanafanya kazi hii hasa ya Mahakama Mtandao katika magereza yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu Serikali iwezeshe Jeshi la Magereza kununua zana na mitambo ya kisasa kwa ajili ya shughuli za kilimo. Serikali kwa kupitia Jeshi la Magereza imeshafanya kazi hii na katika mwaka wa fedha 2024/2025, tayari Serikali ilitenga shilingi bilioni 2.378 kwa ajili ya kuboresha uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuongeza mitambo na zana za kisasa kama matrekta na zana nyingine. Haya yote ni katika kuboresha kilimo chetu katika magereza yetu hapa nchini, ili kujikidhi kwa chakula na pia kujitosheleza kwa mahitaji mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye ushauri wa Kamati yetu ya NUU. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti kwa taarifa nzuri aliyowasilisha mahali hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja au ushauri wa Kamati Serikali ihakikishe kwamba, imetenga fedha kukamilisha magereza mapya mawili na kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa magereza manne ya zamani. Tumetenga fedha kwenye mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo nimhakikishie Mheshimiwa Mwenyekiti na Kamati yake kwamba ushauri wao umezingatiwa na nia ya Serikali ni kuboresha magereza yetu yaliyochakaa hapa nchini. Nimhakikishie katika mwaka wa fedha 2025/2026 tumetenga fedha na tutasimamia kuhakikisha kwamba magereza yetu haya mapya yanakamilika pamoja na kurekebisha haya mengine kuu kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya Kamati ni kwamba ili kufikia tija na malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa mafunzo ya urekebu; Serikali iboreshe miundombinu chakavu ya magereza. Kama ilivyoeleza hotuba ya Mheshimiwa Waziri aya ya 102, Serikali ilitenga shilingi milioni 3.37 na zilipokelewa Mwezi Aprili, 2025 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu. Katika huu mwaka wa fedha pia Serikali imetenga shilingi bilioni 3.9 kuhakikisha kwamba tunakarabati magereza mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali iendelee kuliwezesha Jeshi la Magereza kupata magari kwa ajili ya kusafirisha mahabusu na kuimarisha Mfumo wa Mahakama Mtandao katika magereza nchini, ikiwa ni sehemu ya uimarishaji wa Mfumo wa Haki Jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati umezingatiwa na hivi karibuni Wizara kupitia Jeshi la Magereza ilipokea magari saba yaliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya huduma za mahabusu. Pia, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 huu tunaoujadili, tayari tumetenga fedha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kununua mabasi mapya kabisa kwa ajili ya kusafirisha wenzetu wanaokwenda kusikia mashauri yao kupitia Mahakama mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mahakama Mtandao, kama alivyosema kwenye aya ya 84 Mheshimiwa Waziri kwenye

hotuba yake, tayari Wizara kupitia Jeshi la Magereza imejipanga kufikisha huduma hiyo katika magereza 63 yaliyobaki ndani ya miaka mitatu kuanzia huu mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu Wizara iweke mkakati wa kuhakikisha vyombo vya ulinzi vilivyo chini ya Wizara vinapata maeneo ya ardhi kwa ajili ya matumizi ya wakati ujao. Jambo hili tumelizingatia, Jeshi la Magereza lina mkakati madhubuti wa kupata maeneo ya ardhi katika halmashauri kote hapa nchini, ili kupeleka huduma hii kwa karibu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, Jeshi limepeleka Maafisa Magereza *(District Prison Officers - DPO's)* katika Wilaya ambazo hazina Magereza. Lengo ni kuhakikisha kwamba, Serikali inatenga maeneo hayo lakini tunajenga magereza kwa ajili ya maeneo mbalimbali ambayo hayana magereza nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hilo, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 ilitenga shilingi milioni 492.9 kwa ajili ya kupima maeneo sita na kulipia fidia kwa maeneo matatu na huu mwaka wa fedha tunaoujadili sasa 2025/2026, Wizara kupitia Jeshi la Magereza imetenga shilingi milioni 795.7 kwa ajili ya kupima maeneo 17 na kulipa fidia maeneo manne. Lengo ni kuhakikisha kwamba, maeneo yote yanakuwa na ardhi kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Magereza hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kengele ya pili hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya kutoa ufafanuzi huo mfupi ninaomba Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wao watupitishie bajeti yetu ili tukafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia fursa ya kuweza kuwa na mjadala mzuri tangu asubuhi mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaomba nikushukuru kwa fursa hii uliyonipatia ya kuhitimisha hoja. Nikushukuru pia, kwa kutuongoza vizuri tangu asubuhi ulituanzishia vizuri na hivi tunaenda kwenye kuhitimisha. Pia, katika shukrani zangu ninaomba pia nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Bunge dada yangu Mheshimiwa Najma Giga kwa namna ambavyo amekusaidia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi mzuri wa hoja za Waheshimiwa Wabunge na nimshukuru na kumpongeza kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kunisaidia katika kusimamia majukumu ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametukabidhi kusimamia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge 21 ambao wamepata fursa ya kuchangia siku ya leo. Pia, nilishukuru Bunge zima kwa namna ambavyo wameonesha umoja na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia michango ambayo tumeipata siku ya leo, ni dhahiri Waheshimiwa Wabunge mmedhihirisha kuwa Taifa letu linapoguswa na mtu au kundi lolote ambao hawana nia njema na Taifa letu, Bunge hili halina muhali na watu wa aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa uzalendo huu. Wamempa moyo sana Mheshimiwa Rais wetu na Amiri Jeshi Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan na ninaamini kule ambako yupo amepata faraja sana kupitia Bunge hili. Kwa niaba yake ninaomba niwashukuru na ninaomba pia niwashukuru kwa niaba ya vyombo vya ulinzi na usalama. Ninawashukuru sana kwa kuwapa moyo na kuwaambia wasiwe na woga, wapige kazi, Taifa hili linawategemea. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi labda nianze na kukumbusha historia kidogo tulifundishwa huko kwenye shule za msingi na sekondari mambo ya *Berlin Conference* mwaka 1884 na mambo ya *Scramble for Africa.* Nitumie nafasi hii kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania, malengo ya nchi ambazo ziligawa Bara letu kwenye *1884 (Scramble for Africa);* malengo ya kipindi kile yalikuwa ni *resource exploitation.* Tusisahau kwamba malengo hayo ya *resource exploitation* yameisha. Walitutawala kupitia njia za ukoloni, baada ya kupata uhuru na wao siyo wajinga, watatafuta njia nyingine ili mradi lengo la kutafuta *resource exploitation* liendelee kuwa palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe sana Watanzania wenzangu hila yoyote ya kuvuruga amani ya nchi, mbinu zozote za kuvuruga amani ya nchi yetu kamwe tusikubali. Waasisi wa Taifa hili wakiona tunaenda nje ya ule wosia ambao walitupatia huko kwenye makaburi yao wanaweza wakageuka wasiamini hawa ndiyo Watanzania ambao tumewaachia hii nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumepata faraja sana kupitia michango ya Waheshimiwa Wabunge. Hakika Tanzania bado wazalendo wapo na Wabunge wameonesha kama viongozi kwamba, Taifa hili linatutegemea sisi wenyewe. Hatuna Tanzania nyingine zaidi ya hii tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, adui anaweza kuja kwa mbinu mbalimbali ikiwemo kuchonganisha vyombo vya ulinzi na usalama na wananchi, ili wakose imani na nyombo vya ulinzi na usalama. Baada ya hapo watakuja na mbinu mbalimbali, wataleta wanaharakati

wavuruge amani na baadaye waseme; tunaona nchi yako uwezo wa kujilinda haupo, tunaomba tukuletee vyombo vyetu viweze kulinda nchi yako. Hii siisemi kama *theory,* angalieni ndani ya Bara la Afrika zipo nchi ambazo zina *mercenaries* wametoka kwenye nchi fulani wameenda kuwa *replacement* ya vyombo vyao vya ulinzi na usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hapo walitumia mbinu za kutenganisha wananchi na vyombo hivyo. Serikali ikaacha kuwekeza kwenye vyombo vya ulinzi na usalama, vikawa dhaifu halafu huyohuyo ambaye ana mbinu ya kukutawala na ku-*exploit resource* yako anakwambia sasa ninaomba nikupatie ulinzi. Polisi anakuwa yeye, uhamiaji ni yeye, Jeshi la Wananchi ni yeye. Sasa ukifikia hatua hiyo uhuru wa nchi unakuwa haupo tena. Kwa hiyo, kamwe Watanzania tusiingie katika hiyo mitego. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo ninaomba nijikite kwenye maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge walihitaji ufafanuzi. Nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri ameshatoa ufafanuzi kwenye baadhi ya taasisi na vyombo ambavyo vipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninaomba nijikite upande wa *NIDA,* Jeshi la Polisi pamoja na michango mingine mahususi ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la usajili wa Watanzania milioni sita kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022, kama ambavyo nimesema kwenye hotuba yangu bado wapo milioni sita. Hata hivyo, tumejipangia kila mwaka wa fedha ikiwemo bajeti hii ambayo tunaomba Wabunge watupitishie ya mwaka wa fedha 2025/2026 angalau kila mwaka tuweze kusajili Watanzania milioni mbili ambao hawajasajiliwa na kwa kipindi cha miaka mitatu tuwe tumekamilisha zoezi zima kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sambamba na hili lipo suala la Jamii Namba. Nitumie nafasi hii kutoa ufafanuzi kwa sababu kumekuwa kuna *confusion* kwamba Jamii Namba ni tofauti na *NIDA* Namba *(National ID)*. Ni jambo hilohilo tofauti yake ni kwamba, *National ID* (Kitambulisho cha *NIDA)* usajili wake tulikuwa tunaanza

miaka 18 na kuendelea. Sasa hivi kwenye kuanzia bajeti hii ambayo tunaomba watupitishie, tunaanza sambamba na kuendelea kusajili Watanzania kuanzia miaka 18 na kuendelea kupata Kitambulisho cha Taifa. Kitambulisho hicho hicho, namba ile ile ndiyo Jamii Namba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho tunayoyafanya ni kwamba kitambulisho hiki sasa tutaanza kuwapatia hii Jamii Namba kuanzia mtoto anapozaliwa, katika utu uzima wake mpaka anafariki anakuwa anatumia namba hiyo na kitambulisho hicho kinakuwa kinatumika kwa matumizi mbalimbali. Ndio maana ikaitwa Jamii Namba kwa maana huduma za kijamii mbalimbali atatumia *National ID* hiyo. Kwa hiyo, ningependa kupitia Bunge hili kuwatolea ufafanuzi Watanzania kwamba, kama una *National ID* tayari, hiyo hiyo ndio itakuwa Jamii Namba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kitambulisho cha *NIDA* ambacho Mtanzania unacho, kinapo-*expire* siyo kwamba namba yako umeipoteza, kwenye mifumo huko namba inakuwa ni hiyohiyo. Kama ile *expiration date* inakukera kwenye kitambulisho, basi unaweza ukaenda kwenye Ofisi ya *NIDA* wakakubadilishia ili kitambulisho chako kiwe kinaonesha hakija-*expire*. Niwaondoe wasiwasi, kitambulisho hicho hicho ukienda mahali popote hautanyimwa huduma kwa sababu ya *expiration date* ambayo ipo kwenye kadi, kwa sababu kwenye mfumo bado ni kitambulisho ambacho ni *valid.* Nimeona hili pia nilitolee ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa fedha maalum. Waheshimiwa Wabunge Wajumbe wa Kamati ya NUU ni mashahidi, shilingi bilioni 45.2 imebidi turudi tena kwenye Kamati kwa sababu, Mheshimiwa Rais baada ya kutambua umuhimu wa kuboresha *NIDA*, umuhimu wa kuanza kusajili Jamii Namba, Mtanzania anapozaliwa aanze kusajiliwa, ndipo Mheshimiwa Rais akaridhia fedha maalum itolewe, shilingi bilioni 45.2 tuwape *NIDA,* ili tuweze kufanya *reforms* ambazo nimewatajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuboresha Taasisi ya *NIDA*, ikiwemo kushughulikia changamoto ambazo Watanzania wamekuwa wakikumbananazo pamoja na masuala ya vitendea kazi hafifu vya *NIDA*, upungufu wa watumishi na ukosefu wa magari. Kwa hiyo, hizi shilingi bilioni 45, Waheshimiwa Wabunge, tunaenda kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye wilaya zetu ulikuwa unakuta tuna watumishi wawili tu, ikitokea mtumishi mmoja amepata dharura, basi anakuwepo mmoja. Kuna foleni nyingi za wananchi wanaohitaji huduma ya *NIDA*, kompyuta unakuta ni mbovu, mtumishi ni mmoja, kero ilikuwa ni kubwa kwelikweli. Kwa hiyo, ninaomba kwa dhati kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa fedha hii maalum, ambayo inaenda kuboresha utendaji wa *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile suala la watumishi kwenye bajeti hii, ambayo tunaomba watupitishie, tumepanga kuajiri watumishi 160 na kuwapeleka kwenye wilaya zetu, ili kupunguza upungufu wa watumishi. Vilevile fedha hii, shilingi bilioni 45, sehemu yake inaenda kununua magari 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko kwenye wilaya Watumishi wa *NIDA* walikuwa wanaomba gari, ama kwa Mkuu wa Wilaya au kwa Mkurugenzi. Ikitokea Mkurugenzi na *CMT* na Mkuu wa Wilaya wana majukumu mengine, basi Ofisi za *NIDA* zilikuwa zinashindwa kutimiza wajibu wao kwa sababu ya upungufu wa magari. Tunaenda kutibu hilo kwa kununua magari 140.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, bajeti hii tunaenda kujenga ofisi za wilaya 31 na kila mwaka tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha kila wilaya inapata Ofisi ya *NIDA*. Tunaanza na hizi 31 na mdogo wangu Mheshimiwa Mariam ametaja hili, tutalizingatia katika vipaumbele vya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, tunaenda kuboresha maslahi ya watumishi na matokeo. Katika hili tutaongeza ufanisi katika kutoa huduma za usajili na utambuzi kwa wananchi kupitia Taasisi ya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, imechangiwa kwa uchungu mkubwa sana namna ambavyo watu wanatumia mitandao vibaya kumdhalilisha Mheshimiwa Rais wetu na ikasemwa vizuri kwamba, hata kama *content* inazalishiwa nje, lakini ndani ya nchi, wanaoisambaza ni Watanzania wenzetu, *cyber bullying*. Nimetumia maneno ya *cyber bullying*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii nimwagize *IGP* Camillus Wambura, tuko naye hapa Bungeni siku ya leo. Kazi nzuri ambayo Jeshi la Polisi linaifanya kwa kushirikiana na *TCRA*, waongeze maradufu kuona watu hao wanashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani unapata *content,* hata kama haijatengenezewa nchini, halafu wewe Mtanzania, watu wanataka kuchoma amani ya nchi yetu, unakuwa ni sehemu ya kuchoma nchi yako! Hatutakubali. Kwa hiyo, *IGP* pamoja na makamanda wakae kikao maalum wabainishe changamoto zilizopo. Waheshimiwa Wabunge tupeni *input,* hata kama ni kwa siri, ili tushughulike na hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Mheshimiwa Rais wetu anafanya kazi nzuri, tumeona, tumeshuhudia kwenye wilaya zetu na kwenye majimbo yetu. Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi umefanyika, haijapata kutokea, halafu inatokea dakika za mwisho hizi watu wenye wivu wanawatumia watu wachache kutuvuruga na kusababisha Watanzania tuanze kunyooshea vidole wakati kuna mambo mengi yamefanyika huko kwenye vijiji, kata na wilaya zetu ambazo Rais huyu anahitaji maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwashukuru sana sana. Wameshuhudia kazi kubwa ambayo Rais wetu amefanya. Hatutakubali kuona anadhalilishwa na huku vyombo tunavyo na teknolojia ipo ya kudhibiti hao wahalifu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hili tunaenda kulifanyia kazi na niwahakikishie vyombo vyetu viko timamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye upande wa Jeshi la Polisi. Kulikuwa kuna michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa kwenye vitendea kazi. Wameona ni mashahidi, tunanunua magari, kwa ajili ya makamanda, mpaka kwenye wilaya ma-*OCD* sasa hivi wana magari. Tunajiandaa kuwapa magari *OCCID, Landcruiser* mpya. Kwa hiyo, kwenye upande wa vitendea kazi kwa kweli, Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu amefanya kazi kubwa sana. Wabunge ni mashahidi magari mapya wameona yanapishana barabarani yakienda kwenye wilaya zetu. Hata hivyo, wakatwambia sambamba na hili, kazi hii nzuri iendane na kuboresha maslahi ya askari wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelekezo ya Bunge tumeyachukua. Waheshimiwa Wabunge hata mkiwauliza askari wetu huko kwenye majimbo yetu, kwenye upande wa *uniform,* Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa. Sasahivi askari wetu wanavaa vizuri na wanapendeza. Kwa hiyo, jitihada hizi nzuri za vitendea kazi na *uniform* kupatikana, sasa kwa niaba ya Serikali tumechukua kwamba, kazi hii nzuri iendane na kujenga ustawi mzuri maeneo ya kazi ya askari wetu, kwa maana ya kuwajengea makazi na kuangalia masuala ya maslahi yao tuweze kuyaboresha. Kwa niaba ya Serikali ninaomba tuchukue hii *commitment* tukaifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shilingi bilioni 80.45 ambazo tayari Jeshi la Polisi wanazo, kwa ajili ya kununua vifaa vya upelelezi, kwa maana ya kuimarisha Kamisheni ya Intelijensia kufanya uchunguzi wa kisanyansi, masuala ya *DNA* na upelelezi wa makosa ya jinai. Sasa hata zile changamoto za wizi wa simu, mwananchi anaibiwa simu, anaweza akajua kupitia *IMEI Number* kwamba, mwizi wangu yuko eneo fulani, lakini mchakato kupitia Jeshi la Polisi umekuwa unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa na *IGP* nimemwambia, kwa teknolojia hii tusingependa kuona Watanzania mtu anaibiwa *smartphone,* mwizi anajulikana alipo, halafu hatumkamati. *IGP* tunamwamini, akajipange na makamanda kuhakikisha, masula ya wizi wa simu, simu inapoibiwa basi askari wetu wawe waaminifu, waende

wamkamate mwizi na aoneshwe hadharani, ili awe fundisho kwa watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala hili shilingi bilioni hizi 80.45 ambazo tumewezeshwa zinaenda kuimarisha Idara ya Upelelezi; makosa ya kimtandao na uhalifu wa kifedha pia, tunaenda kushughulika nayo. Kwa sababu, tuna vifaa vya kisasa na hatua ya manunuzi, ya shilingi bilioni hizi 80.45, iko mwisho kwa hiyo, vifaa hivi tutavipata miezi ya karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshasema upande wa maslahi ya askari kwamba, tunaenda kujipanga ili yaendane na kazi nzuri ya kuwapa vitendea kazi. Tumelichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye maombi na michango ya Waheshimiwa Wabunge kwenye majimbo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Vituo vya Polisi ambavyo vinajengwa na vingine vinavyohitaji ukarabati, makazi ya askari katika maeneo ya Waheshimiwa Wabunge huko majimboni, masuala ya boti, Mheshimiwa Naibu Waziri ameshazungumza kwa Mama yangu Mheshimiwa *Eng.* Stella Manyanya na Wabunge ambao wanatoka kwenye Maeneo ya Maziwa Makuu. Hili jambo linaenda kuwa historia, maboti yale ni ya kisasa sana. Kwa hiyo, yatasaidia sana kwenye maeneo ya maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Zuena wa Same Mashariki, Mheshimiwa Usonge wa Kaskazini Unguja, Mheshimiwa Profesa mzee wangu Ndakidemi kuhusu Mabogini, Mheshimiwa Esther Matiko kule Tarime kwa watani zangu; kule kwenye magari wako vizuri na kwenye mipango wapo. Kwa hiyo, hata haya ambayo ameyasema ngoja tuyachukue tukayafanyie kazi, lakini wapo wengi ambao wamesema, *specifically,* kwenye maeneo. Ninaomba waamini kabisa katika ile michango 21 Waheshimiwa Wabunge waliyochangia na maeneo ambayo wameomba, tumeyachukua tunaenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kupitia mchango wa Mheshimiwa Profesa Manya, ninaomba nikiri, hata sisi kwenye upande wa Ofisi ya Msajili wa Jumuiya, kwanza tumepokea mapendekezo ya kamati kwamba, taasisi hii ina majukumu makubwa ni vizuri tukaiangalia katika mwelekeo wa kuifanya iwe ni taasisi iliyokamilika. Kwa sababu, ukienda kwenye wilaya zetu na hili siyo jambo la kisiasa ni suala la kitaalamu, kuna utitiri wa uandikishaji wa hizi taasisi. Kama Mheshimiwa Profesa Manya ulivyosema na sisi tunalitazama hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mtu hajasajili Kanisa, anatoa huduma. Anaamka anasema ameomba, ameoteshwa kwamba, sijui itatokea nini. Kama umeona umeoteshwa kutakuwa kuna hali ambayo siyo nzuri, basi nenda uombe Mwenyezi Mungu aizuie isitokee kwenye Taifa letu, lakini siyo kutoa taharuki kwa Taifa kwamba, jana nimelala nimeota, mimi ni nabii, kutakuwa kuna taharuki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea huyo kiongozi angeenda amwombe Mwenyezi Mungu azuie hilo balaa lisitokee, lakini kiongozi huyu analeta taharuki kwa nchi, Watanzania waache kufanya shughuli zao waanze ku-*panic*. Ukifuatilia unakuta hajasajiliwa, ukimgusa anasema Serikali inavamia viongozi wa dini! Kwa hiyo, tunaenda kufanya uchambuzi vizuri, tutaleta mbele ya Bunge hili tuwaoneshe wale ambao wanafanya kazi kinyume na utaratibu, ili tutakapowachukulia hatua Watanzania wajue kwamba, siyo mambo ya kisiasa. Nadhani Waheshimiwa Wabunge wananielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni masuala ya biashara haramu za usafirishaji binadamu, hii ni changamoto kubwa. Mheshimiwa Tauhida amechangia katika eneo hili, lakini wakuu wa vyombo wamesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tutaenda kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa sababu, vijana wetu hawa wanaokwenda kufanya kazi huko nje ya nchi. Tunawapa *passport* sawa, uhamiaji ni sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaanza kuangalia ndani ya Serikali ni aina gani ya watu wanashiriki katika huu mtandao wa kuwawezesha kupata nyaraka za kusafiri kwa kutumia *agents* ambao wanakuwa

wanafahamu kabisa wakati wana-*recruit* hawa watoto wetu. Wanajua wanaenda kufanyiwa vitu ambavyo ndivyo sivyo, huyo ndiye anamsaidia apate *passport*, lakini anayempa *passport* ndani ya Serikali, Idara ya Uhamiaji, tumbaini ni nani, ili tuweze kushughulika na huu mtandao haramu wa kusafirisha binadamu na kwenda kuwatumikisha kama watumwa huko kwenye nchi za nje. Kwa hiyo, hili tunalishughulikia. Tutashirikiana na vyombo vyote kuhakikisha tunakuwa na mkakati wa kutokomeza changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamezungumziwa masuala ya utaratibu wa ajira na ushauri kutoka kwa ndugu zetu upande wa Zanzibar. Tumechukua ushauri wenu, tutakaa na vyombo tuangalie namna ambavyo utaratibu uliopo na mawazo haya ambayo wametupatia yanavyoweza kuboresha utaratibu wa ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyosemwa ni mengi. Hata Mheshimiwa Esther Matiko amezungumzia suala la *4R*. Kwamba, Rais huyu, Mama yetu huyu, alitoa fursa ya kipekee na mimi siyo kwamba natabiri, sidhani kama tutakuja kupata Rais msikivu kama Rais huyu, akaweza kutoa fursa kwa upinzani kukaa mezani pamoja, halafu ninyi wenyewe wame-*abuse* hii *space*. Sidhani kama watakuja kupata Rais mwingine, ambaye ata-*entertain* kutoa nafasi. Amesema Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Rais wetu alienda Ubelgiji akamwambia mdogo wangu Lissu njoo tukajenge nchi, lakini sasa unambeba mtoto kwenye mbeleko anakung'ata mgongoni, si unaachia mbeleko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *4R* imekuwa *abused* na sidhani kama itakuja kutokea fursa kama hii, kupata Rais msikivu, ambaye ni mshirikishi. Mtu anaweza akawa na tabia nzuri, lakini matendo ya watu yakamfanya abadilike kwa sababu, ya namna watu wanavyochukulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nisiendelee zaidi nikaja nikaharibu, maana haya mambo mengine yanaudhi. Unaweza ukawa hapa, yaani ukaamua kusema vitu ambavyo baadaye vitaleta shida, lakini Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema, michango ya leo, wakuu wa vyombo ambao sisi tukilala wao wanakuwa macho kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. Kupitia Bunge hili Wabunge wamewapa moyo sana, wamewapa morali ya kufanya kazi. Ninaomba niwahakikishie, kazi nzuri ambayo inafanywa na vyombo vya ulinzi na usalama, kwa wale ambao wako ndani ya vyombo wanaenda kinyume na maadili tutaendelea kuchukua hatua dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano, kwa Jeshi la Polisi peke yake; hapa ilichangiwa kwamba, askari wazingatie sheria, kanuni na taratibu. Kwa Jeshi la Polisi peke yake, askari ambao wamechukuliwa hatua za kinidhamu ni 232 wameitwa kwenye Kamati za Maadili, 796 wameshtakiwa Kijeshi na kupewa adhabu mbalimbali, 16 wameshushwa vyeo, 62 wamefukuzwa kazi na 44 mashtaka yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua kuhakikisha wale wachache ambao wanachafua *image* ya Jeshi la Polisi wanachukuliwa hatua, lakini wengi wanaofanya kazi nzuri tuendelee kuwatia moyo. Ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa moyo huu ambao wamewapa Wakuu wa Vyombo, Makamanda, pamoja na Askari na pia, Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu, *guillotine*. *(Makofi)*

**NDG. I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*…………..Sh. 17,075,905,000
Kifungu 3002 – *Fire and Rescue Services Training Institute*……………………………………Sh. 785,957,000
Kifungu 3003 – *Fire Safety*…………………….………..Sh. 863,467,000
Kifungu 3004 – *Operations*…………………….………Sh. 1,021,077,000
Kifungu 3005 – *Legal Services Unit*……….……..……....Sh. 329,832,000
Kifungu 3006 – *Arusha Regional Office*…………..…..Sh. 1,713,836,000
Kifungu 3007 – *Dodoma Regional Office*………..…..Sh. 2,650,154,000
Kifungu 3008 – *Mwanza Regional Office*…….....…....Sh. 2,330,842,000
Kifungu 3009 – *Mbeya Regional Office*……...……....Sh. 1,990,239,000
Kifungu 3010 – *Kinondoni Regional Office*…………Sh. 1,591,281,000
Kifungu 3011 – *Mara Regional Office*……..……..……Sh. 963,448,000
Kifungu 3012 – *Kigoma Regional Office*…..…………Sh. 1,385,235,000
Kifungu 3013 – *Pwani Regional Office*….……………Sh. 2,111,082,000
Kifungu 3014 – *Manyara Regional Office*…………...Sh. 1,365,819,000
Kifungu 3015 – *Geita Regional Office*………………..Sh. 1,215,206,000
Kifungu 3016 – *Temeke Regional Office*…………….Sh. 4,194,469,000
Kifungu 3017 – *Singida Regional Office*……………….Sh. 990,695,000
Kifungu 3018 – *Tabora Regional Office*……………...Sh. 1,353,731,000
Kifungu 3019 – *Iringa Regional Office*………………..Sh. 1,477,556,000
Kifungu 3020 – *Rukwa Regional Office*…….…………Sh. 1,215,470,000
Kifungu 3021 – *Ruvuma Regional Office*………..…..Sh. 1,276,223,000

Kifungu 3022 – *Kagera Regional Office*……………...Sh. 1,179,681,000
Kifungu 3023 – *Mtwara Regional Office*……..……...Sh. 1,157,402,000
Kifungu 3024 – *Lindi Regional Office*…………………Sh. 1,092,338,000
Kifungu 3025 – *Njombe Regional Office*……………..Sh. 1,102,574,000
Kifungu 3026 – *Shinyanga Regional Office*…………Sh. 1,260,500,000
Kifungu 3027 – *Ilala Regional Office*………..………..Sh. 2,035,931,000
Kifungu 3028 – *Kilimanjaro Regional Office*……...…Sh. 1,304,681,000
Kifungu 3029 – *Morogoro Regional Office*………….Sh. 1,566,215,000
Kifungu 3030 – *Katavi Regional Office*…………………Sh. 935,248,000
Kifungu 3031 – *Tanga Regional Office*………………Sh. 1,887,954,000
Kifungu 3032 – *Simiyu Regional Office*…………………Sh. 968,125,000
Kifungu 3033 – *Songwe Regional Office*……………..Sh. 1,107,476,000
Kifungu 3034 – *Fire and Rescue Training College*....Sh. 4,277,870,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………....Sh. 187,951,372,061
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*………...…Sh. 319,415,816,221
Kifungu 1003 – *Internal Monitoring and Evaluation Unit*…………………………..Sh. 338,260,678
Kifungu 1004 – *Legal and Research Services Unit*…...Sh. 298,443,147
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……………………..Sh. 540,907,064
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*….....Sh. 213,364,920
Kifungu 2001 – *Police Main Force*……………………..Sh. 6,180,161,293
Kifungu 2002 – *Police Marine*……………...…………...Sh. 1,767,900,960
Kifungu 2003 – *Railway Police Division*……...……….Sh. 5,683,845,760
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*………………....Sh. 4,339,798,800
Kifungu 2005 – *Police Zanzibar*………...……………..Sh. 10,214,251,757
Kifungu 2006 – *Police Air Wing*……………………….....Sh. 2,999,700,824
Kifungu 2007 – *TAZARA Police*…………………………Sh. 2,220,175,899
Kifungu 2008 – *Field Force Unit*……..………………....Sh. 2,292,799,291
Kifungu 2009 – *Traffic Police*……………...…………….....Sh. 947,436,030
Kifungu 2010 – *Police Airport*………………………....Sh. 4,251,250,189
Kifungu 2011 – *Police Dog and Horses*………………Sh. 1,207,192,000

Kifungu 2012 – *Dar es Salaam Special Zone*…..…...Sh. 3,131,946,051
Kifungu 2013 – *Police Ilala*…………………………….Sh. 12,533,410,853
Kifungu 2014 – *Police Kinondoni*……….……………..Sh. 15,965,061,790
Kifungu 2015 – *Police Temeke*…………………………Sh. 9,496,911,669
Kifungu 2016 – *Police Arusha*…………..……………Sh. 17,584,505,854
Kifungu 2017 – *Police Iringa*………………………...Sh. 10,643,608,973
Kifungu 2018 – *Police Kilimanjaro*……………………Sh. 15,246,089,146
Kifungu 2019 – *Police Kigoma*…………..…………...Sh. 12,632,030,250
Kifungu 2020 – *Police Kagera*………………………...Sh. 13,755,659,438
Kifungu 2021 – *Police Lindi*……………………………...Sh. 9,508,817,000
Kifungu 2022 – *Police Mwanza*………………………Sh. 18,901,460,064
Kifungu 2023 – *Police Mara*…………………………...Sh. 10,434,183,854
Kifungu 2024 – *Police Tarime-Rorya*………..………..Sh. 9,421,621,641
Kifungu 2025 – *Police Mbeya*……….……………....Sh. 14,072,538,664
Kifungu 2026 – *Police Mtwara*…...…………………...Sh. 11,250,605,608
Kifungu 2027 – *Police Morogoro*……..……………...Sh. 17,760,801,060
Kifungu 2028 – *Police Manyara*…………………….Sh. 11,496,391,270
Kifungu 2029 – *Police Singida*……….…………….....Sh. 11,105,680,440
Kifungu 2030 – *Police Pwani*………………………….Sh. 11,886,930,260
Kifungu 2031 – *Police Ruvuma*……………………….Sh. 10,489,100,840
Kifungu 2032 – *Police Rukwa*…………………………...Sh. 8,782,368,904
Kifungu 2033 – *Police Shinyanga*……..……………..Sh. 11,192,279,266
Kifungu 2034 – *Police Tabora*………………………....Sh. 11,777,619,858
Kifungu 2035 – *Police Tanga*…………..…………..Sh. 14,797,825,590
Kifungu 2036 – *Police Mjini Magharibi*………..……Sh. 12,025,677,314
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja*.........................Sh. 5,288,582,880
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja*...................Sh. 4,759,643,178
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*.........................Sh. 4,608,742,276
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba*..................Sh. 4,816,034,533
Kifungu 2041 – *Police Dodoma*…………..………Sh. 20,239,401,000
Kifungu 2042 – *Police Geita*…………..…………...Sh. 10,837,076,365
Kifungu 2043 – *Police Katavi*..................................Sh. 6,958,102,325
Kifungu 2044 – *Police Njombe*…………..……………Sh. 8,346,628,234
Kifungu 2045 – *Police Simiyu*……………….…..……Sh. 7,976,807,990
Kifungu 2046 – *Police Songwe*………..………………Sh. 7,385,561,038
Kifungu 2047 – *Police Rufiji*…………………………..…Sh. 6,574,382,630
Kifungu 2048 – *TPF Corporation Sole Unit*……………....Sh. 133,908,000
Kifungu 2049 - *Police Bandari*………..……………….Sh. 3,056,018,344

Kifungu 2050 – *Police Band*……………………………..Sh. 2,067,453,672
Kifungu 2051 – *Police Bohari*………..………………..Sh. 15,854,744,320
Kifungu 3001 – *Police College Moshi*………………..Sh. 34,866,535,942
Kifungu 3002 – *Police College*………...………………Sh. 3,378,018,144
Kifungu 3003 – *Operations and Training*…………….Sh. 5,529,120,288
Kifungu 3004 – *Zanzibar Police College*……………...Sh. 1,278,102,080
Kifungu 3005 – *Mwanza Marine Police College*…...Sh. 1,343,953,530
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College – Kidatu*………………………………...Sh. 2,093,703,694
Kifungu 4001 – *Police Vehicles Maintenance Unit*……………………………………..Sh. 5,237,806,360
Kifungu 5001 – *Police Medical Unit*…..……………....Sh. 3,941,250,291
Kifungu 6001 – *Police Ujenzi*…………………………Sh. 1,019,704,254
Kifungu 7001 – *Criminal Investigation Division*…….Sh. 10,222,614,627
Kifungu 7002 – *Stock Theft Prevention Unit*……………Sh. 841,240,107
Kifungu 7003 – *Criminal Intelligence Bureau*……….Sh. 2,944,754,156
Kifungu 7004 – *Forensic Intelligence Bureau*……….Sh. 4,999,283,909
Kifungu 7005 – *Community Engagement*…………...Sh. 1,370,204,282

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………….……….Sh. 41,609,007,696
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……..….Sh. 1,900,198,800
Kifungu 1003 – *Public Relations and Communication Unit*……………………..……………...Sh. 226,374,400
Kifungu 1004 – *Intelligence and Operations Unit*…....Sh. 498,560,600
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……..……………...Sh. 1,361,823,940
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…..Sh. 1,312,313,632
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*…..…………………...Sh. 1,745,973,940
Kifungu 2001 – *Legal and Prisons Unit*………………...Sh. 5,490,819,268
Kifungu 2002 – *Correctional and Rehabilitation*..Sh. 128,196,140,796
Kifungu 2003 – *Resettlement of Offenders*………….Sh. 6,141,259,420
Kifungu 2004 – *Prisons Arusha*………………………..Sh. 6,660,143,024

Kifungu 2005 – *Prisons Dar es Salaam*………………Sh. 14,932,421,168
Kifungu 2006 – *Prisons Dodoma*……………………..Sh. 7,271,600,952
Kifungu 2007 – *Prisons Kigoma*……..…………………Sh. 1,149,186,696
Kifungu 2008 – *Prisons Tanga*………………………...Sh. 6,603,949,824
Kifungu 2009 – *Prisons Kagera*…………………………Sh. 5,173,867,612
Kifungu 2010 – *Prisons Mwanza*………...…………..Sh. 4,478,470,540
Kifungu 2011 – *Prisons Tabora*…………...……………Sh. 1,321,246,240
Kifungu 2012 – *Prisons Mbeya*…...…………………..Sh. 6,071,274,868
Kifungu 2013 – *Prisons Singida*…………………………Sh. 3,254,210,800
Kifungu 2014 – *Prisons Coast*…………...…………....Sh. 7,483,892,532
Kifungu 2015 – *Prisons Lindi*……………..……………..Sh. 1,833,355,300
Kifungu 2016 – *Prisons Manyara*………...…………….Sh. 3,821,000,020
Kifungu 2017 – *Prisons Mtwara*……………………....Sh. 3,649,399,560
Kifungu 2018 – *Prisons Ruvuma*………………………..Sh. 856,944,200
Kifungu 2019 – *Prisons Rukwa*…………………………..Sh. 3,362,664,464
Kifungu 2020 – *Prisons Mara*……………………………Sh. 4,590,589,312
Kifungu 2021 – *Prisons Iringa*…………...………………Sh. 2,941,985,108
Kifungu 2022 – *Prisons Kilimanjaro*……………………..Sh. 6,106,409,232
Kifungu 2023 – *Prisons Morogoro*………..…………..Sh. 11,621,513,476
Kifungu 2024 – *Prisons Geita*……...……………………Sh. 3,085,098,276
Kifungu 2025 – *Prisons Katavi*…………………………...Sh. 1,989,491,156
Kifungu 2026 – *Prisons Njombe*…………………………...Sh. 537,607,820
Kifungu 2027 – *Prisons Simiyu*……...……………………...Sh. 892,974,020
Kifungu 2028 – *Prisons Shinyanga*……………………….Sh. 646,824,800
Kifungu 2029 – *Prisons Songwe*……...………………....Sh. 2,553,954,520
Kifungu 3001 – *Ukonga Prisons Staff College*……….Sh. 5,689,263,536
Kifungu 3002 – *Kingolwira Prisons Driving School*…..Sh. 1,430,227,860
Kifungu 3003 – *Ruanda Prisons Trade School*…...…..Sh. 1,524,314,932
Kifungu 3004 – *Prisons College Kiwira*………………..Sh. 1,999,361,660
Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade*…..…………..Sh. 5,021,506,000
Kifungu 4002 – *Prison Industries*…………..…………………………..Sh. 0
Kifungu 4003 – *Prison Farms*……………………………………………Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………………..…..Sh. 41,185,635,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…...……Sh. 1,034,074,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………….Sh. 1,639,972,000
Kifungu 1004 – *Probation Services Division*………….Sh. 5,987,698,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*….Sh. 979,871,000
Kifungu 1006 – *Information and Communication Technology Unit*……………………….....Sh. 833,107,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*……………………..Sh. 772,560,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…......Sh. 964,822,000
Kifungu 1009 – *Complaints Unit*………………………..Sh. 636,860,000
Kifungu 1010 – *Legal Services Unit*…...…………………Sh. 904,594,000
Kifungu 1011 – *The Police, Prisons, Fire & Rescue and Immigration Services Commission*….…………...Sh. 1,121,758,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*………Sh. 881,312,000
Kifungu 2001 – *Registrar of Societies Unit*……………Sh. 1,162,826,000
Kifungu 4001 – *Refugees Services Division*…….....…...Sh. 3,525,031,000
Kifungu 4002 – *Anti-Trafficking in Person Secretariat*…………………………..Sh. 1,345,420,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji

Kifungu 2001 – *Immigration Zanzibar*……………….Sh. 18,830,000,000
Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*…….....Sh. 125,260,707,000
Kifungu 2003 – *Immigration Ilala*………………………..Sh. 70,680,000
Kifungu 2004 – *Tanzania Regional Immigration Training Academy*…..…………………..Sh. 348,000,000
Kifungu 2005 – *Immigration Kinondoni*…………………...Sh. 70,680,000
Kifungu 2006 – *Immigration Temeke*……………………...Sh. 70,680,000
Kifungu 2007 – *Immigration Arusha*………...…………...Sh. 199,605,000
Kifungu 2008 – *Immigration Dar es Salaam*………….....Sh. 170,280,000
Kifungu 2009 – *Immigration Dodoma*…….....…………...Sh. 171,072,000
Kifungu 2010 – *Immigration Geita*……………………Sh. 170,403,000

Kifungu 2011 – *Immigration Iringa*………………………Sh. 154,173,000
Kifungu 2012 – *Immigration Kilimanjaro*………………..Sh. 199,017,000
Kifungu 2013 – *Immigration Kigoma*……………………Sh. 240,924,000
Kifungu 2014 – *Immigration Katavi*..............................Sh. 172,041,000
Kifungu 2015 – *Immigration Kagera*............................Sh. 247,692,000
Kifungu 2016 – *Immigration Lindi*................................Sh. 162,270,000
Kifungu 2017 – *Immigration Mwanza*..........................Sh. 201,315,000
Kifungu 2018 – *Immigration Manyara*.........................Sh. 175,632,000
Kifungu 2019 – *Immigration Mbeya*.............................Sh. 192,636,000
Kifungu 2020 – *Immigration Morogoro*........................Sh. 191,082,000
Kifungu 2021 – *Immigration Mtwara*............................Sh. 192,546,000
Kifungu 2022 – *Immigration Mara*................................Sh. 206,349,000
Kifungu 2023 – *Immigration Njombe*...........................Sh. 173,445,000
Kifungu 2024 – *Immigration Pwani*...............................Sh. 201,561,000
Kifungu 2025 – *Immigration Ruvuma*...........................Sh. 180,213,000
Kifungu 2026 – *Immigration Rukwa*..............................Sh. 180,051,000
Kifungu 2027 – *Immigration Simiyu*...............................Sh. 172,080,000
Kifungu 2028 – *Immigration Singida*............................Sh. 177,345,000
Kifungu 2029 – *Immigration Shinyanga*.......................Sh. 156,015,000
Kifungu 2030 – *Immigration Tanga*………………..……...Sh. 206,079,000
Kifungu 2031 – *Immigration Tabora*…………………….Sh. 183,546,000
Kifungu 2032 – *Immigration Songwe*……..……………Sh. 177,795,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIRADI YA MAENDELEO**

**Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

Kifungu 3001 – *Fire and Rescue Services*…..……….Sh. 8,286,371,000
Kifungu 3008 – *Mwanza Regional Office*……………...Sh. 400,000,000
Kifungu 3009 – *Mbeya Regional Office*………………..Sh. 200,000,000
Kifungu 3011 – *Mara Regional Office*………………...Sh. 2,026,505,000
Kifungu 3013 – *Pwani Regional Office*…….…………...Sh. 400,000,000
Kifungu 3014 – *Manyara Regional Office*…………………………...Sh. 0

Kifungu 3015 – *Geita Regional Office*……………………………….Sh. 0
Kifungu 3017 – *Singida Regional Office*……………...Sh. 1,626,505,000
Kifungu 3018 – *Tabora Regional Office*………………...Sh. 400,000,000
Kifungu 3019 – *Iringa Regional Office*…………………..Sh. 400,000,000
Kifungu 3021 – *Ruvuma Regional Office*………………Sh. 200,000,000
Kifungu 3022 – *Kagera Regional Office*………….………………...Sh. 0
Kifungu 3025 – *Njombe Regional Office*……………..……………..Sh. 0
Kifungu 3029 – *Morogoro Regional Office*……..……..Sh. 400,000,000
Kifungu 3030 – *Katavi Regional Office*……………..………………Sh. 0
Kifungu 3031 – *Tanga Regional Office*………..………Sh. 400,000,000
Kifungu 3032 – *Simiyu Regional Office*………………………………Sh. 0
Kifungu 3033 – *Songwe Regional Office*……………………………Sh. 0
Kifungu 3034 – *Fire and Rescue Training College*....Sh. 2,874,132,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts*…..………Sh. 154,145,822,000
Kifungu 2004 – *Police Signals Branch*……………….Sh. 24,326,339,400
Kifungu 2006 – *Police Air Wing*………………………………………..Sh. 0
Kifungu 2015 – *Police Temeke*………………………Sh. 1,252,184,152
Kifungu 2016 – *Police Arusha*…………………………..Sh. 139,000,000
Kifungu 2020 – *Police Kagera*………..……………….Sh. 1,503,630,200
Kifungu 2023 – *Police Mara*……………………………Sh. 109,630,000
Kifungu 2026 – *Police Mtwara*…………………………..…………Sh. 0
Kifungu 2027 – *Police Morogoro*………………………..Sh. 90,251,000
Kifungu 2028 – *Police Manyara*………..……………….Sh. 400,000,000
Kifungu 2032 – *Police Rukwa*…………………………..Sh. 115,000,000
Kifungu 2035 – *Police Tanga*…………………………...Sh. 220,000,000
Kifungu 2036 - *Police Mjini Magharibi*……………………..…...Sh. 0
Kifungu 2037 – *Police Kusini Unguja*..........................................Sh. 0
Kifungu 2038 – *Police Kaskazini Unguja*.......................Sh. 445,672,400
Kifungu 2039 – *Police Kusini Pemba*...........................................Sh. 0
Kifungu 2040 – *Police Kaskazini Pemba*.....................Sh. 250,000,000
Kifungu 2044 – *Police Njombe*………..………………...Sh. 150,000,000
Kifungu 2045 – *Police Simiyu*…………………………...Sh. 1,200,000,000

Kifungu 2046 – *Police Songwe*……………..……………Sh. 1,000,000,000
Kifungu 2051 – *Police Bohari*……………..…………..Sh. 16,479,000,000
Kifungu 3006 – *Tanzania Police Staff College Kidatu*……………………..…Sh. 928,513,848
Kifungu 7005 – *Community Engagement*……………...Sh. 600,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*………………………....Sh. 2,309,540,000
Kifungu 2002 – *Correctional and Rehabilitation*…...Sh. 4,047,565,000
Kifungu 4001 – *Prison Building Brigade*……..………..Sh. 7,135,481,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*……………...Sh. 98,550,077,000
Kifungu 4002 – *Anti-Trafficking in Person Secretariat*……………………………..Sh. 4,143,877,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji**

Kifungu 2002 – *Immigration Head Quarter*…...…...Sh. 77,585,245,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kutoa Taarifa kwamba, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake. Ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji; kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wote wameafiki na bajeti imepita.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hongera sana, wewe na Naibu wako na vyombo vyako ambavyo viko hapa; Polisi, Uhamiaji, Magereza, *Fire* na vingine ambavyo wanashughulika navyo. Hongereni sana kwa kazi nzuri, simamieni Sheria za Nchi, ndicho kiapo

ambacho mlikula na vyombo vyako viko vizuri, watiifu na waaminifu. *(Makofi)*

Tatizo ambalo tunapitia sasa hivi, hatutaki kuambizana ukweli, tunaoneana huruma kwa makosa yanayofanywa, ya matusi na kejeli, kwa mamlaka ya nchi. Hivi ukiwa na hoja yako, mimi mara nyingi nina mifano myepesi sana, kuna timu hapa inaweka mpira kwapani, lakini hawakumtukana mtu, walipeleka hoja, hoja ikakubaliwa na sasa wanakwenda vizuri. Ukiwa na hoja yako, ipeleke kwenye maeneo inakotakiwa iende. *(Makofi)*

Ndiyo maana kuna R nne; hoja hii ni *reforms*. Kitu unakiona hakikufai, peleka hoja yako kwenye mstari unaotakiwa kwa heshima na taadhima, utasikilizwa. Unapoanza kejeli na vitisho, kuitia nchi katika matatizo, ndiyo maana ninaomba sana, tena sana, kwa unyenyekevu mkubwa na kuwapigia magoti, taasisi zote za dini, zikemee aina ya uovu kama huu. *(Makofi)*

Rais wa nchi si wa kudhihakiwa. Kanuni zetu za Bunge hapa, humu ndani, zinakataza kumsema vibaya Rais sababu ni mamlaka iliyowekwa na Mungu. Nimesema hapa, Warumi 13:1-2, mimi ninasoma vitabu vyote; kwa hiyo, niombe sana, haya mambo yanaweza kurekebishwa kwa ustaarabu kwa mtu kukubali nimetumia njia siyo sahihi kwenye nchi ambayo ina waungwana, nchi ambayo ina Rais, ambaye ana huruma, Rais aliyeita watu wake warudi nchini kuja kujenga Taifa lao pamoja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana. Nipongeze vyombo vyako, fanyeni kazi kwa mujibu wa Sheria.

Vilevile nimshukuru Mama Bashungwa, toka asubuhi yuko ndani. Kwa hiyo, siyo vibaya leo ukaandaa kahawa nzuri ya maziwa nyumbani mpumzike na mzee. *(Makofi/Kicheko)*

Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.24 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 27 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*